BUNGE LA TANZANIA

_____

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Tatu – Tarehe 14 Mei, 2015

(Mkutano Ulianza Saa 03:00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Selemani Said Jafo, atauliza swali la kwanza, kwa niaba yake Mheshimiwa Bahati.

Na. 20

Madai Mbalimbali ya Wauguzi – Kisarawe

MHE. BAHATI ALI ABEID (K.n.y. MHE. SELEMANI S. JAFO) aliuliza:-

Je, ni lini madai mbalimbali ya Wauguzi wa Wilaya ya Kisarawe kama vile posho ya kutoa huduma kwa muda wa ziada na posho ya mazingira magumu yatalipwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Afya ya Kisarawe ina jumla ya vituo 30 vya kutolea huduma za afya ambavyo ni Hospitali moja ya Wilaya, Vituo vya Afya vitatu na Zahanati 26. Aidha, Idara ina jumla ya watumishi 432 wa kada mbalimbali za afya na kati ya hao 248 ambao ni sawa na 57% ni Wauguzi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watumishi hawa wamekuwa wakidai madai mbalimbali kama vile posho ya kufanya kazi kwa muda wa ziada, fedha za kujikimu kwa waajiriwa wapya, malimbikizo ya mishahara, gharama za masomo, gharama za kusafirisha mizigo kwa waajiriwa wapya, gharama za uhamisho kwa watumishi pamoja na madai ya likizo. Hadi sasa yapo madai ya kiasi cha Sh.366,606,230/= na kati ya hizo Sh.103,264,070.23 sawa na 28% ni madai mbalimbali ya Wauguzi.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupunguza malimbikizo ya madai mbalimbali ya watumishi wa afya mwaka 2000, Serikali ilifuta *Hardship Allowance* na badala yake ilichukua hatua ya kuongeza mishahara ya watumishi wa kada ya afya ili kuboresha mafao yao ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia mwaka wa fedha wa 2014/2015, jumla ya Sh.55,150,728.95 zilikuwa zimelipwa na Serikali kwa wauguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe wenye madai mbalimbali. Aidha, ili kuendelea kupunguza tatizo hili la madai ya wauguzi katika bajeti ya fedha ya mwaka 2015/2016, Halmashauri imetenga jumla ya Sh.112,594,450/= ambazo ni kiasi kikubwa ambacho kitapunguza madai mbalimbali ya watumishi wa kada za afya wakiwemo wauguzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa madai ya Wauguzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwa kadiri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Bahati maswali ya nyongeza.

MHE. BAHATI ALI ABEID (K.n.y. MHE. SELEMANI S. JAFO): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini tulipitisha Bungeni hapa kwamba wanaofanya kazi katika mazingira magumu walipwe. Je, Naibu Waziri haoni sasa ni wakati muafaka wa Wauguzi hawa wanaofanya kazi katika mazingira magumu kulipwa haki zao na malimbikizo yao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hayo yote yanayozungumzwa na Mheshimiwa Bahati ni mambo ambayo Serikali imeshayatolea matamshi hapa ndani. Wale ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu katika Halmashauri zetu tumekwenda zaidi ya hapo. Zipo Halmashauri zetu za Mkoa wa Katavi na Rukwa, mtakumbuka kwamba wameweka *allowance* maalum ambazo zinahudumiwa na Halmashauri zenyewe. Kama Mganga Mkuu anakwenda pale au Daktari anakwenda pale wanampokea kwa *package* hizo. *Package* nyingi ambazo nimezieleza hapa, kwa mfano *Risk Allowance* ambayo imeuliziwa imekuwa *consolidated,* imeingizwa katika mshahara wa mtumishi ili kuweza kusaidia malipo ya uzeeni yaweze kuongezeka kidogo, ndicho kilichofanyika. Hata hivyo, nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kuangalia suala hili lakini kwa sasa wale wanaokwenda katika mazingira magumu tumeanza kuwaangalia kwa tofauti zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo kubwa sana la watumishi walioshikizwa katika Hospitali zetu za Kanisa za *DDH* na zile za *Voluntary Agency* kutokupata mishahara yao kwa wakati. Je, Naibu Waziri analizungumziaje suala hili? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hawa anaowazungumzia Mheshimiwa Mbunge ni wale wanaotoka katika *Designated District Hospital,* zinaitwa Hospitali Teule. Kabla ya kuanza kwa mfumo huu Halmashauri pamoja na hospitali hizi wanakubaliana kwamba sisi Halmashauri tutalipa hivi na watumishi watakaopelekwa pale ni hawa na watumishi wengine hawa wataendelea kulipwa na hilo shirika linalohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama inatokea kwamba wameshikizwa pale na hawalipwi, nakumbuka nimewahi kukutana na kesi hiyo katika hospitali moja ya *Baptist* kule Kigoma, kama kuna hali ya namna hiyo, kuna haja ya kwenda kuungalia mkataba wenyewe unasema nini ili tuweze kuona *discrepancy* anayoieleza pale inatokana na nini. Kwa hiyo, nataka niseme

kwamba namkaribisha Dokta Mbassa anitajie jambo lenyewe ili niweze kulifuatilia mara moja na tuweze kuondoka katika hali hiyo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Suala la matatizo ya Wauguzi na Madaktari hapa Tanzania ni kubwa sana na tumekuwa tukiongea mara nyingi kuhusu upungufu wa Madaktari, upungufu wa Wauguzi, lakini tatizo hili bado halijapatiwa dawa. Pamoja na kwamba Serikali inasema inaendelea kudahili wanafunzi wengi katika fani hizo lakini tunagundua kwamba wahitimu wengi wanaenda kufanya kazi nje ya nchi na hivyo kufanya upungufu uendelee kuwepo nchini. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inaweka mazingira bora kwa Wauguzi wetu ili waendelee kubaki nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ukiwa na upungufu mahali, upungufu wa kitu chochote, unachofanya ni kuongeza. Kudahili hii aliyoisema hapa, ndicho tunachofanya hapa, ukimuuliza Dokta Seif hapa, atakuambia sisi tumeongeza idadi ya watu wanaokwenda katika vyuo vyetu. Kwa hiyo, *you are right madame,* nakubaliana na wewe kabisa.

Mheshimiwa Spika, anazungumza pia habari ya Madaktari wetu ambao wanaondoka kwenda katika nchi za nje, wanakwenda kufanya kazi Botswana, Malawi na maeneo mengine. Tunachotakiwa kufanya sisi hapa ni kuweka mazingira mazuri tu ya kuvutia ili wale Madaktari badala ya kwenda kule warudi kwetu hapa wafanye kazi hapa nchini, ndiyo changamoto kubwa ambayo naiona inakuja hapa.

Mheshimiwa Spika, wakati huo unapo-*sort out* hayo yote, tumesema nini? Madaktari wetu sasa hivi hatuwapeleki Wizarani halafu ndiyo waende kule, anachukuliwa kutoka kwa Dokta Seif kule kama ni Mpanda anakwenda moja kwa moja ili kuweza kuondokana na tatizo hili. La pili, ni hili la kuongeza idadi ambapo atakuwa anafuatilia kwa karibu lakini nakubaliana na yeye kwamba kuna haja ya kuboresha mazingira ya wafanyakazi wetu hasa Madaktari na wale wengine wote walioko nje katika *diaspora,* warudi nyumbani hapa wakaijenge nchi yao, wakawahudumie Watanzania.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, kwa niaba yake Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

Na. 21

Upimaji wa Viwanja Unaosababisha
Wananchi Kudhulumiwa

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI) aliuliza:-

Baadhi ya wapimaji wa viwanja binafsi huingia katika maeneo ya wananchi wa Kimbiji, Pembamnazi, Runa na Kisarawe na hutoa masharti ya kugawana viwanja na wananchi ili wapate hati miliki:-

(a) Je, hali hii haisababishi wananchi kudhulumiwa na kuleta migogoro ya ardhi?

(b) Je, Maafisa Mipango Miji, Upimaji na Ramani katika Halmashauri hufanya kazi gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kampuni binafsi zinazoruhusiwa kufanya kazi ya upimaji wa ardhi ni zile ambazo zimesajiliwa na Bodi ya Taifa ya Wapima *(The National Council of Professional Surveyor)*. Kampuni hizi zimeruhusiwa kufanya kazi chini ya Sheria ya Ardhi Namba 4 na Namba 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Upimaji Ardhi, Sura 390.

Mheshimiwa Spika, mmiliki wa asili ana hiari ya kuingia makubaliano na kampuni husika kwa ajili ya kupimiwa eneo lake. Mpimaji binafsi anaposhindwa kutimiza taratibu zilizowekwa kisheria, matokeo yake ni mwananchi kudhulimiwa haki yake kama ilivyotokea katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ambapo wananchi watatu wanailalamikia Kampuni ya *Ardhi Plan Limited* kwa kuwadhulumu wananchi ambapo kampuni ilihitaji kulipwa 40% ya mauzo ya viwanja na wananchi 60%.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko hayo, Kamati imeundwa na Halmashauri ili kushughulikia malalamiko haya ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi. Hivyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua kwa wapima binafsi yanapojitokeza malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa taratibu za upimaji ardhi ikiwemo kuwadhulumu wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya Maafisa Mipango wa Miji, Upimaji na Ramani katika Halmashauri ni usimamizi wa masuala yote yanayohusu ardhi ikiwa ni pamoja na upangaji, uthamini, upimaji, umilikishaji ardhi kwa mujibu wa sheria. Umilikishaji wa ardhi iliyopimwa na Wapimaji binafsi hufanywa na Afisa Mteule wa Manispaa na usajili hufanywa na Mkurugenzi wa Upimaji wa Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hivyo, Maafisa hao wana jukumu la kusimamia wapimaji binafsi kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua unapojitokeza ukiukwaji wa sheria hizo.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Napenda niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha zaidi ya miaka nane, eneo lote la Kigamboni, kwa maana ya kuanzia Kata ya Kigamboni mpaka Pembamnazi na maeneo mengine, wananchi wamezuiwa, hazitolewi hati za umiliki, wananchi wanadhulumiwa maeneo yao kwa maana kwamba hawawezi kuhuisha maeneo hayo, nini tamko la Serikali kuhusiana na mradi wa Kigamboni na kwa nini wananchi wasiruhusiwe kuendeleza maeneo yao? Mmekaa kimya siku zote.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika majibu yake amesema kwamba, Maafisa wa Mipango Miji kazi yao ni pamoja na kupima maeneo hayo kwa ajili ya kuwapatia wananchi. Tatizo lililokuwepo Halmashauri na Wizara ya Ardhi mnatupiana mpira kuhusiana na pesa za upimaji wa ardhi katika maeneo yote nchini. Sasa tuambieni nani mwenye jukumu la upimaji wa ardhi, TAMISEMI au Wizara ya Ardhi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu Maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ametaka kujua ni nini hatma ya Kigamboni au Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni. Kama ambavyo tumekuwa tukisema, Mji wa Kigamboni kama mnavyotambua ipo rasimu ya uendelezaji ambao uko kabambe lakini rasimu hiyo bado haijaidhinishwa rasmi kwenye mkutano wa hadhara ambao kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Namba 7 ni wananchi ndiyo wenye jukumu hilo. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mangungu pamoja Watanzania wote kwa ujumla, hususan wananchi wa Kigamboni, tayari vikao mbalimbali vilishaanza kufanyika tarehe 29 Machi lakini vilevile tumeshaanza kuchukua hatua kwa kufanyia mapitio baadhi ya Matamko au Matangazo ya Serikali ambayo yalishafanyika na muda si mrefu matangazo haya yatachapishwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kwa mujibu wa mwelekeo ambao tunao hivi sasa ni kwamba wananchi hawataondolewa katika maeneo yao na kimsingi wananchi wenyewe ndiyo watakaokuwa waendelezaji. Kama wao wenyewe hawana mitaji, basi wataweza kuingia ubia na watakaokuwa na mitaji lakini hilo litakaposhindikana basi wataweza kuuza maeneo yao au vilevile ikishindikana wataweza kulipwa fidia. Niseme tu kwamba, kwa upande wa Serikali sisi hatutakuwa waendelezaji wakubwa, tutakachokifanya ni kufidia zaidi maeneo yatakayopitiwa na miondombinu muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili kwamba ni nani mwenye jukumu la upimaji. Niseme tu kwamba jukumu kuu liko kulekule Halmashauri, wako maafisa wa sekta ya ardhi katika Halmashauri zetu. Vilevile kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI alivyoeleza wako wapima binafsi na wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa swali lenyewe la msingi, niseme tu kwamba, tumekuwa tukipata tatizo kubwa na hawa wapimaji binafsi wanaokwenda kuchukua maeneo ya watu bila kuwafidia inavyotakiwa. Hivi sasa tumesimamisha shughuli hizi na tumeshatoa Mwongozo kwa ma-*RAS* wote Mikoani na tutakuja na Mwongozo mpya sasa ni kwa mujibu wa taratibu zipi wapimaji hawa binafsi wanaochukua maeneo ya watu waweze kufuata. Haiwezekani mtu analipwa Sh.200,000/= au Sh.500,000/= halafu eneo hilihili linakuja kuuzwa kwa Sh.20,000,000/= na yule mwenyewe ambaye ndiyo alikuwa mmiliki wa awali hapati chochote.

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti yetu tutatoa utaratibu kamili na hatua gani ambazo tumeweza kuzichukua. Nashukuru, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Diana Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa maeneo yote yanayoingia kwenye migogoro ya ardhi na Serikali, wananchi wa maeneo hayo huathirika kwa kuchelewa kuanza ujenzi na kusitisha shughuli zote za kijamii na za kimaendeleo. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kumaliza migogoro hiyo kwa muda mfupi ili wananchi wasiathirike na kucheleweshewa maendeleo yao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa anasema jambo la msingi sana. Wakati mwingine katika Halmashauri tunafika mahali zinakuwa ni vurugu. Jambo linalotakiwa hapa ni watu wote tuwe waaminifu. Hii migogoro inapotokea pale utasema simamisha kwa sababu akienda mtu Mahakamani kwa mfano, kuna *dispute* hapo lazima kutakuwepo sasa na *court injuction* pale itasema simamisha kwanza tu-*solve* hii *problem* tujue hili shamba au hili eneo ni mali ya nani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *problem* ninayoiona hapa ni kwamba sisi anachotuambia Mheshimiwa Diana Chilolo ni kutukumbusha kuhusu wajibu wetu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika jambo hili kwa sababu sisi ni sehemu ya Halmashauri pia. Ikitokea *dispute* pale, *there is no way* mnaweza mkaendelea, hata kama ni mradi utasimama kwanza mpaka tuamue kwamba sasa hili jambo linakwishaje ili tuweze kuendelea. Vinginevyo ukiruhusu wakienda tu, litajengwa jengo hapa halafu baadaye utaambiwa libomoe, nayo itakuwa ni kilio, itakuwa ni fujo na vurugu. Tunachukua anachosema Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba ni jambo la msingi kuhakikisha kwamba taratibu zinafuatwa kama nilivyojibu hapa.

SPIKA: Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa katika Halmashauri zetu hawa Wapima Ardhi na Maafisa Ardhi hawajishughulishi sana kupima maeneo ya umma kama zahanati, shule na mipaka ya vijiji. Mfano mzuri ni shule ya sekondari Bagara iliyoko katika Halmashauri ya Mji wa Babati na shule ya msingi Sinai, mipaka haijulikani. Ni lini Serikali itaelekeza maafisa hawa kupima maeneo ya umma kwanza badala ya kukimbizana na viwanja?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, anachosema wala siwezi kubishana naye kabisa. Wakati mwingine tunafika mahali unakuwa kama mshona kiatu, unashona viatu vya watu wengine cha kwako hushoni. Ndiyo hicho anachosema kwa sababu Halmashauri ndiyo inayopima viwanja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni jambo la msingi, anaweza akaingia mwendawazimu pale akachukua shule ya msingi yote akabeba akaenda nayo, unaulizwa hati miliki iko wapi, huna. Unaulizwa hii hospitali hapa mmejenga nyie hebu nipatieni hati miliki, mtakwenda pale tunataka haki zetu, tunaonewa na vitu vingine lakini ni tatizo. Tumetoa maelekezo katika Halmashauri zetu na ziara zote tulizofanya Mkoani, sauti hii ni msisitizo tu mama yangu, tumewaambia kwamba hakikisheni mnapima maeneo yote ambayo ni mali ya Halmashauri kwa maana ya *public land* ili asije akatoka mtu hapa aka-*encroach* na tumekuwa na matatizo hayo. Kwa hiyo, tunalichukua hili, tunaendelea kusisitiza, tunawaandikia Wakurugenzi wetu kuwaambia kwamba liko tatizo hili lakini ni jambo ambalo tunalifahamu na tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutukumbusha kuhusu jukumu hilo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Arfi umefuta swali lako la nyongeza?

MHE. SAID A. ARFI: Wameshanijibu.

SPIKA: *Okay* tunaendelelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa atauliza swali hilo.

Na. 22

Uharibifu wa Miundombuni ya Maji

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA aliuliza:-

Kuna wimbi kubwa sana la wizi wa mabomba, mifuniko ya chemba za maji taka, vyuma chakavu ambavyo huuzwa mitaani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uharibifu huo wa miundombinu?

(b) Uyeyushaji wa vyuma hivi viwandani unasababisha kutengenezwa kwa vifaa vya ujenzi visivyo na ubora, je, Serikali inatoa tamko gani juu ya suala hili?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbuka kuwa katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge lako Tukufu, Wizara yangu ilitoa maelezo kuhusu suala hili la chuma chakavu kupitia majibu swali namba 4731 lililoulizwa na Mheshimiwa Philipa Godfrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum.

(a) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uharibifu wa miundombinu unaotokana na biashara ya chuma chakavu, Wizara imekwishaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri na kupendekeza kutungwa kwa sheria itakayoweka bayana taratibu za mfumo wa usimamizi na udhibiti wa sheria ya chuma chakavu katika hatua ya uzalishaji, ukusanyaji, usambazaji, uuzaji na uyeyushaji wake kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira kwa manufaa ya Taifa. Aidha, Muswada uliondaliwa umeweka bayana bayana adhabu itakayotolewa kwa mtu atakayebainika kuharibu miundombinu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Viwango *(TBS)*, imekuwa ikihakikisha kuwa bidhaa zote zinazozalishwa nchini zinakidhi matakwa ya kiwango cha kimataifa cha bidhaa husika. Uthibitishaji wa ubora wa bidhaa hizo ni pamoja na vifaa vya ujenzi kama vile nondo zinazozalishwa kwa kutumia chuma chakavu kama malighafi. Hivyo mzalishaji yoyote anatakiwa kuzalisha bidhaa bora kwa kuzingatia kiwango na si vinginevyo na endapo itabainika mzalishaji huzalisha bidhaa hizo zilizo chini ya kiwango, *TBS* kwa idhini ya Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye ana mamlaka ya kusitisha uzalishaji chini ya kifungu cha 25 cha Sheria Na. 2 ya mwaka 2009, atasitisha uzalishaji wa bidhaa hiyo na kumuamuru mzalishaji kuziondoa bidhaa hizo sokoni. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mbassa swali la nyongeza.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Suala hili la wizi wa mabomba, mifuniko ya *chamber* linahusu vilevile na wizi au ung'oaji wa alama za barabarani na kingo za barabara jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa ajali nyingi. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba Muswada unaandaliwa, je, Muswada huo utaletwa ili uweze kujadiliwa na hatimaye sheria itungwe na kabla ya hapo anatoa tamko gani kwa hii hali inayoendelea?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tumeshushuhudia majengo mengi yakiporomoka na sababu inaonekana ni hizi nondo ambazo zinatengenezwa chini ya kiwango au hata misumari ambayo haiko kwenye kiwango stahiki. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwaagiza hawa *TBS* pamoja na kusubiri hii bidhaa itengenezwe wakawa wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye viwanda hivi ili kuzuia tatizo hili lisiendelee? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la wale wanaoharibu alama za barabarani, napenda kutoa wito wananchi waone kwamba alama zile zinasaidia katika usalama wao kwa vile zinaonyesha nini kifuatwe katika suala la zima la usafiri katika barabara hizo. Kwa hiyo, tunawaomba wananchi kwamba wakiondoa alama zile wanaleta hasara katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba Sheria hii ya Chuma Chakavu ingawaje mwanzo tuliendelea kuihusisha na sheria nyingine ya *Business Administration Registration Act (BARA)*. Sasa baada ya kuona kwamba sheria ile ya *BARA* inahitaji marekebisho, tunaifanyia marekebisho sasa hivi ili kuendana na sheria ambayo itaendana vizuri na hii ya uzuiaji wa chuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, pia ameulizia kuhusu haya majengo ambayo hayakidhi viwango kwa maana ya vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa majengo hayo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tunafanya ukaguzi wa mara kwa mara na zaidi ya hapo tumeshatoa viwango vya aina ya nondo ambayo inazalishwa na kila nondo lazima iwe na mhuri na alama ya kiwanda inachozalisha ili tujue kwamba nondo zile zinakidhi mahitaji ya ujenzi huo au lah!

SPIKA: Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la *recycling* ni jambo la kawaida katika dunia ya leo. Serikali ina mpango gani wa kufanya utaratibu hasa katika haya mambo ya nondo, kwa sababu chuma kinachotumika ziko *HMS I, HMS II and HMS III*. Sasa wakati mwingine haukagui kabla ya kufanya uzalishaji, unakwenda baada ya uzalishaji, kuna udanganyifu katika kuzichanganya hizi *HMS I, HMS II and HMS III* na ndiyo maana unapata *quality* mbaya. Kwa nini Serikali isifanye ukaguzi kabla chuma hakijachanganywa ili ikajulikana *quality* ile inayochanganywa ni ile inayotakiwa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakubali, ni kweli kuna umuhimu wa kukagua kabla ya utengenezaji wa nondo hizi au bidhaa nyingine yoyote ya ujenzi na tunalichukua hilo na tutalifanyia kazi.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba niulize tu swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hili tatizo la wizi wa mifuniko limekuwa likiathiri sana miundombinu, je, Serikali haina mkakati wowote au njia nyingine mbadala hata ya kutumia labda mifuniko ya *plastic* au njia nyingine kwa sababu pia inaweza ikapunguza hata gharama ya kutumia nondo? Kwa sababu karibu nchi nzima wizi umekuwa mkubwa na wananchi wanapoiba, wao hawajui labda hivi vyuma havihitajiki tena bado wanajua kwamba wakipelekwa kwenye viwanda hivi vyuma vinahitajika. Sasa nilikuwa naomba kama kuna mbadala mwingine hata wa kutengeneza kwa *plastic* pia itapunguza hata gharama za matengenezo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ni kweli pamoja na miundombinu ambayo huwa inaathirika ni mifuniko inayozuia maji machafu barabarani. Kwa kweli suala la kuangalia jinsi ya kutengeneza mifuniko hiyo bila kutumia chuma limekuwa likifanyiwa kazi, naamini tunaweza tukaendelea kuliboresha kwa kutumia labda *cement* au vitu

vingine ambavyo havitawavutia wale wezi wa vyuma chakavu kuja kuvitumia. Kwa hiyo, tunalichukua nalo hili pia na tutaendelea kulifanyia kazi.

SPIKA: Sasa tunaenda Wizara ya Fedha, swali la Mheshimiwa Clara Mwatuka.

Na. 23

VAT kwa Bidhaa za Madukani

MHE. CLARA D. MWATUKA aliuliza:-

Bei ya bidhaa za madukani ni pamoja na kodi ya *VAT* lakini inashangaza kuona wafanyabiashara wakiwatoza au wakiuza bidhaa zao kwa bei zaidi wakidai ni kwa ajili ya *VAT*:-

Je, Serikali inalijua jambo hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA) aliuliza:-

Mheshimiwa spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Sura 148, bidhaa zote zinazotengenezwa na mfanyabiashara aliyesajiliwa na *VAT* zinapaswa kuwa na tangazo la bei ya bidhaa. Bei inayooneshwa kwenye tangazo hilo inajumuisha *VAT* anayoilipia mnunuzi. Endapo mnunuzi wa bidhaa atatakiwa kujua *VAT* halisi iliyojumuishwa katika bei ya bidhaa, mnunuzi anatakiwa kukokotoa *VAT* kwenye bidhaa kwa kutumia *formula* maalum inayofahamika kama *VAT fraction* ambayo 18/118 au 9/59. Kwa msingi huo wafanyabishara hawatakiwi kutoza *VAT* kwa kuikokotoa tofauti na bei iliyooneshwa kwenye tangazo la bei la bidhaa au kuongeza bei zaidi ya ile iliyooneshwa kwenye bidhaa kwa kisingizio cha *VAT*. Kufanya hivyo ni kinyume na matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inalichukua suala la Mheshimiwa Mbunge kama taarifa ya kwamba wafanyabiashara wanaongeza bei juu ya bei iliyoonyeshwa kwenye tangazo la bei kwa kisingizio cha *VAT*. Pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Mbunge Mwatuka kwa taarifa hii, naomba nilijulishe Bunge kuwa Serikali imekuwa inafuatilia suala hili kwa lengo la kubaini mianya na changamoto zilizokuwepo katika kuimarisha usimamizi wa *VAT*. Aidha, Serikali inaendelea kuwahimiza wafanyabiashara kwamba kudai bei mbili tofauti kwa bidhaa moja ni kukiuka sheria na watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

SPIKA: Mheshimiwa Mwatuka swali la nyongeza.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri lakini pamoja na uzuri huo wa majibu hayo napenda kuuliza maswali madogo tu ya nyongeza. Pamoja na tangazo la ukinunua kitu dai risiti, kumekuwa na utata mkubwa katika utoaji wa risiti hizo. Wananchi au watu wanapokwenda kununua bidhaa hasa kama ni ndogo ndogo siyo wengi wanaokumbuka kudai risiti, risiti hudaiwa tu labda kama mtu ananunua redio au kitu cha bei kubwa lakini vitu vidogo vidogo siyo rahisi kukumbuka kudai risiti. Sasa wafanyabiashara hivi sasa wamepata kisingizio cha kushuka au kupanda kwa dola, hivyo utoaji wa risiti unakuwa wa utata. Je, ni juhudi gani Serikali inafanya kuhakikisha bei hizo zinazotumika ni zile ambazo zimeonyeshwa kwenye tangazo la Serikali?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali inasimamia lakini lazima iwe na mtu wa kufuatilia, ni nani huyo ambaye anahakikisha kwamba mambo hayo sasa hayafanyiki na kwamba ni kweli yanayofanyika kwa sababu hivi sasa hawa hawamuibii mnunuzi peke yake, hata Serikali inaibiwa kwa sababu risiti nyingi hawatoi, kwa hiyo, mapato inakuwa hayapatikani vizuri. Ni nani sasa mwajibikaji wa suala hili?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, kwanza nieleze kwamba kwenye biashara ya aina yoyote ile unatakiwa upewe risiti kwa huduma uliyopewa. Sasa huu utaratibu wa kudai risiti, kimsingi hutakiwi kudai risiti, risiti ni haki yako unatakiwa kupewa tu. Ukilipia *service*, ukienda *petrol station*, ukienda kununua redio na kama alivyosema ni kweli kwamba kitu kama redio mtu anadai risiti kwa sababu ikienda ikimharibikia anataka awe na ushahidi kwamba amerudisha hiyo redio lakini unatakiwa upate risiti kwa biashara yoyote. Ni kweli kabisa na ndiyo maana nimesema tatizo hili limeonekana limekuwa pana sana kwamba wafanyabiashara hawatoi risiti, lakini hata sisi wenyewe wateja *(consumers)* hatuidai kwa hiyo, matokeo yake tunaacha umbwe *(vacuum)* ambayo inaruhusu kitu hiki kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba kwanza Serikali haipangi bei kwenye bidhaa hizo, bei ni ya mfanyabiashara lakini katika bei ile anatakiwa kuwa ameshakokotoa *VAT* kama hajakokotoa iseme pale kwamba ukilipa 1000 hii na nyongeza ya *VAT* kama inavyofanywa kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo, kwa namna hiyo, bei ni moja tu, bei ya bidhaa ambayo tayari ina *VAT* au bei ya bidhaa na *VAT* yake unalipia zote jumla pale hutakiwi kudaiwa bei mbili.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, *TRA* ndiyo mwenye jukumu la kufuatilia suala hili chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na chini ya usimamizi wetu sisi wote kama Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako hili tunalotengeneza sheria. Kwa hiyo, naomba niseme sheria ya *VAT* ipo na ziko kanuni zaidi ya nne ambazo zinatoa nguvu katika sheria hii na mfuatiliaji ni *TRA*. Naomba niseme tu kwamba *TRA* yuko kwenye kuimarisha mikakati hii ili kuhakikisha kwamba suala hili linapata ufumbuzi wa moja kwa moja.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Suala la *VAT* limekuwa ni tatizo ambalo limejitokeza mara kwa mara na hasa kwa wafanyabiashara. Sijui Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili waweze kuelewa kwa sababu suala hili ni kama siyo muhimu kwao. Naomba Serikali iniambie ina mkakati gani wa kuwaelimisha wafanyabiashara wengi kuhusiana na suala hili?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Mwanjale kwamba inaonekana kuna kisingizio cha kutokufahamu utendaji au umuhimu wa kulipa *VAT* na hili jambo linapanuka. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, *TRA* wanatoa elimu kwa mlipa kodi kila mwaka, kuna siku yao na wanatoa kwenye magazeti, vipeperushi na kadhalika. Kwa hiyo, kimsingi hakuna sababu maalum ambayo mtu ambaye anafanya biashara na anatakiwa kulipa kodi asiwe na ufahamu wa misingi ya kwa nini anatakiwa pia kulipa *VAT* au kuwasilisha risiti zake ili *VAT* ipate kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba suala hili la elimu kwa umma ni mkakati wa kudumu wa *TRA*. Pamoja na sheria zilizokuwepo, elimu hii kwa umma itakuwa ni msingi wa kuwafikisha watu kwenye sheria pale ambapo wanakiuka utaratibu wa ulipaji wa *VAT* na juhudi hizi za utoaji wa elimu zimekuwa pana.

SPIKA: Mheshimiwa Godfrey Mgimwa.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la *VAT* limekuwa ni tatizo kubwa hasa kwenye maeneo ya vijijini. Napenda kujua Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba elimu kwa wafanyabiashara ya kutoa na kupokea risiti linakuwa ni suala la kawaida kabisa katika jamii yetu hasa kwa wale wananchi wa vijijini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu lililotangulia au kwenye swali lililotangulia ni kweli kabisa hasa kama ulivyosema Mheshimiwa Godfrey kwenye *rural economy* ya Tanzania ambako ndiko kwenye asilimia 70 ya Watanzania wanaozalisha na wengi wao baada ya kuzalisha ile ziada inaenda kufanyiwa biashara, utaratibu wa kufanya biashara kwa kutoa risiti imeonekana bado haijakuwa ni jambo la kawaida. Kwa sababu *TRA* ina ofisi zao kwenye kila Wilaya za Tanzania, elimu kwa mlipa kodi inaendelea kufanyiwa kazi na elimu hiyo inatakiwa kuwa siyo ulipaji kodi kwa shuruti, elimu inayosisitizwa ni ulipaji kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimelipokea hili na najua linafanyiwa kazi na namshukuru Mheshimiwa Godfrey Mgimwa kwa kulisisitiza. Elimu hii kwa umma inatolewa kupitia maeneo mbalimbali redio, televisheni, magazeti, vipeperushi lakini tutaendelea kuhimizana sote ili elimu hii ya mlipa mkodi iwe imeenda kwa Watanzania wote ambao tunatakiwa kulipa kodi ya *VAT*.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Grace Puja.

MHE. DKT. GRACE K. PUJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali langu la kwanza la nyongeza. Napenda kujua ziko aina ngapi za risiti ambazo zinatambuliwa na Serikali kwa sababu baadhi ya wafanyabiashara wakishapata huduma au ukinunua kitu anakuuliza unataka risiti ya aina gani?

SPIKA: Hiyo inaitwa *maiden speech*. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Spika, risiti inatakiwa kuwa moja tu lakini kwa sababu ya kutokukamilika kwa huu mkakati wa *EFD* ambapo risiti zinatakiwa zitoke kwa mashine bado *TRA* inapokea risiti zinazotoka kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli na mimi mwenyewe nimeishuhudia kwa mfano ukienda kwenye *petrol station* unaweza ukaambiwa risiti ya *EFD* mashine ziko *down,* haifanyi kazi lakini kama unataka upewe risiti ya mkono. Tunachosema ni kwamba, kwa yule mwenye mashine ya *EFD* anatakiwa atoe risiti ya *EFD*, ambaye hana mashine anatakiwa atoe risiti ya mkono. Pale ambapo tuna mgogoro ni yule ambaye anapokea fedha, anafanya biashara lakini hatoi risiti kabisa.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa. Tuendelee na swali linalofuata la Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mtutura Abdalah Mtutura kwa niaba yake Mheshimiwa Vita Kawawa.

Na.24

Mradi wa Maji wa Mchoteka

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y MHE. MTUTURA A. MTUTURA) aliuliza:-

Mradi wa maji Mchoteka unaofadhiliwa na Benki ya Dunia haukufanikiwa kwa sababu eneo walilotoboa halikuwa na maji ya kutosha.

Je, nini hatma ya mradi huo?

NAIBU WAZIRI MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, inatekeleza mradi wa maji wa vijiji 10 katika Halmashauri zote nchini. Katika Wilaya ya Tunduru, vijiji vilivyopewa kipaumbele katika mradi huu ni Nandembo, Matemanga, Mtina, Mchoteka, Nalasi, *Mbesa Phase I*, Amani, Chiungo, Meamtwaro, Nakapanya, Majimaji, Muhesi na Lukumbule. Utekelezaji wa miradi hii ulianza kwa kuchimba visima virefu katika vijiji vya Mchoteka, Mtina, Nakapanya, Majimaji, Muhuwesi na Lukumbule. Vijiji vya Nandembo, Matemanga, Nalasi, *Mbesa Phase I*, Amani, Chiungo na Meamtwaro vilitumia vyanzo vya mtiririko. Katika Kijiji cha Mchoteka vilichimbwa visima viwili ambavyo havikuwa na maji ya kutosha kwa mujibu wa takwimu za kitaalam.

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyokosa vyanzo vya maji katika awamu ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Serikali itavipa kipaumbele katika utekelezaji wa awamu ya pili ya programu kikiwemo Kijiji cha Mchoteka.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeahidi kutapeleka kipaumbele katika Kijiji cha Mchoteka, tunaomba Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tatizo la uchimbaji wa visima hivi pia limejitokeza katika Wilaya ya Namtumbo na Mheshimiwa Naibu Waziri tunamshukuru sana alifika kutembelea miradi hiyo na kuona matatizo haya. Kuna visima viwili ambavyo vilitakiwa vichimbwe mita 150 lakini vilichimbwa mita 71 na maji yake hayataweza kutosheleza kujaza tenki linalotakiwa ujazo wa lita 10,000 kwa saa. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa maelekezo, naomba kumbukumbu ziingizwe katika Bunge lako Tukufu leo, maelekezo ya Serikali yaliyotolewa siku ile kwamba visima vile virudiwe kuchimbwa tena katika kijiji cha Milonji na Magazini, naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Taifa kuhusiana na maagizo yale aliyoyatoa.

SPIKA: Haya alieleze Taifa siyo huko kwenu? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumejibu katika jibu la msingi, Kijiji cha Mchoteka tutakipa kipaumbele katika awamu ya pili na uzuri napafahamu nimekaa pale, iko katika Tarafa ya Nalalasi, tutatekeleza hili katika awamu hiyo ya pili.

Mheshimiwa Spika, suala la Milonji na Magazini ambapo tulifika katika Kijiji cha Milonji tukagundua hiyo dosari kisima kilikuwa kiwe na mita 150 wakachimba 71. Maelezo na maagizo yangu yako palepale na kama alivyoahidi Mhandisi, visima vile vichimbwe kama ambavyo iliekezwa na Mtaalam Mshauri na siyo vinginevyo. Nitafuatilia agizo hili na utekelezaji na hasa Milonji ambako tulitoa matumaini kwamba kazi hiyo itanza ndani ya wiki moja.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Suzan Kiwanga!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Matatizo ya maji nchini ni mengi sana lakini nataka tu niiulize Wizara, naona anacheka lakini safari hii nakupeleka Tanganyika Masagati Kitongoji cha Mfenesini kuna tenki pale kubwa limejengwa, lilienda kuzinduliwa mpaka sasa lile lina ufa na linaonekana lilitumia gharama za shilingi milioni 300. Je, ni lini sasa atatembelea Kata ile ya Tanganyika Msagati karibu kabisa na Njombe kwenda kuangalia ule mradi wa maji ambao hauna manufaa kwa wananchi?

SPIKA: Hapa umechomekea Njombe tu. Mheshimiwa Waziri majibu, *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nimelipokea hili suala la Tanganyika Masagati lakini nitaanza utekelezaji kwa maana ya kuuliza na kufuatilia bado tukiwa hapa Bungeni kwa sababu nikikuahidi hapahapa kwamba baada ya Bunge hili na wakati Bunge litakuwa limevunjwa nitakuwa nakudanganya. Kwa hiyo, kwa sababu wote ni wa Mkoa wa Morogoro na mimi ni Mwenyekiti wako wa Mkoa kwa maana ya Wabunge, nitalichukilia kwa uzito wake kuona kwamba jambo hili tunalisukuma na ikibidi basi kufika eneo hilo lakini kwa sasa sitoahidi kwamba nitafika lakini nitaagiza utekelezaji ufanyike.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililoko katika maeneo haya halina tofauti na lililoko Wilaya ya Misenyi katika vijiji vifuatavyo. Katika Kata ya Kakunyu, Kata ya Bugandika, Kata ya Luzinga kuna visima vilichimbwa na havikutoa maji na siyo hilo tu hata tenki lililojengwa pale Kilimilile lina matatizo sana, lina ufa na ile pampu ya kuingiza maji kila mara inapasuka. Sasa napenda kujua hizi sehemu ambazo hazikupata maji na wale wamelipwa hela, ni lini tutapatiwa visima hivyo kwa ku-*compensate* vile ambavyo tumeshawapatia pesa zetu?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, tatizo la Kakunyu na maeneo mengine ndiyo *concern* ya Wabunge walio wengi na Waziri hapa aliwahi kutoa taarifa ya maeneo ambayo visima vilichimbwa, maji yalipatikana na maji hayakupatikana. Pia ni kwamba, vipo visima ambavyo vimechimbwa lakini bado ujenzi wa miundombinu haujafanyika na hii yote ni kutokana na tatizo la fedha. Mjadala mzima katika Bunge hili ni upokeaji wa fedha katika Wizara mbalimbali ambapo imekuwa ni kikwazo kwetu kutekeleza mambo haya ambayo tulikuwa tumeyakusudia. Nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa haya aliyoniambia, mimi nitayabeba na tutawasiliana na Mhandisi wa Maji wa Wilaya na Mkoa kuona nini hasa tatizo na namna gani tunaweza tukasaidia.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mabama, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora kuna chanzo kikubwa sana cha maji ambapo aliyekuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mahenge alitembelea

pale mwaka 2012 na kuona kile chanzo kinaweza kikalisha Wilaya ya Uyui nzima na Wilaya ya Urambo yote lakini mpaka leo hakuna juhudi zozote za Serikali kuhakikisha kwamba maji yale yanaondoka pale yasambazwe kwa wananchi. Tunaomba kujua, nini mipango mikakati ya Serikali kuhakikisha kwamba shida ya maji ya Uyui na Urambo inaondoka kwa njia ya kusambaza chanzo hiki cha maji ambacho ni kikubwa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, tumepokea suala la Mabama lakini yeye ni shahidi na ni Mjumbe mzuri tu na mchangiaji mzuri kwenye Kamati yetu ya Kilimo, Maji na Mifugo, anaelewa mpango mkubwa wa Serikali wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya Tabora Mjini na Wilaya nyingine. Mimi nasema kwamba hilo tumelipokea lakini pia tunatekeleza hili ambalo sasa tunataka kutekeleza mradi huu mkubwa wa maji.

SPIKA: Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ili na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mradi wa bwawa la Matwiga, Wilayani Chunya katika Kata ya Matwiga umeanza siku nyingi sana toka mwaka 2008 lakini kwenye bajeti ya mwaka jana, Wizara iliweka bajeti yake na kusema kwamba wataweka mkandarasi wa Serikali lakini mpaka sasa hakuna kinachofanyika. Je, nini hali ya bwawa hilo ambalo lingesaidia upatikanaji wa maji kwa Kata ya Matwiga, Mtanila na Lupa?

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri, mmemuuliza maswali ya nchi nzima ngoja na Waziri naye ajibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Bwawa la Matwiga limeanza ujenzi wake muda mrefu lakini Mkandarasi aliyekuwepo hakufanya kazi nzuri na ilibidi aachishwe kazi na baadaye tukateua Shirika la Serikali la Ujenzi wa Mabwawa na Uchimbaji wa Visima ili liweze kutekeleza kazi hiyo. Kazi ya kwanza ambayo walitekeleza ni kwenda kufanya usanifu upya na kuangalia ni namna gani wanaweza kusasahisha makosa ambayo yalifanywa na Mkandarasi aliyeshindwa kazi. Hivi sasa Shirika la *DDCA* linajikusanya kupeleka vifaa Matwiga ili ujenzi huo sasa uendelee na bwawa likamilike.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa swali la msingi linaendana kabisa na tatizo lililopo kwenye Kata ya Nyarukoba, Kijiji cha Kibaso ambako kuna mradi wa *World Bank* wenye thamani wa zaidi ya shilingi milioni 350 ulikamilika mwaka 2012 na mpaka sasa hivi wananchi hawapati maji hata tone. Nilitaka tu kujua kwamba, Serikali inalitambua hili na kama inalitambua inafanya juhudi gani ili wale wananchi waweze kupata maji?

NAIBU WAZIRI MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikiri tu kwamba tunapokea taarifa hiyo na tutaifuatilia leoleo na Mheshimiwa Mbunge uwe tayari tu kushirikiana nasi kuweza kukupa majibu juu ya mradi huo.

SPIKA: Mheshimiwa Rage.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nilikuwa naomba tu maelezo kutoka kwa Waziri. Serikali imepata pesa zaidi ya shilingi milioni 268, je, huo mradi kambambe wa maji kutoka *Lake Victoria* kwenda Tabora utaanza lini?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa kwenye majadiliano na Serikali ya India ili kukamilisha ufadhili wa mradi huo na tunategemea kwamba kabla ya tarehe 15 Juni, mkataba wa fedha kwa ajili ya mradi huo utawekwa saini na Serikali zetu mbili na baada ya hapo tutatangaza kumtafuta mkandarasi. Nategemea sana kwamba mkandarasi atakuwa amepatikana mwezi Septemba, 2015 na ujenzi utaanza mara moja.

SPIKA: Ahsante. Msidhani kama kila siku mtakuwa mnapewa maswali ya nyongeza yote haya, leo ni bahati mbaya. Ahsanteni sana kwa kujibu maswali, wangekuwa wanatoa digrii za heshima hapa mngepewa maana mmejibu maswali ya nchi nzima.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambue wageni. Leo baada ya kipindi hiki nitamuachia Mwenyekiti aendelee, mimi nimepata mgeni, Spika Mstaafu wa Jamhuri ya Msumbiji, amekuja kunitembelea. Kwa hiyo, naomba nimtambue yuko pale, Mheshimiwa Eduardo Joaquim Mulembwe. Karibu sana Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tulifanya naye kazi vizuri sana katika mikutano yetu ya *SADC*. Mheshimiwa Spika, alikuwa muungwana sana na mtu mmoja ambaye alikuwa anatusaidia sana katika mambo mengi. *(Makofi)*

Sasa Spika Mstaafu huyo ameongozana na wasaidizi wake, yuko Bwana Jose Mazula, yeye ni *Economic Adviser to the Speaker*. Yuko Ndugu Jose Madroba, yeye ni *Personal Assistant of the former Speaker*. Yupo Ndugu Pedro Neves, yeye ni Mkalimani. Yupo Ndugu Pedro Ubisse, yeye ni Msaidizi wake, ni kama *ADC*. Yupo Ndugu Luis Dava kutoka *Department of International Relations*, huyo anatoka Wizara ya Mambo ya Nje. Karibuni sana na tutaonana tu baada ya kipindi hiki kumalizika. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Ismail Rage ambao ni wanafunzi 66 na Walimu wanne pamoja na Katibu wa Bunge kutoka shule ya sekondari ya *New Era* ya Tabora. Karibuni sana na kama ninyi wanafunzi mnatoka *New Era* basi msome kwelikweli. Karibuni sana na tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Tuna wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo Bungeni pamoja na hawa pia ni mafunzo lakini wapo wengine, ni wanafunzi 76 na Walimu watano kutoka shule ya sekondari Bwawani Morogoro. Naomba na hawa wasimame tuwaone. Ahsante sana na ninyi pia nimefurahi kuwaona pia mjitahidi kusoma kwani elimu ndiyo ufunguo wa maisha.

Matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa nane mchana watakuwa na kikao katika ukumbi wa Hazina Ndogo, muda ni mfupi lakini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa nane mchana katika ukumbi namba 135 na wenyewe pia Hazina.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa nane mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 231, wao ni hapa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo na kama nilivyosema tunaendelea na mjadala, nashukuru wawakilishi wa vyama vyote wameleta majina ya

wachangiaji, kwa hiyo, naomba sasa nimwachie nafasi Mheshimiwa Mwenyekiti ili aweze kuendelea na kikao.

Atakapokuja Mwenyekiti, watakaoanza kuchangia atakuwa Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Shabiby-, Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma-, Mheshimiwa Lucy Owenya-, Mheshimiwa Mchuchuli, hapana, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, yeye ni mkubwa wenu, kwa hiyo, ataanza yeye kwanza, halafu na wengine atawataja Mwenyekiti. Kwa hiyo, namwachia Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 - Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja ya Waziri Mkuu, tunaanza na Mheshimiwa Kayombo.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Kwanza, niseme naiunga mkono kwa asilimia 100 na naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo imeifanya katika kipindi chote cha miaka hii mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi muda wote huu wa kufanya kazi katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Pia napenda kuwashukuru sana viongozi wa Mkoa wa Ruvuma, Mkuu wa Mkoa Mwambungu na timu yake ya Mkoani pale lakini na Mkuu wangu wa Wilaya, Dada Senyi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya na timu yao na Baraza la Madiwani. Kipekee nimshukuru sana Katibu wa Wilaya wa Chama cha Mapinduzi wa pale Mbinga pamoja na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii pia kuipongeza sana Wizara ya Maji kwa kazi nzuri waliyoifanya huko Mbinga na hasa Naibu Waziri Makalla, ambaye alifanya kazi *overtime* kule Mbinga, kuanzia saa mbili asubuhi mpaka karibu saa moja usiku kwa kutembelea vijiji vya Kingole, Tumanjosi, Mabuni, Mkako na Kigonsela na kufanya mikutano katika maeneo yote hayo. Hongera sana Naibu Waziri, nakutakia kila la kheri katika Jimbo lako la Mvomero uchaguliwe kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia wakulima wa Mbinga kwa kazi kubwa wanayofanya kuzalisha mahindi ambayo hata Serikali imeshindwa kuyanunua. Pia niwashukuru wakulima wa kahawa ambao wamefanya kazi nzuri na kuungana katika ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza pia shirika la *NSSF* kupitia Mkurugenzi wao Dokta Dau na wafanyakazi wote pamoja na Wakurugenzi kwa kukopesha wana ushirika wa Mbiga shilingi bilioni mbili msimu uliopita na sasa wanaendelea ku-*process* maombi ya wana ushirika zaidi ya shilingi bilioni saba na nusu ambazo tuna hakika tutazipata hivi karibuni. Hongereni sana *NSSF* kwa kuwakomboa wakulima wa Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya ujumla, kwanza ni madeni, Serikali yetu inadaiwa nje na ndani na mimi nataka kuongelea habari ya madeni ya ndani. Mimi naamini kwamba

yanapokuwa manung'uniko mengi kwa wananchi, wananchi ambao uchumi wao bado si mkumbwa sana, Serikali ingeweza kuweka kipaumbele cha kuwalipa mapema. Wakulima wana ushirika wa MBIKU wanaidai Serikali shilingi milioni 423, Waziri Mkuu alishalipa shilingi milioni nne, tunaomba amalizie hizi shilingi milioni 423 ili deni hili liweze kulipwa kikamilifu kabla ya mwaka wa fedha huu kuisha ili hawa wakulima waone kwamba wameangaliwa na Serikali yao, hili deni lina zaidi ya miaka 10 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yako madeni ya wakulima wa mahindi waliikopesha Serikali bado hawajalipwa na wako wafanyabiashara waliokopesha pembejeo, bado hawajalipwa mpaka sasa. Ni vizuri wangelipwa kwa sababu wanasumbuliwa na mabenki ambako walikopa hizo fedha na mali zao ziko katika hatihati ya kupigwa mnada lakini pia wanashindwa kuzimudu familia zao kwa sababu madeni haya hayajalipwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuongelea habari ya maji. Yako matatizo makubwa ya maji katika vijiji vya Luhagala na Paradiso lakini pia katika kipindi cha kwanza cha Ubunge wangu, niliwahi kutoa pendekezo kwamba Wizara ya Maji ingeweza kufikiria kuchukua maji kutoka Ziwa Nyasa na kuhakikisha kwamba vijiji vya Mkoa wa Ruvuma vyote vinapata maji kutoka Ziwa Nyasa. Napenda kuwatia moyo waweze kuangalia uwezekano huu, kama imewezekana kuanza mradi kule Ziwa Victoria, nafikiri inawezekana pia kuanza mradi wa Ziwa Nyasa kwa sababu maji tunayo mengi. Profesa Maghembe utapata taabu sana, utakapofika kwa Mungu atakuuliza kwa nini umewanyima wale watu maji wakati mimi nimeweka maziwa yote yale na bahari zote zile na wale watu hawana maji. Mimi nataka kukusaidia tu ili uweze kufika Mbinguni vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni umeme vijijini, Serikali yetu ina mpango mzuri sana wa umeme vijijini, ni *idea* nzuri, wazo zuri, nguzo zipo, lakini nyaya haziendi na umeme bado haujawaka. Tunaomba Serikali ingemalizia hii kazi vizuri. Tunaipongeza sana Serikali kwa jambo hili na kule Mbinga tuna vijiji zaidi ya 80 na nguzo hizo zipo lakini bado umeme haujavutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni madini, kule Mbinga hasa tarafa ya Namswea, inafahamika kwa madini mengi lakini sehemu kubwa sana inahodhiwa na wenye leseni kubwa na ambao hawafanyi kitu chochote kile, hawaendelezi na hawafanyi lolote. Kwa hiyo, ningeomba Wizara ya Nishati na Madini iangalie uwezekano wa kukabidhi maeneo haya kwa wachimbaji wadogo kule Wilayani Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo maalumu kwa Mbinga, maeneo ya utawala. Kwanza nashukuru, kipindi cha uchaguzi cha mwaka jana tulipata Kata saba pale mjini na vijiji vichache. Tunashukuru sana, hii inaweza ikatufanya tukaweza kufanya maandalizi ya kufanya Mji wa Mbinga kuwa Mamlaka ya Mji wa Mbinga. Hata hivyo, tunayo maombi ya Kata 10 na vijiji 41 ambavyo ni muhimu sana na vilitusumbua sana katika uchaguzi huo uliopita. Kwa hiyo, tungeomba Ofisi ya Waziri Mkuu ingeweza kutafakari maombi haya na kutupatia tunachoomba. Hapa ninayo barua ya Halmashauri inayoelezea mambo haya na ningeomba kuiweka mbele ya Meza yako, vijana wangeweza kuichukua ili iweze kuwasaidia Waheshimiwa Mawaziri katika kulitafakari jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunayo maombi ya Mamlaka ya Mji, yamekwishaiva, yamekwishapita katika hatua zote na hapa pia ninalo jedwali la hayo mapendekezo ambalo ningependa kuliweka Mezani kwako. Naomba vijana waweze kulichukua ili liweze kuwasaidia Waheshimiwa Mawaziri katika kulitafakari jambo hili pamoja na wataalamu wao. Nitashukuru sana kama maombi haya ya Mamlaka ya Mji, maombi haya ya Kata hizi 10 na Vijiji 41 yangeweza kupata kibali ili kuweza kurahisisha kazi za mawasiliano kule Wilayani Mbinga. Mbinga ni Wilaya ya milima, kuna milima mingi sana na kwa hiyo watu wanatembea muda

mrefu sana kufuata Makao Makuu ya Kata au Kijiji. Kama tutakubaliwa hizi Kata na vijiji hivi, itatusaidia sana kuweza kuleta huduma za Serikali karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kampeni ya mwaka 2010, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kwamba Mbinga itakuwa Mamlaka ya Mji na barabara ya Mbinga-Litembo itajengwa, imejengwa kilomita moja na barabara ya Nyoni-Mkoa pia itajengwa. Bado naona kuna *process* mbalimbali katika hili, tungeomba matunda haya yangeweza kuendelea kuonekana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika upande wa barabara nimeona Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia amezungumzia Serikali inavyojenga barabara katika Halmashauri. Napenda sana itusaidie kujenga barabara ya lami Kitai-Rwanda ambako kuna makao ya mawe ili kuweza kurahisisha usafiri na kuondoa vumbi linalowakabili wale wananchi. Vilevile barabara Kigonsela-Matili-Kilindi mpaka Barabara, halafu Mbinga-Kitumbaromo mpaka Matili na Mbinga-Mpepai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda sana kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote katika Wizara hii na Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri wanayofanya, wametusaidia sana Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mbinga kuna wagombea wachache wanataka Ubunge na wanafanya mbinu, wanachanga fedha wanataka kuja kwa Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba *DC* na *DED* wanahama kwa kazi zao nzuri wanazozifanya, hao msiwasikilize, muwapuuze kwa sababu ni watu ambao hawapendi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Dkt. Ishengoma ajiandae Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kutoa shukurani kwa Chama changu cha Mapinduzi, pia shukurani kwa wanawake wa Morogoro ambao wameniwezesha kuingia kwenye Bunge hili. Wanawake wa Morogoro nawapenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi kwako wewe kwa kutuongoza vizuri humu Bungeni. Natoa pia pongezi kwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo ameitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imefanya mambo mengi ambayo yanaonekana, kwa mfano barabara zimejengwa, shule zimejengwa, umeme upo na maji yapo. Hata hivyo, kwa upande wa maji, naomba mradi wa Gairo unaoendelea uangaliwe vizuri pamoja na maji mjini Morogoro yaweze kuwa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mazuri lakini nikija kwenye bajeti, bajeti tunapanga, tunapitisha, bajeti ni nzuri, lakini mtiririko wa fedha zinazokwenda huko kwenye Mikoa na Halmashauri ni ndogo sana na haziendi kwa wakati. Kwa kweli Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wanapata shida. Naomba bajeti ambayo tunapitisha iweze kuwafikia kwa wakati kusudi waweze kufanya kazi inayoonekana hasa kwenye miradi ya maendeleo. Kama inawezekana basi tuweze kupanga bajeti ambayo inatekelezeka, kwa sababu tayari tumeshaona sura ya bajeti inavyokwenda na fedha tunazozipokea. Tusipange bajeti ya shilingi trilioni 22, ambazo hazitaonekana na wala hatutazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu asilimia tano inayokwenda kwa vijana na asilimia tano kwa akina mama. Naomba sana iwe ni lazima kwa kila Halmashauri iweze kutoa hiyo asilimia kusudi iweze kufanya kazi kuweza kuwapa mikopo vijana pamoja na akina mama ili waweze kujiajiri. Halmashauri nyingi hazitoi hizi asilimia, kwa hiyo, iwe lazima kwa Halmashauri kutoa hizi asilimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Uwezeshaji Vijana uweze kuongezewa fedha kwa wakati huu wa bajeti tunayokwenda nayo. Tunajua kuwa vijana wengi hasa vijana wa vyuo vikuu wanamaliza vyuo vikuu lakini hawapati kazi lakini wakiwa na fedha hizi za Mfuko wa Vijana wanaweza wakajiajiri vizuri bila ya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, Serikali inafanya vizuri ndiyo kwenye uchumi na hasa tumeona kuwa viwanda vimechangia na hasa viwanda vidogo na vya kati lakini kuna viwanda ambavyo vimekufa. Kwa mfano, kiwanda cha ngozi na kiwanda cha *juice* Morogoro. Tunaomba viwanda vile ambavyo vimekufa viweze kufanya kazi na hata kwenye Mikoa mingine, kulikuwa na viwanda vingi lakini vingi vimekufa viweze kufufuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani pia kwa Serikali kwa upande wa ujenzi wa madaraja. Kwa upande wa Morogoro, tunashukuru daraja la Mwatisi limekamilika na daraja la Kilombero linaendelea kujengwa ambalo litasaidia wananchi wa Wilaya ya Kilombero pamoja na wananchi wa Wilaya ya Ulanga kuweza kufanya kazi na wananchi wengine wanaokwenda kuchimba madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi, Serikali inajitahidi kupima ardhi, kumaliza migogoro lakini naomba kuuliza, migogoro ya Kilosa, migogoro ya Mvumero itaisha lini? Ardhi inapimwa lakini wakulima na wafugaji wanapigana mara kwa mara. Serikali naomba ijidhatiti, iangalie jinsi ya kumaliza migogoro hii inayotokea mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu, elimu kuanzia shule ya msingi mpaka vyuo vikuu naomba iangaliwe hasa kwa wafanyakazi na walimu wa vyuo vikuu, wana madai yao na stahili zao. Naomba walipwe kusudi waweze kuwa na mazingira mazuri na kufanya kazi zao vizuri ya kuwafundisha wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia pia bajeti kuhusu mambo ya lishe, UKIMWI na madawa ya kulevya. Tunajua kuwa mambo haya bado ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, lishe iko duni, madawa ya kulevya yanatumika kwa kiasi kikubwa pamoja na UKIMWI hauna dawa mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, naomba bajeti iliyotengwa kwa mambo haya itolewe kama itakavyokuwa imesomwa na wahusika na tayari imeshasomwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakulima, wakulima wanalima mazao yao lakini tatizo ni masoko. *NFRA* haiwezi kumaliza mazao kwa kuyanunua.

Pia kuna mifugo ambayo haina *NFRA,* kwa hiyo, naomba nao muwaangalie kusudi muweze kuwatafutia masoko kwa sababu tunakwenda nje mara kwa mara, Ulaya tunakwenda lakini masoko hatuyaoni. Naomba sana tuweze kuwahudumia hawa wakulima pamoja na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za mawasiliano. Katika Mkoa wangu wa Morogoro kuna vijiji ambavyo bado havijapata mawasiliano, kwa mfano Kolero, Kasanga, Mkulanzi,

Tanganyika Masagati na vijiji vingine. Naomba sana vijiji hivi viangaliwe viweze kupata mawasiliano kwa sababu sasa hivi ni *science and technology. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi kweli mazuri ambayo Serikali kwa kipindi hiki cha miaka mitano imefanya lakini huwezi kufanya mambo yote ukayamaliza kwa muda wa miaka mitano. Hata mtoto anapozaliwa, anazaliwa, kuna hatua ya kukaa, kuna hatua ya kutambaa, kuna hatua ya kusimama, kuna hatua ya kutembea na kuna hatua ya kukimbia. Kwa hiyo, yale mambo ambayo bado Serikali haijayafanya, naomba yakaendelezwe kwenye Serikali inayokuja ya Awamu ya Tano. Nawatakia mafanikio mema viongozi watakaochaguliwa kwenye Awamu ya Tano ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba yale yote ambayo hayakufanyika vizuri, tuweze kushauriana, tuko hapa kuishauri Serikali iweze kufanya vizuri mambo yake lakini sanasana bajeti inayopangwa iendane na mambo yatakayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Margaret Sitta ajiandae Mheshimiwa Zarina Madabida.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kusimama siku ya leo ndani ya Bunge hili Tukufu. Pia nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Tabora kwa ushirikiano wao ambao wamenipa kwa miaka yote hii nikiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora. Vilevile nawashukuru wananchi wa Wilaya ya Urambo ambao tumekuwa tukishirikiana nao kwa karibu sana, naomba ushirikiano huo uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia hasa masuala makubwa mawili lakini nikipata nafasi nitaongezea mengine. La kwanza kabisa ni kuhusu Walimu. Huwezi kuzungumzia elimu bora bila kushughulikia masuala ya Walimu kwa kuwaandaa wao wenyewe vyuoni, kuwaendeleza lakini pia kuhakikisha kwamba wanapata huduma yao kikamilifu maana yake ni kwamba wanapata hazi zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kutambua matatizo wanayoyapata Walimu, wakitaka kuhama wanaambiwa watafute Walimu wenzao wabadilishane, kupandishwa madaraja ni shida, wakitaka kurekebishiwa mishahara yao ni matatizo, lakini Serikali yetu kwa kutambua matatizo wanayoyapata Walimu imeona kuna umuhimu wa kuwa na chombo kitakachohudumia Walimu *(Teachers Service Commission)*, nawapongeza Serikali kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa, swali langu ambalo ningependa lijibiwe Waziri Mkuu atakapokuwa akijibu hoja zetu hapa, ni nini msimamo wa Serikali kuhusu kuunda chombo hiki kwa kukipa sheria ambayo itawezesha kuanza kwake mwezi wa saba yaani mwaka mpya wa fedha wa 2015/2016. Kwa sababu Serikali ilishatoa tamko lake Bungeni kwamba chombo hicho kitaanza mwezi wa saba lakini pia Muswada wa kuanzisha hiyo Tume ya Huduma kwa Walimu Ulishasomwa kwa Mara ya Kwanza. Sasa ninataka kujua msimamo wa Serikali kuhusu kupitisha sheria hiyo katika Bunge hili la bajeti linaloendelea la bajeti ili maandalizi ya kuanza chombo hicho mwaka mpya wa fedha. Naishukuru Kamati yangu kwa sababu kwa pamoja tumepigania suala hili na sisi tungependa kabla ya kutoka hapa Bungeni kwa kuwa na sheria itakayowezesha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi pia kwa kutatua baadhi ya matatizo yanayowakabili wakulima na leo najikita kwa wakulima wa zao la tumbaku.

Zao la tumbaku linaiingizia nchi hii zaidi ya asilimia 50 ya mapato yote ya fedha za kigeni zinazotokana na mazao yanayouzwa nchi za nje. Mkoa wa Tabora peke yake kwa zao la tumbaku wanatoa asilimia 62 ya tumbaku yote inayolimwa hapa nchini. Hata hivyo, Mkoa wa Tabora una matatizo mengi na hasa nikilinganisha wakulima wa Wilaya ya Urambo, wana matatizo sana na masoko, kna makampuni matatu tu yanayonunua tumbaku Wilayani Urambo na tungependa sasa Serikali itujibu. Katika hotuba yake tangu ukurasa wa 32 - 38 imezungumzia suala la masoko, sasa ni vipi Serikali itasaidia wananchi wa Mkoa wa Tabora na hususan Wilaya ya Urambo kupata masoko zaidi? Kulikuwa na uvumi au jitihada fulani za kupata wafanyabiashara kutoka China lakini hatujui juhudi hizo zimeishia wapi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itakapokuwa inatoa majibu hapa itueleze imechukua jitihada gani za kupata masoko zaidi ili tusitegemee hizi kampuni tatu zilizoko Mkoani Tabora zinazonunua mazao ya tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia siyo masoko tu, wakulima wana matatizo ya uhaba wa *classifiers*. Hawa *classifiers* ndiyo wanaosaidia kupanga tumbaku katika *grade* mbalimbali kuwezesha soko lifanye kazi. Tumekuwa na uhaba mkubwa wa *classifiers* ambapo wengi wamestaafu lakini Serikali haiongezi wengine. Kwa hiyo, Serikali itakapokuja hapa kutoa majibu ya hoja zetu ituambie inafanya juhudi gani au ina utaratibu gani wa kuongeza *classifiers* ili wasaidie kulipanga zao hili vizuri kuwezesha soko likutane mara nyingi. Kwa mfano, sasa hivi wakati soko likifanya vizuri ilikuwa kila wiki kunakuwa na soko lakini sasa hivi inapita hata miezi miwili au mitatu wakulima hawana fedha, tumbaku yao haiwezi kununuliwa kwa sababu *classifiers* ambao wanaandaa masoko ni wachache na wamestaafu. Kwa hiyo, tunaona hili suala ni lazima lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo na Serikali itoe jibu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa upande wa zao hilohilo, wakulima wanapokopa fedha za pembejeo kwenye mabenki wanakatwa riba kubwa sana wengine mpaka asilimia 20 wengine 12. Sasa tunafikiria kama kweli zao la tumbaku linaheshimika kutokana na mchango wake wa fedha za kigeni zinazokuja, kwa nini Serikali isisaidie ili riba ya mikopo ya pembejeo ishushwe hata kufikia asilimia saba. Tunajua Serikali inafanya jitihada ya kuwa na benki ya wakulima lakini hadi hapo itakapoanzishwa wakulima bado wana matatizo makubwa. Kwa hiyo, tunaomba kwamba Serikali ijitahidi kadiri iwezekanavyo kupunguza riba kutokana na fedha ambazo wakulima wanakopo kwa ajili ya pembejeo ili angalau ifike hata asilimia saba au sita kuwawezesha wakulima kukopa na kuendeleza zao hili la tumbaku ambalo ni tegemeo kubwa sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo, naiomba Serikali kwa kweli kwa kutambua kiasi cha fedha kinachoingizwa na zao la tumbaku, tupate majibu ya maana kuhusu mambo matatu hayo. Kuongeza soko na hasa la Uchina na kwingineko kutakapopatikana, kupunguza riba lakini pia kuongeza idadi ya *classifiers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kuwakumbuka wenzetu wenye mahitaji maalum yaani wenzetu wenye ulemavu wa ngozi, wenzetu wasioweza kuona, wasiosikia yaani wote wenye mahitaji maalum. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa muda mrefu Kamati ya Huduma za Jamii imeitaka Serikali kuhamisha Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Afya iende chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu yenyewe ni mtambuka! Inaweza ikaagiza Wizara ya Elimu fanya hiki, inaweza kuagiza Wizara yoyote ile mfano Wizara ya Kazi watafutie kazi hawa na kadhalika lakini ilivyowekwa kwenye Wizara ya Afya haifanyi kazi kikamilifu, haipewi fedha, haina mamlaka ya kuamuru Wizara nyingine. Kwa hiyo, nafikiria hilo suala ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ningependa kumalizia kwa kusema hivi, fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya akina mama asilimia tano kwenye kila Halmashauri na asilimia tano kwa ajili ya vijana zitolewe. Mheshimiwa Waziri Mkuu, TAMISEMI iko chini ya ofisi

yako, wewe ndio mkubwa wa TAMISEMI, toa agizo na lisipotekelezwa hatua zichukuliwe kwamba asilimia 10 inayotengwa, tano kwa ajili ya akina mama na tano kwa ajili ya vijana itolewe ili akina mama na vijana wapate mikopo, wajiendeleze wenyewe kwa sababu mpaka sasa hivi Serikali imeshindwa kuwapa kazi, basi wawawezeshe basi waweze kuwa wajasiriamali ili waendeshe maisha yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ikija hapa izungumzie lini chombo cha Walimu kinapita, Muswada usomwe Bunge hilihili, Waheshimiwa Wabunge wote mniunge mkono ili chombo cha Walimu kipitishwe kwa kupitisha sheria na wakulima wa tumbaku waangaliwe, ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Madabida ajiandae Mheshimiwa Lucy Owenya.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehma ambaye amenijalia afya siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba pia niwashukuru sana wapiga kura wangu wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kunipa nafasi hii na ninafikiri nimewawakilisha vyema na sikuwaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba niipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Mimi nimetoka Mkoa wa Dar es Salaam lakini wakati nakuja Dodoma nimeona na sisi wote Wabunge hapa ni mashahidi jinsi gani Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi kubwa. Mtu ambaye amekuwa nje ya nchi, amekuja miaka mitano au kumi iliyopita akija leo anaweza akapotea hata nyumbani kwao. Takwimu zimezungumzwa lakini hata bila takwimu barabara zinaonekana, shule zinaeleweka, hospitali zinaonekana hakuna ambacho hakionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi waelewe, mimi sijawahi kumsikia mtu anamsifia mke mwenzie, mtu ukimsikia anamsifia mke mwenzie ujue ana walakini huyo kichwani. Kwa hiyo, tusitegemee labda pengine *opposition* watatusifia. Upinzani ni kama mke mwenza, huwezi kutarajia akupongeze hata siku moja, siku zote yeye anataka wewe uonekane mbaya tu. Kwa hiyo, hiyo Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nzuri, isishtuke, isitishike iende mbele, nginja nginja mpaka Ikulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nijikite sana Dar es Salaam. Dar es Salaam kuna gharika, Dar es Salaam tumechanganyikiwa, Dar es Salam miundombinu yote imeharibika, mvua za miaka miwili mfululizo… *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi naomba muwaelewe hawa kazi yao kubwa ni kuzomea, hiyo ndiyo juhudi yao. Ninawaomba mnisikilize mimi.

Mheshimwia Mwenyekiti, Dar es Salaam mvua kubwa sana imenyesha na inaendelea kunyesha. Mvua hii si ya mwaka huu tu, huu ni mwaka wa pili mfululizo. Tunaelewa jitihada kubwa sana zimefanywa, Manispaa zimejenga barabara nyingi, Serikali imejenga barabara nyingi tena za mzunguko ambazo zilikuwa zinasaidia sana katika kuondoa foleni. Kwa sababu ya mvua kubwa sana ambazo zimenyesha na zimeendelea kunyesha zimeharibika. Mwenyekiti wewe ni mtu wa Dar es Salaam unajua mafuriko yaliyoko sasa hivi, ile ni amri ya Mwenyezi Mungu, huwezi kusema kwa nini mafuriko yametokea, kwa nini mvua imenyesha, lakini barabara nyingi sana na hasa za pembezoni, zile barabara kubwa ambazo zilijengwa kwa

kiwango kikubwa ziko vizuri lakini barabara zile za michepuko haziko vizuri. Siyo kwa bahati mbaya, hapana, wale wa Manispaa kama ya kwangu mimi Kinondoni lakini naamini pamoja na Manispaa nyingine tuliamua kabisa kwamba badala ya kujenga barabara za changarawe tujenge barabara za lami hafifu ili kusudi matengenezo yasiwe kila mwaka. Mvua hizi zilizokuja zile barabara zimeshindwa kuhimili mvua zile. Kwa hiyo, barabara nyingi sana zimeharibika. Niombe sana Ofisi ya Waziri Mkuu waichukulie hali hiyo kama ni dharura, ni janga na ni maafa ili kusudi barabara hizo zijengwe. Mbona hamzomei tena? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukitoka Lugalo unakwenda Masaki inakuchukua masaa manne, kwa nini? Kwa sababu watu wote kila mmoja ameondoka kwenye zile barabara za mchepuko amekwenda kwenye barabara kubwa. Kwa hiyo, ile hali ambayo Serikali ilikuwa imejitahidi kufanya kuondoa ile misongamano, misongamano imerudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wote tunajua kwamba Dar es Salaam ndiyo inayotoa makusanyo makubwa katika nchi yetu. Asilimia themanini ya mapato ya nchi hii yanakusanywa Dar es Salaam. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba miundombinu inarudia katika hali yake ya kawaida ili kusudi tuweze kufanya maendeleo. Tunapoteza masaa mengi sana, kama utapoteza saa mawili, matatu kwenda, saa mawili, matatu kurudi inamaanisha asilimia 50 ya muda wa kufanya kazi unapotea barabarani. Haya ni maneno ya wana Dar es Salaam ambao wamenituma kuja kusema pamoja na hawa wenzetu ambao huwa wanatumia barabara kuandamana, wamenituma kuja kusema maneno haya kwa sababu barabara zimeharibika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka mitatu nimekuwa nikizungumzia daraja la *Surrender* pamoja na daraja la Gerezani.

Mimi naomba niseme niko katika Kamati ya Miundombinu na nafahamu mikakati ambayo Serikali inajaribu kuifanya ili kutengeneza sehemu hizi mbili. Mimi niombe sana suala hili la madaraja haya mawili, Waziri Mkuu yachukue katika ofisi yako. Wanataka kutengeneza daraja lingine lakini hapa tunachohitaji ni kuongeza *lane*, mbili upande mmoja na mbili upande mwingine, sasa hivi ziko mbili upande mmoja na mbili upande mwingine. Hata hivyo, tunapovuka kule mbele kuna *lane* nne na huku nyuma kuna barabara nne. Kwa hiyo, zinapotoka nne zinapokuja kwenye mbili zinabana. Pale katika daraja la *Surrender* ni *reclaimed land*. Kwa hiyo, naomba tuongeze huku mbili na huku mbili ili kusudi tufanye mikakati ya haraka kuweza kukwamua tatizo hii lakini pia na kwenye daraja lile la Gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie daraja la Kigamboni. Daraja la Kigamboni ni zuri sana, limejengwa kwa umakini mkubwa sana na naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikivu, Serikali makini. Naomba niiambie Ofisi ya Waziri Mkuu ili kusudi wachukue hatua za haraka upande wa Kigamboni. Upande wa Kigamboni kule ile *contract* inaishia kama kilometa moja tu baada ya hapo inaungana na barabara ambayo ni nyembamba sana ya *lane* mbili. Tusipofanya maarifa kule, lile daraja litakuwa *white elephant* ambalo halitatumika kwa sababu litatengeneza foleni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba tulizungumza wakati wa Kamati na *NSSF* walikuwa tayari kuchukua hilo jukumu kutengeneza barabara hiyo kwa sababu lile daraja wamelijenga wao na wao watakuwa wanalipisha ushuru fulani. Kwa hiyo, kama halikutumika hela za wananchi zinaweza kuzama bila kurudi. Niiombe sana Ofisi ya Waziri Mkuu suala hilo ilichukue na kulipa unyeti wake ili kusudi daraja lile liweze kutumika lakini siyo tu kutumika liweze kurudisha fedha ambazo *NSSF* wamezitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Lucy Owenya, ajiandae Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli na Mheshimiwa Iddi Azzan atachangia badala ya Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami pia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama hapa na kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu na namwomba Mwenyezi Mungu azidi kunilinda mpaka Oktoba 2015 wakati wa Uchaguzi Mkuu ili niweze kushuhudia CCM itakapoanguka na UKAWA kuchukua nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema Chama cha Mapinduzi kimezeeka, kimechoka na wanatakiwa kustaafu, tunasema hivyo kwa sababu Wabunge wengi humu ndani wote na wa Chama cha Mapinduzi wamekuwa wakilalamika barabara ni mbovu, afya haiko vizuri, elimu yaani kila kitu wamekuwa wakilalamika lakini mwisho wa hoja wanasema wanaunga mkono hoja. Hii inadhihirisha kwamba Chama cha Mapinduzi mmechoka mnatakiwa kustaafu. Kwa hiyo, naomba 2015 wakati wa uchaguzi mtuachie UKAWA tuchukue nchi ikiwa na amani na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika jana kuna mchangiaji ambaye amesema kwamba CHADEMA ilifanya uchaguzi ukaahirishwa. CHADEMA hatukuahirisha uchaguzi mwaka 2005, wakati ule ni kifo kilitokea na kifo hakina muda kwa hiyo msije mkasingizia kwamba mtaahirisha uchaguzi kwa visingizio visivyokuwa na maana, uchaguzi uko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Moshi Vijijini, Kata ya Mabogini, Kijiji cha Mvuleni, kuna shamba la mwanakijiji Mathias Minde lenye heka 27 alilikabidhi kwa wanakijiji. Wanakijiji walitaka kuliendeleza shamba lile kwa kujenga kituo cha afya, shule, kituo cha mabasi na vitu mbalimbali vya kijamii. Inasemekana kuna kigogo wa CCM ambaye amechukua baadhi ya heka zile na amezuia wanakijiji wale kuchukua shamba lile. Kwa sababu Mkuu wa Mkoa yuko hapa na shauri hili limeshapelekwa kwake, tunataka Serikali waende pale wahakikishe wanakijiji wale wanarudishiwa shamba lile kwa sababu hawajaliendeleza, liko vilevile wanalima tu sehemu chache lakini shamba liko pale na wanakijiji wako tayari kuliendeleza shamba lile ambalo walikabidhiwa na Ndugu Mathias. Kwa hiyo, tunategemea Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kujumuisha atatuelezea nini hatma ya shamba lile kwa sababu Mkuu wa Mkoa yuko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu upungufu wa Walimu. Katika hotuba ya Waziri Mkuu pia amesema kwamba wamepeleka Walimu wengi kwenye mashule lakini Kata ya Kibosho Kati, kijiji cha Uri kuna shule mbili pale, shule ya msingi Uri na Masesereni. Mwaka 2011, shule zote mbili zilikuwa na Walimu nane lakini kwa sasa hivi tunavyozungumza shule zile zina Walimu watatu tu na mwaka wa jana wamepasisha watoto 20 katika shule zote mbili. Wananchi wa Moshi Vijijini katika kijiji cha Uri wanataka Serikali iwapelekee Walimu wa kutosha kwa sababu shule ile ni nzuri ina miundombinu yote kasoro Walimu hawapo. Mmekuwa mkiahidi kwamba mtapeleka Walimu lakini mpaka sasa hivi hakuna Walimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwanri nategemea ukija hapa utatueleza ni lini mtapeleka Walimu katika kijiji cha Uri katika shule ya Uri na Msesereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema CCM imechoka wengine mnabeza, tunawaambia mstaafu. Barabara ya Old Moshi kupitia Kiboriloni, Kidiya kwenda mpaka Old Moshi kwenye *gate* ya kupanda Mlima Kilimanjaro, mwaka jana Mheshimiwa Magufuli alipokuwa anahitimisha hotuba yake alisema barabara ile kilomita 10.8 imetengewa fedha kwa ajili ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Barabara ile inaweza kupeleka watalii, kuna *water falls,* ni njia fupi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya *acclimatization*, kuna vipepeo, kuna ndege wengi na ni njia nzuri sana ambayo ni vivutio vya utalii.

Hata hivyo, mpaka leo Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmesema mtapeleka lami, mmewaahidi wananchi uwongo, tukiwaambia ninyi ni waongo, mmechoka hamkubali. Tunaomba Waziri anapokuja kuhitimisha hotuba yake atueleze wamefikia wapi kuhakikisha kwamba ile barabara inatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu mfululizo wa ajali…

TAARIFA

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwa msemaji anayeongea sasa hivi kwamba barabara ya *Old Moshi* inayotoka *Kiboriloni Primary* kwenda Kijiji cha Kikarara, Suduni na baadaye Kidia imeahidiwa kuwekwa lami na Mheshimiwa Rais. Sasa hivi napoongea shilingi bilioni mbili zimefika Kilimanjaro, usanifu unafanyika, wakandarasi wote wamekutana na wananchi wa *Old Moshi* ili kuangalia ambao wataathirika na ujenzi wa barabara hiyo ili walipwe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa anayechangia kwamba kama anataka Ubunge afanye utafiti na aseme mambo ya ukweli katika Bunge. Barabara ile inajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kusema kwamba Serikali imechoka nafikiri yeye ndiye amekuwa mchovu kwa kuwaza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Owenya.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, atambue kwamba mimi ni Mbunge wa Wanawake Mkoa wa Kilimanjaro na Ubunge wa Moshi Vijijini natamka kwamba nautaka kwa sababu ameshindwa kuwatetea wananchi wa Moshi Vijijini na hii ni kazi yetu nikiwa kama mmoja wa wananchi wa Moshi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfululizo wa ajali ambao umeikumba nchi yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anatoa hotuba yake watu takribani 2,883 wamepoteza maisha na ajali zinazotokana na uzembe wa madereva aidha kwa kuendesha kwa mwendo wa kasi au mara nyingine wanawapa taniboi waendeshe mabasi yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani mabasi ya abiria yalikuwa na *speed governor,* naomba kuiuliza Serikali, zile *speed governor* zimekwenda wapi au ulikuwa ni mradi wa vigogo? Pili, kulikuwa na tamko kwamba mabasi yote yenye kutumia *chassis* za malori yangekaguliwa ili yaondoke barabarani lakini mpaka leo hatujajulishwa ni mabasi mangapi yaliyogundulika kwamba yanatumia *chassis* za malori na malori yalikuwa yakiendeshwa usiku lakini sasa hivi malori yanaendeshwa mchana na tumeona *accidents* nyingi zinatokea ni malori na mabasi ya abiria kugongana na ajali nyingi zinatokana na barabara kuwa mbovu. Kwa mfano, barabara Dar es Salaam – Mlandizi - Chalinze – Moshi, pale Mlandizi - Chalinze barabara ile inanepa, ni mbaya sana. Mheshimiwa Magufuli alisema wametenga fedha, watashirikiana na *private sectors* ili watengeneze barabara ya njia sita na barabara zile zingezuia ajali kwa kiasi fulani lakini mpaka leo hii hatujajua ni kwa kiasi gani wamefikia kuhakikisha barabara zile sita zinajengwa na vilevile kuhakikisha kwamba ile reli ya Dar es Salaam - Arusha inafanya kazi hata kwa kubeba tu mizigo, kwa kiasi fulani ingepunguza ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu amesema wanawajali wazee kwani wazee ni hazina ya Taifa lakini mmesema wazee hawa watakuwa wanatibiwa bure, mpaka sasa hivi wazee wakienda hospitalini hawatibiwi bure, wananunua dawa. Wazee wengine ni wastaafu na mstaafu analipwa Sh.70,000/=, wastaafu wengine wanatakiwa watunzwe, wawe na mfanyakazi nyumbani, tunajua kima cha mfanyakazi wa nyumbani siyo chini ya Sh.80,000/=, hebu niambie mzee huyu atafanya nini? Atamlipa mfanyakazi, atanunua chakula, atajikimu namna gani? Kwa hiyo, Serikali inayosema inawajali wazee, wazee watambue kwamba ni uwongo wa Chama cha Mapinduzi, hakuna chochote hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia Jeshi la Polisi. Serikali imeonyesha kwamba inalijali sana Jeshi la Polisi, wameagiza magari 300 na mojawapo ya magari hayo ni magari yenye maji ya kuwasha. Mimi nauliza, hivi kipaumbele cha Jeshi la Polisi ni magari au makazi ya kuishi? Ni jambo la aibu katika karne ya 21 bado Polisi wanaishi kwenye *full suit,* nyumba ya bati juu mpaka chini. Hali ya hewa imebadilika, ni joto, Polisi anakaa barabarani tangu asubuhi mpaka jioni na ikifika jioni anakwenda kwenye nyumba ya bati ambayo imepigwa jua tangu asubuhi mpaka jioni na chumba chenyewe kimoja. Anahitaji kuwa na makazi mazuri ili afanye kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo Polisi mnawapa posho ya shilingi 180,000/= lakini Wanajeshi mnawapa shilingi 235,000/=. Chochote kikitokea kwenye nchi hii Polisi wote wanachukuliwa kwenda kwenye vita. Mimi naomba wote wapewe posho ambazo zinafanana ili na wao wajisikie kwamba wanapendwa na Serikali yao lakini mnawahadaa kwa kusema kwamba mnalijali sana Jeshi la Polisi lakini upande mwingine makazi yao ni mabovu, nyumba zilijengwa tangu enzi za Mwalimu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mchuchuli jiandae Mheshimiwa Iddi Azzan.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya tele na kwa uwezo wake, *inshallah* nitendelea kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia Watanzania, siku moja nilikuwa napita nikakuta vijana wenzangu wanaongea, wakaniuliza 'K' unakwenda kwenye Bunge la Bajeti? Nikawaambia ndiyo linaanza tarehe 12. Wakasema hivi, sisi vijana wa Tanzania tunaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo kwa sera na bajeti za Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri Mkuu anasoma bajeti yake nikataka nithibitishe yale maneno ya vijana, hivi ni kweli wanaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu au kwa sera, bajeti na mipango ya Chama cha Mapinduzi? Nikiangalia ukurasa wa 27 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anaongelea mambo ya uwekezaji kwenye kilimo, anasema, miradi ya dola za Kimarekani 214 kwenye kilimo mpaka sasa 2014/2015 ilikuwa imewekezwa. Mwisho anamalizia kwa kusema Serikali inakamilisha sera mahsusi itakayohusu uwekezaji katika sekta ya kilimo. Yaani mpaka sasa Chama cha Mapinduzi, miaka 54 ya Uhuru, bado inakamilisha sera itakayowafanya wawekezaji wavutike kwenye sekta ya kilimo wakati sekta ya kilimo ndiyo inachukua takribani 75% ya Watanzania.

Sasa tukisema kwamba wakulima wa Tanzania wanaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo kwa mipango ya Chama cha Mapinduzi tunakosea? Ndiyo maana mwaka jana wakulima wamepata mazao mengi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo kwa sera za Chama

cha Mapinduzi, mazao yao wakayakopa mpaka leo hawajawalipa, mwaka huu mvua zimekataa wakulima hawana kitu. Ndiyo maana tunasema wakulima wa Tanzania wanaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo sera na mipango ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati Waziri wa Uvuvi anajibu swali la Mheshimiwa Rukia anasema mpaka kufikia mwaka huu, Serikali imewapa mafunzo ya uvuvi wavuvi 50 Tanzania Bara na 50 Tanzania Visiwani. Wakati kila siku mimi tangu nimeingia kwenye Bunge hili mwaka 2010, watu wanaongelea kwamba Serikali hii inaweza kukusanya pesa nyingi sana kutoka kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. Serikali inaweza kukusanya pesa nyingi sana kutoka kwenye maziwa kama Tanganyika na Victoria lakini mpaka sasa Serikali inasema eti imewawezesha wavuvi 50 kupata mafunzo. Tukisema kwamba wavuvi wa Tanzania wanaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo kwa sera za Chama cha Mapinduzi tunakosea?

Kwa hiyo, watu wanavyosema Chama cha Mapinduzi kimechoka siyo kwamba wanabahatisha, wanasema kutokana na uthibitisho ambao wenyewe Chama cha Mapinduzi wanatuonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza maabara na watu wakalazimishwa Sh.10,000, Sh.60,000/=, zile maabara mimi nawaambia Watanzania, Kuruthum naweza kufa nyingine hata hazijaanza kutumika. Mimi naweza kufa au nikazeeka zile maabara hazina *apparatus, chemicals* na kadhalika, hicho ndicho Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wametengeneza hizo maabara na nyingine zimekwisha, shule nyingi hazina Walimu wa Sayansi. Kwa mfano, ukienda kwangu Rufiji, shule ya Umwe, Mbwala na Mwaseni hakuna hata Mwalimu mmoja wa Sayansi. Sasa unatengeneza maabara nani anakwenda kufundisha kwenye hizo maabara? Hizo *test tubes* na *apparatus* nani anakwenda kuwafundisha wanafunzi? Kwa hiyo, wanafunzi wa Tanzania hii watafaulu kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo Chama cha Mapinduzi kuwawezesha. Kwa hiyo, tunaposema wamechoka au tunaposema hawana mpya Watanzania watuelewe lakini Watanzania wanawaona na wanafahamu kwamba hakuna mpya na ninyi sasa mmechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia *SACCOs* na amezitaja katika ukurasa wa 30 wa hotuba yake kwamba vijana wanawezeshwa kupitia *SACCOs* na *VICOBA*, mitaji iliyotolewa ni kwa vijana 20,000, vijana Tanzania hii wapo milioni 16, tunaongelea vijana 20,000 katika Bunge hili, *shame*! Ndiyo maana tunasema vijana wa Tanzania wanaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilijaribu kuangalia *Vote* ya Mkoa wa Pwani ili kuona hivyo vikundi vya vijana watakaowezeshwa kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza maisha yao, nilikuwa naangalia *Vote* za Mkoa wa Pwani, kwa mfano, nikaenda Bagamoyo, Mafia na Rufiji, wanasema kikundi kama Jitihada kipo Rufiji kitapewa shilingi milioni tano, *SACCOs* ya vijana Ikwiriri watapewa shilingi milioni tano, wanasema *Bupu Women Group* kipo Mkuranga watapewa shilingi laki tano. Sasa kweli tunaongelea kuwawezesha eti kwamba hawa wanakwenda kupata mikopo ya kujiajiri ili watoke kwenye umaskini? Kwa hiyo, tunaposema wataishi vijana hawa siyo kwa mikopo ya Chama cha Mapinduzi bali kwa kudra za Mwenyezi Mungu tuna ushahidi wa kutosha. Unapeleka shilingi milioni moja kwenye kikundi ambacho kina vijana takribani 50 au 30 wanagawana shilingi ngapi katika shilingi milioni moja? Hivi kijana wa Kitanzania anaweza kujikwamua kwa Sh.30,000/=? Tunafanya masihara na maisha ya vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Taarifa.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Unataka taarifa, nani?

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mama Mkwe wako. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Huyu mdada amekuwa akichangia akisema kwamba vijana wanasema wanaishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu na siyo kwa bajeti ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Humu Bungeni kuna Waislam na Wakristo, vitabu vimeandika wazi, vinasema hatutakula chakula kwa mtu yeyote bure bali kwa taabu na masumbufu. Siyo hivyo tu, vinasema kwa jasho la uso wako utakula chakula hata utakapoirudia ardhi. Mtu asiyeweza kufanya kazi yoyote atapata wapi utajiri? Maskini hawatakoma milele kwa sababu hawataki kujishughulisha, CHADEMA na CCM, naomba uipokee taarifa hiyo. *(Makofi)*

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu Mama Mkwe wangu lakini vijana hao wa Tanzania wamesoma, wana *degree* zao tatu au mbili lakini hawana ajira halafu mnasema Mungu, anafanya kazi gani? Kama ninyi mmempa elimu ambayo haimuwezeshi kijana huyo kujiajiri wakati ana *degree* mbili wewe unategemea atajitoa vipi katika umaskini? Hayo ndiyo mambo ya msingi tunayoyaongea, hatuongei *blahblah*, tunaongea *fact*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuwaambia, Watanzania sasa hivi wala msiwe na wasiwasi, nawapa rai Watanzania, CCM imeshaelekea kibra kama ng'ombe anasubiri kisu kuchinjwa mwezi wa kumi. Ili Watanzania tuweze kuwachinja CCM mwezi wa kumi lazima tukajiandikishe kwa wingi, ikifika tarehe 25 hatuna shaka kwa sababu tumeshachoka kuishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu, tunataka kuishi kwa kufaidi rasilimali zetu ambazo Mwenyezi Mungu ametupa na tupate viongozi kutoka UKAWA watakaokuja kusimamia rasilimali hizi kwa maslahi ya wananchi. Kwa hiyo, msiwe na shaka Watanzania, ng'ombe kashaelekea kibra, mwezi wa kumi tunatia kisu, UKAWA tunaingia Ikulu mambo yatajipa na rasilimali mtaziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Iddi Azzan ajiandae Mheshimiwa Salehe Pamba na Mheshimiwa Dkt. Grace Puja.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kutoa mchango wangu naomba niseme kwamba miaka ya 70 na 80 waliokuwa wanasafiri kwenye Mtwara walikuwa wakifika Rufiji wanakaa kwa maana palikuwa na shida sana ya kivuko. Jamaa zangu hawa wakifika pale Rufiji huwa wanakwenda mitaani kununua chochote mkate ama chai, lakini anapoanza kula anajiuliza nianze 'sai au nianze nkate' lakini vyote atavila na atashiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kumwambia tu mzungumzaji aliyemaliza kwamba ujenzi wetu wa maabara, Chama cha Mapinduzi kimeona kijenge maabara halafu Walimu watakwenda. Kwa maneno yake, hata tungeanza kupeleka Walimu bado angesema mbona mnapeleka Walimu hakuna maabara? Sasa tumejenga maabara na Walimu watakwenda kwenye maabara hizo kwa ajili ya kufundisha somo la sayansi. Chama cha Mapinduzi kina

mipango imara, kinatekeleza mipango yake kwa mwelekeo imara na makini sana, kwa hiyo tuache kuwapotosha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mchango wangu sasa, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya. Tangu tumeingia madarakani tumeona tulipokuwa na tulipo hivi sasa. Utekelezaji wa Ilani umefanyika kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, niseme kwa kweli kwenye bajeti yetu hii ya mwisho tunakamilisha yale ambayo yalikuwa hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hali yoyote ilivyo hakuna Rais ama kiongozi yeyote atakayekuja kumaliza matatizo yote ya wanananchi, ni lazima…

TAARIFA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba CCM kama CCM haina uwezo wa kujenga maabara kwenye nchi hii, haiwezi wala haijawahi kujenga na haitajenga. Wanaojenga maabara sasa hivi ni wananchi, watu maskini kutoka vyama mbalimbali na ambao hawana vyama. Kusema CCM inaweza kujenga maabara ni jambo ambalo haliwezekani kabisa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Iddi Azzan endelea! Serikali ya CCM ndiyo imejenga maabara. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Hawa wengine tena hata nikiwajibu nitakuwa napoteza muda tu. Niseme tu kwamba nchi hii itajengwa na wananchi wenye moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao ndiyo wanafanya mikutano ya kuwaambia wananchi wasichangie maendeleo…

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi wenye nia ya kuendelea kwenye nchi hii kupitia Chama cha Mapinduzi watatoa michango yao tena bila kulazimishwa, ni kwa hiari yao. Chama cha Mapinduzi kitaendelea kusimamia na kuhakikisha tunajenga maabara na zimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ziara aliyoifanya hivi majuzi kutembelea waathirika wa mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam ambapo amekwenda kuwapa pole lakini kubwa zaidi ni kwenda kuangalia ni jinsi gani miundombinu ilivyoharibika. Jiji la Dar es Salaam limekutwa na maafa makubwa sana na maafa haya yalianza kutokea tangu mwaka 2011, mvua kubwa zilinyesha na miundombinu iliharibika. Kwa bahati nzuri sana wakati ule Serikali iliahidi kuwasaidia wananchi kwa maana ya kuwapa viwanja katika maeneo ya Mabwepande. Serikali imetekeleza hivyo wapo wananchi wamepata viwanja na wamehamia Mabwepande. Naiomba Serikali kwa sababu wapo wananchi wengine bado wako katika athari hizo, naomba sana Serikali iangalie uwezekano

mwingine wa kupima viwanja vingine na kuwasaidia wananchi ambao wameathirika na mafuriko kwa kiasi kikubwa ili na wao wapate sehemu ambazo ni salama kwa ajili ya kuishi na familia zao kwa sababu maeneo haya ambayo tumeyategemea kuishi siku zote yameshakuwa sasa ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuriko haya mara nyingine ni kudra za Mungu na hatuwezi kuyazuia lakini mara nyingine ni kwa sisi wenyewe ama kwa kuharibu au kujenga miundombinu ambayo haikidhi au kuangalia athari za mazingira. Eneo la Jangwani hivi sasa ikinyesha mvua kidogo tu maji yanapita juu ya barabara na hii imesababishwa na ujenzi ambao unaendelea kufanyika wa barabara ya mabasi yaendayo kasi. Miaka ya nyuma eneo la Jangwani lilikuwa ni eneo ambalo maji yakija kwa wingi yanajaa pale na barabara ilikuwa juu na kwa kipindi chote maji hayakuwahi kuvuka barabara. Kwa ujenzi ambao umefanyika sasa hivi na vifusi ambavyo wamevisambaza pale, hivi sasa maji yanapita juu ya barabara na sasa ni hatari hata kwa lile daraja ambalo liko pale. Kwa hiyo, tuangalie uwezekano wa Serikali yetu kuona ni jinsi gani itatatua tatizo lile kwa sababu limekuwa kubwa sana. Maji yale sasa kwa wingi ule yanaingia kwenye makazi ya watu ambayo siku za nyuma walikuwa hawapati adha hiyo lakini kutokana na hali ile ambayo imefanyika pale Jangwani sasa maji yanaenda mpaka kwenye maeneo ambayo yalikuwa hayafiki. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha kasoro zilizopo ili kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si Jangwani tu, hata ukienda maeneo ya Kinondoni ambapo barabara hiyo ya mabasi ya kasi imejengwa, nako pia wamefukia mifereji ya maji ile iliyokuwepo awali iliyokuwa inatoa maji ya mvua na hivi sasa maji yale hayana pa kwenda na mwisho wake yamejaa kwenye nyumba za wananchi. Maeneo yote ya Kinondoni B, mtaa wa Kanazi na mitaa mingine inayofuatia pale hivi sasa ukienda maji yamejaa, nyumba hazikaliki na hata mvua zikiisha maji yale hayawezi kuondoka kwa sababu hayana pa kwenda. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie jinsi ambavyo itaweza kuwasaidia wananchi wa mitaa hii ambayo imekumbwa na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naiomba Serikali itusaidie ni kwamba, wengi ambao wamekumbwa na mafuriko si wale wa mabondeni peke yao, wapo ambao wako kwenye maeneo ya juu ambao athari hizi za ujenzi zimewaathiri nao wamepata adha hiyo. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia kwa sababu wako wengine wanaishi kwenye shule hivi sasa, kwa jamaa zao na wapo ambao wanaishi vibarazani, hawana chakula, magodoro, nguo wala chochote. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia watu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni jinsi gani Serikali itusaidie sasa, nashukuru sasa angalau Mkuu wangu wa Mkoa amepeleka maombi Ofisi ya Waziri Mkuu kuangalia uwezekano wa kutusaidia kwa sababu Halmashauri zetu zimeshapitisha bajeti na hatukuangalia athari hii ambayo imetokea kama maafa. Kwa hiyo, niiombe Ofisi ya Waziri Mkuu iangalie uwezekano wa kuisaidia Dar es Salaam. Dar es Salaam ndipo ambapo tunapata pato kubwa la Taifa, sasa hivi imebanwa pumzi na imeshindwa kupumua. Niiombe Serikali iangalie jinsi ya kuzisaidia Halmashauri zetu kwa maana ya kuziongezea fedha kwa ajili ya kukabiliana na uharibifu ambao umetokana na mafuriko haya kwa sababu yamekuja hatukuwa tumeyatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru pia Serikali kupitia Benki ya Dunia kwa mradi ule ambao utakuja kuboresha Mto Msimbazi, Mto Ng'ombe na mito mingine pamoja na ujenzi wa barabara kwenye Jimbo la Kinondoni. Angalau barabara zote za Kijitonyama, Mto Ng'ombe na yenyewe itapanuliwa, kufukuliwa na kujengwa vizuri. Nafikiri hilo likifanyika litasaidia kuondoa mafuriko ambayo yanajitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe tu Serikali kwa sababu kwenye fedha zile kuna fedha za fidia ambazo zinatakiwa zitolewe na Halmashauri zetu. Tunafahamu uwezo mdogo wa Halmashauri zetu, kwa hiyo, tuone jinsi gani pia tutasaidia ili tuweze kulipa fidia haraka na mwisho wa siku mradi ule uanze ili wananchi wetu waondokane na kero ambazo zinajitokeza hasa katika kipindi hiki ambacho kuna mvua ambazo zinakuja bila mpangilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nichukue nafasi hii kuendelea kuwashukuru wakazi wangu wa Jimbo la Kinondoni kwa kunipa moyo na kuni- *support* kwa kipindi chote ambacho nimekuwa Mbunge wao. Niseme tu nitaendelea kuwatumikia kwa kipindi hiki kilichobakia ili kuhakikisha zile kero tunaziondoa. Nina hakika kipindi kinachokuja, hao wanaosema watachukua sijui watachukua kitu gani, nawakaribisha sana waje Kinondoni halafu wataona habari yao. Nina hakika wananchi wa Kinondoni imani ipo kubwa sana kwa Chama cha Mapinduzi na tutapata ushindi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa kweli tunatoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais, amefanya ziara kwenye maeneo ya mafuriko, ameonesha *quality leadership,* ametoa maagizo ya miundombinu na Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ndiye kimbilio letu maana hili mfuko la maafa unao wewe, basi na wewe uko hapa umesikia kilio hiki. Kwa kweli hali ya Dar es Salaam ni mbaya sana tunaomba ulitazame kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Pamba, halafu jiandae Mheshimiwa Dkt.Grace Puja.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi pia napenda niungane na wenzangu kuipongeza sana Serikali. Nitoe shukrani sana kwa wananchi wangu wa Pangani ambao katika kipindi chote hiki tumeshirikiana pamoja katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii vilevile nimshukuru sana *DC*, Ndugu Regina Chonjo, ni mchapa kazi kwelikweli. Niwapongeze sana Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, wananchi, Watendaji na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri ambayo inafanyika pale Pangani. Nasema kwamba tuko pamoja kwa yale yote ambayo tumeyatekeleza na yale yote yaliyobaki tutaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafsi hii kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa yale ambayo yamefanyika katika Wilaya yangu katika maeneo ya maendeleo ambayo yanawagusa wananchi. Nitaanza kuzungumzia suala la maji. Wilaya ya Pangani ni eneo mojawapo ambalo lilikuwa na shida sana ya maji. Nashukuru wafadhili ambao wamenisaidia mimi binafsi nimeweza kujenga visima 15 katika vijiji mbalimbali katika Wilaya yetu ili kuhakikisha kwamba tunapunguza kabisa tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesaidia ujenzi wa visima na miradi mikubwa mitatu ambapo sasa hivi wananchi wanapata maji katika vijiji vya Madanga, Bweni na Kwa Kibuyu. Kwa hiyo, ukiangalia kwa ujumla wake ni kwamba Wilaya ya Pangani sasa hivi kule vijijini inapata maji kwa asilimia 60 ambapo lengo la Taifa ni asilimia 65. Nina uhakika kabisa tutafikia lengo hilo kwa miradi mipya mitano ambayo imepangwa chini ya Mradi wa Benki ya Dunia kwa Vijiji vya Mwera, Mikocheni, Kimang'a, Mikinguni na Mkalambo. Hivi vyote ni kwa ajili ya mwaka huu wa fedha wa 2015/2016. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa kwamba suala hili la maji tutakuwa tumefikia lengo la Taifa hasa pale kijijini. Hongereni sana Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji mijini, napenda niishukuru pia Serikali wametupatia shilingi milioni 200 ambazo sasa hivi mkandarasi tayari atapatikana ili kuweza kutanua mtandao wa maji pale Pangani. Imebaki shilingi milioni 100 ili mradi huu uweze kufika katika maeneo mengi pale mjini. Naiomba Serikali watakapokuja kujibu hasa Wizara ya Maji, tuhakikishe kwamba fedha hizo shilingi milioni 100 zilizobaki zinapatikana ili tufike *coverage* ya asilimia 85 kwa ajili ya Mji wa Pangani. Nina uhakika kwamba suala hili litafanyiwa kazi na hizo fedha zitapatikana katika kipindi hiki kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepiga hatua kubwa sana kwa upande wa Umeme Vijijini. Katika maeneo ya Mkaramo, Kigurusimba, Mseko, sasa hivi nguzo zinawekwa na nyaya zinavutwa na itakapofika mwezi Julai, wananchi wataanza kuwasha umeme. Kama tulivyosema kwamba umeme ni maendeleo, ukipeleka umeme unapeleka elimu bora, unawasaidia wananchi katika shughuli za kiuchumi na kadhalika. Kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kwa Wilaya yangu. Ni maeneo makubwa kwa sababu vijiji hivi vilikuwa havina umeme tangu vilipozaliwa. Kwa hiyo, hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo yapo na nimezungumza na Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* ambao wameahidi kwamba itakapofika mwezi Julai, 2015, vijiji vitano vile ambavyo umeme umepita lakini hawajapata na wao watapata umeme mwaka huu, hiyo ni hatua kubwa sana. Vijiji kama Kimang'a, Choba, Mikinguni, Sange na Kikokwe, ni ni vijiji ambapo *REA* sasa hivi kuna mkandarasi anafanya kazi, akimaliza kule ambako anafanya mradi mkubwa wa shilingi milioni 800 *then* atakuja kukamilisha hivi vijiji vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa ni upande wa barabara. Barabara zetu za vijijini hasa katika Wilaya ya Pangani zinapitika vizuri. Tunaishukuru sana *TANROADS* kwamba barabara ya Mkaramo sasa hivi inafanyiwa kazi na mkandarasi yuko kule kuhakikisha barabara hii inapitika hata wakati wa majira ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la barabara kubwa ya Tanga – Pangani – Saadani. Mchoro na *feasibility study* vimeshamalizika, kwa hiyo, kazi inayofanyika sasa hivi ni tathmini na kuhakikisha wananchi watalipwa fidia ili barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami. Ipo katika Ilani yetu ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na nina uhakika kwamba Chama cha Mapinduzi kikiahidi kinatekeleza na barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, wananchi inabidi wasubiri fidia ili kusudi kazi iweze kuanza na kuhakikisha kwamba mambo hayo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya tumepiga hatua, zahanati zinajengwa. Kuna zahanati mpya zinazojengwa na Serikali kupitia Halmashauri yetu.

Vilevile kwa upande wa Hospitali ya Wilaya, Mbunge kwa kushirikiana na wahisani wake, tumepata *Ultra Sound* kwa hisani kutoka Ujerumani ambayo inatumika katika Hospitali ya Wilaya ya Pangani. Hospitali zote za Wilaya hakuna ambayo ina *Ultra Sound* isipokuwa Hospitali ya Wilaya ya Pangani. Kwa hiyo, hili ni suala kubwa sana na limewafanya wananchi wetu waweze kupata huduma zilizo karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuna Mbunge wa chama cha Upinzani ambaye anatoka Pangani alijaribu kuponda sana na kusema hakuna chochote kinachofanyika na CCM haijafanya kazi. Haya ninayoyasema ndiyo ambayo yamefanywa na Serikali ya CCM pale katika Wilaya ya Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge huyo anasema hakuna *ambulance* Pangani. Pangani kuna a*mbulances* mbili; moja ni ya Hospitali ya Wilaya na nyingine ni ya Kituo cha Afya. *Ambulance* ya Wilaya inafanya kazi kwa sababu mimi nimetoka Pangani siku ya Jumapili, sasa sijui mwenzangu yeye alikuwa wapi. Kuna a*mbulance* moja ambayo iko *garage* lakini viongozi wa pale wanachukua hatua ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ajira ambalo ni suala kubwa sana tunalolizungumzia, kuna mradi mkubwa kuanzisha kiwanda cha sukari katika Wilaya ya Pangani. Tayari mwekezaji ameshapata eneo na huko ndiko tunakopeleka umeme mkubwa. Tutawapatia ajira karibu vijana 3,000 katika shamba la miwa na kiwanda cha sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo changamoto ambazo ni matatizo ya ardhi, kuna mashamba ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu analifahamu suala hili kwani tumezungumza sana. Mashamba ya Mivumoni na Kilima Ngwidu, naomba sasa ifikie mwisho ili kusudi wananchi wale waweze kupata ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la ukuta wa bahari ambapo ni programu iliyoanza tangu mwaka 2012 hivyo ni lazima lifikie mwisho kwa sababu pale Pangani bahari inaumeza mji. Tayari *UNEP* wameshatoa fedha lakini mkandarasi hajapatikana. Naiomba Ofisi ya Makamu wa Rais ihakikishe kwamba mradi huu unaanza katika kipindi hiki ili kuokoa Mji wa Pangani usije ukamezwa na bahari. Fedha zipo, *UNEP* wameishatoa fedha, *UNOPS* wapo tayari kufanya kazi hiyo, kwa hiyo, ni suala la kuwasukuma na kuhakikisha kwamba, masuala haya yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa kusema kitu kimoja. Sisi wote ni viongozi na tunatakiwa tuwe na kauli nzuri za kutowachochea na kuwachonganisha wananchi na Serikali yao. Wananchi wa Pangani wanaipenda Serikali yao ya CCM ndiyo maana wameichagua CCM kwa asilimia 76 katika Uchaguzi wa Vitongoji na Vijiji na wembe ni uleule. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Dokta Grace Puja, ajindae Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh.

MHE. DKT. GRACE K. PUJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa wakati huu ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa namna ya pekee Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunipa heshima ya pekee kuwa kati ya Wabunge 10 ambao amewateua katika kipindi chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia familia yangu kwa kuniwezesha kuwa katika hali hii ya kuja kuchangia hapa katika Bunge Tukufu wakitambua kwamba, kuna umuhimu sana wa kuwa mmojawapo wa Wabunge wa Taifa hili. Pia nawashukuru sana ndugu zangu wote wa Mkoa wa Singida, Tarafa ya Ihanja, Kata ya Iseke, Wilaya ya Ikungi. Nawashukuru sana wanawake wote wa Mkoa wa Singida kwa ushirikiano wao katika chaguzi mbalimbali ambazo nilishiriki na hatimaye kuonekana mimi ni Mwana-CCM anayependa kutumikia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa mchango wake mkubwa wa kuendesha Serikali hii kwa mafanikio makubwa tangu mwaka 2005 mpaka kufikia hiki kipindi cha miaka 10 na kabla ya hapo.

MBUNGE FULANI: Acha uongo wewe.

MHE. DKT. GRACE K. PUJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza juu ya maendeleo haya nikiwa miongoni mwa watu ambao tumefaidi katika Mkoa wa Singida kwa kuundiwa Wilaya mbili mpya za Mkalama na Ikungi na Kata kadhaa ikiwamo Kata yangu ya Iseke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo. Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa kuwahudumia watoto wa mitaani. Hawa watoto siyo wa mitaani, hakuna mtoto anayeitwa mtoto wa mtaani. Hawa ni watoto wetu ambao napenda kusema kwamba wametelekezwa na wazazi, wanaume na wanawake ambao wanapata watoto wanasema nje ya ndoa halafu wanawapeleka kwa Bibi zao au wanawaacha wanazagaa mitaani na wanaenda kuishi peke yao kwenye vituo vya mabasi na maeneo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa Watanzania wote, wazazi na viongozi kwamba hawa Watoto ni jukumu letu. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. DKT. GRACE K. PUJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshiriki kwa kiwango kidogo kusaidia kituo kimoja kinaitwa Kituo cha Malezi Kititimo kule Singida. Mwaka 2007, nilienda katika kituo kile nikakuta kuna matatizo makubwa, nikaenda Canada nikakiomba chuo kimoja kinaitwa *University of Wenzao* kwamba jamani naomba msaada. Walikubali na mpaka sasa hivi wanaendelea kukisaidai kituo kile lakini hilo ni jukumu la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa wito kwa Serikali kuona kwamba watoto hawa wakiachwa peke yao wanatengeneza tabaka la watu ambao watajiona wako nje ya jamii. Wanasemwa ni watoto wa nje ya ndoa lakini sasa watakuwa nje ya jamii kwa sababu hawapati huduma wanazopata Watoto wengine waliozaliwa ndani ya ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia juu ya Kituo cha Afya cha Ihanja ambako ndiko ninakotoka. Kituo kile kina umeme na kinatoa huduma nzuri lakini ukosefu wa huduma ya upasuaji unasababisha akina mama wengi kufa kutokana na ujauzito kwa sababu wanatakiwa wasafiri mwendo mrefu kwenda Singida Mjini, Puma au wapi tena?

MBUNGE FULANI: Huko huko.

MHE. DKT. GRACE K. PUJA: Nje ya eneo lao ili kutafuta huduma hiyo na wengi huwa wanapata matatizo aidha mzazi au mtoto anakufa au wote wawili. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kutoa huduma ya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Ihanja. *(Makofi)*

Ningependa kuiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iongeze Vituo vya Polisi katika Tarafa ya Ihanja na maeneo mengine pote ambapo vituo viko mbali na wananchi. Hali hiyo inasababisha kutokuwa usalama wa kutosha pale panapotokea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kwa kumalizia, kuiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iongeze juhudi katika kujenga barabara zinazounganisha Wilaya mpya ya Ikungi na vijiji vyote vinavyopata huduma kutoka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MJUMBE FULANI: CCM oyee! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Muhammad Amour Chombo!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu. Ninakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla ya yote, ninatamka kwamba, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Ninachukua nafasi hii kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Magomeni kule Zanzibar, kwa ridhaa yao walinipa nafasi ya kuwa Mbunge wao kwa vipindi viwili. Ninakishukuru Chama changu kwa kunipa baraka hiyo na *Inshallah*, uchaguzi unaofuata wa 2015 kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, ninaamini kupitia kwao Wananchi wa Magomeni, watanipa ridhaa yao nirudi tena kuitetea nchi yangu, chama changu na wao wenyewe kama watu wa Magomeni na Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapa pole sana wananchi wangu waliopata maafa ya mafuriko, tuko pamoja, machungu ni yetu sote, hiyo ni katika mitihani tu ya Mwenyezi Mungu, muwe na subira na *Inshallah* mitihani ndiyo maisha na itatoka na tutakuwa salama.

Katika kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu leo, ningependa kwanza kuipongeza Serikali kwa mamuzi yake ya kuamua sasa kuwa na bajeti yetu wenyewe bila kutegemea wahisani. Jambo ambalo litakuwa linatufunza mambo mengi sana, kwa kujua kwamba tunachokipata tuweze kukitumia kwa uangalifu, uadilifu na kwa masilahi ya nchi yetu.

Kitu kikubwa sasa hivi ambacho Serikali inatakiwa kukifanya, ihakikishe nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali inakuwepo na Mipango ambayo tumejipangia inakwenda kwa mujibu wa vile ambavyo tumekubaliana. Tusipokuwa na nidhamu na usimamizi wa matumizi ya fedha zote, itakuwa Mipango yetu ni bure kila siku, kazi yetu itakuwa ni kulalamika na kulalamikiwa. Jambo ambalo tuna uwezo kabisa, kama tumeamua kweli kujifunga mkanda na kuweza kutafuta vyanzo vyetu vya mapato wenyewe na kupata mapato kwa nguvu zetu na kuweza kuwa na Bajeti yetu bila ya kutegemea wahisani. Ninaamini wazi kuwa, tutaweza kusimamia hizi na kuhakikisha yanatekelezeka tuliyoyapanga na hicho kitu kinawezekana ilimradi kila mmoja atimize wajibu wake pale alipo.

Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kila mfanyakazi anafanya kazi yake kwa mujibu wa Sheria kwa mujibu wa Mkataba aliosaini katika makubaliano na mwajiri wake. Tuache kuajiri watu kupokea mishahara, Serikali inaajiri watu sasa hivi kupokea mishahara tu na siyo kufanya kazi. Mtu anaajiriwa kwa muda wa saa nane au saa saba kufanya kazi, anafanya kazi kwa saa mbili au tatu tu, mengine yote anajifanyia shughuli zake bila tija yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inasimamia Sheria na Kanuni, isiwe wafanyakazi wanadai haki zako tu wakati wajibu wao hawatimizi. Serikali mna wajibu wa

kuhakikisha kila anayelipwa mshahara, anafanya kazi kwa mujibu wa mshahara anaolipwa; vinginevyo, tutajkuwa tunatwanga maji kinuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuchangia mbinu kubwa ya kuweza kufanikiwa katika mapato haya. Serikali itumie fedha nyingi sana na ipeleke pesa katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; ni jambo ambalo litatusaidia sana, kwa sababu tutakapokuwa na Vitambulisho vya Taifa tutamjua fulani yuko wapi, anafanya nini na amelipa kodi au hajalipa kodi. Duniani kote watu wanalipa kodi kwa kuwa wanatambulika wako wapi na wanakuwa na *identity cards.* Sasa na sisi bila ya kuwa na taarifa maalumu ya kila Mtanzania yuko wapi, hatutaweza kukusanya kodi kwa mujibu wa taratibu tunazotaka. Lazima Serikali itie nguvu zake zote kuhakikisha *NIDA* inapata fedha za kutosha na Watanzania wote wanakuwa na Vitambulisho vya Taifa. Hiyo ndiyo njia nzuri sana ya kuweza kuhakikisha makusanyo ya kodi yanapatikana na hakuna mtu anayeweza kukwepa kodi.

Kuhusu barabara au usalama barabarani, Serikali ina wajibu sasa hivi wa kuweza kusimamia. Ninashauri ya kwamba, lile wazo au ile Mamlaka inayoitwa *SUMATRA,* isishughulike tu na kupanga ratiba za safari, wao pia washiriki kuhakikisha usalama wa barabarani. Ajali nyingi zinazotokea ni kwa sababu ya uzembe na kutokufuatilia suala hili linakwenda vipi.

SUMATRA wakiwa na wajibu wa kuweza kufuatilia mambo haya, wao wenyewe washirikiane na polisi katika kuhakikisha yale ambayo wanayapanga kwa mujibu wa taratibu zao, basi yanatekelezeka na yanatekelezwa. Wakiwakamata madereva wanaokwenda nje ya Sheria wawashitaki na wawachukulie hatua. Polisi hawawezi kufanya kazi hiyo peke yao, wana majukumu mengi na ya muhimu, lakini usalama barabarani lazima watataka msaada fulani. *(Makofi)*

Kuna maneo ambayo yalizungumzwa na Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, alisema hivi: "Ninapenda kuwahakikishia wale wote hususan walioko madarakani kwamba, UKAWA una dhamira ya dhati kurejesha Utawala Bora kwenye kuzingatia sheria, usimamizi makini na *blah, blah,* ikaendelea mwisho … bila ya kubagua misingi ya kiitikadi, dini, kabila, jinsia au rangi kama ilivyo leo."

Anamaanisha kwamba, leo kuna mambo kama hayo. Binadamu yeyote yule mwenye akili zake timamu, hawezi kutembea mwenzake anatembea utupu wakati yeye suruali yake huku nyuma imepasuka. Kwanza, ninajihakikishia hivi; katika watu wabaguzi nambari moja ni UKAWA. Waangalie *structure* za Vyama vyao zilivyo na Uongozi wao, lakini hawa UKAWA hasa *CUF,* kule Zanzibar wana ubaguzi *hundred percent.*

Zanzibar kuna visiwa viwili; kuna cha Pemba na cha Unguja, basi Kiongozi yeyote anayeomba Ubunge au Uwakilishi, ikiwa ni Muunguja hawezi kupata Uongozi huko Pemba. Huo ni Ubaguzi. Vilevile hawa Waunguja sasa hivi waliokuwa na asili ya Unguja, basi pia wanaondolewa katika kugombea Ubunge au Uwakilishi, wanaletwa wale wale wenye asili ya Pemba pale Zanzibar; huo siyo Ubaguzi ni nini?

Hamjijui tu, hebu tazameni *stucture* ya CHADEMA, uongozi wote mtiririko uko katika Kanda moja; huo ni ubaguzi. Tazameni Chama cha Mapinduzi, uongozi wake umetawanyika, hatuna ubaguzi wa rangi, dini wala kabila. Hicho ndicho kinachoendelea sasa. Msilinganishe kwamba na sasa hivi mnataka igeni basi, mjirekebishe na muweze kufanya …

MHE. HALIMA J. MDEE: Taarifa.

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshalia. Mheshimiwa Halima kaa, Mheshimiwa Godbless Lema!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Msemaji aliyetoka kuzungumza sasa hivi ni mtu mzima sana, lakini ukiona Mbunge anaongea habari ya rangi na ukabila ndani ya Bunge lako Tukufu, huyu mtu ingekuwa ni Korea Kaskazini, Waziri wa Ulinzi angeshaamuru apigwe risasi. *(Makofi)*

Kwa namna anavyoongea, tukianza kuendesha nchi katika mfumo wa kuangalia kabila, dini na rangi, Taifa hili …

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chomboh, hebu kaa chini.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kutafakari uongozi wa nchi hii kwa kuangalia ukabila, udini, Taifa hili litapasuka. Kwa bahati mbaya sana hata mchakato wa Urais katika Taifa hili, tunawasikia Viongozi wakiongea chini chini na wakiongea vitu ambavyo havina msingi; unaposikia mtu anasema hii miaka kumi ilioyopita ilikuwa inaongozwa na Muislamu, sasa muda unaofuata ni muda wa Mkristo, huyo mtu ni mjinga na hana *sense* ya nchi inataka kwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili halitampata kiongozi kwa sababu ya dini yake, halitampata kiongozi kwa sababu ya kabila lake, litampata kiongozi kwa sababu ya uadilifu wake na ushupavu wake, hata kama huyo mtu ni Mchina. Kinachoendelea sasa katika Taifa hili na nimeshawahi kuongea ndani ya Bunge hili, hata kinachoendelea ndani ya Vyama vyenu ni kwamba, mnaanza kutafuta Urais *regarding* kwa udini. Hicho ndiyo anachokiongea Yule, hakiongei kwa bahati mbaya, anakiongea kilekile. Sasa ukiangalia namna ambavyo Wabunge wanaongea, Wajumbe wa *NEC* wanavyoongea wa Chama cha Mapinduzi, haya mambo yasipodhibitiwa mapema, Taifa hili litaingia katika mgogoro mkubwa sana wa kidini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa nchi hii Jakaya Mrisho Kikwete ni Muislamu, Makamu wa Rais ni Muislamu, Taifa hili siyo la Kiislamu. Jakaya alichaguliwa na Wakristo, Waislamu na Wapagani na akamteua Makamu ambaye alikuwa na uwezo. Sasa leo mtu anapokwenda kukosa nafasi mahali akasema anabaguliwa, wanaoleta udini katika Taifa hili ni Wanasiasa ambao wameanza kuishiwa Sera. Wanaoleta Ukabila katika Taifa hili ni Wanasiasa ambao wameanza kuishiwa Sera. Ingekuwa tunapigania nia njema ya Taifa hili, usingeuliza mimi ni kabila gani, ni dini, ili kuwa kiongozi, ungeangalia ninataka nikufanyie nini. *(Makofi)*

CCM mkileta Rais Mkurya, Waziri Mkuu Mkurya, Makamu wa Rais Mkurya na wote ni Wakristo au Waislamu, lakini wana uwezo wa ku-*deliver,* tutakubali kuongozwa na watu wa kabila moja, tutakubali kuongozwa na watu wa dini moja; tunachotaka ni kuona *implementation* ya *policy* katika ukombozi wa Taifa letu na siyo kabila. Ninyi mmetuma watu wanakwenda mitaani wanaongea CHADEMA ni Chama cha Wachaga, Wachaga siyo Warundi, Wachaga siyo Wasudani! Hii ina kera kweli, hizi kampeni mmezifanya nchi nzima, Mwenezi wenu kafanya nchi nzima kubagua watu kwa makabila yao, lakini hawa Wachaga wanaopigwa vita sana siyo watu wabaya, ni watu wakakamavu tu, leo Wachaga wanazunguka mnasema Chama cha Wachaga!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkianza hivyo, hili Taifa halitaishia CHADEMA ni Chama cha Wachaga, CHADEMA ni Chama cha Kaskazini, hawa watu nao wataanza kusema CCM ni

Chama cha Waislamu; Kikwete ni Muislamu, Katibu Mkuu ni Muislamu, Makamu wa Rais ni Muislamu, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa ni Muislamu! Wataanza kusema maneno mengi na ndiyo maana leo ukienda kwenye mitandao ya jamii, Rais anateua mtu wanaanza kuandika huyo ni kabila gani na huyo ni dini gani! Ukiona Taifa linaelekea huko, jueni maana yake mnaua hii nchi. *(Makofi)*

Rais ateue mtu yeyote, wa kabila lolote, lakini awe mchapakazi, asiwe mwizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Meja Jenerali Godefroid Niyombare, aliyefanya Mapinduzi huko Burundi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, zungumzia jambo lililoko kwenye ajenda yetu, masuala ya nchi nyingine usiyalete kwenye Bunge hili. Futa maneno yako yote, Bunge hili halihusiani na siasa zozote za nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuheshimu sana. Ninawapongeza sana Wananchi wa Burundi siyo Major General, kwa kile ambacho walikikataa cha ukiukwaji wa Katiba, ambacho hivi punde kama Serikali haitakubali kukaa na Viongozi wa Upinzani, kujadili mchakato wa *BVR* na Kura ya Maoni inavyoendelea, pengine kinachowatokea Burundi leo kinaweza kulitokea katika Taifa letu. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, usi-*pre-empt* vitu, please, jenga hoja yako kwa masuala ya mustakabali wa nchi yetu. Masuala ya Burundi, masuala ya nchi yoyote nje ya nchi yetu, hayahusiani na mijadala iliyoko mbele yetu. Jadili hoja iliyoko mbele yetu. Halima kaa chini!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumaini utalinda muda wangu tu kwa sababu nimeingiliwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uandikishaji unaendelea nchini hivi sasa, tuna uchaguzi Oktoba, ukiangalia kasi ya uandikishwaji na vifaa vilivyopo, hakuna dalili yoyote kwamba, Tume inaweza kuitisha uchaguzi tarehe 25 Oktoba. Haya ni masuala muhimu sana na mimi ningemwomba Waziri Mkuu, atambue kwamba, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, ulijulikana mwaka 2010 baada ya sisi kuchaguliwa; hii siyo surprise.

Ukiangalia jinsi inavyokwenda, mimi nimetoka Iringa jana, nimeona mwenendo wa hili zoezi, kuna uwezekano mkubwa sana zaidi ya nusu ya Watanzania wanaweza wakajikuta hawako kwenye daftari au orodha ya kuwa waandikishwaji wapiga kura.

Jambo muhimu ambalo ninataka kusema hapa siyo tu kufanya uandikishaji Mikoa yote, unafanya kwa ufanisi wa kiwango gani. Katika watu milioni 24 ambao wamekisiwa kuandikishwa, ukiandikisha watu milioni 12 au milioni 15, ukaacha watu zaidi ya milioni kumi hawajaandikishwa, unaweza ukatengeneza kundi kubwa la watu ambao wataamini walinyimwa haki na pengine tunaweza kuleta kasoro kubwa na kupoteza amani katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, suala hili la uandikishwaji, muda ulivyo pamoja na uchaguzi wa kesho kutwa na jinsi ambavyo mmesisitiza kuwa lazima kutakuwepo na Kura ya Maoni, sioni haya mambo yakifanyika kwa ufasaha na kwa ufanisi na uchaguzi ukawepo Oktoba. Mkiweza kulazimisha, mnaweza kuingiza watu kwenye hisia mbaya na tukaliletea Taifa letu madhara makubwa siku zijazo.

Ninataka kuongelea suala la ajira, vijana hawana kazi mitaani. Ameongea Mbunge mmoja hapa amesema, hata mikopo ya vijana inayoamriwa itolewe kule Halmashauri haitoshi kuwa *effective* kwa ajili ya kusaidia vijana. Nilishawahi kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali wakati wa Maswali kwa Waziri Mkuu kwamba; tatizo kubwa katika Taifa letu linalifanya nchi hii iwe na wachuuzi badala ya kuwa na *investors* ni riba katika Mabenki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mabenki ya Biashara, huwezi kuanzisha *investment* yoyote kubwa ambayo inahitaji mtaji mkubwa ama inahitaji muda mrefu kwa ajili ya ku-*pick,* kwa sababu riba ni kubwa sana. Leo … *rate* ya *BoT 16% to 18%.* Leo unaongelea kwamba, riba kwenye Benki za Biashara ni 18% mpaka 22%. Maana yake mtu akikopa bilioni moja kwa ajili ya biashara, unaongea arudishe zaidi ya milioni 200 riba kwa mwaka. Kwa riba hizi, Taifa hili haliwezi kujenga *investors,* litaendelea kujenga wachuuzi. Ndiyo maana wafanyabiashara wengi tulionao ni wafanyabiashara wa *buy and sale,* wanakwenda China, wanakwenda Malaysia, wanakuleta computer, Laptop na magari.

Tungekuwa na riba ambazo zina-*attract investors* wa ndani, riba ndogo, Japani na Marekani wana riba mpaka ya 3%, kwetu riba ni *22 percent;* huwezi kuwa na riba kubwa kwa kiwango hicho, ukategemea kuwa na Taifa ambalo wenyeji wa Taifa hilo watakuwa na viwanda. Ndiyo sababu wanaokuja ku-*invest* hapa ni watu kutoka nje ya nchi kwa sababu wanachukua mikopo kwao kwa riba nafuu, wanakuja ku-*invest* hapa, mpaka *investment* inaanza ku-*pick* ule mkopo unakuwa ni rahisi kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Lema, tuheshimu muda na Kanuni. Mheshimiwa Sakaya, ajiandae Mheshimiwa Innocent Sebba na Mheshimiwa Juma Kapuya!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na Mipango mingi kwenye vitabu ambayo kwa kiasi kikubwa haitekelezwi ni kuendelea kuwahadaa Watanzania kiukweli kabisa. Mwaka jana tumekaa hapa miezi miwili, tunakula kodi za Watanzania, tunapanga Bajeti ya Serikali, 28% tu ndiyo imekwenda kwenye Bajeti ya Maendeleo, 17% tu ndiyo imekwenda kwenye Mikoa; sasa hivi tunakaa hapa tunajadili nini? *(Makofi)*

Kama 72% ya Bajeti haikwenda kwenye Miradi ya Maendeleo, asilimia karibu 87% haikwenda kwenye Mikoa kufanya kazi za wananchi za maendeleo, tunakaa hapa tena kwa miezi miwili, tuna uhakika gani kama Wabunge kwamba hata Bajeti ambayo tunaijadili wiki nzima itakwenda kutekelezwa? Mimi nilikuwa ninafikiri ni bora tungefupisha muda, tukawa na wiki moja ya kuangalia ni namna gani ya kusimamia Serikali, kuhakikisha Bajeti iliyopita mwaka jana imetekelezwa. Kuendelea kuwa na vitabu kama hivi malundo kwa malundo ambavyo havitekelezeki tunawahadaa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye suala la Vitambulisho vya Taifa, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatuambia kwamba, kuanzia mwaka 2012 tumeanza zoezi la uandikishaji. NIDA imefanya Mikoa mitano; Dar es salaam, Tanga, Morogoro, Lindi na Mtwara na hata hii Mikoa mitano, siyo wote walioandikishwa, lakini cha ajabu kuliko yote, kwa muda wa miaka minne tumeandikisha watu milioni tano Tanzania Bara!

Kwa mahesabu yangu ya haraka haraka ili tuweze kwenda na spidi ambayo Serikali inakwenda nayo, itahitaji miaka kumi tumalize Watanzania ambapo ni milioni 50.

Hivi kweli tunachukua miaka kumi kuwaandika Watanzania; *are we serious? Ten years!* Tunaposema jamani Serikali imechoka, hebu nendeni na viwango. Miaka kumi kwa takwimu za Waziri Mkuu hapa, *ten years* tumalize Watanzania; hii ni aibu. Tulitoa bilioni mia mbili hapa mpaka leo tunashangaa zoezi hata robo halijafika. Hatuwatendei haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *speech* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, *page 24* anasema: "Serikali ina mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na mpango wa kuimarisha mashauriano na sekta binafsi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu, kwa sehemu kubwa sekta binafsi ndiyo inasaidia Taifa hili; ndiyo inayoajiri na ndiyo inachangia sana kwenye Pato la Taifa. Nimekuwa nashangazwa na namna ambavyo Serikali inashindwa kushughulikia matatizo ya wafanyabiashara. Hii inashangaza kabisa!

Wafanyabiashara kila leo wanagoma, ni jambo la ajabu kuona Kariakoo maduka yanafungwa wiki nzima, Mbeya maduka yamefungwa wiki nzima, kila Mkoa; Dodoma, Arusha wiki nzima! Serikali inajua kabisa inavyokosa mapato ya siku moja Kariakoo peke yake ambalo ni Soko la Taifa, ni fedha kiasi gani kinapotea. Serikali kukubali siku saba maduka yamefungwa ni aibu, aibu, aibu! Cha ajabu, sikuona kiongozi yeyote aliyaguswa na fedha inayopotea, kuwaita wafanyabiashara kukaa nao. Nilichosikia ni kwamba, Waziri wa Fedha anasema ninasema watu watalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashauriano yanayozungumzwa kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, wafanyabiashara wana matatizo yao, wanataka wakae wasikilizwe. Serikali ikae nao iwasikilize. Msiendelee kuwashinikiza watu, watu hawaongozwi kama punda. Watu wanaongozwa kwa mashirikiano na kwa majadiliano. Mnaweka tatizo ni nini, mnakaa mnalijadili. Kuendelea kupoteza fedha za walipa kodi, wakati huo huo mnakwenda kutembeza kibakuli nje mnaomba fedha za Miradi ya Maendeleo.

Fedha ya wiki nzima Kariakoo, mlifanya utafiti mkagundua ni kiasi gani kinapotea? Huo ni Mkoa mmoja, hujaenda Mbeya, hujaenda Mwanza, hujaenda Musoma na Mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa kweli Serikali kuendelea kukaa kimya, ninachokiona mimi, Serikali imezoea kufunika kombe mwanaharamu apite. Tatizo likitokea, usifunike kombe mwanaharamu apite. Tatizo likitokea, kaa chini litatue. Mpaka tunapoongea sasa hivi, bado wafanyabiashara matatizo yao yako palepale na ni wachangiaji wa Pato la Taifa hili. Hawakatai kulipa kodi, wanataka mkae chini muwekeane mipango vizuri.

Hizo mashine za *EFD* hawakatai kuzitumia. Wanataka mkae muelekezane, kwa nini hamuwapi muda wa kukaa na kuongea nao? Mnatumia nguvu, hamuwezi kuongoza kwa nguvu mkafanikiwa. Zaidi kabisa, mnaleta hasara kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wanalalamika, pale bandarini wanaingiza kontena la futi ishirini, linatakiwa lilipiwe shilingi milioni 20. Wanachajiwa milioni 40 kwenye risiti inaandikwa milioni 20, Serikali haijui wala haikai nao iwaeleze. Kontena la futi 40 wanatakiwa walipie milioni 40, wanadaiwa milioni 80 kwenye risiti inaandikwa milioni 40! Hayo yote hamkai nao, hili ni tatizo, hata wafanyabiashara mnashindwa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la Stand ya Ubungo. Hii ni aibu; hivi kweli ile Stand ya Ubungo, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri, huwa mnapita pale na kuangalia adha wanayopata wasafiri? Hivi kweli miaka yote Stand ya Makao Makuu ya Mji wa Biashara, mvua zikinyesha ni maji mtindo mmoja, ni mabwawa ya kuogelea. Jua linawaka, wasafiri wanateseka, watoto wanateseka na akina mama wanateseka; Serikali hamwoni; hivi hamwoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu ukiingia pale Stand sasa hivi kwanza mlango wa kuingilia hakuna, lakini unachajiwa shilingi mia mbili. Hii mia mbili inafanya nini miaka yote? Mbona hatuoni maendeleo yoyote yanayofanywa? Mbona hamna vibanda vya kupumzika wasafiri? Kwa kweli ni mateso.

Mheshimiwa Waziri, msikae kwenye magari kwenye VX mkafunga *tinted* mkapita pale kama Kituo cha Polisi. Ingieni mle ndani mkaangalie adha wanayoipata Watanzania; ni tatizo kubwa sana Kituo cha Ubungo. Kituo ni kikubwa, miundombinu ni mibovu, maji yamefurika, uchafu, takataka zote ni adha kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitisha na jambo moja kubwa sana, nilizungumza hapa Bungeni; Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wameshindwa kushughulikia tatizo la mtu anayelipwa ambaye siyo Diwani kutoka Tanga Mjini, Mheshimiwa Mohamed Mambeya. Hili ni jambo la aibu. Hata suala dogo Serikali mnashindwa, ndiyo maana mnaambiwa mmechoka! *(Makofi)*

Suala dogo, tangu mwezi Agosti, 2014 siyo Diwani mpaka leo, amerudisha kadi ya CUF kwa CCM, kwa kuwa CCM mnapenda kukumbatia uchafu mnaendelea kumkumbatia, analipwa posho, analipwa mshahara, anaitwa vikaoni. Sasa hivi ni miezi kumi, Kikao cha Halmashauri hakijawahi kufanyika kwa sababu ya hili na hata hilo limewashinda. Bajeti ya Tanga haikupitishwa na Halmashauri, imepitishwa na Kamati ya Fedha, lakini mmeipokea, mmeifanyia kazi. Hata suala dogo kama hili, mnashindwa kusimamia! Kwa kweli inasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaudhi na inakera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Serikali kusafisha Mawaziri. Kwa kweli hili limeuma, limekumbusha machungu yote ya Watanzania, limekumbusha maumivu yote ya Watanzania. Kweli Serikali imeona muhimu ni Mawaziri walio-*resign* kazi zao, muhimu siyo Watanzania ambao wamepoteza maisha? Hivi kweli tumefikia hapo?

Watu wanasubiri walipwe ng'ombe wao ni maskini wamefilisiwa. Watu wanasubiri walipwe mali zao. Watoto ni yatima wameachwa na wazazi wao wameuawa kinyama. Watu wameuawa vifo vya ajabu. Badala ya Serikali ije na majibu tunafanya nini, inakwenda kukaa kwenye vyombo vya habari na kuwasafisha Mawaziri ambao tayari wana maisha mazuri, hawana shida, wamewajibika kisiasa. Kwa kweli hii ni aibu, ndiyo maana hata Watanzania wamechoka, mambo yanayofanyika yanasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie suala la kilimo. Asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima na wafugaji. Serikali inaposubiri viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo, vijengwe na wafadhili au wawekezaji ambao hawaji kwa miaka yote, tatizo lake tunakosa masoko ya mazao, ni aibu … *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha

kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Innocent Sebba, ajiandae Mheshimiwa Juma Kapuya na Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. INNOCENT R. SEBBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenipa nafasi hii ya pekee na ni neema kuwepo katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Chama kinachotawala Tanzania. *(Makofi)*

Ninamshukuru kwa nafasi hii ya pekee na heshima ambayo amenipa mimi binafsi pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Kagera na Wilaya yangu ya Kyerwa. Hii ni nafasi pekee katika utafiti nilioufanya ni kwa mara ya kwanza Mkoa wa Kagera unampata Mbunge wa Kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ninamshukuru kwa heshima hii ya pekee aliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake, kwa kazi nzuri wanayoifanya, Watanzania wanaona, wana macho na wana masikio, haya yanayosemwa wanajua ukweli huko wapi. Wamefanya kazi kubwa, mimi nitoe mfano; mara ya kwanza wakati nakuja Dar es Salaam, nilikaa njiani siku tatu kutoka Bukoba kufika Dar es Salaam. Leo unaweza kutoka Dar es Salaam ukafika Bukoba siku hiyo hiyo. Hiyo ni kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lazima tuipongeze. Siyo hivyo tu, yapo mambo mengi ambayo yamefanyika, tunaona Vyuo Vikuu na hata katika Jengo hili la Bunge tuliposimama leo ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Jengo zuri linalopendeza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi niwaambie wenzangu ambao wanaajiita wachungaji, tusiwe wanafiki, Serikali inapofanya, tuseme hapa mmefanya na hapa mmekosea. Mtu mzima lazima useme ukweli, siyo kila kitu mnasema hapana. Mimi kwa muda niliokaa hapa Bungeni, nimeona mkienda kukaa na Mawaziri ambao mnasema hawasikii, hawaelewi; mnaenda kukaa nao kujadili nini! *(Makofi)*

Nimeona wengine wa upande wa pili mkimwendea Waziri Mkuu, mnamwendea afanye nini maana hasikii, hajui! *(Makofi)*

Ndugu zangu niseme haya maneno lazima tuwaeleze ukweli Watanzania, maana ukweli unajulikana kuwa ni ukweli na uongo unajulikana kuwa ni uongo.

Baada ya kusema hayo, naishukuru familia yangu, ambayo imeniunga mkono akiwemo baba yangu mzazi Sebba Bilakwate. Nichukue nafasi hii kumshukuru Askofu wangu Mkuu Barnabas Mtokambali, pamoja na Mchungaji wangu Paulo Mulokozi, wamekuwa wakiniombea na kunitia moyo katika safari hii ambayo Mungu amenipa. *(Makofi)*

Katika kuchangia, nitaanza na upande wa afya kwa Halmashauri yetu ya Kyerwa. Katika ziara yangu ambayo niliifanya baada ya kuteuliwa, nimezunguka katika Wilaya yetu. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kutupa Wilaya Mpya ya Kyerwa na katika hili jambo lolote jipya linapoanzishwa, kuna changamoto mbalimbali. Nimebaini baadhi ya changamoto katika Wilaya yetu ya Kyerwa, ya kwanza ni suala la afya.

Kwa kweli mikutano yote niliyoifanya, wazee, akina mama na watoto wadogo chini ya miaka mitano, walinililia sana wakisema gharama za matibabu kwa Hospitali za Mission ni kubwa na Zahanati zetu hazina madawa. Wanapoenda kwenye zahanati wanatozwa shilingi elfu tatu na bado hawapatiwi dawa.

Hawa watu wameniomba kama Mbunge wa Kuteuliwa, nifikishe haya ambayo wamenituma. Pale Kyerwa tuna Hospitali ya Mission inayomilikiwa na Kanisa Katoliki. Baada ya kusikia maneno ya watu, kusikia matatizo ya wananchi, nilienda kukutana na Uongozi wa ile Hospitali ya Mission ya Isingilo. Nikawauliza kwa nini Hospitali hii isiwe *DDH?* Wakasema sisi tupo tayari na tumejaribu kufuatilia jambo hili, ili hawa wazee na akina mama na watoto wa chini ya miaka mitano waweze kupata huduma bure, lakini kuna baadhi ya Viongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa wanazuia jambo hili.

Mimi naiomba Serikali, katika kipindi hiki ambacho bado haijatupatia Hospitali ya Wilaya, Hospitali hii imekamilika, ina vitu vingi, ina mazingira mazuri na ina vifaa vya kutosha; katika hitimisho Serikali mnatoa jibu gani au mnawaeleza nini Wananchi wa Kyerwa katika kuipitisha Hospitali hii ili iwe *DDH*? Ninaomba nipewe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee juu ya Halmashauri yetu. Halmashauri ya Kyerwa bado ni changa, lakini hii inazo changamoto mbalimbali. Changamoto ya kwanza, wale watendaji wote waliopelekwa pale, Wakuu wa Idara, wote wana kaimu nafasi zile kwa kipindi cha miaka miwili. Hawa watu wamefanya kazi katika mazingira magumu, hawajiamini katika nafasi zao. Mimi naiomba Serikali, hawa watu kama wamekaimu katika kipindi hicho cha miaka miwili, Serikali iwathibitishe katika nafasi zao au ituletee wengine ambao wanaona wanaweza wakachukua hizo nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimekutana nalo katika Halmashauri, hawana vitendea kazi, wafanyakazi hawana magari ya kutosha, kwa ujumla kila Idara haina gari.

Jambo lingine ambalo nimekutana nalo, hawa watu wanafanya kazi katika mazingira magumu, Serikali ni kama kuna namna fulani imewaacha. Naiomba Serikali, ile Halmashauri haina Mwanasheria, haina Ofisi ya Mwanasheria, Walimu hawana gari na hawana vitendea kazi. Ukienda Uhamiaji hivyo hivyo, hakuna Ofisi ya Uhamiaji. Idara ya Afya hakuna vifaa vya kubebea madawa ya chanjo hata gari maalum la kusafirisha madawa hakuna! Ninaiomba Serikali pamoja na kuwa ni Wilaya Mpya, iikumbuke katika fungu hili mkate huu ambao mmeutenga mwaka huu 2015/16 na sisi Wanakyerwa mtumegee tukumbuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Ofisi ya Wilaya bado kuna watendaji wachache, hakuna ofisi wapo kwenye ofisi za kupanga, kila kitu ni cha kupanga. Ninaiomba Serikali, wanapohitimisha Hotuba ya Waziri Mkuu, itueleze ni fungu gani limetengwa kwa ajili ya kuhakikisha hao watu wanapatiwa ofisi waweze kufanya kazi katika mazingira ambayo ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya mawasiliano. Kule Kyerwa sisi tupo mpakani mwa Uganda na Rwanda, kuna maeneo mengine ambayo unafika unaanza kukaribishwa Rwanda na unakaribishwa Uganda. Hakuna mawasiliano ya simu na hii imesababisha wananchi wanachajiwa gharama kubwa kwenye mitandao ya simu. Tunaomba Serikali, kwa kushirikiana na Makampuni ya Simu, tupata mawasiliano na sisi … *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha

kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kapuya, ajiandae Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya ya kuendelea kuwepo hapa.

Pili, nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Urambo Magharibi, ambalo sasa linaitwa Jimbo Jipya la Kaliua. Nashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmenipa, tumefanya mambo mengi, sina haja ya kuyaorodhesha hapa kwa sababu wao wanayajua na nina hakika utakapofika wakati, watakumbuka yale yote halafu tuweze kusonga mbele pamoja.

Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba nzuri aliyotoa hapa Bungeni. Kwa sababu kwa kweli inaashiria utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi, ambao ni mzuri na inastahili Serikali hii kwa maana ya Chama hiki kurejeshwa tena madarakani. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Katika mchango huu naanza kujielekeza katika masuala ya elimu.

Tanzania ni nchi ambayo ni Mwanachama wa Kanda, Kanda ya Afrika Mashariki na Kanda ya *SADC*. Kama tukicheza na elimu yetu vibaya, tutashindwa kuingia katika ushindani tunaostahili. Hapa naomba nijielekeze hasa hasa katika *medium of instruction,* lugha ya kufundishia.

Ukiangalia *SADC* wakati tulipokuwa tunahudhuria mikutano yao, mlengo ni kwamba, tuwe na mfumo mmoja wa elimu. Mfumo mmoja wa elimu ni pamoja na kwamba na lugha ya kufundishia iwe moja. Ukija Afrika Mashariki ukiangalia jinsi tunavyokwenda, napo vilevile tunaelekea huko huko kwamba lugha ya kufundishia itakuwa ni moja.

Nimekwenda Rwanda juzi juzi hapa, Rwanda pale nimekuta wenzetu wamebadilisha kabisa kutoka kwenye Kifaransa kuja kwenye Kiingereza, wana miaka saba sasa. Nenda kazungumze na kijana wa darasa la saba wa Rwanda uone anavyoweza kuzungumza Kiingereza sawasawa. Sisi hapa tunafanya mzaha na lugha, tunasahau kabisa hata usia wa Baba wa Taifa ambaye alisema kwamba, Kiingereza ndiyo Kiswahili cha Dunia. Huwa ninawasilikiza sana wale wazee wangu, kipindi cha Jumamosi kwenye Radio One, wanapozungumza habari za lugha aushi, lugha adhimu, lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kusema, tutafanya makosa makubwa kama ilivyoelekezwa katika Sera ya Elimu kwamba, eti kuanzia sasa lugha ya kufundishia iwe Kiswahili tangu shule za chekechea mpaka vyuo vikuu. Tunawaweka vijana wetu katika *disadvantage* kubwa sana ya kushindana katika kazi.

Leo hii tumefungua soko la ajira limekuwa pamoja na wenzetu wa Kenya, Uganda, Rwanda na nchi zote za Afrika Mashariki. Atashindanaje huyu kwa kuwa Mtaalamu wa Kiswahili tu?

Hoja ambayo huwa inayotolewa na watu wanaotetea sana Kiswahili ni kwamba, ukimfundisha mtoto kwa Kiswahili ataelewa vizuri zaidi na nchi yetu itasonga mbele vizuri zaidi, tutaingia katika Mapinduzi ya Elimu; tunakwamishana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano wanayoitoa ni Japani, Uchina na kadhalika, mnasahau kwamba, Uchina na Japani wana historia yao wenyewe ya *academic history* na *academic intelligence*. Kwa hiyo, ninachosema ukienda nchi zingine kwa mfano, Singapore, nenda Singapore ukaone, kule kuna Wachina asilimia 75, kuna Wamalay na kuna Wahindi. Kwa makusudi waliamua kabisa kwamba, Kiingereza ndiyo kitakuwa lugha ya kufindishia. Kaangalie Mapinduzi ya Elimu waliyoleta Singapore, mpaka hivi sasa Singapore hata Dunia ya Kwanza inakwenda kujifunza baadhi ya mambo, kwa maana ya ugunduzi wa kisayansi na kila kitu. Leo sisi hapa tunataka kusema tufundishe kwa Kiswahili; haiwezekani, tutakuwa tumekwamisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoyasema hayo ni wanafiki tu, ni waongo tu, kwa sababu wao wenyewe watoto wao hawasomi hata kwenye hizo shule ambazo zitakuwa zinafundisha kwa Kiswahili. Leo hii tutaleta mgawanyiko mkubwa katika Taifa hili hata amani itakuja kutishiwa, kwa sababu tutatengeneza kundi dogo la watoto wa watu wakubwa kama mimi ni ninyi, watasoma katika shule za kiingereza, shule safi, halafu watoto wa Wakulima na Wafanyakazi wa kawaida watasoma katika shule za kawaida. Inapokuja kushindania kazi, watoto wetu ndiyo watakaopata kazi. Hili tuliangalie kwa uangalifu sana, Sera ya Elimu ile mimi ninasema tafadhalini sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, inatuponza, itateketeza amani ya nchi hii. Ninawasihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu hili tunahitaji mapinduzi. Ukiangalia Afrika ya Kusini wale moja ya sababu walipopata *Soweto Massacre* ni kwa sababu watoto na wazazi walipambana kukataa kufundishwa katika Lugha ya Kiafrikana na Kizulu. Walitaka wafundishwe kwa Kiingereza ili na sisi wao wawe na *access* na Dunia. Watu wakauwawa kwa sababu ya kupigania kufundishwa kwa kutumia lugha ambayo inaeleweka. Leo sisi tunasema hapana Kiingereza twende Kiswahili na wanatoa mifano kwamba, eti Uingereza sasa hivi kuna *University* zinafundisha Kiswahili, sijui wapi kuna *University* inafundisha Kiswahili, sawa zinafundisha Kiswahili, lakini siyo kwa maana kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya kubadilishana elimu, hapana.

Tutalazimika sisi watoto wetu hawa wawe wanasoma vitabu ambavyo vimetafsiriwa na mtu mmoja tu kwa sababu hakuna atakayejifungia. Mnawaambia watu tungeni vitabu, mtu hawezi kutunga kitabu kwa kuamrishwa, hapana. Anatunga kitabu kwa kujisikia yeye mwenyewe. Sasa mtawalazimisha watu wajifungie mahala, watafsiri vitabu vya mawazo ya watu wengine; hii inakuwa ni hatari. Mtu anaposoma na kufika ngazi ya *University,* awe na uwezo wa kusoma vitabu kadhaa, hatimaye afikie mwenyewe *conclusion* yake. Ukimlazimisha umfunge katika boksi la kusoma Vitabu vya Kiswahili tu hapa, mtatengeneza maroboti tu hapa. Mimi ninasema katika Sera ya Elimu kwa kweli hilo mliangalie sana na tunahitaji mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala la kilimo hasa kilimo cha tumbaku. Kilimo cha tumbaku hiki kwa Mkoa wa Tabora ndiyo mkombozi. Sisi tunapozungumza habari za ajira ni kilimo cha tumbaku. Kina matatizo kama alivyozungumza Mheshimiwa Magreth Sitta pale. Matatizo yetu sisi ni hawa *classifiers* hawatoshi, waliopo wamezeeka, matokeo yake soko ni moja kwa mwezi. *(Makofi)*

La pili, kitu kinachotusumbua ni kiasi kinachouzwa katika soko la Dunia kimepungua na kule chini tunashushiwa tulazimishwa kupunguza uzalishaji, yaani ni nchi pekee, zao pekee ambalo mtu unaambiwa usilime sana. Sasa sisi kuna watoto wanamaliza darasa la saba, wanamaliza darasa la kumi na mbili, waende wapi? Tunasema wajiajiri, wajiajiri hata mikopo ya vijana tumejaribu kuelekeza hawa watu waweze kulima tumbaku au mazao mengine, leo unapomwambia huruhusiwi kulima hakuelewi. Hii nayo inatuletea vurugu katika maeneo yetu ya Mkoa wa Tabora hasa Wilaya ya Kaliua pale.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wale wanunuzi wa Kichina waliokuwa wanakuja kunua tumbaku pale Katavi hebu tuwafuatilie sasa ili tuweze kuongeza nguvu, soko lipanuke waje kununua tumbaku hapa Tanzania. Mimi nina uhakika kwa uwingi wa Wachina, wanavuta tumbaku nyingi zaidi, wale wakija kununua tumbaku hapa kwetu, nina uhakika ushindani utakuwa mkubwa na tutaruhusiwa kulima tumbaku nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni maji, kabla hatujawa Wilaya, Kaliua ilikuwa ndogo sana, sasa tumekuwa Wilaya watu wameongezeka sana, maji hayatoshi. Nikizungumza na Waziri wa Maji ananiambia usiwe na wasiwasi tumeshaanza kutengeneza *design* ya kuleta maji kutoka Mto Ugala. Mheshimiwa Waziri wa Maji, hivi *design* inaisha lini? Hebu njoo unisaidie na wewe uje uzungumze katika majukwaa ya siasa ya Kaliua uwaeleweshe basi, mimi ninawaelewesha lakini hawaelewi sasa, kwa sababu mtu mwenye kiu hawezi kuendelea kusubiri. Mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, hili suala la maji ulizingatie kwa mapana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichimba kisima cha maji pale Ushokola kinachoitwa *Wold Bank*, mpaka leo hela za kusambaza maji yale katika vijiji vilivyo karibu hakuna. Matokeo yake tumebaki na shimo tu, maji yapo ndani, tunaambiwa maji ni mengi sana. Mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri uje utusaidie kuleta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme nadhani lenyewe linaenda vizuri, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Tatizo ni kwamba, kuna kile Kijiji cha Usinga bado haujanipa majibu na kule Usinge ndiyo kabisa, mpaka sasa nguzo hazijaenda, wananchi wanaendelea kulalamika. Nimezungumza na mkandarasi wa umeme pale Tabora anaitwa Tom, akaniambia nguzo za Usinge karibu zitaanza kwenda, sasa hiyo karibu hebu iwe leo basi ili ndugu zangu wa Usinge nao waendelee kufurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mawasiliano, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano kwa kutuletea Kampuni ya Vietel. Hawa nao watakapokwenda kule, wasisahau Kijiji cha Ulindanoni, Ichemba, Kanoge, Mwongozo na pale kwa Mnange. Haya ndiyo maeneo ambayo yalikuwa yamebaki kama visiwa, hakuna mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni barabara, ninakupongeza sana, tulishirikiana mpaka barabara ya kutoka Mpanda – Kaliua – Kashishi – Makaze – Kahama ikaingia katika Ilani. Matengenezo yake kwa kiwango cha changarawe yanaenda vizuri, lakini mwaka huu itahitajika hela zaidi, naomba hizo hela zipatikane. Usanifu wake umekamilika, ninachoomba basi Ilani inayokuja isiisahau barabara ile kwa sababu ilikuwa imekusudiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hayo ndiyo nilikuwa nimekusudia kuyazungumzia, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Bukwimba, ajiandae Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Nassari!

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba nzuri. Nawapongeza pia Mawaziri waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuanza na suala la madini. Nilipokuwa nikiangalia kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kurasa za 46, 47 na 48, ambazo zinazungumzia kuhusu Sekta Ndogo ya Madini, nimeona jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameainisha maeneo ambapo wachimbaji wadogo wametengewa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uchimbaji. Amezungumzia vilevile jinsi ambavyo Serikali imeweza kutoa leseni mbalimbali kwa wachimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuikumbusha Serikali kwamba, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi Mwaka 2010 - 2015 imezungumzia habari ya kutoa maeneo ya wachimbaji wadogo katika eneo la Nyarugusu. Ninapenda kulizungumzia hili kila wakati wa bajeti, lakini sijaweza kupata utekelezaji juu ya suala hili. Kwa hiyo, ningependa kupata majibu wakati wa majumuisho, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha Wananchi wa Nyarugusu wanapewa eneo la *STAMICO* pale ili waweze kuendeleza shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapoongea, wananchi hawa wamezaliwa hapo hapo, wengine mpaka wamepata wajukuu, shughuli zao ni hizo za uchimbaji hawajui kazi nyingine ya kufanya. Sasa hivi kila mahali unapogusa unakuta ni eneo la mtu fulani, kila eneo unapogusa ni eneo la mtu fulani, kwa hiyo, ningependa Serikali inihakikishie hili; kwa sababu Mheshimiwa Rais, alipokuja mwaka 2010, yeye mwenyewe alisema atalishughulikia na wananchi watapewa maeneo haya. Mpaka sasa ni miaka mitano bado hatua ya utekelezaji haijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulisisitiza hili kwa sababu imekuwa ni changamoto na ni kero kubwa. Tunazungumzia nchi ya Tanzania ina vijana wengi, lakini hawana ajira. Ninapenda kusema kwamba, ajira ndiyo hizo ndogondogo za wachimbaji wadogo. Vijana wengi wanajishughulisha na shughuli za uchimbaji, lakini hawana maeneo ya uchimbaji. Sasa tunawasaidiaje hawa ili waweze kujipatia kipato chao kwa njia ya uchimbaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuiomba sasa Serikali itilie mkazo suala hili, hasa kwa Wilaya ya Geita na Mkoa wa Geita, ambapo ndiyo shughuli yao kubwa ya kiuchumi. Hii ndiyo maana kila nikisimama ni lazima nizungumzie suala hili, kwa sababu ni suala la kiuchumi katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maeneo ya uchimbaji, napenda pia kuzungumzia Mradi mkubwa sana ambao mwaka 2014 tuliuzindua pale Rwamgasa. Hakuna chochote kinachoendelea, huu ni Mradi wa *World Bank*, napenda Serikali iwaeleze wananchi Mradi huu umefikia wapi au ilikuwa ni kiini macho kwa sababu tangu ulipozinduliwa hatuoni chochote kinachoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, katika shughuli za uchimbaji ningependa Serikali itilie mkazo suala hili hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo. Tukiwawezesha hawa tuna uhakika hata ajira ndogondogo kwa vijana zitakuwepo na wataweza kujipatia kipato chao kupitia shughuli hizi za uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini alikuja kutembelea Mkoa wetu wa Geita. Katika ziara yake alitoa matamko fulani kwamba, wachimbaji wadogo wachukuliwe hatua wapigwe hata mabomu. Hili limekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi, wanaishi kwa hofu hasa wachimbaji wadogo wadogo. Naomba Serikali itolee maelezo kuhusiana na suala hili, kwa sababu wananchi wamepata hofu sana hasa wachimbaji wadogo wa madini. Mheshimiwa Naibu Waziri alitamka akasema watapigwa

mabomu watakaofanya shughuli zao za madini. Napenda suala hili lipatiwe majibu na maelezo ili wananchi wapate uhakika wa kufanya shughuli zao kwa amani kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu barabara. Nilipokuwa nikiangalia bajeti hasa ya TAMISEMI, kwa upande wa Mheshimiwa Hawa Ghasia, amezungumzia kwamba, mwaka 2014/15 tulitenga shilingi bilioni 226 kwa ajili ya barabara za vijijini. Fedha ambazo tayari zimeshapelekwa kwenye Serikali za Mitaa ni shilingi bilioni 50.6 tu, ni kiwango kidogo sana kiasi kwamba, barabara nyingi sasa za vijijini hazipitiki. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ihakikishe kwa kipindi hiki inapeleka fedha za kutosha kuhakikisha barabara hizi zinatengenezwa.

Mvua zilizonyesha mwaka huu ni nyingi, barabara nyingi hazipitiki. Kwa mfano, katika Jimbo la Busanda, Kata ya Rwamgasa, imekuwa kisiwa, watu wanashindwa kwenda sehemu mbalimbali kwa sababu barabara nyingi hazipitiki. Nanaiomba Serikali pale penye uwezekano basi fedha zipelekwe kwa wingi katika Halmashauri, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa upande wa barabara ili barabara ziweze kutengenezwa, kwa sababu hazipitiki kabisa. Kata mpya ya Butundwe barabara hazipitiki.

Vilevile kuna barabara muhimu sana za kiuchumi kama barabara ya kutoka Mwingiro - Kamena kwenda Busanda - Nyakamwaga mpaka Katoro, ni barabara muhimu sana kiuchumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Kwa hiyo, naiomba TAMISEMI ihakikishe fedha zinapelekwa kwa wingi ili wananchi waweze kutumia barabara hizi, kwa manufaa na kuwezesha kupeleka bidhaa zao sokoni. Kwa sababu kwa kipindi hiki pamoja na kwamba, mazao yameiva, lakini hawawezi kupeleka sokoni kwa sababu barabara hazipitiki.

Ninaiomba Serikali ihakikishe inapeleka fedha za kutosha kwenye Halmashauri ili wananchi waweze kunufaika na barabara hizi zitakazotengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maji. Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Maji, kwa sababu tayari kuna Miradi mbalimbali ambayo imeshaanza. Kwa mfano, kuna Mradi wa Maji wa kutoa Ziwa Viktoria kupitia Kituo cha Chankolongo. Tayari Mradi huu umekwishaanza. Kwa muda mrefu nimekuwa nikisimama hapa kuzungumzia habari ya maji, lakini sasa hivi tayari kuna Mradi ambao unaendelea. Naiomba Serikali sasa ipeleke fedha ili kuweza kuuendeleza huu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Viktoria kupitia Chankolongo. Tayari wameshaanza kujenga kituo katika hatua za awali, kwa hiyo, ninaiomba tu Serikali ihakikishe Mradi huu unatekelezwa ili wananchi katika Jimbo hili waweze kupata maji ya uhakika, kwa sababu ni kipindi kirefu wamekuwa na changamoto kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashukuru kwa visima sita ambavyo vipo tayari sasa katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro. Serikali iliahidi kuchimba visima vinane, tayari visima sita vipo tayari. Naomba visima vingine viwili viweze kukamilika. Pamoja na hayo, idadi ya watu pale Katoro ni kubwa sana kiasi kwamba, hata hivyo visima havitoshelezi. Ninaomba Serikali iweke mpango mkakati maalum wa kuona umuhimu wa kuanzisha visima vya kutosha hata ikiwezekana yale maji yanayotoka Chankolongo yafike maeneo yote mpaka Katoro na sehemu mbalimbali ili kuwapa wananchi maji ya uhakika kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Vijiji Kumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, ninaiomba Serikali imalizie kuwalipa Wakandarasi wa Maji ambao tayari wameshafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Kasembe, ajiandae Mheshimiwa Nassari, badala yake ameacha nafasi yake atachukua Mheshimiwa Selasini!

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Masasi, kwa jinsi ambavyo wanaendelea kunipa ushirikiano. Bado ninawaomba waendelee kunipa ushirikiano, nitaendelea kuwatumikia kwa kipindi changu chote kilichobakia. Ninawaomba wasinisahau mwezi wa kumi utakapofika ili niweze kuwatumikia vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Mtwara hivi sasa tunaendelea na zoezi la uandikishaji. Ninawaomba sana ndugu zangu wa Mkoa wa Mtwara, tujitokeze kwa wingi katika uandikishaji huu hasa vijana, akina mama na wazee, kwa sababu hii ni nafasi ya pekee, wakishamaliza mkoa wetu wakienda katika mikoa mingine, itakuwa vigumu kuipata tena nafasi hiyo. Ninawaomba sana tujitokeze kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 tulipokuwa tunaingia katika uchaguzi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilikuwa na Ilani ya Utekelezaji. Ilani ile iligusia mambo mengi sana katika Mkoa wetu wa Mtwara na hasa katika Jimbo langu la Masasi ninalotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kwa kuishukuru Serikali kwa yale ambayo yalikuwepo katika Ilani ya Uchaguzi na yameweza kutekelezeka katika Wilaya yetu ya Masasi. Jambo la kwanza ambalo lilikuwa kero kubwa sana tena sana kwa miaka mingi toka ukoloni, ilikuwa ni suala la Barabara ya Kibiti - Lindi. Tunaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu hii ya Nne, barabara wameweza kuikamilisha kwa kiwango cha lami, hivi sasa tumeshasahau tabu zote tulizokuwa tunazipata za kulala njiani wiki nzima, leo hii Mtwara unaweza ukatoka Dar es Salaam kwenda na kurudi. Yapo mabasi yanayoondoka asubuhi kwenda Mtwara, mchana yanarudi Dar es Salaam. Hiyo ni hatua ya maendeleo na ni kazi iliyofanywa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mingi ambacho miundombinu yetu ilikuwa mibovu, watumishi walio wengi walikuwa hawataki kuja kufanya kazi Mtwara, hata Viongozi ilikuwa ni adimu kufika katika Mkoa wetu wa Mtwara. Kwa hiyo, kwa miaka hiyo yote ambayo tulikuwa kama kisiwani, ni Chama cha Mapinduzi pekee ndiyo kilikuwa kimbilio la wanyonge katika Mkoa wetu wa Mtwara. Wananchi walikuwa wakiwa na matatizo wanakimbilia Chama cha Mapinduzi, wakiwa na kero mbalimbali wanakimbilia Chama cha Mapinduzi. Leo hii mambo yamebadilika, miundombinu imefunguliwa, barabara zinapitika, Viongozi tunawaona kila kukicha wanakuja Mtwara. Viongozi wa Kisiasa sasa wanaonekana usiku na mchana Mtwara. Ninawaomba ndugu zangu wa Mkoa wa Mtwara, tutulie, tuwe na akili timamu, uchaguzi unakuja, usiache mbachao kwa msala upitao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi bado kipo imara na ninawaomba mwezi Oktoba mfanye kila litakalowezekana, Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mtwara tushike nafasi ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Chama cha Mapinduzi kimeweza kulitekeleza ni ujenzi wa barabara kutoka Masasi kwenda Mangaka kwa kiwango cha lami. Kama nilivyotangulia kusema kwamba, katika Mkoa wetu, miundombinu yetu ilikuwa mibovu,

lakini leo hii ukifika kwenye Mkoa wa Mtwara, kwa kweli ni raha tupu, barabara za lami zinaonekana, ujenzi wa barabara umefanywa katika kiwango kinachotakiwa. Vilevile ujenzi wa madaraja yaliyokuwa mabovu ambayo tulikuwa tunashindwa kupita, kwa kipindi hiki Serikali ya Chama cha Mapinduzi wamejitahidi kuyatengeneza, likiwemo na Daraja la Mto Nangoo, ambalo lilitokea mafuriko mwaka 1990, watu wengi wamepoteza maisha katika daraja hili, lakini leo hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetengeneza daraja tunapita bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jambo moja kubwa sana kwa Mji wa Masasi. Masasi ilikuwa ni sehemu ambayo ilikuwa na tatizo kubwa sana la maji, lakini Awamu hii ya Nne, Mji wa Masasi sasa hivi tunapata maji bila matatizo yoyote. Maji yameshafika Masasi, akina mama wamepumzika kukesha visimani, akina mama sasa hivi ndoa zao zinadumu, kwa sababu wakati ule walikuwa wanaweza kukaa siku tatu visimani nyumbani hawaonekani. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila penye mafanikio hapakosi changamoto. Yapo mambo ambayo tuliahidi katika Ilani yetu ya Uchaguzi, naomba niikumbushe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, yapo mambo ambayo tumeanza lakini hayajakamilika. Ni vyema tukawa wawazi kuwaambia wananchi, ili tunapoingia kwenye uchaguzi wawe wanajua tumefikia hatua gani. Kwa mfano, katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, tuliahidi kwa Mji wa Masasi tungejenga bwawa katika Mto Myesi, lakini hadi sasa tumefanya upembuzi yakinifu tu, bwawa halijaanza kujengwa. Naomba niikumbushe Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidi upanuzi wa barabara kutoka Masasi kwenda Mtwara. Kazi imeanza ya upembuzi yakinifu, lakini upanuzi wa barabara bado haujakamilika. Ninaomba kazi iliyoanza ikamilike kabla uchaguzi haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi ujenzi wa reli kutoka Mtwara kwenda Mchuchuma. Upembuzi yakinifu Serikali mmefanya, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, utueleze utakapokuwa unatoa ufafanuzi hapa Bungeni, tuweze kujua ujenzi wa reli kutoka Mtwara kwenda Mchuchuma hadi sasa tumefikia hatua gani, ili na sisi tunapoingia katika uchaguzi tuwe na majibu ya kuwaeleza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tuliahidi ambalo bado hatujalikamilisha japokuwa tumelianza ni ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mtwara. Ninaomba sana, sisi watu wa Kusini tungekamilishiwa ile Hospitali ya Rufaa, ingetupunguzia adha kubwa sana ya kuja Muhimbili na tungeweza kupunguza msongamano kwa kiasi fulani katika Hospitali yetu ya Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia nataka nilizungumze hapa ni suala la usambazaji wa umeme vijijini. Sasa hivi Mtwara kuna gesi, ili Wananchi wa Mtwara waone manufaa ya gesi, ili kweli waamini Mtwara kuna gesi na itawaletea manufaa, mimi kwa akili yangu nilikuwa ninafikiria kwamba, jambo la kwanza Serikali ingeweza kuweka mkakati wa kupeleka umeme vijijini kwa vijiji vyote vya Mkoa wa Mtwara na Lindi. Ninaomba sana Serikali waangalie hilo jambo. Kwa sasa hivi watu wa Mtwara hatuelewi; kwa mfano, Masasi ninakotoka, umeme siyo wa uhakika, lakini tunasimama majukwaani tunawaambia wananchi tutapata umeme wa uhakika kwa sababu gesi iko hapa!

Masasi umeme siyo wa uhakika, ni wa kukatikakatika kila wakati na nina vijiji 68 hadi sasa hawajawa katika Mpango wa Kuwekewa Umeme. Ninaomba wakati wa bajeti hii nielezwe vijiji 68 vilivyobaki vya Jimbo la Masasi ni lini watapatiwa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niikumbushe Serikali; tuliahidi kwamba, tutajenga Zahanati katika kila kijiji na Vituo vya Afya katika kila Kata...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Ya pili?

MWENYEKITI: Ndiyo ya pili, ahsante.

Mheshimiwa Selasini, jiandae Mheshimiwa Arfi!

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii ya Waziri Mkuu. Vilevile ningependa kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Viongozi wa Chama changu na Wanachama wote wa Chama changu, kwa kunipa nafasi ambayo imenifanya nikawa Mbunge na kuwawakilisha Wananchi wangu wa Rombo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Wananchi wa Rombo, wale walio kule Jimboni na nje ya Jimbo, kwa misaada mingi wanayonipa, ili kuweza kulihudumia Jimbo langu sawasawa. Kipekee, nawashukuru wale ambao wako kule Jimboni, kwa sababu kazi wanazozifanya kwa kuniunga mkono, tumeweza kufanya mambo makubwa katika miaka hii mitano. Moja kati ya mambo ambayo ninajivunia sana ni ushindi mkubwa tulioupata katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CHADEMA ni washindi katika Jimbo la Rombo kwa 55%, kati ya vijiji 68 sisi tuna vijiji 38. Kati ya vitongoji 311 tuna vitongoji 157 na kati ya Wajumbe 800 sisi tuna Wajumbe 600. Pamoja na ushindi huo, yapo matatizo na mateso ambayo Wananchi wa Rombo wanayapata hivi sasa. Namshukuru sana Waziri Mkuu, yuko hapa mchana huu wakati mimi nikichangia, kwa sababu jambo hili nilizungumza naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tunavyoongea sasa hivi, wale Viongozi wetu walioshinda katika Serikali za Vijiji wanasumbuliwa kukabidhiwa ofisi pamoja na mali za ofisi! Ninavyozungumza hivi, sasa hivi Mwenyekiti wa Kijiji cha Mutamburu pale Tarakea ana kesi na hiyo kesi ni kwa sababu wananchi walifunga ofisi, wakisema ofisi ile siyo ya chama ni ofisi yao! Kijiji cha Shimbwimasho Mwenyekiti Pius Adrian na yeye yuko Mahakamani, kwa sababu eti alivamia Ofisi ya Chama wakati ni Ofisi ya Kijiji! Mwenyekiti wa Kijiji cha Keni Mengeni, Bernard Shao naye ana matatizo hayo hayo! Mwenyekiti wa Kijiji cha Mengwe Chini, tena Mwanamama Regina Lyakurwa, naye ana tatizo hilo hilo! Mwenyekiti wa Kijiji cha Ngareni, Damiani Swai, naye ana tatizo hilo hilo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya ya Rombo, yanafanana na matatizo yaliyo katika Jimbo la Arumeru Mashariki, ambapo Kijiji cha Kiwawa, Kikatiti, Nkwaranga na Seda, hawa Wenyeviti nao wako Mahakamani kwa shida hiyo hiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nilikufuata kwenye Kiti chako kwa ajili ya shida hii, kwa sababu ofisi zote hizi zilikuwa ni Ofisi za Serikali hadi mwezi Desemba baada ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka 53, Wananchi wa Rombo walitumia ofisi hizi kama ni Ofisi za Serikali. Watendaji wa Serikali walikuwa wanakaa katika Ofisi hizi. Ofisi hizi viwanja vyake, waliotoa hivi viwanja kwa Vijiji ili zijengwe Ofisi za Vijiji, wako hai hadi leo hii. Wajenzi wapo na risiti za michango kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hizi zipo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulipokuwa tunaongea wawili uliniuliza maswali mawili; swali la kwanza uliniuliza je, wananchi walipokuwa wanachangishwa kujenga waliambiwa kama ni Ofisi za Chama au ni Ofisi za Vijiji? Mimi nikakujibu kwamba, waliambiwa ni Ofisi za Vijiji.

Ukaniuliza tena je, Watendaji wa Serikali mpaka kufikia wakati huo walikuwa wanakaa kwenye Ofisi hizo au walikuwa wanakaa wapi? Nikakwambia walikuwa wanakaa kwenye Ofisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa, kwa sababu wananchi wameamua hawataziachia hizi ofisi! Tatizo hili ni kubwa kwa sababu ofisi hizi walioweka kufuli ni wananchi wenyewe. Wananchi wenyewe wameahidi, iwe kwa vitisho au kwa namna yoyote ile, hawatakubali ofisi walizojenga kwa nguvu zao ziende kwenye chama kimoja cha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Halmashauri aliwaambia wananchi kwamba, katika bajeti ya mwaka huu Serikali itatenga fedha kujenga ofisi nyingine za vijiji. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nataka utakapohitimisha bajeti yako uwaambie Wananchi wa Rombo kama hizo pesa za kujenga ofisi mpya za vijiji zipo kweli kwenye bajeti au hazipo; na kama zipo Wananchi wa Rombo wanauliza ni kwa nini wachangie maabara wakati Serikali ina pesa za kujenga ofisi mpya na kuachia ofisi zao kwa chama kimoja cha siasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Rombo ni watu wapole, ni watu wasio na fujo. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, Jimbo la Rombo halijawahi kuingia kwenye fujo zozote za kisiasa mpaka baada ya uchaguzi huu. Hii mimi najua ni kwa sababu ya hofu na *frustration* baada ya kushindwa vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo ndiyo sababu, mimi nataka niwaambie ndugu zangu; mtashindwa vibaya zaidi kwa sababu hata wazee waliojenga hizi ofisi sasa wana hasira kwamba. nguvu zao zinataka zichukuliwe kwenda kwenye chama kimoja. Kwa hiyo, kutoka 55% sasa ushindi utakuwa wa 95% na kuendelea, kwa sababu ya chuki na hasira ambayo wananchi wanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo niseme tu kwamba, sisi Wananchi wa Rombo hatuna tatizo la kuchangia maendeleo, kwa sababu karne na karne mnajua, Wananchi wa Rombo wamekuwa wakichangia zahanati, mashule, vituo vya afya na kadhalika. Hata sasa hivi Wananchi wa Jimbo la Rombo wanachangia ujenzi wa vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokataa Wananchi wa Rombo ni kwamba, vijiji vingi pale Rombo, wananchi wanachanga, hawasomewi mapato na matumizi! Wananchi wanachanga, hawaelezwi *BOQ* iko wapi! Unaambiwa ujenge maabara, mchango 60,000/=, huambiwi mabati ni mangapi, misumari ni kiasi gani, matofali ni kiasi gani na fundi atalipwa kiasi gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi. Nami nimewaambia Wananchi wa Rombo, kijiji chochote bila kupewa mchanganuo wa kwamba, jengo hili linajengwa, mabati ni kiasi gani, matofali ni kiasi gani, fundi ni kiasi gani, wachangaji ni kiasi gani na kila mtu atachanga kiasi gani cha fedha; wasichange hadi waelezwe ni kwa sababu gani Halmashauri haitaki kuwaweka wananchi wazi fedha zinazohitajika kwa ajili ya Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, wananchi wa Rombo wanajua kwamba, maendeleo ya Rombo yataletwa kwa kushirikiana na Serikali; lakini hawako tayari wanachanga, halafu baadhi ya Viongozi wako barabarani wanakunywa bia na nyama choma kwa fedha za Halmashauri na hakuna Kiongozi yeyote wa Serikali anayeibana Serikali iwaambie wananchi mapato na matumizi ya fedha zile wanazochanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninajua michango hii inafanyika kwa tabu sana. Kwa sababu uchumi wa Wananchi wa Rombo ulikuwa unategemea sana Zao la Kahawa, ambalo sasa limekufa. Limekufa kwa sababu hakuna pembejeo, bei ni duni na kadhalika. Wananchi wengi wa Rombo uchumi wao sasa hivi unategemea soko la ndizi, ambalo nalo sasa ni hafifu. Ombi langu kwa Serikali, ninaomba uangaliwe uwezekano wa kufufua Zao la Kahawa, ambalo ndiyo lililokuwa linanyanyua uchumi wa Watu wa Rombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa anakuja Mheshimiwa Arfi, ajiandae Mheshimiwa Rweikiza, Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Abas Mtemvu!

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye anastahiki kushukuriwa kwa neema na fadhila zake nyingi. Ninakushukuru wewe pia Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa namna ya kipekee kabisa nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini, kwa uvumilivu wao na kwa ushirikiano wao walionipa katika kipindi chote cha uongozi, ambao waliniamini na kunipa dhamana ya kuwawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshirikiana vizuri na Uongozi uliopo hususan Baraza la Madiwani na Watendaji wa Serikali. Tumeweza kufanikisha mengi katika yale ambayo tulikuwa tunataka kuifikisha Mpanda tunapohitaji ifike. Ninawashukuru sana kwa michango yao, uvumilivu wao, msaada wao na ushauri wao wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo, nianze kusema kwamba, ninaunga mkono mapendekezo ya Kamati ya TAMISEMI kwa ujumla wake, hasa yale maoni ya ujumla. Naiomba Serikali kwamba, Maoni ya Kamati yana hoja za msingi sana ambazo Serikali ni lazima ijitazame upya na hasa Muundo wa Serikali; ni kwamba, fedha nyingi zinaelekezwa katika Wizara ambazo hazina mahusiano ya moja kwa moja na huduma za Wananchi na Halmashauri zinapata fedha kidogo. Hivyo basi, yale malengo na mafanikio tunashindwa kufikia kwa sababu tu ya kuwa na mfumo ambao hauna maingiliano ya kuweza kutoa huduma stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bajeti. Inasikitisha sana tunapokaa hapa na kupitisha bajeti ya mabilioni, ya matrilioni, ambayo haitekelezeki! Tufike mahali sasa tutengeneze bajeti ambazo zinatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi, Simiyu, Njombe na Geita ni Mikoa mipya. Ni Mikoa ambayo ina changamoto nyingi kwa sababu ndiyo Mikoa imeanza, lakini inasikitisha kabisa katika fedha zilizopelekwa katika Mikoa hii minne mpaka ifikapo Machi, 2015, ilikuwa ni 10% tu ya mahitaji ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi ulikuwa umetengewa jumla ya fedha zilizoidhinishwa zaidi ya shilingi bilioni tatu, hela za ndani. Mpaka Machi imepata shilingi milioni 308, asilimia kumi, kuna bakaa ya bilioni 2.7, zimebakia siku kadhaa Mwaka wa Fedha wa Serikali uishe. Yale yote ambayo tulikusudia kuyafanya katika Mwaka wa Fedha ambao tunaumaliza tarehe 30 Juni mwaka huu, hayajatekelezeka kwa sababu fedha hazikupelekwa. Kwa bahati mbaya sana Serikali haielezi ni kwa nini imeshindwa kufikia malengo na kupeleka fedha! Imeshindwa kukusanya kodi, kama mlikusanya kodi kwa jinsi mlivyokuwa mmepanga katika bajeti, fedha zimekwenda wapi? Tatizo ni nini? Lazima wananchi waelezwe ili wajue kwa nini Serikali imeshindwa kuteremsha fedha huku kwa kadiri zilivyokuwa zimeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha ya Mfuko wa Barabara katika Mkoa mzima wa Katavi, ulikuwa umetengewa jumla ya shilingi bilioni 2.9, lakini kwa ujumla wake Mkoa mzima na Halmashauri zake nne umepata jumla ya shilingi milioni 601. Mpanda Halmashauri ya Mji, ambayo mimi naiwakilisha, malengo yetu kutoka katika Mfuko wa Barabara ilikuwa ni shilingi bilioni 1.1, tumepata shilingi milioni 231.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua fedha za Mfuko wa Barabara liko tozo la Kisheria la zaidi ya shilingi 260 ambazo ni kwa kila lita ya mafuta inayouzwa inayoingia katika Mfuko wa Barabara. Je, mmezikusanya fedha hizi; na kama mmezikusanya kwa nini hazikwenda kwenye Mfuko wa Barabara mmezipeleka wapi? Tunahitaji tupate maelezo ya fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme bado tunalo tatizo. Tumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya kupata jenereta mbili mpya, lakini mpaka sasa hazijafika.

Ninataka kujua tu huu Mradi wa *Orio* umefikia wapi? Tumeshindwa kulipa zile fedha na sasa huo Mradi umehamishwa haupo kabisa ili Wananchi wa Mpanda waondoe matumaini juu ya Mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili bado ni tatizo, hatuna umeme wa uhakika mpaka tutakapopata hizo jenereta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee sana niwapongeze Wizara ya Maji chini ya Profesa Maghemb. Wamefanya kazi nzuri, wamekamilisha Mradi wa Maji wa Ikorongo. Ninawashukuru sana Mradi huu umekamilika, ni Mradi ambao umechukua fedha nyingi na sasa tuna uhakika wa kupata maji. Tatizo ni kwamba, maji yamefika katika matanki ya kuhifadhia maji, lakini hayajafika kwa walaji.

Ninaiomba sana Wizara isaidie nguvu za Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mpanda ili iweze kusambaza maji kwa wateja waweze kujiongezea kipato na kujiendesha. Hivi sasa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mpanda inashindwa kujiendesha kwa sababu haina kipato cha kutosheleza. Wateja wapo lakini bado maji hatujaweza kuwafikishia. Ninaiomba Serikali iliangalie sana eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa reli; hivi sasa ninapozungumza na wewe, kuna gari la mizigo ambalo limeshindwa kufika Mpanda, kwa sababu *engine* imeharibika imezimika, ipo kati ya Stesheni ya Katumba na Mpanda. Hivi sasa ninavyoongea na wewe. Tumaini ni kwamba, gari la abiria lililotoka Tabora leo saa mbili asubuhi, litakapofika ndiyo liende kusukuma ile *engine*

iweze kufika Mpanda ili abiria waweze kufika Mpanda. Tatizo ni kubwa sana katika njia ya Mpanda, lakini kwa taarifa na Serikali mnafahamu, kuanzia tarehe 14 Aprili, 2015 mpaka tarehe 7 Mei, usafiri wa reli ulisimama kabisa, hakuna gari yoyote ya abiria wala mazigo iliyokuwa ikipita katika njia hiyo, sababu ni ukosefu wa *engine*.

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inasema kwamba, wamenunua *engine* 13 mpya, wamekarabati *engine* nane na zingine saba na kadhalika. *Engine* ya treni siyo kiberiti ambacho unaweza kuweka mfukoni, *engine* ya treni ni lazima ionekane, ziko wapi hizo 13 mbona hatuzioni? Kwa nini tunaendelea kupata matatizo ya usafiri wakati mnazo *engine* 13 mpya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Wakala wa Makusanyo ya Fedha kwa niaba ya Halmashauri. TAMISEMI mmefanya utafiti wa kutosha juu ya mpango huu wa kuondoa mamlaka ya kukusanya ushuru na tozo mbalimbali za Halmashauri na kuwapa Mawakala? Mawakala sasa wananufaika zaidi kuliko Halmashauri zenyewe. Naiomba TAMISEMI ifanye utafiti wa kina kama bado tunayo haja ya kuwaweka mawakala wa kukusanya tozo mbalimbali au Halmashauri zikusanye zenyewe moja kwa moja. Ninaomba TAMISEMI ilifanyie kazi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mpanda una nyumba chache sana za askari polisi zilizojengwa miaka ya 50. Idadi ya askari imeongezeka, nyumba zenyewe ni chakavu, zimechoka, vivyo hivyo hata askari wa magereza. Kuna mkakati gani wa makusudi wa Serikali kuboresha makazi ya askari polisi na askari wa magereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda Serikali ieleze kwa nini Msimu wa Tumbaku mwaka huu umechelewa? Sababu zipi ambazo zimefanya soko la tumbaku ambalo kwa kawaida mwezi huu huwa limeshafunguliwa mpaka leo halijafunguliwa; tatizo ni nini?

Tumbaku ndiyo Zao la Biashara katika Mkoa wa Katavi, wananchi wengi kipato chao kinategemea Zao la Tumbaku, hivyo basi, ni muhimu Serikali ikawaeleza wananchi hawa juu ya suala na hatima ya zao lao ambalo wameendelea kuhifadhi katika majumba yao. Nini soko la tumbaku litaanza? Hilo ni tatizo kubwa ambalo linatukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na migogoro ya ardhi. Tuna tatizo la mgogoro wa ardhi na fidia katika eneo la Kazima kuhusu Chuo Kikuu cha Katavi. Eneo hili limepimwa imetolewa hati, hati hiyo kwa maelezo niliyopata, imewekwa rehani kwenye Benki ya *CBA,* hatujui wamekopa kiasi gani, nani aliidhinisha mkopo huo na wananchi hawajalipwa fidia.

Ninataka kujua ni kwa nini hati itolewe kabla ya wananchi kupewa fidia na kama kutolewa hati hiyo bila wananchi kulipwa fidia ilikuwa ni sahihi? Kama ilikuwa ni makosa mnachukua hatua gani na lini wananchi hawa watalipwa fidia zao?

Mapunjo ya fidia kwa waliopisha ujenzi wa kiwanja cha ndege mpaka sasa wanaendelea kulalamika. Tumekwenda nao kwa Waziri, tumekwenda nao kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, lakini ufumbuzi wa tatizo lao mpaka sasa hivi haujapatikana. Tunaomba kupata maelezo hayo mawili. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Mtemvu!

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niongeze mchango wangu kwenye Hotuba hii ya Waziri Mkuu. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwenye Taarifa yangu niliyotoa kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu,

nilisema mambo kadha wa kadha, ambayo Serikali imefanya vizuri na upungufu niliusema. Leo niseme tena mambo ambayo sikuyasema.

La kwanza ni ajira, tatizo la ajira hasa kwa vijana. Ukisoma Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 31 kuna takwimu pale zinaonyesha kwamba, vijana wa Tanzania wenye uwezo wa kufanya kazi na umri wa kufanya kazi ni takribani milioni 16, ambayo ni sawa na asilimia 35 ya Wananchi wa Tanzania. Walioajiriwa kwenye sekta rasmi na isiyokuwa rasmi ni takribani milioni 1.2. Kwa hiyo, vijana yapata milioni 15 hawana ajira, wanahangaika, wanabangaiza, wanashughulika na shughuli ambazo hazina tija na wako wengi mijini na vijijini.

Niliwahi kusema humu ndani kwamba, ajira pekee kwa watu wa nchi hii ni kilimo. Hatuna viwanda, tungekuwa na viwanda vingeajiri vijana wengi sana au watu wengi sana, lakini hatuna, viwanda uchumi wetu una kilimo, asilimia karibu 80 ya Watanzania wanategemea kilimo. Kwa hiyo, nikasema tuongeze kasi kwenye kilimo kwa nguvu nyingi sana. Serikali ibajeti iwe fedha ya kutosha kwenye kilimo kwa ajili ya vijana. Nilipendekeza kwamba, tuwe na Makambi ya Kilimo ya Vijana.

Sasa ukisema kilimo ufikirie jembe la mkono unajidanganya, ni mateso kwa mkulima, haina tija kwa uchumi, ni kazi bure. Lazima Serikali ibajeti vya kutosha, iwekeze vya kutosha katika kilimo, makambi haya yaweze kuwa na tija. Nilipendekeza kwamba, tuna ardhi nzuri sana, maeneo karibu yote ya nchi hii mvua inanyesha, kuna mito mingi sana ukifunga maji yale unapata umwagiliaji mzuri kama kuna uwezo wa fedha.

Kwa hiyo, tukiwekeza kwenye kilimo kwa njia hiyo, makambi yakaanzishwa, vijana wakapewa matrekta, ukipanga vijana 1000 au 2000 ukawapa kambi moja, ukawajengea nyumba za muda pale zile *full suit* kwa kuanzia, ukawapa trekta moja au mbili, *power tiller,* ukawapa mbolea na mbengu nzuri na dawa na nini, wazalishe mazao kwa wingi, kwa njia hii tutaajiri vijana wengi sana. Masoko yapo, katika Mpango wa Serikali kuwe na utaratibu mzuri wa kutafuta masoko. Hivi ninavyoongea, nina taarifa kwamba, wamekuja Wanijeria hapa wanatafuta mahindi wamekosa, wamekuja Ghana wanataka tani 30,000 za mahindi wamekosa, Kenya wamekuja wanataka tani 100,000 za mahindi wamekosa. Kwa hiyo, masoko yapo mengi sana.

Nchi za Uarabuni hawalimi kabisa wale ni jangwa, chakula chao chote wanatoa nchi ambazo zinalima za Afrika na sehemu zingine, kwa hiyo masoko ni mengi sana. Tukiwa na uratibu mzuri na vijana wakalima sana kwenye makambi haya yenye *mechanization*, mashine, madawa, mbolea na pembejeo mbalimbali, tutafufua uchumi na tutapata ajira kwa vijana wetu kwa kutosha sana. Hili ni jambo ambalo ndiyo ukombozi, tutapata mazao mengi, tutapata ajira nyingi na tutafufua uchumi kwa kasi kubwa sana. *(Makofi)*

La pili, ni kuhusu maji; naipongeza Serikali ya CCM, kwa kazi kubwa iliyofanya kuhusu maji. Kule kwangu Bukoba Vijijini, mwaka 2010 shida ya maji ilikuwa kubwa sana. Vipo vijiji kule kama Kyamolaile au Mashule walikuwa wanatembea kilomita saba mpaka nane, kutafuta maji na maji yenyewe machafu utafikiri chai ya maziwa. Leo ninavyozungumza, kuna mabomba ya maji kila kijiji na kila kitongoji. Mabomba ya maji mazuri, wanapata maji mazuri, naipongeza Serikali ya CCM kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Maeneo mbalimbali Omukiisi na kwingineko na maeneo mengine kama Lukindo, Katale, Kibona, Mradi unaendelea vizuri. Bituntu unaendelea vizuri, Ibwera, Itongo, Kibilizi na Kitaiya. Kasi yake ya uendelezaji wa Mradi siyo nzuri sana na kuna maeneo mengine ambayo bado tuna

shida kubwa sana; kuna vijiji kama Hombwea, kuna kijiji kama Rugaze, bado wanatembea kilomita tisa kutafuta maji, maji yenyewe machafu.

Sasa tulizungumza humu ndani zaidi ya mara moja na mimi nilitoa hoja na Wabunge wakaunga mkono, tukapitisha uamuzi kwamba, tuanzishe Mfuko wa Maji au Wakala wa Maji Vijijini kama ilivyo *REA* kwa umeme, isimamie mchakato wa kutengeneza miundombinu ya maji vijijini. Tulikubaliana humu ndani tukapitisha uamuzi, lakini hakuna utekelezaji. Sheria haijafika humu Bungeni, tulipitisha Sheria ya Maji Vijijini, hatujaona Wakala huo unaanzishwa. Hii ndiyo njia pekee ya kusaidia jambo hili maji kuweza kuwaokoa wananchi wa vijijini.

Naomba maelezo kuhusu jambo hili tumefikia wapi au tumekwamia wapi? Watu wanatembea kilomita nane, kilomita tisa maji, maji yenyewe machafu hawana maji. Wanaugua magonjwa ya milipuko sababu ni maji na kama tulivyosema, ufumbuzi ni kuwa na Mfuko wa Maji au Wakala wa Maji. Tulishatoa uamuzi humu ndani lakini bado utekelezaji haujaanza. Naomba jambo hili nipate maelezo na tujue tumefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie usafiri na uchukuzi. Kule Kanda ya Ziwa tuliahidiwa meli ya mpya na Mheshimiwa Rais, hadi leo hakuna meli. Ile iliyokuwepo Victoria imechoka sana. Namshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, John Mongella, amesimamisha, asingefanya hivyo ingeua watu, maana inakwenda imelala upande mmoja hivi kama MV Bukoba ilivyofanya. Ameitoa hafanyi kazi imesimama. Kwa hiyo, hatuna usafiri wa meli pale Ziwa Victoria. Kila nikiuliza hapa zaidi ya mara mbili nimeuliza, anajibu Waziri anasema meli inatengenezwa; inatengenezwa wapi ambayo haikamiliki hiyo? *(Makofi)*

Tunaomba meli iletwe Bukoba pale na Mwanza na Musoma tupate huduma ya meli. *(Makofi)*

Leo kujenga Bukoba ni ndoto, maana mfuko wa sementi umekuwa shilingi 21,000, Dar es Salaam 11,000 au 12,000, sababu ni usafiri hakuna. Kubeba sementi kwa malori ni gharama kubwa sana. Haya malori yakibeba sementi tani 40 kutoka Dar es Salaam kwenda Bukoba yanaharibu barabara. Serikali ya CCM imejenga barabara nzuri sana za lami, lakini hazitadumu hizi kwa sababu hakuna usafiri mbadala wa meli au treni, kama alivyosema Mheshimiwa sasa hivi. Treni haifanyi kazi, kuna reli kati ya Dar es Salaam na Mwanza, treni hakuna. Kwa hiyo, tungepata treni pale na meli ikafanya kazi Mwanza - Bukoba, Mwanza - Musoma na kadhalika, hata gharama zingekuwa chini. *(Makofi)*

Leo kutoa ndizi Bukoba hazina bei kwa sababu hakuna usafiri. Mkungu mkubwa shilingi 3,000 au 4,000, zamani wakati meli inafanya kazi ilikuwa shilingi 10,000 mpaka 15,000. Tunaomba meli ipatikane na usafiri wa reli nao uangaliwe uanze vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru Wananchi wa Bukoba, wapiga kura na wananchi wote, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na msaada mzuri wanaonipa kwenye shughuli zangu za Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii ya kipekee kabisa, kwa sababu ni Bunge la mwisho la Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo matatu; eneo la Utawala Bora, Sekta ya Kilimo na Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa Sera nzuri kuhusu masuala na Sera ya Utawala Bora. Ninachelea kusema kwamba, Sera hii sasa imeanza kuingia dosari. Kwanza, kumekuwa na tabia ya watu kutofautishwa katika nyadhifa zao, makabila, rangi, dini na hata ukanda wanakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ambayo iliundwa na Bunge hili kuangalia jinsi zoezi la Operesheni Tokomeza lilivyofanyika. Ripoti ya Operesheni Tokomeza ya Kamati iliweka bayana kabisa kwamba, katika Mawaziri wanne waliojiuzulu, wale watatu Kamati haikuwaona wana makosa. Sasa juzi nilishtuka sana, Serikali inasema hawa Mawaziri hawana kosa! Kulikuwa na sababu gani ya Taarifa ile kwa umma wakati ikijua kabisa Ripoti ya Operesheni Tokomeza Mawaziri wale haikuwagusa na iliwa-*clear* kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yanaanza kujenga hisia mbovu miongoni mwa wananchi. Ripoti ile ilielezea na kutoa vielelezo watu waliouwawa, watu walionyang'anywa mali zao, wafugaji ambao ng'ombe wao walipigwa risasi, mambo mengi. Ripoti ya Serikali haizungumzii hawa wananchi ambao waliathirika watafidiwa vipi au Serikali itawafanyia nini, badala yake imejikita kusafisha watu watatu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni baya sana, halafu hii habari ya kusafisha safisha watu, kuna watu wengi hapa wamekutana na madhila mbalimbali, wengine wamejiuzulu na wengine wako mahakamani. *ESCROW,* kuna watu hapa ndani ya Bunge hili, tumezungumza mpaka leo mnasema aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini hana hatia, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Nishati na Madini hana hatia. Sasa inakuwaje; walioidhinisha miamala hii ni wao; hawa akina Chenge wanahangaishwa huko barabarani kwa nini?

Mheshimiwa Tibaijuka ambaye ni matokeo tu ya mtu aliyesaini pesa hizi zitoke hajasafishwa! Wako watu wengi, Maige ndugu yangu mpaka leo anahangaika hajasafishwa. Kwa nini watu wachache? Ndiyo maana nasema tabia ya kuanza kusafisha wachache na wengine kuwaacha ni mbaya sana. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Lowassa hapa, mimi sipendi ufisadi, sipendi mtu mwizi, lakini sioni jitihada za kumsafisha na yeye kama hao wengine. Nilikuwa miongoni mwa Wabunge waliosimama kuhusu suala la Richmond, lakini naona sasa kama wenzake wanasafishwa yeye je? Lazima kama ni msumeno ukate sehemu zote mbili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema, nchi hii inaelekea pabaya. Watu sasa wanawekwa katika makundi; haya makundi mwisho wake nini? *(Makofi)*

Ndugu yangu Chenge hapa wakati wa *ESCROW,* mimi nilisema amepewa hela hii kwa sababu *consultancy* sijui nini na nini; ni halali yake lakini kwa nini hasafishwi na anaendelea kubughudhiwa? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kama ni kusafishana tusafishane wote, tuanze upya, nchi hii itakwenda. Vinginevyo, huko mbele ya safari kuna giza. Hiyo ilikuwa ni Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; tangu Uhuru wa nchi hii tumekuwa tukiimba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Kweli, japo sasa hivi kuna madini, gesi asilia na kadhalika, bado kilimo ndiyo tegemeo la Watanzania walio wengi hapa nchini. Katika wilaya ya Kahama, Jimbo la Kahama, licha ya Wilaya hii kuwa tajiri sana katika masuala ya rasilimali kama vile dhahabu, mazao ya misitu na kadhalika, bado wakulima, bado wananchi walio wengi wa Jimbo la Kahama, wanategemea kilimo. Wanalima mpunga, pamba, tumbaku na kadhalika. Badala ya

kilimo hiki kuwafanya wakulima wajisikie na wao ni sehemu ya Taifa hili, sasa hivi kule Kanda ya Ziwa, kule Kahama, kulima pamba sasa ni kukaribisha umaskini, kukaribisha ufukara ndani ya nyumba.

Zao la Pamba halina tija kabisa, kila mwaka bei ya pamba inateremka na Serikali iko kimya, haitafuti njia mbadala au namna ya kuwawezesha wakulima hao wa pamba waweze kurejesha walau sehemu ya nguvu kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi wananiuliza wakulima wa pamba kwamba, Lembeli mwaka huu bei vipi? Jibu langu ni kwamba, kila mtu ana nywele na kila mtu ana macho na ana masikio, ni kwa nini ulime pamba ambayo bei yake ni shilingi 600 heka moja utapata kilo 300, ukizidisha mara mia 600 utapita 180,000, kwa nini usilime mahindi heka moja utapata magunia 30, gunia la mahindi ni shilingi 30,000, unapata shilingi laki tisa. Kwa hiyo, Serikali hii kama inataka Zao la Pamba liendelee kulimwa hapa nchini, ni lazima ije na utaratibu wa kuliboresha.

Vivyo hivyo Zao la Tumbaku. Kule Kahama tumbaku inalimwa, lakini ninavyozungumza sasa hivi wakulima wa tumbaku hawajui masoko yataanza lini, yalitakiwa kuwa yameanza hivi sasa. Serikali inawaonea wananchi, wakati inajua hawajauza mazao yao, wanaambiwa wachangie maabara, hela watatoa wapi; ajira yao na mshahara wao ni kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati na madini. Binafsi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kahama hasa wa Kata za Zongomela, Nyandekwa, Mpunze, Sabasabini, Burungwa na kadhalika, naipongeza sana Serikali kwa kupeleka umeme wa *REA* katika maeneo haya. Umeme ni ufunguo wa maendeleo, nina hakika mara baada ya umeme huu kuunganishwa, maeneo haya yote niliyoyataja yatapata maendeleo makubwa. Matumaini yangu ni kuwa, *REA* Awamu ya Pili katika Jimbo la Kahama, itapeleka umeme katika Kata zilizosalia ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Kahama na Mkoa wa Shinyanga. Kata hizo ni Ukune, Kisuke, Uyogo, Ushetu, Ulowa hadi Ubagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kusimamia vizuri migodi kutekeleza majukumu.

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. JAMES D. LEMBELI: Ya kwanza?

MWENYEKITI: Ya pili. Ahsante Mheshimiwa Lembeli.

Mheshimiwa Abas Mtemvu, ajiandae Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Sugu!

MHE. ABAS ZUBERI MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tumesema Bunge hili ni Bunge la shukrani la kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Rais na ametusikia malalamiko yetu ya mafuriko. Hivi tuko hapa, huko Kinondoni amefanya jambo kubwa sana, amefanya maamuzi makubwa sana kuhusu wananchi wale. Kwa hiyo, namshukuru sana na nimwombee dua Mwenyezi Mungu amjalie afya njema. *(Makofi)*

Naishukuru Hotuba ya Waziri Mkuu na Wasaidizi wake; dada yetu Mama Hawa Ghasia na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri. Nakishukuru chama changu cha CCM, Katibu Mkuu Mzee Kinana, Mungu akuzidishie endelea hivyo hivyo. Nawashukuru Viongozi wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam; Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti na Timu yao. Namshukuru kipenzi chetu Mkuu wa Wilaya Temeke, Dada yangu Sofia Mjema, Mkurugenzi Kagibo, Uongozi wa Chama Temeke, ukiongozwa na Yahaya Sikunjema na Wananchi wote wa Temeke, kwa mapenzi makubwa na heshima kubwa. Mwisho familia yangu, nawashukuru sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia machache tu, lakini kubwa ambalo Wabunge wengi wameongea ni hali ya Dar es Salaam ya msongamano. Nami nashukuru, mwaka sasa wa tisa, Wabunge wa Dar es Salaam tumekuwa tukizungumza juu ya mateso ya msongamano wa Dar es Salaam. Nami nimekuwa nikirudia, wakati ule Mzee Sitta akiwa Spika, nakumbuka niliwahi kumwambia Mzee Sitta wewe Spika unaishi Dar es Salaam, lakini unashindwa kuisaidia Dar es Salaam. Hata Mama Makinda, nimewahi kumwambia hilo. Leo nashukuru Wabunge wote mmezungumzia hali ya kutisha ya Dar es Salaam. Leo unatoka katikati ya mji kwenda Oysterbay, kwenda Temeke, kwenda mahala popote, utatumia saa sita mpaka saa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bajeti ya Waziri Mkuu hatuna tatizo nayo, lakini bajeti ya miundombinu ya kaka yetu Magufuli, hatumwoni hapa, Wabunge wa Dar es Salaam hatutaiunga mkono. Tunakumbuka wakati Waziri Magufuli anaapishwa, kauli yake ya kwanza alitamka amepata dawa ya kuondoa msongamano Dar es Salaam. Matokeo yake anamaliza muda wake akiwa amezidisha msongamano Dar es Salaam wa kutisha. *(Makofi)*

Tulikuwa na *feasibility study* mwaka 2007 ya kuanza *flyover*, Ubungo – TAZARA, lakini cha kusikitisha zimekuwa nyimbo za kila siku mpaka bajeti iliyokwisha, tumeambiwa *flyover* zitaanza lakini hadi leo hazijaanza. Kwa kweli Mwenyekiti wewe ni shahidi, umeshaniambia mara mbili, umetoka Bungeni saa saba umefika nyumbani saa kumi, hukuweza kutoka tena na wewe unakaa Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaombe wenzetu Wabunge ambao wengi mnaishi Dar es Salaam, tuwe na kauli moja ya kuondoa msongamano Dar es Salaam. Tumeeleza Mipango mingi lakini utekelezaji hakuna. Kila Mbunge anayekuja hapa atatetea eneo lake, lakini tunasahau uchumi wa nchi hii asilimia 75 unatoka Dar es Salaam. Kwa hiyo, niwaombe siyo suala la huruma, lakini hebu tutazame foleni zile, tabu zile, ni kiasi gani cha uchumi kinapotea katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine ni *Traffic* wetu. Sasa sijui kama kuna *allowance* maalum wanayoipata wakati huu wa mvua, wakati wa dharura. Maana ilifika mahala wakati wa zile mvua nyingi barabarani hawakuwepo. Sasa inawezekana hawawezeshwi, hawana vifaa, hebu tuangalie umuhimu wa hawa *traffic*; ndugu zangu wanafanya kazi sana usiku na mchana, wanakaa barabarani wakati wa jua na mvua, tuwawezeshe kwa vifaa, *allowance* na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote mpya zilizojengwa ni tatizo la mafuriko Dar es Salaam. Barabara ya Tegeta - Mwenge, maji yote yanakwenda sasa kwenye nyumba za watu. Barabara ya Kilwa maji yote yanakwenda kwenye nyumba za watu. Barabara ya Mandela kwa kiasi kikubwa maji yanakwenda majumbani, lakini ukifika Soko la TAZARA maji yote yanakwenda Soko la Tazara, kwa hiyo, naomba tuangalie hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Wizara ya TAMISEMI kwa Mradi wa *DMDP,* lakini tuwaombe wawezeshe Halmashauri zetu, wawape uwezo waweze kulipa fidia. Bila hivyo,

hatutaweza kulipa fidia. Temeke peke yake tunahitaji shilingi bilioni kumi na saba, kwa hiyo, tunaomba na hilo linaweza kusaidia kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Wapo Makandarasi ambao wanadai; Kilwa Road imechimbwa imesimama, Scola hajalipwa malipo yake. Kwa hiyo, tunaomba Makandarasi wanaodai wawezeshwe ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yangu yote nimekuwa nikilalamika Kurasini, Kurasini, lakini leo naomba niwapongeze Waziri Lukuvi, Naibu Waziri dada yangu Angella na Katibu Mkuu Kidata, wamefanya kazi ya fidia nzuri sana Kurasini, tumebakiza eneo moja tu. Tumebakiza soko, soko karibu watalipwa fidia, tumebakiza eneo moja la Mama Komba, nalo wanafanya kazi vizuri wakati wowote fidia italipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Keko ni la siku nyingi, halina ukarabati pamoja na nyumba za maaskari. Naomba Serikali waliangalie hilo kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana, kwa sisi mijini njia bora ya kusaidia vijana ni kuwezesha VICOBA na *SACCOS* kupata pesa ili vijana waweze kupata mikopo wajiajiri waweze kufanya kazi zao. Kwa hiyo, naomba sana hilo tujitahidi tuwawezeshe vijana waweze kupata pesa zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Wenje, ajiandae Mheshimiwa Sugu, Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Abdul Marombwa!

MHE. EZEKIAH D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba, nampa pole ndugu yangu Rweikiza, ambaye amesimama anashangaa kwa nini ahadi ya Rais ya kupeleka meli Ziwa Viktoria haijatekelezwa mpaka leo. Kuiomba Serikali hii inunue meli ambayo hata madawati haiwezi kununua, nafikiri Mheshimiwa Rweikiza hajui anachofanya au amesahau kwamba Serikali hii haina uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia Wabunge wachache wanalalamika kuhusu baadhi ya Mawaziri au baadhi ya watu waliofanya makosa mbalimbali kusafishwa huku wengine hawasafishwi. Nami pia naamini kwamba, katika kosa la *Escrow* wenye matatizo makubwa ni wale watu walioidhinisha hiyo pesa kutoka. Hata hivyo, ukisikia Mbunge anatoka huko nje yeye kila *deal* kwenye Taifa hili yumo, halafu anafika huko nje anajisifia yeye ni nyoka mwenye makengeza kwamba, yeye kila *deal* yumo anajua kutafuta pesa; huyu mtu unamsafishaje? *(Makofi)*

Unaposikia Kiongozi mkubwa wa nchi anasema milioni kumi ametumia kununua mboga; huyu mtu unamsafishaje wakati Taifa watu wanaangamia hakuna hata dawa kwenye hospitali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba, wakati umefika, tunahitaji Rais nchi hii anayetambua kwamba, rushwa ndiyo tatizo kubwa linalokwamisha maendeleo katika Taifa hili. Rushwa inafanya tunakosa maji, rushwa inafanya hata makusanyo yanayokusanywa na *TRA* yawezekana tukakusanya nusu tu ya makusanyo tunayotakiwa kukusanya. Rushwa inafanya

akina mama wanakufa hospitalini kwa kukosa dawa, Serikali kwenye vitabu wanapeleka dawa hospitali lakini hazifiki kwa sababu ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Rais atakayesimama na kutuambia na anaelewa kwamba rushwa ndiyo tatizo namba moja linalokwamisha maendeleo katika Taifa hili. Rais atakayetueleza bayana ni mfumo gani na mkakati gani atakaotumia kwenda kupambana na rushwa. Rushwa ndiyo tatizo la msingi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika Taarifa ya Waziri Mkuu, anasema katika ukurasa wa 12 kuhusu ajali za barabarani kwamba, kuanzia Julai mwaka 2014 mpaka Machi 2015, Watanzania 2,883 wamepoteza maisha na watu 9,370 wamepata majeraha katika ajali hizi za barabarani. Siku moja nilikuwa naangalia TV nikashangaa sana, ajali ilitokea maeneo ya Mafinga, basi liligongana na lori, picha zilizopigwa zinaonyesha kabisa kwamba, tatizo lilikuwa ni *pothole* kubwa barabarani na inaonekana; alichofanya Rais kesho yake ni kutuma salamu za rambirambi bila kutoa agizo la ile *pothole* kwenda kuzibwa. Tatizo wakati mwingine siyo kulaumu madereva tu, tatizo ni aina ya miundombinu, tunajenga *disposable roads.* Barabara zinazojengwa leo kwenye hili Taifa haziwezi ikadumu miaka miwili kabla haijatoa *potholes*.

Ukienda Dar es Salaam kuna sehemu pale panaitwa eneo la *Mabatini Police Station,* karibu na kwa Mama Anna Makinda, barabara imejengwa ndani ya miezi sita haipo tena. *Disposable roads* tunazojenga, halafu kazi tunayofanya tunalaumu madereva tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Ripoti ya Waziri Mkuu kuhusu ajali za barabarani ni aibu, hakuna *solution* inayotolewa hapa. Anachosema Waziri Mkuu kwenye Hotuba yake ni kwamba, wameunda Kamati. Watu wameanza kufa toka mwaka jana Julai mpaka leo, lakini kinachofanyika tunachoambiwa hakuna *solution*, eti *solution* ni Kamati imeundwa. Watu wanaendelea kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu *basic* ambavyo havihitaji kuundia Kamati; kwa mfano, watu wanapanda mabasi rundo, hakuna *safety belts* hata moja, basi likipinduka watu wanakufa wengi kwa sababu hakuna *safety belts* kwenye mabasi. Hivi kweli unahitaji kuunda Kamati ili uweke *safety belts* kwenye mabasi? Mabasi yana *overload,* kuna rushwa barabarani, hizi ni *basic understanding* hauhitaji kuunda Kamati. Watanzania wanakufa, tunachoambia kwenye Ripoti ya Waziri Mkuu kwamba, wameunda Kamati huku watu wameshakufa 2,883 na wengine wameshapata majeraha makubwa ambayo hayawezi kusaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine waliloandikwa kwenye Ripoti ya Waziri Mkuu ni mauwaji ya *albino*. *Pathetic,* ukisoma Taarifa ya Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 13, yote hiyo ukija unateremka, hakuna *solution* inayokuwa *offered* kwa ajili ya mauaji ya *albino* pamoja na wanaouwa vikongwe katika Taifa hili. Wanachoandika pale ni *story* za kila siku, *business as usual. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema hii Serikali imechoka mnashangaa kwa nini tunayasema haya. Hii ni *evidence* kwamba, Serikali imechoka. Sisi Wapinzani tunapotaka kufanya mikutano nchi hii, kila siku tunaambiwa sababu mbalimbali na polisi, mara leo wanasema kuna sababu za kiintelijensia msifanye mkutano, mara kutatokea vurugu. Hizi sababu za kiintelijensia mnapata kwenye mikutano ya Wapinzani tu. Mauwaji ya *albino* na vikongwe hakuna taarifa za kiintelijensia mnazopata! Taarifa mnayotoa hapa ni Serikali gani hii ambayo haiwezi ikalinda wananchi wake, *albino* na vikongwe ni sehemu ya Wananchi wa Tanzania, mmeshindwa kuwalinda. *(Makofi)*

Katika Ripoti ya Waziri Mkuu anasema, watu 13 wamehukumiwa kunyongwa kwa sababu ya mauwaji ya *albino*. Hakuna hata mmoja hadi leo ambaye amekwishanyongwa; mnafanya nini? *Albino* wanauwawa kila siku, mnatupa tu *story* za kawaida, yaani Ripoti hii ni kawaida, ni *business as usual*. Tukisema mmeshindwa kazi eti mnasema tunawaonea, sasa tuseme nini? Tuwaambieni nini sasa mtakachoelewa? Hamuelewi hata tukisema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili Serikali hii wakiwakilishwa na Waziri Mkuu, wamesema mara nyingi mno, mpaka Februari kipindi tunafunga Bunge, mlituambia hapa kwamba, Kura ya Maoni itafanyika tarehe 30 *April* kama ilivyopangwa; iko wapi leo? Hata Sheria ya Kura ya Maoni imeshapitwa na wakati, kwa sababu Sheria hii ili-*stipulate* muda *within which* Kura ya Maoni ingefanywa, ambapo ikisha-*elapse,* Kura ya Maoni inakuwa *invalid* tena kisheria. Pamoja na kwamba, imeshakuwa *invalid* kisheria, Sheria hiyo haijabadilishwa tena kutoa *room* kwa ajili ya kufanya Kura ya Maoni, halafu Waziri Mkuu katika Hotuba yake, anaendelea kutoa *commitment* ya kufanya Kura ya Maoni kabla Sheria haijabadilishwa. Huu ni uhuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafanya mambo gani haya? Mnakiuka mpaka sheria, mnataka kuwa Nkurunzinza; mnafanya mambo gani haya? Leo tunawahoji hapa kuhusu *BVR, Biometric Voters Registration* inayoendelea, mnaona kama vile tunaongea ongea tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *experience*, Kenya walikuwa na *BVR Kits* 16,000, lakini iliwachukua miezi sita kusajili wapiga kura wao. *Six months with 16,000 BVR Kits*. Sisi *BVR Kits* tulizonazo mpaka leo hazifiki hata 4,000 na kampeni zinatakiwa zianze *August* tena mwanzoni. Hivi miujiza iko wapi ya ku-*register* hawa watu au mnaenda ku-*register* watu wenu tu watu wengine hamuendi kuwa-*register*?

Mnachofanya hapa ni nini? Ukimsikiliza Waziri Mkuu, anaendelea kutudanganya jinsi alivyokuwa anatudanganya kuhusu Kura za Maoni; kila siku mlikuwa mnasema kura iko pale pale na leo mmeanza kutudanganya tena hivyo hivyo, watu watakuwa *registered*, uchaguzi uko pale pale, kama mlivyokuwa mnatudanganya kwenye Kura ya Maoni. Mnafanya mambo gani haya?

What is happening? Tukiwaambia mnakuwaje na Serikali ambayo ni *so unpredictable*, yaani huwezi uka-*predict* hii Serikali, *it cannot plan?* Mnafanya mambo gani haya? Tukiwaambia mmechoka mnasema eti tunawaonea, sisi Wapinzani tunaongea ongea tu. Tumeshawashauri mno, wakati mwingine tunachoka hadi kuwashauri. *Last time* niliwaambieni hapa, ndani ya Bunge niliwahi kuwaambia kwamba, Serikali lazima tufanye kazi ya ku-*cut down cost*. Kila ikifika bajeti tunaleta Wakuu wa Mikoa hapa, wanakuja kufanya nini? *(Makofi)*

Wamejazana tu hapa wamekuja kufanya nini? Mkuu wa Mkoa anasafiri kutoka Mwanza anakuja hapa kusilikiza bajeti, akae kwenye TV aangalizie huko Mwanza, halafu chukueni makaratasi mpelekeeni akasome. Anakuja hapa kufanya nini? *(Makofi)*

Hizi ni gharama tu, halafu mnachangisha wananchi kwa nguvu kwenye ujenzi wa maabara, wakati mnasababisha gharama za ovyo ovyo tu. Mkuu wa Mkoa anakuja hapa na mafuta, *tear and wear* ya gari, anakuja na msaidizi, analipwa posho, hajibu hata maswali humu ndani kuhusu hii bajeti; anakuja kutafuta nini? *(Makofi)*

Hivi ninyi mnataka tuwashauri vipi sasa kama ni kushauri tunashauri kila siku? Nchi hii leo, mimi niko pale Nyamagana, kutoka Ziwa Viktoria kuja Jimboni kwangu, tumezungukwa na Ziwa Viktoria. Ukienda Buhongwa, kwa miaka 50 ya Uhuru hakuna maji na Ziwa Viktoria liko palepale na ninyi ndiyo mnakusanya ushuru kila… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Sugu, ajiandae Mheshimiwa Chatanda na Mheshimiwa Abdul Marombwa!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi sitawashukuru Wanambeya hapa, kwa sababu agano letu tuliwekeana kwenye ardhi ya Mbeya, kwa hiyo, nitarudi kuwashukuru kwenye ardhi ya Mbeya. Baada ya kumaliza Bunge hili, nitafanya mkutano mkubwa pale wa kuwaaga au kuwashukuru *I mean. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuungana na Mzee Mugabe, kulaani mauwaji ya Waafrika Weusi yaliyotokea *South Africa*. Watu wa *South Africa* ni wa ajabu sana, wanaua Waafrika Weusi wenzao, wameshasahau mara hii kwamba, walikuwepo katika hizi nchi zetu ikiwemo Tanzania; wakati huo tukiwa wadogo sisi tunakunywa uji wa chumvi kwenda shuleni, wao wanakunywa chai ya maziwa, wanakula mikate na siagi kwenye kambi kule Matombo na kwingine, leo hii wanaua ndugu zetu kule *South Africa,* kwa sababu tu hawataki wakae katika nchi yao wakati wao walikaa. Kwa hiyo, naungana na Mzee Mugabe kuwalaani hawa watu kwa vitendo wanavyovifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii Bajeti ya Waziri Mkuu, mimi nitasema kitu kimoja tu; punguzeni ku-*panic* CCM, Waziri Mkuu ame-*panic*, Mawaziri mme-*panic*, Wabunge wa CCM mme-*panic* hasa wale wanoko wanoko wanaozomea zomea, wame-*panic* katika kipindi hiki. Hamtakiwi ku-*panic*, kwa sababu sisi tunachofanya humu ni kuwashauri na *always* tumekuwa tunawashauri kwa *facts* na *numbers*. Ninakumbuka Wazungu wana msemo wanakwambia, *men lie, women lie, but numbers don't lie*, kama ni moja moja, kama ni mbili mbili, haipindishwi. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa tumewashauri kwa *numbers* kwamba, Kura ya Maoni *by numbers,* ukihesabu *numbers*, sheria na namba zake, haiwezekani Aprili 30, Waziri Mkuu akasimama akabisha, Rais akabisha, ninyi mkabisha, aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge lile Mzee Sitta akasimama kabisa akabisha; iko wapi Kura ya Maoni leo hii? *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tunawashauri, hatuna ugomvi na ninyi, hatuna ugomvi na rangi ya Chama chenu, tunawashauri kwa masilahi ya taifa hili, *by numbers*. Mnakaa humu ndani mnawadanganya watu, mnawaambia watu, Pinda hayupo Mheshimiwa Waziri Mkuu, iko wapi Mahakama ya Kadhi? *(Makofi)*

Inaweza ikawa vyovyote ilivyo, lakini iko wapi? Mnafika sehemu mnakuja na *solution* nyepesi ili tu kuvuka huo usiku bila kujali asubuhi kesho mtaamka na nini. Iko wapi? Sisi tunawashauri kwa nia njema kabisa, *by numbers, numbers don't lie* kwamba, hicho kitu mnachokitaka kwa *numbers* hakiwezekani, mnasimama humu mnabisha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu amewaahidi wazee pensheni ya wazee. Kamati za Bunge zimesafiri Dunia nzima; China, India, sijui wapi, kwenda Malaysia, kwenda kujifunza kuhusiana na nini kifanyike katika ku-*implement* Sheria ya Pensheni kwa wazee wetu hawa ambao wanahangaika kila siku. Waziri Mkuu kawahakikishia, juzi tukiwa kwenye Kamati, Waziri tunamwuliza watu tumeshasafiri kwa fedha za umma, fedha za wananchi, Jenista ulikuwa Mwenyekiti unajua, utajibu hili. Tumesafiri, leo hii Waziri wa Kazi na Ajira anakuja anasema hili suala bado, lakini hata hivyo litaingizwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ijayo. *Come on*

men! Hivi hamuoni hii hali, ndiyo maana ninasema msi-*panic*, ninyi mnaona kabisa uwezekano wa kuchukua nchi hamna halafu mnapanga Mipango ya nchi hii kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi cha wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Kama kuna kitu chochote ambacho hamtaweza kukifanya *between now and October, it's over. (Makofi)*

It's over, now na *October* kama hakuna kitu, ndiyo maana katika bajeti hii hutasikia mimi naomba kitu, kwa sababu itakuwa ni uongo tu. Ukiangalie ile Mipango, tumeisoma Mipango ya Waziri wa Fedha uongo! Mikakati kibao ya kuboresha sijui reli, sijui kuboresha nini, kwa mwaka mmoja mtafanya wapi; mmeshindwa miaka mitano tumo humu ndani? *(Makofi)*

Kwa miaka mitano niko humu ndani, *business as usual,* kila hotuba ni vilevile. Waziri Mkuu vilevile, Waziri sijui wa Nishani vilevile, Maliasili na Utalii vilevile. Hotuba zote kwa miaka mitano ni vilevile. Sisi tunawashauri *by numbers, numbers don't lie, men lie, women lie, numbers don't lie*! Sasa nyinyi mnataka kubishana na *numbers!*

Sasa hivi hapa tunawashauri kuhusiana na Uchaguzi wa *October by numbers,* tunawaambia *numbers* zinavyo-*calculate*, tunatoka nje ya namba, ninyi mnakaa humu mnabisha. Mnaacha kuipa Tume fedha, kuagiza magari kwa Tume, kuwapa fedha kwa ajili ya kufanya machapisho ya maandalizi, mnaagiza magari ya polisi 700, magari ya washawasha 700! Katika hayo magari 700, 500 yaleteni Mbeya kule, sisi tunajua nini tutayafanya. *(Makofi)*

Mnaandaa vita dhidi ya nani; wananchi wasio na silaha? Mtakuwa Nkurunzinza! *(Makofi)*

Haki ya Mungu nakwambia, angalia Burkinafaso, angalia Burundi, Afrika ya leo, Dunia ya leo, siyo ile, imebadilika.

Mimi nasema hivi, Oktoba ndiyo mwisho wenu, njooni na magari hata 7,000 nini 700, njooni na magari ya washawasha 7,000, hamng'oi safari hii. Oktoba mnakaa chini mnatupisha, twende tukafanye kazi kwa masilahi ya Taifa hili na siyo vinginevyo ndugu zangu. Ninyi kinawashinda kila kitu, kila kitu kinawashinda! *(Makofi)*

Mimi nawahimiza tu ndugu zangu Mbeya, maana danadana zimekuwa nyingi, mara tarehe 4 kujiandikisha, niko njiani nafika Mikumi wananipigia simu wameghairisha nageuza kuendelea na kamati. Wakasema tarehe 15, nilikuwa najiandaa kuondoka leo, leo tena napata taarifa ni tarehe 19. Sasa mtaneng'eneka mtafanya, lakini daftari litakuja na tutatoka kwa maelfu yetu kwenda kujiandikisha. Ninawaambia Wanambeya kaeni tayari, tegeni sikio, tutapitisha *PA* za kufa mtu kuwatangazia tarehe. Kwa sasa walivyotuambia ni 19, msikilizeni Mbunge ni hiyo tunaifuata, wakibadilisha tena nitawaambieni, hakuna kulala tunakesha tukisubiri kujiandikisha kwa ajili ya kuwang'oa hawa watu. *(Makofi)*

Ninyi mmeshindwa kila kitu, kama alivyosema Wenje, eti wanadai meli, watu wanadai ndege, mmeshindwa kujenga madawati ninyi? Mnashindwa kushughulikia madawati, mnashindwa hata kusikiliza mawazo ya watu wanaokuja kuwasaidia kutatua suala la madawati.

Juzi nilikuwa kwenye Maonyesho ya Elimu, nikawakuta wajasiriamali pale wabunifu wa Kitanzania, wakanipa na *brochure* yao. Wana programu yao, wao wanachotaka ni *support* tu ya Serikali, wanataka Serikali iwape *cubic meters* kama laki mbili za miti, wanunue, siyo bure,

lakini wakiwauzia hiyo *cubic meters* laki mbili za miti, wao watakuwa wanaipa Serikali madawati bure, 75,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

Madawati 75,000 bure, ambayo yangegharimu bilioni tisa. Sasa suala kama hili unashindwaje kulifanyia kazi; halihitaji fedha, halihitaji bajeti; linahitaji ku-*adapt* tu pale na pale unakuwa umesaidia wale wabunifu, umesaidia wale wajasiriamali, umesaidia wanafunzi ambao wanaenda kukalia hayo madawati na zaidi umeisaidia Benki ya *TIB* naiona hapa ambayo ndiyo wanaenda kutoa mikopo kwa wale wajasiriamali? Umesaidia vitu vinne kwa pamoja, halafu unaikalia tu *politic*, kazi hutaki kufanya; hii maana yake nini? *(Kicheko/Makofi)*

Sasa mimi nasema, dawa ipo inakuja na nitoe *big up* sana na nizidi kuwatia moyo Viongozi wa UKAWA; Profesa Lipumba, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Mbatia na Dkt, Emmanuel Makaidi, maana yake madongo yamekuwa mengi sana, eee… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mary Chatanda, ajiandae Mheshimiwa Abdul Marombwa!

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kabla sijachangia chochote, naomba niwaeleze Watanzania kwamba, mtusikilize na hatimaye muweze kutuchambua kadiri ambavyo tunajikung'uta humu ndani kama vile tumeumwa na sisimizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilimsikiliza sana mchangiaji mmoja, ndugu yangu Grace Kiwelu. Nimekaa ndani ya Bunge hili sasa ni mwaka wa tano, ninavyomjua mimi Grace Kiwelu ni binti ambaye ana nidhamu ya hali ya juu, ni mwadilifu, ni msikivu, ni mtulivu, lakini kwa jana nimemshangaa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshangaa kwa kuzungumza maneno ya uongo na uongo wa mchana jua kali linawaka, Mwenyezi Mungu huwa hasamehe hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana amelizungumza suala la ugonjwa wa Rose Kamili kwamba, Rose Kamili amelazwa nchini India kwa sababu CCM walimpiga kwenye kampeni kule Kalenga.

MHE. HALIMA J. MDEE: Taarifa.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwamba, Rose Kamili namfahamu mimi vizuri.

T A A R I F A

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako una thamani sana. Suala analolizungumza Mheshimiwa Rose Kamili amepigwa na CCM, mimi nilikuwepo kwenye Uchaguzi wa Kalenga, Rose Kamili ulemavu wake leo umesababishwa na Chama cha Mapinduzi, umesababishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa, anaitwa Jesca. Tulikuwepo Kalenga, Polisi Iringa wanajua…

MHE. HALIMA J. MDEE: Siyo anaongea ongea tu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima umeshatoa taarifa, umeshaeleweka, kaa chini. Umeshatoa taarifa, usitake mjadala.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anayezungumza hamjui vizuri Rose Kamili, mimi namjua Rose Kamili. Rose Kamili alikuwa Kiongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi kabla hajaingia CHADEMA. Kwa hiyo, mimi namjua Rose Kamili, Rose Kamili ni wifi yake na rafiki yangu.

Rose Kamili alipata ajali. Rose Kamili mimi niko naye kwenye…

MBUNGE FULANI: Watu wangapi walipata ajali!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary Chatanda subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, vumilianeni, mmesema sana, sasa wanajibu na ninyi vumilieni. *(Makofi)*

Vumilieni, naomba utulivu humu ndani, kama mtu ana taarifa nani kapigwa na nani, mtazipeleka kwa *IGP* huko siyo hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Endelea!

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa sababu wanajua ninachokisema mimi ni sahihi, ndiyo maana wanapiga kelele. Rose Kamili ni rafiki yangu sana, Rose Kamili ninaye Kamati moja. Rose Kamili kabla hajaenda kwenye uchaguzi kule Kalenga, mimi niliongea naye, kwa sababu alikuwa tayari ameshaniambia juu ya tatizo lake la bega alipokuwa amepata ajali, alikuwa anafanya utaratibu wa kwenda India kutibiwa. *(Makofi)*

Mimi nikamweleza, bwana wewe unakwenda kwenye uchaguzi unaacha kwenda India; akasema bwana tafadhali, nikiacha kwenda huko, wenzetu hawa kama mnavyowajua, mambo yataniharibikia!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassari! Waheshimiwa Wabunge, muda wetu unakwisha, hatuna taarifa, vumilia Nassari utakuwa mchangiaji wa mwanzo jioni utachangia na wewe, vumilia.

MBUNGE FULANI: Mwache aongee.

MWENYEKITI: Tulia, tulia kama nini, tulia tu.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, watulie kama wananyolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rose Kamili amerudi kutoka Kalenga mimi nimeenda kumwangalia, nikamwambia rafiki yangu siku ile nimekwambia kwa nini unaenda Kalenga unaacha kwenda India, angalia sasa umeenda wamekutonesha kidonda! Rose Kamili alikuwa amewekewa chuma cha ajali akasema kinamsumbua!

Kwa hiyo, hawa wasizungumze uongo kuwaeleza Watanzania kwamba, CCM ndiyo iliyomfanya Rose Kamili amepigwa kule, kule ameenda kutoneshwa tu kidonda, alipata ajali!

(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele kuonyesha kutoridhishwa na maelezo ya mzungumzaji)

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vibaya sana kuzungumza uongo na Mwenyezi Mungu hapendi kitu cha namna hiyo. Litawauma sana kwa sababu huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la ufisadi, jana nimemsikiliza Cecilia, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, anatokea Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Karatu ni ya CHADEMA. Mwenyekiti wa Halmashauri Karatu ni wa CHADEMA pamoja na Madiwani ni wa CHADEMA, CCM wako watatu tu, lakini kuna ufisadi uliopindikia katika Halmashauri ile ya Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo usemwao, nyani haoni kundule huona la mwenziwe. Mwenyekiti wa Halmashauri amefanya ufisadi mkubwa pale, Cecilia mwenyewe ni shahidi, leo asubuhi nimemwuliza Cecilia, hivi yule Mwenyekiti wa Halmashauri lile tatizo limeishia wapi la ufisadi alioufanya pale kwenye ile Halmashauri? Ameniambia sikiliza Dada Chatanda, yule sidhani kama safari hii atagombea, kwa sababu mambo aliyoyafanya ya ufisadi kwenye ile Halmashauri, hana nafasi ya kuweza kupita. Sasa nani fisadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu mimi Halmashauri ya Karatu ninaijua, nilikuwa Katibu wa CCM wa Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, suala la ufisadi wanalolizungumza kuizungumza CCM, nyani haoni kundule bali huona kundu la mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ikungi; Jimbo la Ikungi kwa Tundu Lissu, Tundu Lissu akisimama hapa anajikung'uta na suala la ufisadi, hakuna mtu fisadi kama Tundu Lissu kwa kutumia Mfuko wa Jimbo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi hivi karibuni nadhani watu walituona kwenye vyombo vya habari tunafanya mkutano tunawaeleza wananchi jinsi ambavyo Tundu Lissu ameufanyia ufisadi Mfuko wa Jimbo. Tumeiomba Serikali ipeleke Mkaguzi wa Hesabu za Serikali akakague ule Mfuko wa Jimbo kwa Tundu Lissu. Ninaomba hili kupitia ndani ya Bunge hili, aende akafanye ukaguzi wa Mfuko ule wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri niwaeleze wenzetu hawa, wasije wakadhani kwamba wao ni safi, siyo safi hata kidogo na wala siyo salama hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshangaa sana Wenje; Serikali, Serikali, anajikung'uta Serikali; hivi Serikali ni nani kama siyo yeye na mimi ni Serikali? Serikali ni nani, kuna dudu lipi ambalo linaonekana ndiyo Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye anaitwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya Serikali ya CCM.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa tafadhali.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hakuna taarifa. Endelea!

MHE. MARY P. CHATANDA: Msinipotezee muda.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassari, unayo nafasi jioni utachangia, unazo dakika kumi, utamjibu jioni, vumilia.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili angalau niweze kuzungumza, nilikuwa nataka kuwajibu jibu kidogo hawa watani zangu; sasa naomba angalau kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imewafanya wenzetu wachanganyikiwe, waendelee kujikung'uta hapo kwa sababu ya mambo mazuri ambayo yamo ndani ya taarifa ile. *(Kicheko)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
Kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tuvumiliane! Waheshimiwa kila pande ivumilie. Kama biashara yenu ndiyo hii, kila mtu avumilie! Mkitaka kuzungumzia maji, mtazungumzia; mkitaka vijembe, vumilianeni. Mheshimiwa Marombwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, *please* kaa chini! Mheshimiwa Marombwa!

MBUNGE FULANI: *It shouldn't be like that,* kaa chini! Bila adabu!

MBUNGE FULANI: Ana mdomo mchafu huyo!

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu na nianze kwa kuunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa *clarification* ndogo tu, wenzetu walikuwa wamezungumza mambo mengi. Mojawapo ambalo walikuwa wamezungumza ni suala zima la kule Rufiji, kwamba Maabara zinazojengwa hazitatumika kwa sababu hakuna Walimu wa Sayansi na akazitaja shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Rufiji; nataka niseme tu kwamba hakuna Wilaya iliyopata upendeleo mkubwa wa kuwa na Walimu wengi kama Wilaya ya Rufiji. Wilaya ya Rufiji tulikuwa na Walimu 431 wa Shule za Sekondari. Shule tunazo 21 tu. Lakini Serikali ikaongeza Walimu 131 mwaka huu, wameajiriwa na wapo shuleni. Jumla ya Walimu kwenye shule zetu 21 za Sekondari Wilaya ya Rufiji ni 536 ambao ni wengi sana. Hivi ninavyozungumza, hakuna hata shule moja ambayo ina Walimu chini ya 20. Haipo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana viongozi wa Idara ya Elimu Wilaya ya Rufiji. Wamefanya kazi kubwa ya kuwagawanya Walimu wa Sayansi waliofika; na hivi ninavyosema, hakuna hata shule moja katika Wilaya ya Rufiji ambayo haina Walimu wa Sayansi. Hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ni zuri, Walimu wanafanya kazi kubwa sana. Nimekwenda katika baadhi ya shule katika Jimbo langu, nimeona wanafunzi wanapata *distinction* ya 4.5 na 4.6. Walimu hawa wanafanya kazi kubwa na matokeo yao ni mazuri. Mkoa wa Pwani kwa mara ya kwanza kwa kupitia shule hizi ambazo wenzetu walikuwa wanazicheka, za yebo yebo, wametoka wanafunzi zamani tulikuwa tunasema wana *point* saba. Ana 'A' zote, kutoka Shule za Sekondari hizi za Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipopitia kwenye shule zangu, kwenye shule ya Sekondari unaona kabisa kwamba mwelekeo wa shule hizi ni mzuri, kwa sababu watoto wanaopata *merit, distinction* na *credit* ni wengi sana, zaidi ya nusu!

Sasa nilikuwa nataka nitoe changamoto kwa Serikali, kwamba wanafunzi sasa hivi wengi kwenye Shule za Kata wanafaulu kutokana na wingi wa Walimu waliokuwepo. Walimu wetu wanafanya kazi kubwa sana! Katika Wilaya ya Rufiji tumenunua *mobile lab.* nyingi kupeleka kwenye shule zetu za sekondari ili waweze kufanya *practices* za masomo ya sayansi. Tumenunua hizo *lab.* nyingi ilimradi waweze kufanya masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba, ni lazima Serikali tufunguke sasa kwamba ufaulu wa wanafunzi kwenda *A' level* utakuwa ni mkubwa sana. Zile Shule za Sekondari za *A' level* ambazo zilitakiwa zianze kila Wilaya, tuziimarishe ili watoto hao wasikose nafasi ya kwenda kusoma *A' level.* Hilo ndilo ombi langu kubwa sana!

La pili, katika eneo hili, nilitaka niiombe Serikali kwamba kwa sasa wamezingatia sana Elimu ya Sekondari, Elimu ya Msingi imesahauliwa. Elimu ya Msingi imesahauliwa, kwa sababu unakwenda kwenye Shule za Sekondari, nyingi zimekamilika; zina maabara, zina madawati ya kutosha; zina Walimu wengi sana! Lakini ukienda kwenye Shule za Msingi, Walimu wako wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezunguka kwenye shule zangu nyingi katika Jimbo langu, nami sifanyi Mkutano bila kwenda shuleni. Nimeona kwamba unakwenda kwenye Shule ya Msingi, ina Walimu wawili, watatu. Hili ni tatizo! Kwa sababu Walimu wengi walioajiriwa mwaka 1979, mwaka 1980, mwaka 1981 wengi ni wazee, wamestaafu. Kwa hiyo, zile Wilaya sasa hivi zime-*paralyze*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Serikali iongeze jitihada kubwa sana katika kuwaongeza Walimu wa *primary* kuliko wa sekondari kwa sababu wa sekondari wapo wengi na wengine ni wa ziada, lakini wa *primary* tuna upungufu mkubwa sana. Hilo ndilo ombi langu kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sisi kwenye Wilaya ya Rufiji tuna Majimbo mawili; kuna Jimbo la Kibiti na Jimbo la Rufiji. Wilaya hii ina ukubwa wa *square kilometer* zaidi ya 13,000. Kwa bahati mbaya sana tuliomba mgawanyo wa Wilaya. Tunaishukuru Serikali kwamba tumeshapata mji mdogo pale Kibiti, lakini umimchukua mtu anayetoka Nyamisati tu, anapotaka kwenda Makao Makuu ya Wilaya, inabidi atembee kilometa zaidi ya 400, kwenda na kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayetoka kule Delta anatembea zaidi ya kilometa 450 au 470 kufuata huduma. Akienda huko hatorudi siku hiyo, lazima alale arudi siku ya pili yake. Mimi

nilikuwa naomba Serikali, yale maombi yetu ya kutaka kuigawanya Wilaya ya Rufiji ili tuwe na Wilaya Mpya ya Kibiti, naomba sana Serikali, maombi hayo tayari tumeshayapitisha katika ngazi zote, tunakuomba Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais na mwenye mamlaka ya mwisho, mtufikirie ombi letu la kuifanya Kibiti kuwa Wilaya. Kinyume cha hivyo, mtatutesa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi ninapotaka kwenda Makao Makuu ya Wilaya inabidi nitembee kilometa 200. Kilometa100 niende, 100 kurudi kutoka Kibiti kwenda Utete. Sasa kwa kweli hebu mtufikirie hili, ilimradi nasi tuweze kupunguza hii adhabu ya usafiri ya kwenda kufuata huduma pale Makao Makuu ya Wilaya.

Lingine ambalo nataka kuiomba Serikali, kuna Walimu wameajiriwa mwaka huu zaidi ya 32,000. Walimu hawa kwa bahati mbaya sana hawajapata posho! Mpaka hivi leo Walimu hawa hawajapata posho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa katika maeneo hayo, hakuna wakati mgumu ambao Mkurugenzi na Afisa Elimu na Wasaidizi wake wanaopata ugumu kama wanapokwenda Walimu wapya. Walimu hao wanatoka katika mikoa tofauti; wanatoka Kagera, Mwanza wanapelekwa Rufiji, wanapelekwa Arusha na maeneo mengine. Wanapokwenda kule, wanategemea kupata zile posho zao. Lakini toka walivyokwenda mpaka hivi leo posho hakuna, ingawa Serikali iliahidi posho hizo zipo, lakini mpaka leo hawajapata!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, wahurumieni wale Walimu; Maafisa Elimu wanapata taabu. Walimu wanafikia hatua ya kuwaambia wale viongozi wa Wilaya kwamba jamani sisi mnataka tufanye nini ili tuweze kujikimu, kupata hela za kula? Tujiuze? Wanafikia hatua hiyo! Naiomba sana Serikali, hao Walimu hebu kabla ya kuajiriwa, wapelekewe zile pesa zao ili wakienda kule wasirudi. Hilo naomba sana, Walimu wetu wanateseka.

Lingine, niishukuru sana Serikali; Wilaya ya Rufiji tumependelewa sana, tuna mambo mengi ambayo yamefanyika katika kipindi hiki cha miaka mitano. Katika zahanati, wananchi wamejenga nyingi; Vituo vya Afya, tumevijenga vingi; kwenye barabara, zipo nyingi; mawasiliano yameongezeka; Shule za Sekondari, umeme, maji; lakini tuna tatizo kubwa la upande wa Delta. Delta siyo eneo dogo kama ninavyozungumza siku zote, ni eneo kubwa, lina vijiji zaidi 20 kule, kuna Shule za Msingi, kuna Shule za Sekondari na Vituo vya Afya

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, hutaweza kupeleka gridi ya Taifa; huwezi kupeleka vitu vingine. Huduma tulizokuwanazo kule, ni mbili tu; huduma ya shule pamoja na zahanati, hakuna huduma nyingine zozote. Hivi, kuna ugumu gani Ofisi ya Waziri Mkuu ikaunda Tume kwa kila Idara, wakaenda Delta kuchunguza ni namna gani Idara ya Elimu itakavyofanya; namna gani Idara ya Maji itakavyofanya; ni namna gani Wizara pengine ya Ujenzi itakavyofanya ili kuwasaidia wale wananchi wa Rufiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mnashindwa kuunda hiyo Tume ya Kuratibu kwenda kuona hali ya kule ilivyo? Mahali wanapokaa watu zaidi 45,000 siyo mahali padogo! Ni pakubwa! Siyo Kisiwa kimoja, kuna Visiwa zaidi ya 40, lakini vijiji viko karibu 20. Naomba sana wenzangu, Serikali iangalie namna ya kuunda timu itakayokwenda kule kwa Idara zote za Serikali kuona itasaidia namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishafika Mbwera, anajua vizuri sana. Vile vile Mheshimiwa Majaliwa anajua vizuri zaidi kwa sababu alishakuwa Mkuu wa Wilaya ya Rufiji na huko ameshakwenda. Mnapata kigugumizi gani katika kuwasaidia huduma za jamii wale watu wa Delta? Naiomba sana Serikali ijitahidi kwa hilo ili pengine tunapoingia katika

kipindi kinachokuja, eneo hili nalo liweze kupata huduma nzuri kama wanavyopata huduma maeneo mengine. *(Makofi)*

La mwisho, ni madeni ya watumishi. Watumishi wetu wana madeni sana! Tulikuwa tunakagua Sekretarieti za Mkoa; mimi niko kwenye Kamati ya *PAC*, unashangaa mkoa nao una madai mengi. Kumbe madai haya hayapo kwa Walimu peke yao, hata watumishi wa Sekretarieti za Mikoa nao wana madai yao na watumishi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijitahidi kulipa madeni haya ili watumishi hawa wawe safi, Serikali iwe safi na tusiweze kuongeza madeni mengine nchi hii iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nashukuru sana, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Martha Umbulla!

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kufanya kazi zangu kwa ufanisi kwa muda huu wote na kunipa afya njema kusimama mahali hapa jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa naomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunipa fursa ya kuwa Mkuu wa Wilaya kwa miaka mitatu kasoro. Hakika kazi ile imeniimarisha, imenijenga na imeweza kunifanikisha kisiasa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba hii na pia kwa kazi kubwa anayoifanya kuisimamia Serikali na kuleta mafanikio makubwa ndani ya Chama cha Mapinduzi kulingana na hotuba yake hii iliyosheheni taarifa na takwimu linganishi ambazo zinaonesha dira ya mafanikio makubwa ya chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Manyara na wananchi wetu wote wa Mkoa wetu kwa kunivumilia na kuweza kunipa ushirikiano na kuonyesha imani kubwa kwangu. Naomba tuendelee kushirikiana kuendeleza mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii au hotuba hii ya Waziri Mkuu imesheheni takwimu linganishi. Tunaielewa kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilipotutoa mwaka 2005, inaonyesha tuko wapi leo mwaka 2015 na kwa takwimu hizi tunajua kwamba miaka mingi ijayo mbele yetu tutakuwa wapi. Kwa hiyo, nashangaa wenzetu wa upinzani wanavyosema kwamba Serikali haina dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dira tosha kuonyesha mafanikio makubwa ya Chama chetu; tulikotoka, tulipo sasa na tunakokwenda katika sekta zote na kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya awamu ya nne kwa mafanikio makubwa. Hongera sana! Mwenye macho haambiwi tazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hii ukurasa wa 65, naomba nichangie kwenye Sekta ya Elimu. Mafanikio makubwa yaliyoonekana kwenye Sekta ya Elimu yameletwa na mambo makubwa matatu; Kwanza Mpango Madhubuti wa Elimu ya Msingi, lakini pia Mpango Madhubuti wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Sekondari na Vyuo vya Juu; na mwisho, kuingiza Sekta ya Elimu katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na Elimu ya Msingi, bali nina hoja na ushauri kwa Serikali kwa Elimu ya Juu na hasa suala zima la *BRN*.

Katika Sekta ya Elimu ya Msingi hatua kubwa imeonekana kwa kweli. Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 43 ni hatua kubwa sana ya mfano, na kwa hiyo, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile zaidi ya pongezi kwa Elimu ya Juu, ongezeko kubwa la wanafunzi wanaohitimu Vyuo Vikuu, ongezeko kubwa la vyumba vya madarasa, wahitimu na kadhalika, tukiacha upeo wa uelewa, bado hii ina-*reflect* nini katika maisha ya wananchi wetu walio masikini na ambao hali yao ni duni? Inatuonesha kwamba bado elimu yetu ama vyuo vyetu tunavyozalisha, au wanaohitimu, bado hatujawatayarisha ili waweze kujiajiri.

Kwa hiyo, natoa ushauri kwa Serikali kwamba pamoja na mipango mizuri na hatua kubwa tuliyopiga, laini tuendelee sasa kuwajenga wahitimu wetu kisaikolojia kwamba waweze kujiajiri kwa sababu haitakaa itokee huko mbele tunakokwenda kwamba ajira itatoka kwenye sifuri kwenda mbili au tatu, bali inaendelea kudidimia kwa sababu ajira siyo janga tu la Kitaifa, ni la Kimataifa na la dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka kujenga mipango yetu katika misingi ya kuwajengea vijana wetu waweze kujiajiri, hata wanapohitimu zaidi ya elimu ya upeo wa uelewa, basi waweze kujikwamua kimaisha wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie matatizo yanayoukabili mkoa wetu. Nizungumzie suala zima la mawasiliano. Kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa kuwa maeneo mengi ya Mkoa wetu wa Manyara umepata umeme, Serikali imesambaza umeme kila mahali, lakini bado tuna tatizo kubwa la mawasiliano. Maeneo ya Tarafa nyingi za Wilaya ya Mbulu, Wilaya ya Kiteto, Simanjiro, hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na takwimu nzuri zinazoonekana katika vitabu, sisi mikoa ya pembezoni kama Mkoa wangu wa Manyara tuna tatizo hilo kubwa la mawasiliano, hususan maeneo ya Endamilai, Dinamu, Kata ya Nambis, Murai na maeneo yote haya. Ni maeneo mengi sana ya Wilaya ya Mbulu, Wilaya zote nilizotaja. Kwa hiyo, tuna tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maendeleo ya nchi yetu, ni pamoja na mawasiliano. Kwa sababu maeneo mengi ya nchi yetu yamepata mawasiliano, nasi tuweze kufikiriwa katika kupatiwa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti tuna tatizo kubwa sana la maji, hii inatokana na kutokamilika kwa miradi mingi ya *World Bank*. Kwa mfano, katika Kata ya Haydom, mahali ambapo tuna hospitali kubwa inayosaidia mikoa zaidi ya Manyara; Mkoa wa Singida, Arusha hata Mkoa wa Mara; lakini tuna tatizo kubwa la maji.

Naomba bajeti ya mwaka huu iweze kufikiria ni namna gani tunaweza tukawasaidia wananchi wa eneo hilo na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba alione hilo kwa jicho la huruma iweze kusaidia katika kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na takwimu linganishi kuhusu watumishi wa afya, lakini tunasikitika katika Mkoa wetu wa Manyara bado tuna upungufu mkubwa sana wa wahudumu wa afya katika zahanati zetu na Vituo vya Afya. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, nimejaribu kumweleza sana tatizo tulilonalo katika zahanati zetu na amekubali kutembelea katika Mkoa wetu mwezi huu wa Tano. Naamini hatavunja ziara hiyo ili ajionee mwenyewe. Kuna tatizo kubwa la wahudumu wa afya na matatizo mengi yanayoikabili Sekta hiyo ya Afya katika mkoa wetu hususan Zahanati ya Dongobash, Hospitali ya Wilaya ya Mbulu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pia katika takwimu hizi linganishi…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mbona dakika zangu hizo…

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na wachangiaji wa mchana wote wamekwisha.

Nina tangazo kutoka kwa Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, Ndugu John Joel, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa vitabu vya bajeti *Volume II*, Makadirio ya Wizara na Taasisi za Serikali na *Volume IV,* Makadirio ya Maendeleo vipo tayari na Waheshimiwa Wabunge wote wataanza kupewa hivi sasa. Aidha, vitabu vya *Volume I,* Makadirio ya Mapato na *Volume III,* Makadirio ya Mikoa vipo katika hatua ya mwisho ya maandalizi ya kuletwa hapa Bungeni, na Waheshimiwa Wabunge watapewa mara vitakapofika.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tuna nafasi 24. Mpaka sasa hivi nafasi za Vyama vyote ni 11 tu. Kwa hiyo, natoa wito kwa Vyama waendelee kuleta majina; tuna nafasi nyingi sana za kuchangia na nafasi zilizopungua hapa ni kama 13. Kwa hiyo, vyama vyote vinavyohusika na kuchangia, naomba walete majina mapema ili Kiti kiweze kuwapa nafasi ya Vyama hivyo.

Mchangiaji wetu wa kwanza jioni atakuwa Mheshimiwa Nassari, atafuatiwa na Mheshimiwa Suzan Kiwanga na Mheshimiwa Zainab Vullu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 8.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wakati naangalia utaratibu wangu hapa, naomba Mheshimiwa Nassari atuanzishie jioni ya leo. Mheshimiwa Nassari!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nikukaribishe kwenye Bunge hili, tumeku-*miss* sana ni muda mrefu hatujakuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kunukuu Maandiko Matakatifu. Biblia kwenye Kitabu cha Ufunuo inasema, "Mwenye masikio na alisikie neno hili ambalo Roho wa Bwana anayaambia Makanisa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nami narudia ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba mwenye masikio na asikie maneno haya ambayo sisi Wapinzani tunaolipenda Taifa letu tunaiambia Serikali iliyopo madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana, tumejadili hotuba ya Waziri Mkuu kwenye Bunge hili na kwa bahati mbaya tunaposema ukweli tunaonekana wabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Wapinzani na hatuwezi kukataa kwamba sisi ni Wapinzani, lakini moja ya siri ambayo ni vema wenzetu wa Chama cha Mapinduzi wakaitambua na kwa bahati mbaya nasikitika kwa sababu Serikali leo haipo, Bunge zima hili naona wapo Mawaziri wawili; Waziri mmoja na Naibu Waziri mmoja peke yake. Nafikiri hii ni dalili nzuri kwamba wapo tayari kuiachia UKAWA Serikali ya nchi hii tarehe 25/10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isiyokuwa sikivu, Serikali iliyochoka; na tunaposema Serikali ya Chama cha Mapinduzi imechoka, hatuwasingizii. Ninyi ni ndugu zetu, ni wajomba zetu, tunawapenda, ni Watanzania wenzetu, lakini kwenye ukweli ni lazima tuuzungumze ukweli kama Watanzania. *(Makofi)*

Serikali iliyochoka dalili zake ni zipi? Serikali iliyochoka ni Serikali isiyokuwa na vipaumbele kwenye Taifa lake; Serikali iliyochoka ni Serikali ambayo leo ukiangalia aina ya Mawaziri na Watendaji tulionao, ni dalili tosha kwamba Serikali hii imechoka. Aina ya Mawaziri tulionao ni aina ya Mawaziri ambao wangekuwa Korea Kaskazini. Juzi kutoka jana Waziri wa Ulinzi wa Korea Kaskazini amepigwa risasi mbele ya Rais na mbele ya wananchi kwa sababu moja tu, kasinzia kwenye Mkutano, Rais akilihutubia Taifa ikaonekana ni dharau kwa Taifa na kwa wananchi. Amepigwa risasi, ameuawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungelikuwa leo ni Korea Kaskazini, aina ya Mawaziri tulionao leo, Serikali inajadili Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri waliopo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu wapo wengi, lakini wapo hotelini wamelala, halafu Wabunge tunachangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu mwenyewe hayupo, sijui tunazungumza na nani, Waheshimiwa Wabunge tuliopo humu ndani, wa Upinzani ndio tunaongoza. Waziri ni mmoja na Naibu Waziri ni mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aina au dalili za Serikali iliyochoka ni Serikali yenye Mawaziri kama hawa akina Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, ambao kazi yao leo; Waziri wa Maliasili na Utalii kazi yake ni kupiga picha na mbwa wa Wazungu; kazi yake ni kupiga picha ameshika risasi; kazi yake ni kupiga picha na *helicopter*; kazi yake ni kwenda na Mamiss Marekani kupiga nao picha, akina Aunt Ezekiel; kazi yake ni kupiga picha amembeba Askari kamshika makalio, kamshika bega; Waziri! Unamshika Askari wa Wanyamapori kwa *style* ile! Mimi ningekuwa Rais wa nchi hii, tungekuwa tunazungumza habari nyingine leo. Subirini tu Oktoba inakuja, nimwambie Dkt. Slaa anipe Uwaziri wa Mambo ya Ndani kwa wiki mbili tu halafu baada ya hapo aniachie, awape watu wengine, tuwafundishe adabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili ya Serikali iliyochoka ni Serikali ambayo inapingana na Bunge lake yenyewe. Ndani ya Bunge hili tumepitisha maazimio, kwenye *Operation Tokomeza*, wananchi wameuawa, nyumba zao zimechomwa moto, Ng'ombe wameuawa, wananchi wamefilisiwa, wameteswa; na wengine wamebakwa mpaka Kiongozi wa Serikali, Diwani! Baada ya miezi michache, anakuja Katibu Mkuu Kiongozi, anawasafisha, anasema hawa ni watu safi. Halafu anaulizwa, vipi? Kwa sababu taarifa ya Tume imeonyesha kwamba wananchi wamepitia mateso, wamenyanyaswa, wameteswa, wameuawa, wamechomewa nyumba moto, ng'ombe wao wameuawa, hawana mbele wala nyuma, wamewekwa ndani na wengine wamenyang'anywa mpaka biashara zao za mbao, lakini Katibu Mkuu Kiongozi anasema, hao tutawafikiria kuhusu fidia. Wewe Sefue wewe, hii ni nchi ya mama yako? Halafu Rais naye anaangalia tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaishia hapo! Serikali iliyochoka, ni kama Serikali hii ambayo Bunge linapitisha maazimio ya *Escrow* Mawaziri wakiwa sehemu yake wamechangia akina Simbachawene hapa, baada ya miezi michache, leo wanasafishwa, wanaambiwa ni watu safi na mambo yanaendelea, *business as usual! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dalili ya Serikali iliyochoka, ni dalili ambayo imeua viwanda kwenye nchi. Tunaongea habari ya ajira kwa vijana, hakuna ajira! Vijana wapo mtaani hawana mbele wala nyuma, wanakunywa pombe chafu kwa sababu wamekosa mwelekeo wa nchi. Halafu leo hii tunawaambia Serikali imechoka, mnakataa! Serikali iliyochoka ni iliyoua viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeua Kiwanda cha Urafiki, *Sunguratex, Kilitex, Tabora Textiles, Mwanza Textile Mills, Mbeya Textile*, *Tanganyika Packers* iliyokuwa inafunga nyama, Kiwanda cha Magunia Moshi na Morogoro, Kiwanda cha Ngozi Morogoro, Kiwanda cha Maziwa, *Tanzania Diaries*, Kiwanda cha Ubungo *Spinning Mills*, *General Tyre* Arusha na mmeua pia kiwanda cha Zana za Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere aliacha nchi hii ina viwanda 11 vya kubangua Korosho, leo vipo viwili. Mwalimu Nyerere ameiacha nchi hii na Shirika la Ndege lina Ndege zaidi ya 10. Leo kuna ndege kutoka Uholanzi imekodishwa. Serikali iliyochoka mtawapaje vijana ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angalieni China; ili uwape watu ajira ni lazima ufanye *industrialization*, sisi tunaua viwanda. Tunawaambia Serikali imechoka, mnatuambia, hapana, mnaisema vibaya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikilizeni ndugu zangu, unajua sisi wote ni Watanzania, nami ni Mtanzania; mnapoiharibu nchi, hata mimi naumia. Wadogo zangu, ndugu zangu na wengine tunaumia wote. Sisi wote ni Watanzania, lakini mnapoharibu mambo, wote tunaharibikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wapinzani wa nchi hii msije mkatuona ni maadui. Mpinzani wa nchi hii ili Serikali ifanye kitu kizuri, inamhitaji mpinzani mzuri. Mpinzani ni kama kioo. Kioo kikiwa kimepasuka, utavaa nguo vibaya kama alivyovaa vibaya Mheshimiwa Wasira, hutajiona ukoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaisaidia nchi hamwelewi, badala yake tuna Mawaziri kama akina Mheshimiwa Nyalandu, wanazurura tu. Nchi inapigana na wizi wa meno ya tembo, yeye anaambatana na watu ambao wanaandikwa kwenye mitandao ya kijamii kwamba ni wezi wa meno ya tembo kwenye nchi hii na wengine watuhumiwa watarajiwa wanawaleta kutafuta Ubunge kwa ajili ya kutafuta *security*.

Mheshimiwa Naibu Spik, namwambia Mheshimiwa Nyalandu na rafiki yake mmoja kule Arumeru anaitwa John, ambaye anataka Ubunge, mwambieni Mkapa na *crew* nzima ya CCM walimshindwa Dogojanja, Arumeru. Yeye na pesa yake ya meno ya tembo akae sana akisubiria. Hii nchi mwezi wa 11 ni nchi ya UKAWA siku tano tu baada ya mwezi wa 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza kwenye Bunge hili, tunapopiga kelele siyo kwamba tunaichukia Tanzania. Tunapoongea habari ya maandalizi ya uchaguzi, angalieni yanayotokea Burundi leo. Ingekuwa nchi hii viongozi wanafanya *performance* nzuri, hata mngetaka kujiongezea muda, tungekuwa wapole, tungetulia. Lakini hakika nawaambieni, kama mna mpango wa kujiongezea muda kwenye utawala kwa Serikali hii legevu iliyochoka ambayo haijui mbele wala nyuma, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawaambia *statement* moja tu, *what is happening in Burundi today, serves as a warning to CCM in Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge nimeagiza *Ambulance* kwa mfano mwezi wa Pili, nimezilipia pesa zimeingia, nimeongea na Waziri wa Fedha Dar es Salaam nimemfuata, *Ambulance* mbili kwa pesa yangu ya mfukoni, zinaingia nchini miezi minne baadaye nahangaika, eti kupewa tu msamaha wa kodi inakuwa ni tatizo. Kwa nini? Ni Mbunge wa Upinzani! Zipo Holili zimekaa pale!

Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia kitu kimoja; mnipe *exemption,* msinipe, nitauza gari yangu ya Ubunge, Jumatatu nitazilipia ziingie zikawasaidie wananchi wa Arumeru Mashariki. Lakini tusije tukawaona mwezi wa 10 mnakuja Arumeru kutafuta kura wakati mmewanyima magari yao ambayo Mbunge amewaagizia kwa pesa ya mfukoni, badala yake mnaingiza magari ya Polisi na magari ya washawasha. Hii nchi hospitali hazina dawa, mnaingiza magari ya Polisi. Hii nchi hakuna mgari ya wagonjwa, mnaingiza magari ya washawasha, hii nchi wananchi wamechoka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa muda huu, lakini ni vyema tu nikawajulisha Watanzania kwamba wajiandae kwa Serikali mpya mwezi wa Kumi tarehe 25 inayotokana na UKAWA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Nassari. Naomba sasa Mheshimiwa Teu afuatie na Mheshimiwa Susan Kiwanda atafuata baada ya Mheshimiwa Teu.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii nami nichangie kidogo bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda ifahamike kwamba unapoomba *exemption* ya gari ambayo labda ni *Ambulance,* halafu hiyo gari ilikuwa itumike kwa ajili ya Hospitali au Halmashauri, lakini kama hujalisajili kwa jina la Halmashauri, huwezi kupata *exemption* hiyo wewe binafsi.

TAARIFA

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa kidogo ili tuweke sawa.

NAIBU SPIKA: Taarifa, Mheshimiwa Nassari!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Gregory Teu kwamba mimi ni Mbunge ambaye nimetoka shule Chuo Kikuu juzi.

NAIBU SPIKA: Naomba uongee na Kiti!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Naomba nimpe taarifa tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Watanzania tu wameona kwamba nina ubongo wa aina gani, mpaka Marais wa nje, akina Obama wameniona, wameniita mwaka jana kwao. Nimeagiza magari kwa pesa yangu binafsi, lakini kwenye kuomba, *exemption* nimeitumia Serikali. Mkuu wa Wilaya ya Arumeru ameandika barua mbili; *form* za 224 za *TRA* zimesainiwa na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru Dkt. Msuya; Nimekwenda *TRA* nimekula kiapo *(affidavit)* kwa Mwanasheria kwamba magari haya yanakwenda kutumika Halmashauri, yaandikwe namba za Serikali, yasiandikwe jina langu, lakini baada ya hapo, bado naendelea kuzungushwa kwa miezi mitatu mfululizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, taratibu zote nimezifanya, *form* za *224* nimezijaza, barua ya Mkuu wa Wilaya imeandikwa, Mkuu wa...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.
MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nimalize *to clear the air.*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, taarifa inakuwa ni fupi.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Baada ya hapo, bado Mbunge anaendelea kuzungushwa. Kama mnafanya hivi kwa mti mbichi, inakuwaje kwa mti mkavu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tumekuelewa Mheshimiwa! Mheshimiwa Teu, naomba uendelee na mambo mengine.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa maelezo hayo, nilitaka tu nitoe hilo angalizo. Kama atakuwa ametimiza hayo hote, basi ni bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwanza kwa kunipa uhai mpaka leo nami nichangie bajeti hii. Napenda kusema kwamba bajeti ya Waziri Mkuu ni bajeti yenye kiwango kikubwa sana. Nampongeza sana kwa bajeti ambayo kwa kweli hata ukiiangalia, pamoja na majedwali ambayo yameambatana na hotuba yake, yana kiwango cha juu sana kwa sababu yana tarakimu kwa maana ya *figures* ambazo ni za uhakika kabisa ukilinganisha na bajeti ya upande wa pili ambayo nayo ukii-*compare* na hii ni vitu viwili tofauti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu nilitegemea sana kwamba bajeti hii ya upande wa pili ya Upinzani ingekuwa ni bajeti mbadala. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia hotuba ya upande wa pili ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ukurasa wa nne anaposema, "mwaka wa tumaini jipya." Anasema, "huu ni mwaka ambao nchi yetu itafanya Uchaguzi Mkuu wa kihistoria ambao utakitoa Chama ambacho kimekuwa madarakani kwa zaidi ya miaka 50 na hivyo kujikuta kimechoka na kukosa mawazo mapya ya kisasa ya kuendesha na kuendeleza nchi yetu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama una mawazo haya mapya lakini huna bajeti mbadala, unategemea kwamba utatawala, au utakwenda Ikulu, utatetekeleza bajeti ipi? Hata mwenyewe imekushinda kuandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu hii inaonyesha kwamba bado hamjaiva, bado wabichi. Kama bado wabichi, iko kauli inayosema hivi, "mbao nzuri ni ile ambayo imekauka." Mbao ikiwa mbichi ni lazima ikaushwe; na unaweza kuiweka sakafuni halafu juu ya mbao mbichi, ukaweka mawe kuinyoosha. Kwa hiyo, nafikiri ubichi au kutokomaa huku kunahitaji kunyooshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kusema tu kwamba mimi binafsi naipongeza sana Serikali yangu na Chama changu kwa kazi nzuri ya maendeleo ambayo wameifanya katika Jimbo langu la Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi hizo hasa kwa maeneo mbalimbali ambayo Serikali imejitahidi sana, nikianza na barabara ya kiwango cha lami inayoanzia eneo la Mbande inakwenda *Kongwa Junction* hadi Mpwapwa. Barabara hiyo inajengwa kwa awamu ya kwanza na lami hiyo imeshaanza pande zote mbili; Kongwa pamoja na Mpwapwa ikiungana

pamoja. Kazi hiyo inafanywa na Serikali yangu, kwa hiyo, naipongeza sana. Hivi ninavyoongea kazi hiyo inaendelea, naishukuru sana Serikali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilikuwa ni sugu sana ni upande wa mawasiliano ambapo kule Mpwapwa kulikuwa na maeneo mawili sugu sana ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamengoja kwa muda mrefu sana, mawasiliano hayakuwepo na wenyewe walikuwa tayari wana simu zao lakini walikuwa hawawezi kupata mawasiliano ya karibu. Maeneo hayo ni Kata ya Mima na Kata ya Matomondo. Hivi sasa ninavyoongea, Kampuni ya Simu ya *Viatel* imehamia Mpwapwa na inafanya kazi hii chini ya Serikali na Chama changu. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Vilevile napenda niseme kwa upande wa Umeme wa *REA* na Umeme wa *TANESCO*; sasa hivi nikiongea, maeneo mengi ambayo yalikuwa hayapati umeme wa vijijini chini ya utaratibu wa *REA,* sasa hivi maeneo hayo yamepata umeme na yanaendelea kupata umeme, hivi sasa ninavyoongea. Kwa hiyo, sehemu zile ndogo ndogo kama Kata ya Lupeta, maeneo kama ya Mazae, pale Mpwapwa Mjini, bado yanaendelea kupata utaratibu wa umeme na kazi inaendelea chini ya utaratibu wa *REA* na Umeme wa *TANESCO* wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kusema kuhusu chakula cha njaa. Kama unavyofahamu kwamba mwaka huu hali ya hewa imekuwa siyo nzuri, mvua haikuwa nzuri na maeneo mengi ya Jimbo la Mpwapwa na Kibakwe ambayo ni sehemu ya Jimbo la Wilaya ya yamekumbwa na uhaba kama ilivyo katika maeneo mengine katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ambaye sasa hivi ni mgeni, amekuja kwetu badala ya *DC* aliyekuwepo zamani, Ndugu Kangoye ambaye amehamia Wilaya ya Arusha Mjini. Huyu *DC* mgeni, Mama Dkt. Jasmine, anafanya kazi nzuri sana na ameanza vizuri sana. Kazi ya kwanza ambayo tumeahidiana kwamba aiangalie sana ni kuhusu tatizo la njaa. Sasa hivi tayari ameshaleta maombi kwa Ofisi ya Waziri ili tuangalie namna ambavyo wananchi watasaidiwa, wale ambao wamejitahidi kulima lakini hali ya hewa haikuwaruhusu kupata chakula cha mwaka huu.

Kwa hiyo, ni mategemeo yangu, nimeshaongea na Ofisi ya Waziri Mkuu, dada yangu Mheshimiwa Waziri, Mama Jenista Mhagama, amelielewa hili na amesititiza kwamba maombi yatakapowasili, msaada huo utapatikana. Naishukuru sana Serikali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusu mikopo ya vijana. Mikopo ya vijana kwa eneo la Mpwapwa tulikuwa tunategemea sana kwamba makundi yote ya vijana yapatayo 82 ambayo yalijiandikisha ili kupata mikopo, kwa bahati mbaya sana hayakupata mikopo kwa wakati huu lakini nategemea sana kwa bajeti inayokuja sasa makundi hayo yataweza kupata mikopo. Ni kundi moja tu ambalo lilipata mkopo.

Kwa hiyo, haya mengine nategemea kwamba bajeti ambayo tunaiandaa sasa hivi inaweza ikaangalia namna ya kuwakopesha vijana mikopo hii, ikizingatiwa kwamba ile 5% ya vijana, 5% ya akina mama na 10% inayotokana na mapato ya Serikali ya Halmashauri, ingesaidia vijana.

Kama hii nayo haipatikani na ile ambayo ilikuwa imeamuliwa kwamba Wizara ilitengewa Shilingi bilioni sita ili kuendeleza mikopo ya vijana, nayo haikutokea. Lakini ni mategemeo yangu kwamba bajeti hii ambayo tunaiombea, itasaidia vijana ili wapate mikopo ya kujikimu na kujikwamua na hali ya uchumi inayoendelea kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kuhusu bajeti. Mchango wangu mkubwa ambao nilitaka niuseme ni kwamba tatizo kubwa la bajeti hii ni kucheleweshwa upatikanaji wa pesa kwa ajili ya matumizi kwa Halmashauri pamoja na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida nyingine kubwa kabisa ni utekelezaji wa bajeti yenyewe. Utekelezaji wa bajeti yenyewe kusema kweli hata kama fedha itatokea, bado unahitaji msaada mkubwa sana. Nalipongeza Bunge hili kwa kuunda Kamati ya Bajeti ambayo itasimamia nidhamu ya matumizi kutokana na bajeti hii. Nategemea kwamba Kamati ya Bunge ya Bajeti itaweza kusimamia vizuri matumizi ya fedha hizi kuanzia mwaka huu kwa kadri itakavyoendelea kukomaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimetoa ushauri hapo nyuma kwa Mheshimiwa Rais na aliupokea ushauri wangu huu wa kuweza kutoa bajeti kwa miezi mitatu, mitatu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Teu.

MHE. GREGORY G. TEU: Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Gregory Teu, Mbunge wa Mpwapwa. nakushukuru sana jirani yangu.

Sasa kama nilivyoahidi mwanzo, ni zamu ya Mheshimiwa Susan Kiwanga, na baada yake ni Mheshimiwa Zaynab Vullu, ajiandae.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami pia nipate kuchangia kwenye hii Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kusema naishukuru Serikali, ndiyo wajibu wake. Iliomba ridhaa ya Watanzania, iwaongoze kwa muda wa miaka mitano, kwa hiyo, tukawaamini. Raslimali zote tulizopewa na Mwenyezi Mungu nchini Tanzania wao ndio wanazimiliki, wakusanye kodi walete maendeleo kwa Watanzania. Wana wajibu! Haiwezekani baba uzae mtoto na mama, halafu ukimpeleka shule, mtoto aseme nakushukuru. Anayeshukuriwa ni Mwenyezi Mungu, siyo baba na mama wala Serikali. Ni wajibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa Serikali ya CCM kwa miaka mitano waliyoomba, Bunge hili ndiyo la mwisho. Watanzania tunatakiwa tujipime, katika miaka mitano waliyopewa baada ya kuomba mwaka 2010 wamewajibika vipi katika kuwaletea maendeleo Watanzania kwa kodi walizokusanya ndani ya nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Mkoa wa Morogoro, mwaka 2014 mlileta hapa bajeti tukaipitisha. Hiyo ndiyo ilikuwa bajeti yenu ya lala salama. Hii siyo bajeti yenu kwa sababu inakuja Serikali ya UKAWA.

MBUNGE FULANI: Sawa sawa!

MHE. SUSAN L. A KIWANGA: Mwaka jana ndiyo ilikuwa bajeti yenu ya mwisho, mmeshindwa kuitekeleza. Mkoa wa Morogoro fedha za maendeleo mmepeleka asilimia 14, leo imebaki miezi mitatu, mtatekeleza vipi asilimia 86 zilizobaki? Mmeshindwa, hamwezi, ni lazima mwajibishwe! Mshukuriwe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya usalama wa raia, naomba niihoji Serikali; mmeshindwa kuwalinda wananchi na mali zao. Kilombero ujangili unatokea pale, sijui wanasema Alshabab, kulipua mabomu; mpaka leo ninavyosema kuna Mwana-CCM Mgambo anaitwa Thomas Manjole, anayeishi pale Msolwa Ujamaa, walikamatwa wale watu wa Alshabab wametoka kule Milima ya Udzungwa. Mnasema mnahifadhi, kumbe mnahifadhi Alshabab.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walikwenda wakawakamata na kuwazingira wale vijana, Mgambo yule ametumwa na Mwenyekiti wa Kijiji akawa-*search* wale vijana, yule wa mwisho akakataa, alipobonyea akaruka, akarusha bomu. Yule baba amevunjika vunjika mikono na miguu. Gari la Halmashauri ikamtelekeza Muhimbili. Aliporuhusiwa nilimchukua kwa gari yangu mpaka Kijiji kwao. Mpaka leo hakuna huduma yoyote mnayoitoa. Kuna usalama hapa wa raia na mali zake? Mmeshindwa, ni lazima mwondoke! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka Kilombero juzi, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilombero, nakwambia ni aibu, askari wale wasichana na wavulana wanaogelea kama bata wanakwenda Kituo cha Polisi cha Wilaya. Ilikuwa Ofisi ya Maliasili! Miaka 50 ya uhuru hamjaipatia Wilaya ya Kilombero Kituo cha Polisi cha Wilaya; hamjawapatia Mahakama ya Wilaya ya Kilombero. Ninyi mnaweza? Mmeshindwa! Ni lazima mwondolewe mwaka huu. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Ndiyo! *(Makofi)*

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi, Makarani wa Mahakama ya Wilaya ya Kilombero hawajalipwa posho zao miezi mitatu, mnatarajia wale waishi vipi? Ni rushwa mpaka kunakucha, mmeshindwa lazima mwondoke.

MBUNGE FULANI: Aah wapi!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, mkizungumzia *SAGCOT* Kilombero; mnazungumzia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu *KPL;* mwaka wa ngapi huu? Barabara tunazungumza kila siku.

Kama kuna uwekezaji wa kilimo, watu wanalima, barabara hazipitiki, mnategemea yale mazao watayabeba angani? Mmeshindwa, mje na majibu ni lini mtajenga barabara kule? Lakini muda umekwisha ni lazima tuwatoe, sisi tujenge barabara ya Kidatu – Ifakara kilomita 80 na Ifakara – Mlimba – Madeke Njombe, tutajenga sisi UKAWA, nyingi tena ubao hamna. Habari ndiyo hiyo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Maliasili, nimetembea nchi mbalimbali. Juzi kama mliniona kwenye luninga, nilikuwa kule Milima ya Meza, tumepandishwa kule hata wagonjwa au wazee wanapanda. Wameupigia kura ule mlima kumbe siyo lolote! Tumeenda juu tumekuta Simbilisi; ule utaulinganisha na milima wetu wa Kilimanjaro? Mmeshindwa kuweka miundombinu ili wananchi waende kwa wingi kule mlimani waupigie kura, matokeo yake mlima wetu mzuri haujaingia kwenye maajabu ya dunia. CCM mmeshindwa ni lazima mwondoke. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii; hamna Hoteli nyie, hamna Ndege nyie! Ndege, mmekula eti mnasema utalii ukue ndani ya nchi hii. Katika utalii Brazil ndiyo ya kwanza, Tanzania ni ya pili kwa vivutio, lakini kwa mapato ni ya 140. Kazi ya nani? CCM ni lazima mwondoke. Tena mwondoke haraka ninyi mmetuletea balaa ndani ya nchi hii. Kiboko yenu ni mwezi wa Kumi tarehe 25 na ole wenu mzidishe hata dakika, kitanuka nchi hii! *(Makofi/Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyote ndani ya nchi hii hususan Mkoa wa Morogoro, mmeua na matokeo yake watoto hawana ajira, Alshabab wanaletea fedha watu wachache, wanawadanganya hawa watoto wasiokuwa na uwezo masikini, wanajificha milimani kujifunza mambo ya Alshabab. Sasa ninyi dhambi ya usaliti itawahukumu tarehe 25 mwezi wa Kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo usiseme. CCM mmeshashindwa! UKAWA tukiingia tutarudisha ardhi. Wananchi msikie, mjitokeze kwa wingi kujiandikisha. Sasa hivi CHADEMA tuna Operesheni Shahada Mkononi, mtakiona cha mtema kuni mwaka huu! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Inauma eh! Haya nakaa, nilindie muda wangu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan muda wako uko pale pale. Malizia, ila nilikuwa nataka kujua, hivi UKAWA ndiyo kitu gani? Endelea tu Mheshimiwa Suzan.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, UKAWA utaujua tarehe 25 mwezi wa Kumi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Posho mishahara na vitendea kazi vya Watumishi. Leo Watumishi ndani ya Wilaya ya Kilombero watu wa Afya na Walimu, hali ni mbaya! Hampeleki fedha za kuwalipa. Nyie TAMISEMI mpo hapo? Nyie nini? Mnaagiza Halmashauri, *capitation* mnapeleka Shilingi ngapi kule chini? Mnakula huko huko juu kwa juu.

Leo mwanafunzi wa Shule ya Msingi mmekopa huko duniani tutakuja kulipa mpaka mwaka 2040 halafu mtawasingizia watoto wetu kwamba baba zenu. Ninyi ile *capitation* hamuifikishi! Mtoto mmoja alitakiwa afikishiwe Dola 10, ninyi mnafikisha Sh. 200/= wezi wakubwa! *(Makofi/Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Oooh!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Ndiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Sekondari vilevile Dola 25 mnazifikisha kule? Kazi yenu ni kuchangisha wananchi. Watu wanalipa michango kwa sababu ya kusimamia mitihani. Ninyi mwisho wenu umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hapa na kazi yenu ya ubaguzi; maafa yakitokea Mkoa wa Morogoro, sawa sawa; yakitokea sehemu nyingine, peleka Wanajeshi, jenga nyumba, nini; ninyi hukumu yenu ni tarehe 25 mwezi wa Kumi. Hata Kilombero juzi maafa yametokea, lakini ni nani leo anazungumzia maafa ya Kilombero? Kituo cha Polisi kule maji kibao, Mahakamani hapapitiki, kwenye shule kote kumejaa maji; mbona hamtuletei taarifa za maafa mmepeleka Shilingi ngapi kule? Hukumu yenu ni tarehe 25 mwezi wa Kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa feki zilichapishwa kwenye Gazeti la Dira la mwezi tarehe 14 Machi, 2014, Daktari feki wa Moyo yuko ndani ya Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Dira wamechapisha, huyu Naibu Waziri alipewa taarifa akasema ataenda kufuatilia, mpaka leo hajaenda. Sasa kimbieni haraka pale Morogoro mkatufute huyo Daktari feki, hatutaki kuwaumiza Watanzania. Habari ndiyo hiyo tunawapa. Eeh, inawa-*pain eh*!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nawaambia hivi, nchi hii ni mali yetu sote. Watanzania wenzangu naomba kuwaambia hawa wameshindwa, hawawezi tena. Kama ni *player* wakati ule, imekuwa machenza, inaimba palepale mpaka uitoe kwa kidole. Sasa kutoa kwa kidole ni mwezi wa Kumi. Kajiandikishe, piga kura yako kwa UKAWA tuwaondoe hawa ili tuongoze hii nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi ya kuugawanya Mkoa wa Morogoro; nawauliza hivi, Mkoa wa Pinda una watu 565,000 kwa mujibu wa Sensa, Wilaya ya Kilombero peke yake ina watu laki nne na kitu, lakini leo kwa Pinda ni Mkoa wenye watu 500,000. Mkoa wa Morogoro una mamilioni ya watu, tumeomba mkoa, mna-*dilly dally*. Ninyi Watanzania wa Morogoro vumilieni, tunachukua nchi mwezi wa Kumi, tunatoa mikoa miwili; Kilombero na Morogoro. Habari ndiyo hiyo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan, muda hauko upande wako!

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Haya ahsante.

NAIBU SPIKA: Habari ndiyo hiyo! *(Makofi/Kicheko)*

Namwita Mheshimiwa Zaynabu Vullu, atafuatiwa Mheshimiwa Mrema.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kabla sijasema yale niliyokusudia, nianze kwa kuwakumbusha watu humu ndani kwamba, Chama chetu kina wimbo unasema "Waache waseme, Cha cha Mapinduzi kina wenyewe!" *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namsikiliza Mjumbe aliyemaliza kuongea na kabla yake. Lakini huyu wa mwisho nilikuwa najiuliza, anazungumzia bajeti, anahubiri au ana-*rap*? Sijapata jibu. *(Kicheko)*

Pia nataka nimwambie, kuna msemo wa Waswahili wanasema, ukichukua paka sita mpaka saba, ukawafunga mikia halafu ukawaweka juu ya meza au juu ya kabati wakatulia; akapita panya chini, sijui kivumbi chake kinakuwaje hapo! Kamba itakatika, wataparaganyika. Kwa hiyo, UKAWA, sijui UPAWA!

MBUNGE FULANI: UKAWA!

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Walijue hilo! *(Makofi/Kicheko)*
Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii adhimu ambayo umenipatia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeniwezesha kusimama hapa na kuweza kuchangia bajeti hii. Halikadhalika, nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wenzangu wa Mkoa wa Pwani hasa akina mama wenzangu walionipa dhamana ya kuingia ndani ya jengo hili ili kuwawakilisha. Pia naomba ushirikiano huu tuendelee nao, waache wao wafungane mikia, sisi tutapita, kazi itabaki kwao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi wa Chama cha Mapinduzi, nawapongeza sana akina mama kwa juhudi wanayoifanya ya kuhakikisha tunashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii niipongeze hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa

mawasilisho mazuri pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mwanri. Hotuba imetulia na imekaa vizuri. Nashangaa wenzetu wamesema kwamba ile bajeti ya mwaka 2014 ilikuwa ya kwetu ya mwisho, yao wameitoa. Lakini mbona hamna chochote humu ndani? Karatasi zenyewe hata 30 hazijafika, halafu unajinadi wewe kwamba umeleta bajeti yako. Naomba mkae vizuri, mjipime, mwone kama mnatosha, lakini bado hamjaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo mengi sana! Imepunguza idadi ya vifo vya mama wajawazito na watoto. Hili halina ubishi wowote, tumeshuhudia Mke wa Rais *(First Lady)* na Mheshimiwa Rais wakipongezwa na Mataifa mbalimbali kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Sekta ya Afya. Mwenye macho haambiwi tazama. Wao wamesema masikio, lakini mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, katika suala la afya, kuna Kitengo cha Moyo kimejengwa Muhimbili. Serikali pale imepiga hatua kubwa sana. Kitengo kile kina manufaa makubwa sana kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kimepunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya Tanzania kwa ajili ya matibabu. Tumesikia sasa hivi wameanza kutibu wagonjwa wa moyo kwa kuanza na watoto wadogo mpaka watu wazima, bila mgonjwa kupasuliwa popote. Bado mnataka kusema nini? Hayo hayawatoshi? Enhe, Serikali imefanya mengi! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Waugue kwanza!

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wetu hapa wanaenda kutibiwa nje kwa fedha za Serikali, mbona hawakatai? Mbona wao ndio wanakuwa mstari wa mbele? Tena kwa bahati mbaya wakiingia humu ndani wananadi, wanaorodhesha na watu wao waliolazwa, wanaokula fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza tena Serikali yangu kwa kazi nzuri iliyofanya ya ujenzi wa barabara. Nina hakika hata wewe uliyeko humu ndani unapojenga nyumba yako au unataka mwenyewe kujipendezesha, huwezi ukafanya vitu vyote kwa siku moja. Utakwenda kwa awamu. Leo umenunua samani ya kiti, kesho utanunua meza ya kulia chakula, mtondogoo utanunua vyombo, ilimradi unahakikisha nyumba yako inakaa mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu, pamoja na kazi nzuri iliyoifanya ya kujenga barabara, iliahidi kujenga baadhi ya barabara za Mkoa wa Pwani ikiwemo ya Kisarawe. Toka mwaka 2005 mpaka leo hii hatujajua. Nina uhakika kwa miezi miwili iliyobaki Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umakini wake atatoa fungu la fedha ili barabara hiyo itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Bandari ya Bagamoyo imezungumziwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini naomba niikumbushe Serikali, kuna bandari kavu katika Wilaya ya Kisarawe eneo linaitwa Mzenga. Eneo lile liliishafanyiwa upembuzi yakinifu, fedha zimeshatolewa zaidi ya Dola milioni 100, lakini nataka kujua mkakati na mpango wa Serikali, imefikia wapi katika kuendeleza hilo eneo? Kwa sababu kuna manufaa ya kuwa bandari kavu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kisarawe, miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Pwani, ni Wilaya ambayo iko karibu sana Mji wa Dar es Salaam. Mji wa Dar es Salaam umeishajaa, Wilaya za Mkoa wa Pwani zina nafasi kubwa sana. Eneo lile la bandari lililochaguliwa, kuna njia mbili za reli; kuna reli ya kati na reli ya *TAZARA*. Halikadhalika ni karibu na barabara kuu inayounganisha nchi jirani kwa kupitia Morogoro, Dodoma na maeneo mengine.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapohitimisha, basi aje na maelezo ya kusema ni vipi Serikali imejipanga kuhakikisha bandari kavu inatengemaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia michezo, tuna maana kubwa sana. Tunataka Serikali yetu ifufue na ijenge suala la michezo. Tumechoka kuwa vichwa vya wendawazimu! Tatizo lililopo, naomba Serikali iangalie ni vipi itaondoa ushuru kwenye vifaa vya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata msaada wa majani kutoka *FIFA* kwa ajili ya kupanda kwenye Viwanja vya Michezo vya Nyamagana na Kaitaba, lakini mpaka leo hii bado majani hayo hayajawezwa kutolewa kwa sababu ya gharama kubwa ya ushuru. Sasa kama tuna nia ya dhati ya kutaka kuimarisha michezo katika nchi yetu na kuinua vipaji vya vijana wetu na wengi tumewaona wakiwa wachezaji wazuri; mimi ni mmojawapo naweza nikatoa mfano wa mdogo wangu, ambaye alikuwa akicheza mpira anaitwa Kassim Matitu, alichukuliwa kwenda kucheza Ulaya miaka hiyo mpaka leo hii. Kwa hiyo, hizo ni fursa. Tunao vijana wengine ambao bado wanachipukia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri tu Serikali kwamba iangalie ni vipi inaweza ikaondoa ushuru kwenye vifaa vya michezo ili tuweze kuinua vijana wetu. Kuna mashirika yamejitolea kuleta timu mbalimbali za Kimataifa, lakini watu hawa wakileta vifaa vyao: Je, watatozwa ushuru wa kiasi gani? Naiomba Serikali iliangalie hilo na pia iangalie suala la Baraza la Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukachukua watu wenye watapia mlo 15 ukawafunga kamba wapigane na mtu mmoja, sijui inakuwaje? *(Makofi/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: *(Aliongea nje ya microphone)*

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Aje tu, aje tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kusema, Baraza la Michezo Tanzania linahitaji msaada wa Serikali, kwa sababu Baraza lenyewe limechoka. Sasa mnategemea litawasimamia akina nani? Naomba Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona uwanja wangu umevamiwa kidogo, lakini mimi sihofu, mwache aje akae!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari, naomba utulie kidogo, Mheshimiwa Vullu endelea!

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wenzetu tunapoongea na wananchi, tuwajenge kimaendeleo, tuwajenge kudumisha uhuru, umoja, amani, mshikamano na upendo, tusiwe na jazba. Inatia hofu, kama unapoongea na wananchi wako unakuwa na jazba, ndani ya famili yako utakuwa unaongea vipi?

Nawaomba ndugu zangu, tuijenge Tanzania yetu, ni nchi ya amani, sote ni mashuhuda, wananchi zaidi la laki mbili wamekimbilia Tanzania; sasa na sisi tutakimbilia wapi ikiwa kona zote hazikaliki?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Zaynab, nakushukuru sana, ahsante sana. Mheshimiwa Mrema atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasemee makundi manne kuhusu ardhi. Naomba nimsemee Marehemu Paul Sananga Lekule ambaye mwaka 2001 kwa upendo wake katika Kijiji cha Kiraracha alitupa heka mbili kwa ajili ya kujenga Shule ya Msingi Kiraracha. Marehemu Sananga amekufa mwaka 2000, mpaka leo watoto wake wanane na wajukuu kumi wamenifuata Sinza, wameweka kambi kwasababu hawajapata fidia. Shule ile tumeikagua, ni shule nzuri sana, ni shule yenye ghorofa, nafikiri ni *one of the best schools* katika nchi hii. *(Makofi)*

Pili, naomba niwasemee watu wa Meresini ambao wameporwa ardhi yao, wanaishi kama wakimbizi kwa kisingizio kuwa ardhi ile imepewa mwekezaji na uwekezaji wenyewe ni wa redio. Naomba niwasemee wananchi wa Lokolova ambao ardhi yao karibu heka 2,700 zinaweza kuporwa wakati wowote na wakabaki wakimbizi. Pia nakwenda mpaka Hai niwasemee watu wa Gararagua, shamba lao linauzwa heka 3,400 kwa Shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kulipia deni la *KNCU.* Shilingi bilioni kumi hatujui zitakwenda wapi, deni la *KNCU* ni Shilingi bilioni nne, basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa maneno ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya mwaka 1958. Alisema, katika nchi kama yetu ambapo Waafrika ni masikini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba Mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi katika miaka 1980 au miaka ijayo, ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri, litaibuka tabala la Watanganyika matajiri wajanja, tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu katika muda mchache tutakuwa na kundi dogo la waafrika wakiwa na ardhi na walio wengi watakuwa ni watwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kuanza na maneno ya Mwalimu Nyerere kwasababu wote tunatakiwa tufuiate alichokuwa anasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye shamba la Meresini ambalo nimekuwa napiga kelele tangu nimeingia katika Bunge hili na sasa naondoka bila ya kupata ufumbuzi, ni aibu kubwa sana! Kumbe viongozi tulionao Mikoani ni madalali wa ardhi, ni madalali wa matajiri. Nathubutu kusema, kwa nyaraka nilizonazo ukiangalia barua tarehe 16 Agosti, 2012 anaandikiwa huyo *the so called* mwekezaji wa redio aliyepewa heka 11.7 anaambiwa uvamizi wa eneo lililoko Meresini Himo.

Mkuu wa Mkoa amefuatilia malalamiko yako na ameridhika na maelezo au kumbukumbu juu ya umiliki wa Kampuni ya *Reactor Public Company* kwenyer shamba namba 1446 lenye hati iliyosajiliwa namba 26216, mtu yeyote atakayeingia kwenye shamba hilo anakiuka sheria za umiliki.

Ndugu zangu, nasema viongozi hamtusaidii. Nyie ndio mnapaka Serikali ya Rais Jakaya Kikwete matope. Barua ya tarehe 16 ya Mkuu wa Mkoa ambayo siyo Afisa wa Ardhi, lakini mwangalie biashara zinazofanyika huko Mikoani na sisi Wabunge tunapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 mwezi wa Tisa, Kamishna wa Ardhi wa Kanda ya Kaskazini anamwandikia Mkurugenzi wa Wilaya Halmashauri ya Moshi, "Malalamiko ya Umilikaji wa Ardhi kinyume cha Sheria, Kijiji cha Himo, eneo la Meresini."

Mheshimiwa Naibu Spika, sisomi yote, kwa barua hii tafadhali chukua hatua za kuzuia hatua zozote za uendelezaji wa eneo hilo mpaka hapo tutakapokutanisha pande zote

zinazohusika na mgogoro wa eneo hili. Huyu ndiye Afisa Ardhi, lakini Mkuu wa Mkoa tayari ameshajiingiza ndani. Lakini haikuishia hapo, huyo Kamishna wa Ardhi, tarehe 11/3/2013 "Malalamiko ya Umilikishaji wa Ardhi Kinyume cha Sheria Kijiji cha Eneo la Meresini," amesema maneno mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakukabidhi barua hizi, lakini kimoja ninachosema, kama Kamati ya Ugawaji wa Ardhi Wilaya ilipaswa kupitia maombi ya ardhi katika eneo hili, endapo utaratibu huo haukuzingatiwa, ni muhimu ukazingatiwa kwa maana ya kufuatwa upya. Amesema na nakala amempa Mkurugenzi, anamwambia, "utaratibu wa kugawa ardhi hii uzingatiwe kwa mujibu wa Kanuni ya Ardhi ya mwaka 2001." Lakini mwenye ardhi hii tayari ameshapewa hati mwaka 2008. Ni vitu gani? Mnatufanya sisi wajinga?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkiambiwa mmechoka, mtasema na Mrema amewatukana. Hiki ni kitu gani? Ni Utawala wa Sheria? Napigania hapa Mawaziri wote wawili niliowajua, labda huyu wa tatu, natoa hizi nyaraka mweze kuona mambo yanakwenda huko Mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo huyu tajiri anaambiwa heka 11.7 ni ya kwake. Je huyu Marehemu Sananga aliyetoa hii ardhi? Miaka 14 mpaka sasa hivi hajapewa hata heka mbili anazodai. Sasa sisi Wabunge twende wapi? Wameamua kukita kambi pale kwenye nyumba yangu Sinza, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema, mnasema Wabunge ni wachokozi, wanawaonea. Hilo ndilo mmenifanya hata mliyosema mmekubaliana nami kwamba mjenge Soko la Kimataifa pale Lokolova; nimekuwa na wasiwasi kwasababu pale kuna heka 2,700. Kweli tutajenga soko la Kimataifa na na Mji wa kisasa, watu wa Kenya na Uganda watakuja. Sawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tabia hii ya viongozi, ina maana kuwa ardhi yote wataimiliki wao au kupitia kwa watu wao wanaowajua? Sasa mtanifanya niwaambie wananchi wa pale Lokolova kwamba pengine hiyo ni biashara kichaa; itakuwaje watu walikuwa ni wakulima na wafugaji leo waporwe eneo lote la heka 2,700 kwa kisingizio cha soko la Kimataifa? Ile hati imefutwa! Mkuu wa Mkoa, naomba nikuulize; aliyemruhusu Mtrajisi wa Ushirika afute hati ya Lokolova ni nani? Akifuta hawa waliokuwa wakimiliki, kwa nini wanafuta halafu tunaanzisha umilikaji mwingine ambao hauna maslahi kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema pale ni kwamba kwa tabia hii ninayoiona, naomba eneo hilo ligawanywe lionekane ni la kuendelezwa na kuwapa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nilikwenda kusali Kanisa la Mamba Kotela. Pale kulikuwa Dkt. Fredrick Shao Mkuu wa Kanisa la KKKT Tanzania, Askofu Mstaafu Dkt. Martin Shao na Askofu Mstaafu Erasto Kweka. Nimekwenda kujitetea kutokana na uongo na uzushi wa wanasiasa, wanataka nikose Ubunge kwenye Jimbo la Vunjo kwa kunisingizia kwamba mimi nimeasisi Mahakama ya Kadhi na kusema nilipobaki Bungeni kwenye Katiba hii nimehusika kuweka kipengele cha Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba watu wote wanaonisingizia, huu ni uchochezi na huu ni uongo. Naomba Maaskofu wote wa Kilimanjaro, Mapadri wote, Wachungaji wote na Wakristo wote, wasome hii Katiba mpya waone kama kuna aya yoyote ya Mahakama ya Kadhi iliyotumbukizwa huku ndani. Kwa nini tunasema uongo? Sisi Wanasiasa kwa nini tunataka ujiko kwa kusema uongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambieni, hii Katiba tusipoipitisha; Kenya Katiba yake ina Mahakama ya Kadhi, Uganda, Mozambique na Afrika ya Kusini. Leo kwa mara ya kwanza tumekaa, tuliobaki ndani mnaotukemea na kutucheka, tumekaa ndani na Waislamu wema,

waadilifu, wachungaji pamoja na Mashehe tukakubaliana tutengeneze nchi ambayo haina udini kama Mwalimu Nyerere alivyotuwekea misingi hiyo kwamba masuala ya dini yafanyike nje ya Katiba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Katiba ni matokeo mazuri na muafaka kati ya Waislamu wema waliokuwa ndani ya Bunge la Katiba na Wakristo wema tuliokuwepo ndani ya Bunge la Katiba. Leo mkikataa hii Katiba, kwa maneno tunayozungumza hapa, mna uhakika gani kwamba tutafika tena katika historia ya nchi hii tupate Katiba ambayo haina udini? Ndicho nilichokiona kule. Halafu lingine, naomba wenzangu wanaotaka Ubunge Vunjo, wautake kwa kusema haki, ukweli. Nashukuru na siku hiyo James Mbatia alikuwepo pale, nikamwambia wewe Mbatia, hebu angalia kitabu chako! Kina Mahakama ya Kadhi? Tulifanya uchaguzi mwaka 1995…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mrema muda hauko upande wetu.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilitaka hilo lieleweke.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Mrema. Mheshimiwa Vita Kawawa nilishakutaja na utafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hotuba hii. Naomba nianze kutoa pongezi na shukrani nyingi sana kwa Serikali nzima kwa kunipa ushirikiano katika kipindi hiki cha miaka mitano nilichokuwa nawakilisha Jimbo langu la Namtumbo toka mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi zangu na shukrani za pekee kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara nyingine zote ambazo zimekuwa zikinipa ushirikiano wa mara kwa mara. Pale ambapo nahitaji ushirikiano nao wamekuwa wakinisikiliza na kunitekelezea yale niliyokuwa nayaomba, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na orodha hii ya majedwali. Tumeonyeshwa humu katika orodha ya majedwali ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna maeneo mbalimbali. Eneo la kwanza linazungumzia makusanyo. Nataka kuzungumza kuhusu makusanyo ya Halmashauri zetu. Makusanyo ya Halmsahuri zetu yanatofautiana. Kuna Halmashauri zenye uwezo mkubwa zinazokusanya nyingine mpaka Shilingi bilioni 24. Lakini kuna wengine wenzangu na mimi hapa, Halmashauri zetu zinakusanya hadi Shilingi milioni 200, wengine 400 na kadhalika. Tunatofautiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapendekezo hapa ambayo yalisomwa na Kamati yetu pia yalikuwa yanasema kwamba asilimia 60 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu zifanye kazi za maendeleo. Sasa nashauri sana Serikali nayo iangalie hili. Tutaendelea kuzigawa Halmashauri zetu hizi kuwa tofauti. Kuna nyingine zinaingiza mabilioni ya hela na nyingine milioni za hela. Kwa hiyo, tulikuwa naomba kuangalia pia Serikali inapopanga mipango yake ituangalie Halmashauri zenye makusanyo madogo hasa sisi Halmashauri tunaotegemea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunategemea wakati wa msimu wa kilimo ndipo hapo tuweze kukusanya mapato yetu na kuendeshea shughuli zile za ndani. Kwa hiyo, naomba sana mtuangalie. Ukitazama katika jedwali hili pia, kuna maeneo hasa mwaka huu ya Mfuko wetu wa barabara; mfuko huu umekuwa ukitoa fedha za kutosha katika kipindi cha mwaka (nikitoa mfano kwangu) 2012/2013. Bajeti iliyopangwa ilikuwa ni Shilingi milioni 538 na zilizotolewa ni

Shilingi 538; mwaka uliofuatia vilevile 2013/2014 ilikuwa Bajeti iliyopangwa na zilitolewa Shilingi milioni 538.

Mwaka uliofuatia Bajeti iliyopangwa, kwa sababu ya ongezeko la mahitaji ya barabara yameongezeka ilikuwa ni Shilingi bilioni 1,457 lakini fedha mpaka Machi zimefika Shilingi milioni 300. Kwa hiyo, tulikuwa tunaiomba sana Serikali iangalie katika eneo hili pia kwamba bado fedha zinahitajika katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niseme katika ushirikiano nilioupata na Serikali, leo hii katika kipindi changu nilichokuwa mwakilishi toka mwaka 2010 mpaka sasa hivi, tumeweza kujenga barabara ya lami kutoka Songea mpaka Namtumbo, tumejenga na kufungua barabara ambazo hazijawahi kujengwa wala kufunguliwa toka tupate uhuru na baada ya uhuru; tumejenga jengo la Hospitali ya Wilaya, kubwa ambalo sasa tuna hospitali ya Wilaya; tumepata umeme katika Makao Makuu yetu ya Wilaya; lakini tumejenga na kumalizia jengo kubwa kabisa la Utawala la Halmashauri yetu ya Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia leo hii tumeanza kuweka lami katika barabara au Mitaa ya Namtumbo. Pia tatizo tulilokuwa tunagubikwa nalo sana la barabara kutoka Namtumbo kwenda Tunduru, sasa limekwisha, Mkandarasi yuko barabarani, Mheshimiwa Rais ndiye alituzindulia kazi ile na kazi inakwenda kwa kasi. Naomba niwaambie watu wa Namtumbo kuanzia Migelegele, Masugulu, Songambele, Nchomolo na Kilimasera, barabara ile itakamilika mwaka huu na watapita kwenye lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafaniko mengi tuliyonayo, lakini tuna changamoto. Changamoto tuliyonayo mwaka huu ni kilimo. Zoezi jipya lililokuwa la upatikanaji wa mbolea limetupa taabu sana; mbolea na masoko. Mbolea mwaka huu ilikuwa vikundi viweze kukopeshwa na vikundi vilijiandaa vikatoa fedha zao kwenda kukopeshwa na kupeleka kwa Mawakala lakini baadhi ya Mawakala hawakuwa waaminifu. Wakulima walitoa fedha zao, mbolea wamepata nusu ya hitaji walilotakiwa. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali, utaratibu huu na watalaamu wauangalie msimu huu unaokuja. Tumepata shida sana na mwaka huu tunategemea pia upatikanaji wa chakula kulichopatikana mwaka 2014, mwaka huu kinaweza kikapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitegemea sana utamaduni wa masoko ya kawaida ya kuuza mali ghafi kwa maana ya mahindi ya kawaida. Tunaomba sana Serikali iendelee kufanikisha mpango wake wa kutuletea umeme wa gridi katika Mkoa wa Ruvuma ili tuwe na viwanda vya kusindika mazao. Wote tunafahamu, wataalamu wanajua kiwanda chochote kinawekwa karibu na malighafi. Sisi tuna malighafi nyingi za kilimo. Tuna mahindi, tuna ufuta, alizeti, maharage, mpunga na kila aina ya mazao ambayo tunalima. Tunahitaji umeme ili tuwe na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vikubwa wawekezaji hawawezi kuweka bila kuangalia kama kuna umeme, maji na barabara. Sisi maji tunayo, barabara tunazo sasa hivi za lami na za vumbi zinatengenezwa. Tunachokihitaji sasa hivi ni umeme wa kawaida ili tuweze kuweka viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku imezungumzwa na watu wengi hapa, lakini nami nataka nielezee kwamba tumbaku ni zao la kwanza linaloingiza fedha nyingi za kigeni. Mwaka 2014 msimu uliopita, limeingiza Dola milioni 462, lakini pia limeingiza zaidi ya Shilingi bilioni 168 fedha za Kitanzania kama kodi, *inland revenue* na wakulima wameendelea kulima zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yote hii inafanyika kutokana na usimamizi wa Serikali kupitia Bodi yake ya Tumbaku, kusimamia uteuzi wa masoko ya tumbaku na kufanya *grading*. Sasa zoezi mwaka huu linaonyesha linaweza likatuangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Tumbaku ilitangaza tarehe 5 Mei, Soko la Tumbaku ndiyo litaanza na wanahitaji Shilingi milioni 518 kuifanya kazi hii ya kuiingizia Serikali Shilingi bilioni zaidi ya 160, kuwaingizia fedha za nje Dola milioni 462. wanahitaji dola milioni 517 tu kufanya kazi hiyo, lakini hakuna fedha hizo mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaambia sasa hivi, tumbaku kama isipouzwa kipindi hiki inanyauka na ikikauka uzito unapungua, tumbaku inaharibu ile *quality* yake na soko pia litaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikal ilitazame jambo hili kwa umakini mkubwa sana sasa hivi ili ipatikane fedha hiyo ili iende kufanya kazi hiyo ya *grading* na *classification* katika Soko la Tumbaku. Pia naomba niendelee na mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu ya msingi tumeweza kupata mafanikio sisi katika Jimbo letu la Namtumbo tumeweza kufaulusha wanafunzi ambao ni kutoka asilimia 23 mpaka asilimia 52 waliofaulu. Tumeendelea kupata Walimu. Tulikuwa na walimu 456 huko nyuma na leo tuna Walimu 967, kati yao wanaume wako 555 na wanawake wako 412 lakini pia tumepokea walimu katika shule za sekondari 38 wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi katika ule mpango wa ujenzi wa maabara, tumeshajenga maabara 68, tunapiga ripu na sasa hivi tunatengeneza Meza za Maabara hizo na tunategemea wakati wowote mpaka mwakani tutakuwa tumekamilisha. Changamoto iliyoko pia katika eneo hili ni kwamba nyumba za Walimu ziko wa Sekondari ziko 87 na tuna upungufu wa nyumba za Walimu 348. Tunaomba Serikali itazame eneo hili pia la nyumba za Walimu wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la afya katika kipindi hiki, tumefanikiwa; tulikuwa na Zahanati 23, sasa hivi tumejenga tuna Zahanati 35 ambazo zinafanya kazi na Zahanati saba zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika Vijiji vya Mawa, Kijiji cha Njomlole, Kijiji cha Namanguli, Ukiwayuyo, Mtumbati-Maji, Mageuzi na Songambele. Kwa hiyo, tunategemea pia tunaweza tukamaliza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru katika eneo hili pia tumepata mwaka huu wafanyakazi kwa maana ya Manesi na Waganga 75. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo. Sasa namwomba Mheshimiwa Ahmed Shabiby, jirani yangu Mbunge wa Gairo achukue nafasi hiyo; na Mheshimiwa Barwany ajiandae. Mheshimiwa Shabiby!

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu kwa moyo wa dhati kabisa. Kwa sababu sina haja ya kupiga kelele nyingi, Jimboni kwangu mambo ni safi, hayana shida, ila tu, ni yale matatizo ambayo lazima tuelezeane na yafanyiwe utatuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi *TRA* inakusanya kwa mwezi Shilingi bilioni 800 mpaka Shilingi bilioni 900 kwenye nchi yetu ya Tanzania. Sasa sioni ni kwanini Wizara ya Fedha inashindwa kumaliza deni la mahindi la wakulima wa Tanzania wa Mkoa wa Morogoro

pamoja na Gairo ambayo yalichukuliwa na *NFRA*. Ni Shilingi bilioni 24 tu! Sasa ukiangalia kama Serikali inaweza ikakusanya Shilingi bilioni 800 mpaka 900 kwa mwezi, mnashindwa Shilingi bilioni 24 tu, mnazitoa kwa mafungu!

Mama yangu Waziri wa Fedha, hebu jiangalie mara mbili, mara tatu, kweli kabisa! Kwa sababu hii ni kama Watumishi. Hii nchi tunasema ni ya wakulima na wafanyakazi. Sasa kama ni ya wakulima na wafanyakazi: Je, kama wafanyakazi wangekuwa hawajapata mishahara ingekuaje? Mnashindwa kuwapa mishahara yao wakulima kwa jasho lao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo wakulima wa Gairo, wanadai toka mwezi wa Tisa. Tumeingia kwenye msimu mwaka huu hawana pesa ya kulimia, wanaingia kwenye njaa kwa pesa yao. Sasa naomba lile *godown* la Gairo mlilonunua mahindi, yale mahindi yasiondoke pale, kwa sababu mmewasababishia wananchi wa Gairo waingie kwenye njaa; na yale mahindi mtayagawa bure pale pale Gairo kwa sababu ya makosa ya kuchelewa kulipa hizo pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mngewahi, ina maana wangepata pesa na wangeweza kulima. Tulizungumza miaka miwili nyuma na Waziri wa Afya kwamba watafanya Kituo cha Afya cha Gairo kiwe kinafanya kazi ya operesheni kwa ajili ya majeruhi kwa *accidents* zinazopatikana kwa wingi. Maana ukitoka hapa hadi Gairo ni kilomita 131, na kutoka Gairo mpaka Morogoro ni kilomita 131. Kwa hiyo, pale ni katikati; na kama mnavyoona au katika hotuba ya Waziri Mkuu *accidents* zimekuwa nyingi sana. Pale ni katikati, viongozi, wananchi wa kawaida ndani ya mwezi uliopita tu, vimetokea zaidi ya vifo 16 kwenye kipande kile cha Gairo tu, majeruhi ni zaidi ya 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walizungumza kwamba wataleta *ambulance*, mpaka leo! Vifaa vya *X-Ray;* tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI, ile ahadi yenu tunaomba itimizwe. Kwa sababu, hospitali ya Gairo ndiyo muafaka katika njia hii kuu kama ilivyokuwa Hospitali ya Tumbi katika kipande cha kutoka Morogoro kuelekea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni Halmashauri. Tunaishukuru Serikali kutupatia Wilaya na Halmashauri mpya ya Gairo. Kwakweli hizi Halmashauri mpya lazima mziangalie kwa jicho la huruma. Toka tuganwanywe toka Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, kuna pesa Halmashauri ya Gairo za *OC*, za kodi zile za ndani, za maendeleo, Shilingi milioni 253 ambapo bado Halmashauri ya Wilaya ya Gairo ilikuwa haina akaunti. Watu wa Wilaya ya Kilosa wamezing'ang'ania zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais mwezi wa Nane mwaka 2014 alitoa amri wazirudishe ziende Gairo, lakini bado hawataki kutoa.

Sasa jamani hata amri ya Rais kuna wababe wanazuia hizo Shilingi milioni 253? Halmashauri ya Wilaya ya Gairo inaenda tu kimungumungu! Imekaa kwenye majumba ya kupanga toka ianze kukaa mpaka leo haijalipa deni! Watu wake, matatizo! Mkurugenzi hana gari, hakuna gari za hospitali wala gari za Idara ya aina yoyote! Mgawanyo wa Wilaya ule, magari yote mabovu, yote yamesimama! Tunaomba mziangalie hizi Halmashauri kwa roho kidogo ya huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme Gairo tumepata Vijiji vya Iyogwe, Kinyolisi, Makuyu, Taragwe, Nguyami, Ijava, Idibo, Leshata, Kitaita, Ngiloli, Taboteli, Henje, Kisitwi, Vijiji vingi tu! Mkalama, Meshugi, Luhaji, lakini mpaka leo Serikali bado haijatoa hela za *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *REA* katika hela ndogo walizopata wamegawa katika Wilaya ambazo Wabunge wake ni Mawaziri. Katika zile Wilaya ambazo Wabunge wake siyo Mawaziri, hawakutoa hata kifungu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishangaa hapa, nimemchukua Mheshimiwa Mwijage, nimemchukua ndugu yangu hapa Mheshimiwa Ndassa kama Mwenyekiti wa Kamati pale, wamekuja kupiga piga bla bla tu, kelele nyingi; hakuna chochote kilichofanyika! Sasa sielewi nini kinachoendelea. Sasa naomba sana, hivyo Vijiji vipatiwe umeme kwa sababu vipo kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utashangaa ukimwuliza mtaalam wa *REA*, eti naye haelewi! Hata hajui bajeti imepitisha nini! Yaani nchi hii kuna watu vichwa tayari vimesha-*retire*, wame-*retire* kiakili na kimwili. Ndiyo maana yake sasa! Yaani hata kitu kilichopitishwa kwenye bajeti, tunashindana mbele ya Mheshimiwa Waziri, mbele ya Mwenyekiti wa Kamati. Mimi naleta kitabu cha hotuba, ndiyo! Yaani ina maana ulikuwa huna taarifa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Waziri wa Umeme umekubaliana na mimi twende Gairo ukashuhudie mwenyewe nikakuonyeshe vituko; na Waheshimiwa Wabunge chunguzeni, mtu anayeshinda sana pale kwenye Ofisi za *REA,* ndiye anayepata umeme. Sasa nani atakuwa na kazi ya kwenda kujibembeleza bembeleza pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni maji. Nashukuru, pale naona miradi yote ya maji pale Gairo; mradi ule mdogo unaendelea lakini ule mradi utakuwa na gharama kubwa sana za umeme. Nimeongea na Waziri wa Maji ameniambia kwamba mwaka huu tumo kwenye bajeti ya kuleta yale maji kutoka kule milimani ambayo ni kilimita 23 tu. Alikuja yule Mkurugenzi wa Mlowasa ambaye sasa hivi ni kijana safi kabisa pale Morogoro, na tuna matumaini katika Mkoa wa Morogoro kwamba atatuletea haki. Ameshuhudia mwenyewe kwamba ni kilomita 23, amekuja hapa juzi; na Mheshimiwa Waziri umetuahidi kwamba utaleta sasa yale maji kutoka milimani pale, yabaki haya maji ambayo yanashughulikiwa sasa hivi yatakayoanza kutoka kabla ya mwezi mmoja.

Vilevile tunaomba zile pesa ambazo mlituahidi katika Vijiji vya Chogwali, Iyogwe, Kinyolisi, Idibo, Leshata, Kitaita, Ndogomi, vyote hivyo na Makuyu pamoja na Talagwe. Mmetuletea Shilingi milioni 200 hazitoshi, tunaomba sasa mtumalizie ili tuanze kuchimba vile visima virefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuja kwenye misitu. Huku kwenye misitu Waziri wetu kila siku yupo kwenye tembo tu. Misitu inakatwa; anajua msitu wa *Sao Hill* tu. Msitu wa *Ukaguru Forest* umevunwa miaka 27, leo hii umeisha, hata mti mmoja haujapandwa.

Mzee, siyo kazi tu ya kukaa huko kwenye wanyama, angalia na misitu hii. Misitu wa Mandege miaka 27 amepanda Mkoloni umevunwa. Leo hii mpaka sasa hivi mmepanda heka mbili tu za misitu.

Halafu ninyi kila siku mpo kwenye magazeti tu, mmezindua helikopta, mmebebana sijui huyu kamlinda nani! Sasa mmekuwa Mawaziri, basi amueni tu muwe Mawaziri wa Wanyama kwenye misitu jitoeni huku. Maana yake msitu mnaangalia *Sao Hill* tu; na kwenye Wizara nzima inaangalia wanyamapori tu. Ile mito yote inayopita Wilaya ya Kilosa, Mkondoa, Ludewa, Mvumi, Msowelo, yote inatoka Gairo. Sasa hivi katika ile Tarafa ya Nungwi, mazingira na misitu yote inakwisha, mito inapungua maji. Sasa mito ikipungua maji hata hao simba na tembo watakunywa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ila naomba mtekeleze, kwa sababu narudi tena. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shabiby. Mheshimiwa Barwany, karibu sana. Atafuatia Mheshimiwa Nassib Omar.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo. Pia nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lindi Mjini kwa kuniamini kunipa fursa hii kuwa Mwakilishi wao kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba wananchi wa Lindi wamejijengea sifa kubwa sana kwa uthubutu wao kwa mara ya kwanza kabisa katika historia ya nchi yetu kumchagua Mwakilishi ambaye tayari ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi walidhani kwamba siwezi. Lakini kwa ujasiri mkubwa wananchi wa Lindi wamefanya jambo ambalo Watanzania wote sasa wanaona kwamba watu wenye ulemavu wanaweza kuwa Wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mara yangu ya tano kuchangia katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu. Katika kipindi chote hiki, nilikuwa najitahidi kusema mambo yafuatayo; kuishauri na kuisimamia Serikali. Haya ndiyo yalikuwa malengo yangu makuu kabisa kwa kuwa Mwakilishi katika jumba hili la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni suala zima la mgawanyo wa rasilimali katika nchi yetu. Haya yote ambayo sasa hivi yanazungumzwa katika Bunge hili ni kutokuwa na uweledi wa kuhakikisha kwamba hii keki ya Taifa ambayo zaidi ya miaka 53 sasa haijafikia malengo ya kugawana kwa kila Mtanzania hata kama ni kidogo akaridhika nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo ndani ya nchi moja, hazina moja, mfuko mmoja wa mapato, lakini unaweza ukashuhudia kabisa kwamba tayari kuna maeneo yana ustawi na maeneo mengine yapo nyuma kimaendeleo. Pamoja na ahadi za Chama cha Mapinduzi kuwaahidi Watanzania katika ilani zake mbalimbali kwamba itahakikisha kwamba inatoa kipaumbele katika maeneo yote ambayo yapo nyuma kimaendeleo, lakini imeshindwa kufanya hivyo takribani miaka 53 sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgawanyo wa rasilimali ni muhimu katika nchi. Suala la mgawanyo wa rasilimali mara nyingi huleta amani katika nchi hizo. Lakini kama Serikali itaanza kubagua baadhi ya maeneo na maeneo mengine kuyaacha nyuma kimaendeleo hususan hali ya hatari na kupotea kwa amani katika nchi hizo, hutokea mara kwa mara. Kwani watu wanastaajabu na kushangaa, kwamba nchi yenye hazina moja, kwanini kuwe na maeneo yenye maendeleo mazuri na maeneo ambayo hayana maendeleo mazuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linathibitisha kwamba ndani ya kipindi cha miaka 53 leo, wananchi wa Mikoa ya Kusini wa Lindi na Mtwara wamethubutu kuilalamikia Serikali na kuilamu Serikali kwa kipindi chote kwa kushindwa kupeleka huduma muhimu za jamii katika maeneo yetu. Lakini leo tunashuhudia jinsi gani Lindi na Mtwara inatajwa katika Bunge hili na Serikali kwa sababu moja tu, eti kwa sababu tuna gesi ambayo inatoka katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma hakukuwa na sababu yoyote ya kuitaja Lindi ama Mtwara, kwa sababu lilikuwa siyo eneo ambalo linatoa uchumi katika nchi hizo; na eneo hili likatengwa kiuchumi na kuachwa tu lijishughulikie lenyewe. Hatima yake, leo maeneo hayo yamekuwa nyuma kimaendeleo na ndiyo maana sasa kunakuwa na migogoro ya mara kwa mara ya kutaka kujua hatma ya rasilimali yao ya gesi itawanufaisha wananchi wale kwa kiasi gani kwani kwa muda mrefu walitupwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nusu karne sasa. Nusu karne ni makumi matano; ni miaka 50. Ni kitu ambacho tayari matarajio ya Watanzania wengi kuona kwamba kipindi hiki Serikali ingefanya makubwa. Leo kuna nchi kadhaa katika dunia hii. Ni miaka 10 mpaka 20 walitumia rasilimali zao vizuri kabisa na kuwaletea maendeleo yao. Katika nchi hizo ambazo tayari zilikuwa na rasilimali za kutosha, ndiyo wafadhili wetu wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata uhuru katika miaka ya 1960 na nchi hizo nazo pia tumepata nazo uchumi pamoja, lakini imefikia mahali leo wametuacha mbali kimaendeleo, kwa sababu tayari walitoa kipaumbele kwa mambo muhimu na kuhakikisha kwamba wananchi wao wanapata maendeleo. Lakini kwetu katika kipindi chote cha miaka 53 hatukuwa na vipaumbele maalum vya kuwafanya Watanzania wanufaike na rasilimali zao katika Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni katika jumla ya matatizo ambayo tayari ndani ya nusu karne ya Taifa letu Watanzania walikuwa na matumaini makubwa. Leo tunatoka hapa tunakwenda katika Majimbo yetu, ni ajabu, ni kichekesho; eti Mbunge anakwenda kuomba kura kwa wananchi kwa ahadi ya maji. "Mkinichagua mimi, nitahakikisha kwamba nitaleta maji hapa!" Miaka 50 unatoa ahadi ya maji kwa wapiga kura wako?

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa leo tunazungumzia mambo mengine ya muhimu kwa maendeleo ya wananchi wetu, siyo ahadi ya maji. Leo tutajenga barabara! Leo utajenga shule! Miaka 50 tunazungumzia maabara ya Shule za Sekondari katika Vijiji! Miaka 50 tunazungumzia leo habari ya *dispensary*! Nusu karne! Hebu tutafakari, makumi matano, ni kipindi kirefu kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali iliweka nia, ikawa na dhamira ya kweli, miaka 50 ni kipindi kirefu kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Waliofikia ustawi, hawakutumia muda mrefu kama huu ambao tayari tunao. Hivyo ni vyema Watanzania sasa wakaona kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa. Kuna haja ya kuthubutu! Mabadiliko ni kanuni! Wala hakuna haja ya kuhofia ndugu zangu Watanzania, ni kwamba mabadiliko yanawezekana! Hakuna haja ya kufanya hofu! Tufanye kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawatakia kila la heri viongozi wangu wa UKAWA. Sasa Watanzania macho yao yako kwenu, mkae pamoja mhakikishe kwamba mnamteua Mgombea Urais makini ambaye tayari atakidhi haja ya Watanzania ya kwenda katika maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la wananchi wa kusini na kunufaika kwa kuwepo kwetu ndani ya Bunge hili kwa kuwepo Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Leo watu wa Kusini tunatajwa, tunazungumzwa kwa sababu ya kuwepo kwa mabadiliko haya ya kisiasa ya Vyama vingi. Ni watu ambao tulikuwa tunadhalilishwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilomita 850 kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi, zimetumia miaka 40. Laiti kama kusingekuwa na Vyama Vingi vya Siasa, mimi niwahakikishie ndugu zangu wa Kusini barabara ya Kibiti Lindi ingekuwa ni ndoto kwetu. Lakini kwa sababu ya kuwepo kwa mfumo huu, wananchi wa Kusini mna kila sababu ya kuunga mkono mabadiliko ya kisiasa! Mna kila sababu ya kuunga mkono Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, ndiyo mkombozi wetu! Ni sisi tuliodhalilishwa kwa muda mrefu katika Taifa letu. Tulionekana hatuwezi kutoa uchumi mzuri katika Taifa hili, sisi ndio tulikuwa na kambi ya kupigania uhuru katika Bara la Afrika, leo ndugu zetu wanakwenda Afrika Kusini huko wanapigwa! Lakini *source* ya wale kuona kwamba hawa wanakuja kuchukua rasilimali zetu, ni sisi watu wa Mikoa ya Kusini Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ndugu zangu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, tumepigania kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba stakabadhi ghalali inakidhi mahitaji yenu. Uti wa mgongo wa Taifa hili ni wakulima, hususan wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa korosho kwa muda mrefu wamekuwa wakinyanyaswa na kudhalilishwa; lakini kupitia Bunge lililopita kwa kelele zetu. Wabunge wa Upinzani leo tunazungumza kwamba Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, mwananchi ana uhuru sasa wa kuuza korosho zake katika soko lolote, siyo lazima wakauze katika Vyama vya Msingi. Hayo ni mafanikio makubwa baada ya kuwepo kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ahadi za Rais. Ahadi za Rais zimezungumzwa nyingi kabisa, lakini bado utekelezaji wake haujapatikana. Ahadi za Rais ni pamoja na Bandari ya Lindi, lakini katika kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu nimeona kuna Bandari ya Bagamoyo tu, bandari ambayo tayari inaonekana kwamba ni ufadhili wa viongozi wa Serikali kukidhi haja ya kuwepo kwao katika nafasi za utumishi. Kwa maana hiyo, ahadi ya Rais kwa Bandari ya Lindi tunamaliza kipindi cha miaka kumi, ameshindwa kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie suala la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Hili wenzangu wamezungumza sana hapa. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kudhibiti mauaji haya. Imeshindwa kuzuia kabisa! Mwisho niseme kwamba mauaji haya yamepatikana ndani ya kipindi cha miaka kumi. Mwaka 2006 mpaka 2015. Haya ndiyo mauaji yaliyotokea ndani ya kipindi cha awamu ya nne.

Tulitarajia Mheshimiwa Rais Kikwete awe ana uchungu mkubwa juu ya hili kwa sababu limetokea ndani ya kipindi chake. Alitakiwa asaini baada ya hukumu kutolewa kwa wale ambao tayari walihukumiwa kifo. Lakini aliona kwamba kuwahukumu kifo kwa kusaini, ni kuwaua watu ambao tayari wanafanana na wao. Unamuuaje mtu aliyekamilika kwa sababu eti amemuua *Albino*?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi wenzetu wasiokuwa na ulemavu na ngozi wana thamani zaidi kuliko sisi? Kama angeona sisi tuna thamani, basi angesaini kwa mujibu wa hali ilivyo katika nchi hii na aibu ambayo Serikali hii ya CCM inapata dunia nzima huko. Tulitarajia Mheshimiwa Rais Kikwete, baada ya kero zetu kumtaka asaini, amebakiza miezi mitano tu. Atasaini lini mauaji haya ambayo tayari yameitikisa dunia na amefanya Watanzania wasiwe na amani hususan watu wenye ulemavu wa ngozi katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linasikitisha sana. Tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba kabla Mheshimiwa Rais Kikwete hajatoka madarakani, asaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Barwany, nakushukuru sana. Mheshimiwa Nassib Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel Mashishanga. Mheshimiwa Nassib!

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza tumshukuru Mungu sana, mwingi wa rehema kwa neema zake nyingi sana juu yetu. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Mwisho, niseme kwamba naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, UKAWA hawawezi kuipata Serikali kwa sababu wameshaanza kugombana hivi sasa. Wameshaanza kutawanyika mbalimbali, lakini hawana uongozi bora, hawana dira na kwa hiyo, hawafai kupewa uongozi. Ni sawasawa na debe tupu. Wamesema Waswahili kwamba "debe tupu haliachi kupiga kelele." Kwa hiyo, mengi ambayo yamezungumzwa hapa ni kelele na baadaye wengine wameanza kulia humu ndani baada ya kuona kwamba wamefanya makosa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuchangia matatizo ya ajira kwa vijana. Tuna vijana zaidi ya milioni 17 katika nchi yetu na hao ni sawa na asilimia 35, theluthi moja ya wananchi wote. Wengi wa vijana wanahangaika vijiweni, hawana kazi, wengine wanazurura kutokana na tatizo kubwa la kukosa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hivyo, kuna vijana wengi sana wanamaliza Vyuo Vikuu wanapata *degree* na baadaye hawapati kazi wanaingia katika magenge mabaya. Kwa hiyo, ni muhimu sasa kutafakari sana na kuweka mikakati ambayo itawezesha vijana hawa kuweza kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tuipongeze Serikali yetu sana kwa kuweka mifuko miwili ambayo inaweza kuwapatia ajira kwa njia ya kupata mikopo yenye riba nafuu. Mfuko wa kwanza upo Wizara ya Habari, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Katika mwaka uliopita 2014/2015 mfuko huu ulipangiwa kupata Shilingi bilioni sita, lakini kwa bahati mbaya mfuko huu ulipatiwa Shilingi bilioni mbili hii ni sawa ya theluthi moja ya bajeti. Kwa hiyo, vijana wengi waliohamasishwa hawakuweza kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa pili ni mfuko wa Wizara ya Kazi. Ni mfuko wa kuajiri vijana, yaani mfuko wa kuwawezesha vijana kupata ajira. Mfuko huu ulipangiwa Shilingi bilioni 2,925 na ulipanga kwamba Shilingi bilioni 2.5 wapatiwe vijana kama mkopo waweze kujiendeleza na Shilingi milioni 425 wapate mafunzo. Kwa bahati mbaya sana, hata senti moja haikutoka katika mfuko huu na vijana walishahamasishwa kwamba watapata pesa hizi. Waliobakia sasa hivi mitaani wanahangaika, pesa za mikopo hawakupata.

Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Fedha kabla ya kufika Juni, awasaidie Wizara ya Kazi waweze kupata japokuwa nusu ya pesa hizi hawa vijana wapewe pesa kidogo angalau kupunguza makali ya hali ya ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zilipangiwa zitoe asilimia tano ya bajeti yao kwa vijana, lakini Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii tulipopitia, tukagundua kwamba Halmashauri nyingi hazitekelezi mpango huu. Wengine wametoa labda nusu, wengine nusu ya nusu ya pesa ambazo walipangiwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu hili suala lipo kwake, aweze kufuatilia na ahakikishe kwamba pesa hizi zinatoka kwa asilimia mia moja ili vijana hawa waweze kupata mikopo ya riba nafuu wafanye kazi zao na kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nitapenda kuzungumza ni pensheni ya Wazee. Suala la pensheni ya Wazee limekuwa likizungumzwa sana katika Bunge hili kwa miaka mingi. Kwa miaka mingi vilevile wazee wamekuwa wakija hapa Bungeni kujaribu kuwashawishi Wabunge na mara kadhaa wamekuja kuonana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii ili kuomba wasaidiwe katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee ambao sasa hivi wapo wenye miaka zaidi ya sabini ni 1,134,664. Hawa ni wazee ambao wana miaka 70 na kuendelea. Wengi katika hawa wapo katika hali ngumu sana, hawawezi hata kupata mlo wao wa siku moja. Wengine hawana watu wa kuwashughulikia na kadhalika. Basi ingekuwa vizuri tukafuata ule mfumo wa Zanzibar ambao kule watu wote hawapatiwi pensheni lakini wanawapatia pensheni wale wazee ambao wapo katika hali ngumu sana. Kwa hiyo, nafikiri tungeiomba Serikali hapa ika-*consider* labda asilimia 25 ya hawa wazee wenye miaka sabini na kuendelea na kuwapatia angalau pensheni ya Sh. 20,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia labda hapa nitazungumzia *TBC*. *TBC* inakabiliwa na kazi mbili tunakokwenda; kwanza, kuna Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, lakini vilevile kuna

kura ya maoni ya Katiba. Chombo cha habari ambacho kinakwenda nchi nzima, ni *TBC*, hakuna kingine. Lakini wao sasa hivi wanakabiliwa na vyombo ambavyo ni chakavu sana, *Camera*, magari na vitu vinginevyo. Hata ukienda katika *Studio* yao huamini kama kweli *Studio* hii ni ya *TBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika wanadai mashirika, taasisi za Serikali na Wizara pesa nyingi sana. Katika bajeti iliyopita tulisema hapa, taasisi zote, Wizara zote na mashirika yote ambayo yanadaiwa na *TBC* basi pesa zao zikatwe katika bajeti, wapelekewe ili waweze kuendesha shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vilevile wana kodi *satellite*, haya matangazo ambayo sasa hivi hapa yanatoka moja kwa moja wanatumia *satellite* ambayo ina gharama kubwa sana. Inabidi walipie gharama za kukodi hii *satellite*. Kwa hiyo, naomba vilevile Serikali ikaliangalia suala hili na kuweza kuwasaidia katika kuwalipia gharama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninasema tena naunga mkono hotuba hii mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nassib Omar. Mheshimiwa Rachel Mashishanga atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Nundu.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba niwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kwa kuendelea kutuamini Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), shukrani za pekee ziwaendee wananchi wa Manispaa ya Shinyanga kwa sababu wamefanya *wonders* katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Vilevile niwashukuru wananchi wote wa Shinyanga kwa sababu wameonesha ushirikiano wao kwangu kwa maana kwamba tumeshirikiana katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa pamoja na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, nimekuwa nikisikiliza hoja za wenzangu toka juzi, nimegundua kwamba Upinzani tunalalamika, wenye Serikali na wenyewe wanalalamika, wakusanyakodi wao wanalalamika. Sasa kama wote tunalia, basi ngoja na mimi nilie za kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze suala la uwekezaji. Nashindwa kuelewa mantiki ya uwekezaji katika nchi yetu. Manispaa ya Shinyanga tumebahatika kuwa na viwanda zaidi ya viwili ambavyo vipo chini ya Wachina. Kuna Kiwanda cha Ngozi na kuna Kiwanda cha Wachina kinaitwa ***Duong Nho Textile***, hiki kiwanda kinatengeneza nyuzi lakini mkataba wake ni kutengeneza nguo. Mbali na kutengeneza nyuzi, kiwanda hiki hakijalipa *building permit* mpaka leo, Shiling milioni 221; kiwanda hiki kiliahidi kitachukua Watanzania wanaoishi yale maeneo jirani 500 wafanye kazi, lakini wamechukua 20 tu, lakini wenyewe wapo 17. Yaani 17 ni wenyewe Wachina, kwa maana hiyo ni watatu tu ndiyo wameajiriwa. Yaani hapa nazungumzia 17 ndiyo wameajiriwa, yaani wao ndio wamejiajiri kwenye hicho kiwanda, lakini wengine wote wanafanya kazi za vibarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuuliza kwanini Serikali inawafanyia hivyo Watanzania? Tunaujua Mkoa wa Shinyanga; Watanzania waliopo Mkoa wa Shinyanga wanalala juu ya dhahabu, almasi inachimbwa pale, lakini nashangaa tupo nyuma kwa kila kitu. Leo hii hawa Wachina tumewafanya miungu watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kuna Viongozi wa Serikali waliopo katika Mkoa wa Shinyanga hususan Manispaa wamekuwa wakienda kupata vitu vidogo kwenye hivi viwanda, matokeo yake mikataba inakuwa haifuatwi, kwa hiyo, usimamizi unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie upya hivi viwanda, kwa maana hata hiyo ardhi yenyewe imeporwa kwa kisingizio tu kwamba iko chini ya *EPZ,* kitu ambacho siyo cha kweli. Naiomba Serikali iviangalie upya hivi viwanda ambavyo vipo Manispaa ya Shinyanga kwa sababu vinafanya kazi pasipo maelewano na Uongozi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna kiwanda cha ngozi. Kiwanda hiki kinadaiwa Shilingi milioni 197, hawajalipa *building permit,* hivi hao Wawekezaji tunawakumbatia kwa kazi gani? Ni Serikali gani hii inayosema ni sikivu, mtu anatoka huko China anakuja kuwekeza lakini halipi *building permit* kwenye eneo la Watanzania? Inasikitisha sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, *product* wanazotengeneza pia hazikaguliwi! Lakini *on top of that,* wafanyakazi wanaofanya kazi katika hicho Kiwanda cha Ngozi, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Yaani fikiria, ngozi zinakaushwa kwa chumvi; wanashika zile ngozi kwa kutumia mikono yao, hawana kitu chochote ambacho kinaweza kikawasaidia afya zao zisitetereke au afya zao zisiwe hatarini. Kwa hiyo, naomba sana hili suala la hivi viwanda vilivyopo Shinyanga viangaliwe kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia tena suala la elimu. Mkoa wa Shinyanga upo nyuma sana kielimu. Kila siku Shinyanga tupo mwisho. Hii sasa imetuchosha! Kwanini kila siku tunakuwa wa mwisho? Labda nizungumzie hususan Manispaa ya Shinyanga. Kwanza, hatuna Walimu wa Sayansi. Utakuta Mwalimu wa Sayansi anafundisha shule tatu kwa siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kwa kweli inasikitisha sana. Naiomba Serikali, basi iangalie uwezekano wa kuwapa *incentives* Walimu ili anapoenda Shinyanga apewe hata motisha ili waendelee kukaa pale na watoto wetu wapate elimu ya sayansi, kwa sababu tunajua kadri siku zinavyoenda teknolojia inazidi kuwa juu. Lakini Walimu tunawasahau sana! Walimu waliopo Shinyanga wanadai hela nyingi sana. Kuna malimbikizo mengi sana ambayo wanadai, mpaka sasa hivi hakuna hata mmoja ambalo wamelipwa. Naomba Serikali iangalie hilo ili Walimu waendelee kufanyakazi zao kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za kufundishia nilishazungumza na mwaka 2014, hawalipwi posho! Kwanini Serikali inashindwa kuwalipa posho? Mbona sisi tunalipwa posho za kukaa tu kwenye Kiti hapa? Sisi tunafanya kazi gani? Kwa nini Walimu wasilipwe? Naomba sana hili suala liangaliwe kwa umakini sana kwa sababu hakuna ambaye hajafundishwa na Mwalimu hapa, kila mtu kafundishwa na Mwalimu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni afya. Tunashukuru Manispaa ya Shinyanga kwa ujumla, tuna Vituo vya Afya tisa na zahanati siyo vijiji vyote ila zipo. Kinachosikitisha ni kwamba umeme unapokatika nyumbani kwangu, basi na kwenye Kituo cha Afya umeme unakatika, kitu ambacho siyo sahihi. Kwa nini hamweki *standby generator*? Kule kuna akina mama wanajifungua, sasa umeme ukikatika mama anajifungua, unafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie hili, matumizi mengine yasiyo ya msingi tuyapunguze, kwa sababu akina mama wanapata shida sana. Mliwaambia wakiwa wanaenda hospitali watakuta *gloves* na kila kitu. Lakini sasa hivi mwanamke akienda kujifungua

ni lazima awe na kibegi amefungasha kila kitu mle ndani. Kwa kweli hii siyo sawa, mnawatendea vibaya Watanzania na huku mnakusanya kodi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kuhusu suala la Hospitali ya Rufaa. Hiyo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa inajengwa sehemu moja inaitwa Mwawaza. Toka imeanza kujengwa, zimetolewa Shilingi bilioni moja tu; na gharama ya huu ujenzi ni Shilingi bilioni 100. Sasa nataka kusema, mnatuhadaa watu wa Shinyanga au vipi? Mnataka kuniambia kila mwaka mtakuwa mnapeleka Shilingi bilioni moja! Kwa maana hiyo hii hospitali itaisha baada ya miaka kumi! Naombeni sasa mwangalie vizuri kwa sababu wananchi wanapata shida sana, wanashindwa hospitali ya Mkoa, gharama zimekuwa kubwa; na hii hospitali ndiyo wanayoitegemea. Vituo vya Afya havina madawa, havina chochote kile, wafanyakazi wenyewe hawatoshi. Kwa hiyo, naomba mwangalie huu Mkoa kwa sababu una mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 71 mpaka 72 alizungumzia kuhusu wazee wenye ulemavu kuwawezesha kiafya, kielimu na mikopo. Nataka kumwuliza Waziri Mkuu, Wazee wa Mkoa wa Shinyanga ni wangapi wamenufaika na hii mikopo? Kama kweli hii mikopo inatolewa, nilikuwa nataka tu nijue mikopo hii imewanufaisha wazee wa Shinyanga kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi mkubwa wa *Lake Victoria*. Mradi huu tunashukuru tumeupata, unaenda vizuri, lakini kuna changamoto. Mradi huu ulikuja Shinyanga kwa makusudi, lakini haujaenea bado Mkoa wa Shinyanga, sasa hivi tayari umeshaanza kwenda Mikoa mingine, wakati Shinyanga Wilaya zake bado, ni Kahama tu ndiyo iliyopata haya maji. Solwa wamepata maji kidogo tu, lakini bado kuna vile vijiji vinavyopita pembeni kilomita 12 za pembeni ya bomba, hakuna kijiji ambacho kimepata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna kijiji kwa mfano Kata ya Mwamalili kuna bomba kinapelekwa Kishapu sawa, maji yanaenda Kishapu kwa sababu ni Wilaya ambayo ipo Mkoa wa Shinyanga, lakini wanavijiji wa pale wamechimbuliwa maeneo yao, wamechimbuliwa mazao yao kwa sababu ya lile bomba lakini hawajalipwa fidia.

Nilikuwa naomba Wizara iangalie kuwalipa fidia hawa wananchi wa hicho kijiji kwa sababu bomba limepita bila maelewano na Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hospitali ya Kolandoto. Hii hospitali inategemewa sana na wakazi wote wa Manispaa ya Shinyanga na Mkoa wote kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba iangaliwe sana kwa sababu ruzuku inaenda kwa kuchelewa, wafanyakazi hawalipwi kwa wakati, madawa hayaendi kwa wakati. Lakini kwenye hii hospitali kuna Kituo cha Wazee, Walemavu wa Ukoma wanaishi katika mazingira magumu sana. Naomba Serikali iangalie wazee hawa ili mwisho wa siku waweze kuishi vizuri na waone Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nizungumzie suala la wachimbaji wadogo wadogo. Hotuba ya Waziri Mkuu imezungumza kwamba zimetolewa Shilingi bilioni 1,400 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo ili wafaidike na kupewa zana za kisasa. Nilikuwa na swali tu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ni wachimbaji wadogo wangapi wa Mkoa wa Shinyanga ambao wamefaidika na hii Shilingi bilioni 1.4?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashishanga tunakushukuru sana, ahsante sana. Mheshimiwa Omar Nundu, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Mallac.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nami nafasi ya kuongelea hotuba hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote ile inapopata Serikali wananchi ambao wana nia njema na nchi yao, wanakusanyana pamoja na kujikita katika maendeleo ya nchi yao, tofauti zao wanaziweka kando.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa uzoefu ambao nimeupata kwa miaka takribani minne na nusu niliyokuwa hapa hivyo sivyo ilivyotokea. Baada ya Uchaguzi, watu hapa walitamka kabisa, nchi hii haitatawalika. Unaposema nchi haitatawalika, kwa mantiki yoyote linalokuja akilini ni kuwa fujo zitaanzishwa na tumeona fujo zikianzishwa hapa; kugoma kutashamiriwa sana, tumeona ugomaji ukishamiriwa; kuvuruga taratibu za Bunge, tumeona taratibu za Bunge zikivurugwa; kuandamana, tumeona watu wakiandamana; kuzuia kwa makusudi maendeleo yasipatikane, hasa kuhakikisha kuwa bajeti iliyopangwa haitekelezwi, tumeona hayo yakitendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu na Watanzania; pamoja na jitihada zote hizo, bajeti imetekelezeka. Imetekelezeka kwa kudra za Mungu pamoja na jitihada za wananchi kwa wingi kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisikiliza kwa makini sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaiunga mkono moja kwa moja. Kuna mambo muhimu yameelezwa na takwimu zimetolewa na hakuna la kupinga kuhusu hilo kwa sababu ndivyo mambo yalivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu miradi yake imeongezeka kwa asilimia 81; maji asilimia 80; nishati asilimia 79; kilimo asilimia 77; barabara kilometa 3,884 zimejengwa kwa lami; mfumuko wa bei umepungua kutoka nukta 6.1 mpaka 4.3; nchi hii inatawalika na inatawalika chini ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliokuwa wakileta fujo hizi, wamefika mahali wamepwelewa kabisa! Saa nyingine naona kama ni mchezo wa kuigiza watoto wanapocheza gololi zile. Kama hutaki kucheza, unasema jamani eeh, nachukua gololi naenda nazo! Unazidi unawaambia watu; yaani yuko kwenye ulinge mtu anakwambia njoo hapa tuoneshane ufundi! Unamwambia toka hapo, nitakupiga! Maneno gani haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maneno ya watu ambao wanajua hawana ubavu wa kushindana na mtu yeyote. Haya ni maneno ya watu ambao wanajua wananchi wa Tanzania ni weledi wanaelewa wanataka maendeleo ya nchi yao, hawataki longolongo. Ndiyo hali ilivyo. Mtupishe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani sera sasa hivi imekuwa mtupishe! Tupisheni! Tuwapishe mfanye nini? Muichafue hii nchi? Hatuko hapa kumpisha mtu yeyote, tutaendelea kuendeleza hii nchi! Tumetoka kwenye inisha! Tumeikomboa Afrika, tumemaliza kazi. Tulikuwa rasilimali zetu hatujazitambua kwa wingi, tumefanya kazi, gesi imepatikana,

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga kule wanaanza kufanya utafiti wa mafuta. Sasa hivi inisha ya maendeleo imekwisha! Kwa hali yoyote tunakokwenda tunakwenda kwa kasi kubwa kuiendeleza hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vitatizo vidogo vidogo vinavyoletwa na mtu mmoja mmoja hivi, tunavipiga virungu tu! Kabisa! Tunawaondoa, tunakwenda mbele! Watanzania mwangalie,

maendeleo makubwa ya nchi hii yanapatikana kwa Chama cha Mapinduzi, Chama ambacho kina uzoefu, kimebobea, kimejipanga katika kila nyanja! Chama ambacho tunabadilishana; leo anakwenda yule anafanya kazi, akishafaulu vizuri, anampisha mwenzake anafanya kazi, tunakwenda. Sio watu ambao wanafikiria watakuja hapa kujaribu jaribu tu. Hatuko katika hali ya kujaribu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Tanga linabadilika sana. Mwaka 2010 tulipoingia pale, ukitaka kwenda Mombasa ni kazi! Ukivuka mpakani unaona aibu huku ulikotoka. Sasa hivi nenda kajaribu kwenda Horohoro uone kazi pale! Barabara safi kabisa. Jiji la Tanga katikati pale angalia lami ilivyojengwa, barabara ya 15 ilikuwa na mashimo shimo; kipindi cha mwaka mmoja tumeweka vitu sawa. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hapo sasa!

MHE. OMARI R. NUNDU: Tumejenga pale Kituo cha Mabasi, Hospitali ya Wilaya tuliona Hospitali ya Bombo haitoshi! Eeh, imezidiwa! Tumeijenga Hospitali ya Wilaya, sasa hivi iko katika hatua za kumalizika. Tumeboresha Vituo vya Afya! Nenda Pongwe ukaone, mpaka *operations* zinafanywa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga mwaka 2010 inahesabika kama ni Jiji la Tanga, imesahauliwa kuwa ina Vijiji na Vitongoji! Nenda kaone maguzo ya umeme sasa hivi mpaka ndani huko! Nenda kaone maji yanavyowekwa! Tunasema tu, nia ya kumaliza kuweka miradi ya maji na umeme ipo na kazi imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoiomba Serikali, tuhakikishe hayo tunayamaliza. Ndiyo maana katika ushauri ambao ningewapa Serikali sasa hivi, tuangalie vitu vikubwa katika bajeti yetu ambavyo tunaweza kufanya kwa pesa zetu wenyewe. Hili suala la maji mliwekee bajeti ya kutosha limalizike kabisa nchi nzima. Hili suala la umeme mliwekee bajeti ya kutosha limalizike nchi nzima! Suala la afya limalizike nchi nzima! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu, watu hawa sijui wamesoma *management* gani, labda kina Peter Drucker huko! Akina Tom Peters ndiyo *management* tunayoitumia sasa hivi. Unajenga mashule halafu unaanza kuyaweka vizuri; na mashule ya Kata yamejengwa; na matokeo yanaonekana sasa hivi. Maabara, tunamaliza. Mlishughulikie suala la elimu hili kikamilifu nalo tulimalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku kwingine kwa mambo ya bandari na reli na nini, tuwaachie watu ambao wana pesa hapa, tukae nao vizuri waweze kuja kujenga hii; watoke nje na watoke ndani. Ni rahisi sana. Mimi nilipokuwa Waziri niliwaita akina Ndugu Bakhresa pale wafanye kazi hii. Tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga ukiondoa suala la barabara, unapokuja suala la Mji wa Tanga wenyewe ulivyo, uchafu wake, kwa kipindi cha mwaka mmoja tumejenga mifereji mikubwa inayopeleka maji mpaka baharini. Mvua ikinyesha baada ya muda mji umekauka kabisa, hauna maji pale! Hayo ni maendeleo ya sasa hivi tunayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumerudisha vibao vile vya kuonesha barabara, sasa hivi huhangaiki! Barabara ya Nane unajua iko wapi, Barabara ya Tisa umewekewa vibao, njia hii unaingia hii, unatoka na nini, yaani Jiji la Tanga linakwenda. Naomba Wizara ya Ardhi sasa hivi tuanze mpango ambao niliuomba. Naona Naibu Waziri ananiambia hii ya kutengeneza *Master Plan* ya mji mzima inaenda kwa *concept!* Tanga siyo cha *concept!* Tumesema Tanga nzima ni

Jiji la Tanga, hakuna mitaa. Sasa hivi inatakiwa, Jiji la Tanga *Master Plan* yake ifanyiwe mpango kabambe ipatikane! Jiji la Tanga liwe mfano wa miji hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kuhakikisha kuwa viwanda vinarudi, tulipofika pale akina Foma wamekufa na Ndugu yangu Mheshimiwa Turky anajua! Tumekazania Foma inafanya kazi sasa hivi; tumeikazania *Tanga Fresh* inafanya kazi sasa hivi; Gardenia inafanya kazi sasa hivi; *Rhino* ilikuwa haiendelei, ni kiwanda cha *Cement* kilikwama. Tumeongeanao, kiwanda kinamaliza kujengwa sasa hivi! Viwanda vya Chuma na viwanda vya **Six** *Saw Mill,* tunaongeanao kwa karibu na tumewapa muda, wakishindwa sisi tutapigana mpaka tuwanyang'anye. Tunahakikisha vile vitu ambavyo vinatakiwa viendelee, vinakwenda na tunapiga hatua kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari nilipoingia mimi mwenyewe, bahati mlinipa Uwaziri wa Uchukuzi, nikakuta bandari inapata hasara Shilingi bilioni sita. Nikatumia nafasi yangu siyo kwa niaba ya Tanga tu, lakini kwa Tanzania nzima, nikawaambia bandari, tia Dola milioni 10 pale! Wakatia Dola milioni 10, bandari ile imetokana kabisa na kupata hasara, iko sasa kwenye kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu Serikali mwangalie suala hapa, mmeongelea Bandari ya Bagamoyo tu. Bandari ya Bagamoyo peke yake haiwezi kutuendesha Tanzania nzima! Bandari ya Tanga nayo muiangalie. Kama ni ya Mtwara, kama ni ya Tanga Mjini mwangalie na hali kadhalika Mtwara. Najua hayo yatafanyika kwa sababu, huko ndiko tunakokwenda. Mweke huko bandari za nchi kavu, ili usafiri huu uandamane vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka sasa Wizara ya Maji na Nishati inisikilize vizuri. Kuna sehemu ambazo hapa kazi imeshafanyika na wanashukuru sana kwa hizo na Manaibu Waziri wa Wizara zote nimekwendanao mara chungu nzima kuangalia hilo, naomba waende, lakini Vijiji hivi ni lazima sasa vifanyiwe kazi, kama siyo sasa hivi kumalizika katika huu mpango ninaosema wa kujikita katika maji na umeme, tunahitaji kazi ile imalizike kwenye vijiji vya Marungu, Mkembe, Geza, Msengenyeni, Mbugani, Kivumbitifu, Majengo, Nema, Masiwani Mwisho, Mgwisha, Mahere, Tongoni, Sadani, Mahere, Mtambuni, Mapojoni, Kilombero, Shaurimoyo, Kirare, Tundauwa, Mpirani, Mijohoroni, Masai, Kiruku na vingine vingi. Nimechanganya zote maji na umeme, kazi hizo mbili nitaongeanao wenyewe kwa kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule wananchi wanasema Chama ambacho kinaweza kututoa kwenye matatizo ni Chama cha Mapinduzi tu, hakuna kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuanze kujikita, tuifanye kazi hii, tutekeleze yale ambayo tunaweza kuyatekeleza kwa kasi hii ambayo imeshaanza kupamba moto sasa hivi; na tukifanya hivyo, nchi hii haitaingiliwa na mtu yeyote kufikiria watakuja hapa waharibuharibu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga tumepigania asilimia tano ya vijana. Halmashauri ya Tanga mwaka huu imetenga Shilingi bilioni moja kwa ajili ya vijana na wanawake. Kazi tuliyonayo ni kuhakikisha pesa hizo zinatoka.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Omar Nundu. *(Makofi)*

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunashukuru sana. Maana mambo ya Tanga hayo yalivyomwagwa hapa, jamaa zangu wamebaki wanatoa macho tu!

Mheshimiwa Anna Mallac, atafuatiwa na Mheshimiwa Gen. Ngwilizi!

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu nami niweze kuchangia kidogo katika suala lililopo mbele yetu. Aidha, nianze kwa kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema na nguvu ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja, kutokana na muda niende kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni miaka mitano sasa tumekuwa tukiongelea kuhusu bajeti na matumizi mengine. Tumeongelea mipango ya miaka mitano; Serikali ni hodari sana wa kupanga mipango, lakini utekelezaji wake ni mgumu sana. Mwananchi anaweza kuipokea bajeti hii ambayo ni tamu sana katika masikio yetu kwa kuisikiliza na kuitamka, lakini tukienda kwenye utendaji, bado tuko katika wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikoa iliyopo hapa nchini kuna baadhi ya Mikoa imesahaulika sana katika utendaji mzima wa bajeti ya Serikali. Nikianza na masikitiko ya Mkoa wangu wa Katavi, japokuwa nchi nzima matatizo yamefanana, niende kwenye suala zima la reli. Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi tuna injini mbili ambazo zinapiga *trip* kutoka Tabora kuja Katavi, Mpanda, lakini injini zile ni mbovu tena ni mitumba. Jamani injini zinatutesa zile! Injini zinafeli njiani huku zimebeba abiria; injini haiwezi kupanda mlima, inashindwa kusukuma hata mabehewa 10! Jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyoongea, mazao yamelundikana Stesheni ambayo yalikuwa yapelekwe Kaskazini. Injini imeshindwa kusukuma mabehewa 10 tu! Abiria wanasafiri; kwa sababu ukiangalia asilimia kubwa ya wananchi wa kipato cha chini wanategemea kusafiri kwa treni, kwenye mabasi hawawezi, gharama! Lakini wengi wanategemea treni, lakini ni kulala njiani, treni haiwezi kupanda mlima, wakati mwingine inafeli inazima na taa, eeh! Usalama wa abiria unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mara ya mwisho naomba kwa kupunga mkono, Serikali itupie macho katika Mkoa masikini ule. Japo ni tajiri wa rasilimali na umekuwa ukiingizia Taifa pato kwa sababu ya rasilimali zake kiuchumi. Kwa hiyo, naomba tupatiwe injini mpya zilizoingia katika hizo 13. Naomba watuondolee hizi injini za *73 class,* ni mbovu na ni mitumba. Naomba tuletewe injini mpya ambazo ni *90 class,* hizi zina nguvu na zitatufaa wana Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inisikilize, naongea kwa mdomo, tena kwa nia nzuri, sio lazima niwatolee macho, niwainulie mikono, niwatikisie kichwa! Naomba mtusikilize wana Katavi mtuhurumie! Hili nimemaliza, nakuja kwenye barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ndiyo njia ya kufungua fursa za kiuchumi, lakini tulipo pale Katavi, lami tunazisikia kwa wenzetu. Imekuwa ni hadithi, barabara za lami, barabara za lami, barabara za lami! Tunakaa mkao wa kupokea, mkao wa kula, mkao wa kunufaika; lakini miaka sasa imeyoyoma, lakini jamani lami hatuna. Eeh! Hatuna kiunganishi cha barabara za lami kutoka Mkoa kwenda Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga imekuwa ni hadithi; inasuasua sana japokuwa kweli, Serikali inaweza kuwa ina nia nzuri, lakini Watendaji utendaji wao ni mbovu, ufuatiliaji wao ni haba. Mmegubikwa na rushwa; naona kuna watu ambao wamekumbatia rushwa, ni wazembe na wenye tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifuatilie, barabara ile itengenzwe haraka ya kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga. Mbona wenzetu wa kutoka Sumbawanga kwenda Tunduma wameweza jamani? Sisi mnatuonaje? Mnatufikiriaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba barabara ya kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga, barabara ya kutoka Mpanda kwenda Koga mpaka Ipole; barabara ya kutoka Mpanda kwenda Mishamo kwa kiwango cha lami. Mtakuwa mmetutendea haki sana na mtakuwa hamjatudumaza kiuchumi. Kwa sababu, mpaka sasa hivi tumedumaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mavuno yameshawadia Mpanda; tunavuna mahindi, mpunga, sijui tutasafirisha kwa kupitia barabara gani! Tukienda kwenye reli ni matatizo, tukienda kwenye barabara ni matatizo! Tumekosa nini kwa Mwenyezi Mungu? Tunaomba Serikali itufikirie sana kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye suala la elimu, elimu ndiyo mmejitahidi, mmejenga Shule za Sekondari kila Kata, lakini shule hizo hazina Maabara! Shule hizo Walimu ni pungufu! Bado Walimu wale wana matatizo chungu nzima, hawana nyumba za kuishi, mazingira yao ya kufanyia kazi ni magumu! Sana sana mkijitahidi kujenga nyumba, labda mbili, tatu, lakini Walimu wengine wote wako uraiani, wanaishi katika mazingira magumu sana na hii ni kwa Walimu wa Sekondari na pia wa Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile miundombinu ya mabweni ya wasichana naomba yajengwe ili tuweze kuondokana na suala la mimba za utotoni kwa wasichana. Kwa sababu mazingira ambayo wanayo ni magumu sana. Msichana anafaulu, anapangiwa shule ya mbali, kwa hiyo, katika kuifikia ile shule inabidi akodi bodaboda kila siku! Mle njiani na huyo dereva wa bodaboda, dada unasemaje? Naomba jioni tuonane. Matokeo yake mimba, mtoto elimu ndiyo inaishia hapo! Kwa hiyo, bado miundombinu iboreshwe katika elimu, *hostel* zijengwe ili watoto waweze kusoma kwa raha na wapate manufaa kwa wakati mgumu kama huu walionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *UKIMWI* kwa sababu ndiyo Kamati yangu, naishukuru na kuipongeza Serikali, kupitia Kamati yangu kwa kuliona suala la kuanzishwa kwa Mfuko wa *UKIMWI* wa Taifa. Hili suala ni jema sana kwa sababu kuanzishwa kwa Mfuko kutakuwa kumetupunguzia ule utegemezi tuliokuwa tumezoea. Kwa sababu, sasa hivi wafadhili wengi wanajitoa kutusaidia.

Kwa hiyo, endapo ule mfuko utasimamiwa vizuri na Serikali, fedha zikatumika jinsi zilivyopangwa, zisichakachuliwe zikapelekwa kwenye miradi mingine, naona tutafanikiwa sana. Kwa sababu, ule mfuko fedha kama zitatumika vizuri zitatusaidia kununua madawa ya *ARV,* zitatusaidia kununua vitendea kazi vya hospitali na dawa nyingine za magonjwa nyemelezi. Kwa hili nawapongezeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona mwisho wangu ndio huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Anna Mallac. Kama nilivyosema mwanzo kwamba Mheshimiwa Gen. Ngwilizi ndiye atakayefuata na baada yake ni Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake ambayo ameitoa humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ni kielelezo cha utekelezaji wa Ilani ya *CCM.* Hotuba hii inaeleza katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imefanya nini, iliahidi nini. Kwa kweli Serikali na Chama cha Mapinduzi ina kila sababu ya kujivunia. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi nawaombeni sana, hakuna sababu ya kuinama chini, Serikali yetu imejitahidi kutekeleza Ilani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengine ambayo hayajatekelezwa, lakini huwezi kutegemea kila kilichoandikwa kikatekelezwa. Utekelezaji wa Ilani, utekelezaji wa matarajio unachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Marekani wana miaka 300 sasa karibu tokea wawe huru, kuna mambo mpaka leo bado wanayafanya! Sisi tuna miaka 50 tu, kwa hiyo, ni lazima tukubali kwamba kuna mambo mengi ambayo tutakuwa hatujayafanya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza sana, Serikali yetu imefanya kazi nzuri sana. Hiyo ni kwa upande wa Hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile na huko Mlalo nako, Ilani ya *CCM* imetekelezwa na wananchi kuonesha kwamba, kweli wanakubali kwamba, *CCM* imesimamia utekelezaji wa Ilani yake, katika Wilaya yetu ya Lushoto katika uchaguzi uliopita Vijiji vyote asilimia mia moja vimekwenda na *CCM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni katika Jimbo la Mlalo, Jimbo la Lushoto, Jimbo la Bumbuli, Vijiji vyote! Tumewaachia Vitongoji 26 katika Wilaya nzima ili wenzetu waanze kujifunza maana ya kutawala ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema kwamba kweli bado zipo changamoto na changamoto hizo hakuna mwingine wa kuzitekeleza isipokuwa ni sisi wenyewe. Siyo wakati wa kusimama na kulaumu na kutegemea kwamba ukijua sana kuonesha kidole ndiyo unapata *point* mbele ya wananchi. Naamini kwamba mwezi wa Kumi CCM itapita uchaguzi, kwa hiyo, wenzetu wanaojipa moyo kwamba sijui kuna UKAWA utaingia wao waangalie ngoma ya mwezi wa Kumi, mwezi wa Kumi CCM itachukua, itaongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimesema Ilani ya CCM huko Mlalo tumetekeleza vizuri tu, upande wa mawasiliano katika Jimbo lile, Kata zote isipokuwa Kata mbili ndizo ambazo hazipata mawasiliano, Kata ya Mbaramo na Kata ya Rangwi, lakini Kata zingine zote mawasiliano yapo, kuna maeneo kwa sababu ya hali ya milima unakuta kwamba mawasiliano hayapatikani moja kwa moja lakini hiyo tunajua na kwamba muda si mrefu mawasiliano yatapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mawasiliano ya barabara; Mlalo hakuna barabara ya lami, lakini barabara zetu zinapitika isipokuwa kuna kipindi cha mvua ambacho saa zingine kwa sababu ni mvua barabara zinaharibika, kwa mfano wakati huu, lakini hatuna wa kumlaumu, ni mvua sasa tumwombe Mungu isinyeshe mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kama ile ya kutoka Lukozi, kupitia Malolo kwenda mpaka Kelei wakati huo mvua haipitiki, nawaomba ndugu zangu wa *TANROAD* wanajitahidi sana kufungua barabara zile za Mlalo, nawaomba waingalie barabara ile kwa sababu wananchi sasa wanapata shida, mabasi hayaendi kule, lakini tunaamini kwamba baada ya mvua hizi barabara ile itatengenezwa na magari yataweza kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa maji, maji yanapatikana kila mahali isipokuwa kwenye Kata ya Sunga, mradi ule wa Kata ya Malolo utatekelezwa hivi karibuni. Kwa hiyo, maji siyo tatizo sana. Kulikuwa na maeneo manne, matano ambayo yalikuwa na matatizo ya maji hayo yamekwishapatiwa maji; Kijiji cha Mkundi wa Mbaru, Mkundi wa Mtae na maeneo ya Kijiji cha Mwandege, lakini kote huko sasa maji yanapatikana vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu, elimu tunaendelea vizuri, tunazo shule za msingi katika kila kitongoji na shule za sekondari katika kila Kata; Jimbo la Mlalo sasa hivi lina sekondari 28, maabara zimejengwa, ziko katika ngazi tofauti hivi karibuni tu tutakuta kwamba nazo tutazikamilisha. Afya kila kijiji sera ile ya Serikali kwamba kila kijiji kiwe na zahanati sisi tunaendelea kutekeleza hilo sasa hivi kuna matatizo ya hapa na pale ya Waganga, lakini tunajua kwamba Waganga watapatikana kwa sababu siyo rahisi kupata Waganga mara moja, inachukua muda kufundishwa. Kwa hiyo, nao tunaamini kwamba watapatikana na dawa zitaendelea kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme katika Jimbo la Mlalo unaendelea kuwekwa, nguzo zinaendelea kukitwa, waya zinavutwa isipokuwa kuna Kata mbili; Kata ya Mbaramo na Kata ya Hemtoye ndizo ambazo hazimo kwenye awamu hii ya pili, lakini awamu ya tatu tunaamini kwamba itakuwepo na mradi wa umeme utakuwa umekamillika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yote hayo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uliangalie suala moja tunaanzisha maeneo mapya ya utawala, tunaanzisha wilaya, mikoa, linalojitokeza sasa hivi ni kwamba wilaya inakatwa kutoka wilaya mama halafu tunapeleka watumishi pale, majengo hayapo, *DC* unamkuta anajibanabana tu, unakuta Polisi hawana mahali pa kukaa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni muhimu sasa tuweke sera kwamba wilaya itagawanywa sawa, lakini *priority* ya kwanza tuhakikishe majengo yanakuwepo. Kwa sababu sasa hivi tunavyokwenda na bajeti zetu hizi tunategemea Wizara ya Mambo ya Ndani ijenge Kituo cha Polisi, tunangojea Mahakama fedha zitengwe kwenye Wizara. Sasa kwa utaratibu huo kwa kweli tutajikuta kwamba wilaya zinaanzishwa na zinachukua muda mrefu sana kutengemaa. Naomba Serikali iliangalie sana jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Jenerali Ngwilizi. Nilishamtaja Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. La kwanza unajua huu ni mwaka wa uchaguzi, sasa ndugu zangu Wabunge wenzangu wanaona kwamba inawezekana uteuzi ndani ya Chama ukawapitia pembeni, wanaanza kujikombakomba wanaongea mawili mazuri, halafu wanaongea 18 mabovu. Sasa unaposifia mawili halafu unalalamikia kumi na nane, tafsiri yako sijui kama ni Serikali imefanikiwa ama ni unafiki wetu tu wa kujiridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshtuka zaidi, nikamuona na bwana Mrema naye amesifia, inaonekana muziki wa UKAWA kule Vunjo unamtisha sana, naye kalalamika. Wenzetu wanajitekenya wenyewe, halafu wanacheka wenyewe, sidhani kama inasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipitia vitabu vya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, huu mpango siyo wangu, ukurasa wa nne wanatuambia kilimo ambao tunaita ni uti wa mgongo wa Taifa hili ambao unaajiri asilimia 75 ya Taifa hili, kwa miaka kumi mfululizo kimekua kwa asilimia 4.2 tu. Kwa hiyo, tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni kwamba toka Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alivyoingia madarakani mwaka 2005 mpaka sasa hivi ameshindwa kupiga hatua hata kiduchu kwenye kilimo. Halafu wanasimama watu hapa, wanaotoka kwenye Majimbo maskini, ambao wengi ni wakulima, wanasifia, halafu Serikali kwenye kilimo ikisema mafanikio yake kwenye maandiko ya Waziri Mkuu, kwenye Taarifa ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa, inasema eti kupata hati mbili za mashamba mawili, hivi ni akili au ni matope? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunavyozungumza mambo *serious* yanayohusiana na mustakabali wa wananchi wetu, tuache kuzungumza biashara ya choo kimoja kimoja tulichokijenga kwenye vijiji huko, tuzungumze *issue* kubwa zinazohusiana na mustakabali wa Taifa. Haiwezekani sekta inachangia asilimia 40 ya pato la Taifa, miaka kumi mfululizo imekuwa kwa asilimia 4.2, mnatueleza nini, mafanikio eti ya Jakaya. *(Makofi)*

Kuna mtu alisema hapa kwa miaka kumi hatujawa na Rais, Mheshimiwa Wenje, kwa takwimu hizi za Serikali tulikuwa tunapiga *mark time* tu, Rais alikuwa yuko *busy* anabadilisha ndege tu, kwa sababu asilimia kubwa muda wa Rais wetu yuko angani. Sasa ukiwa angani unawezaje kusimamia nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, deni la Taifa, Rais Jakaya Mrisho Kikwete anaingia madarakani mwaka 2005 deni la trilioni saba kwenda trilioni nane miaka kumi baadaye, Ilani ya CCM hiyo, si myaseme haya siyo mnaongea biashara ya vyoo, sijui vizahanati huko, deni la Taifa limeongezeka kutoka trilioni saba mpaka 35, hilo deni analipa nani? Sasa tukiwauliza, kuna uhusiano gani kati ya nyongeza ya deni la Taifa na mabadiliko ya kiuchumi ya Mtanzania mmoja mmoja, hakuna? Stori tu!

Mnasimama hapa ooh! Mama Kamili alikwambia sijui alikuwa ana tatizo, halafu unakiri labda alitoneshwa, kama alitoneshwa alitoneshwa na nani? Kwa hiyo, unakiri mbele ya Televisheni ya Taifa, mbele ya umma, kwamba Vijana wa UVCM kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walimpiga Mheshimiwa Rose Kamili, ndiyo maana tuliwaambia, mnaua raia, mnawapa ulemavu raia. Tuunde Tume huru ya Majaji; tuna ushahidi kwamba Polisi wanashiriki kwenye mauaji, mnachikichia, kwa sababu mnajua, ikiundwa ufedhuli utajulikana. Kwa hiyo, tukikaa tukijadili mambo hapa tuache siasa nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio eti mabehewa, haya! Cheki mabehewa 214, juzi Mheshimiwa Sitta anatuambia katika mabehewa 214 yaliyokuwa yaletwe ambayo Waziri Mkuu anajisifia, ambao Mpango wa Taifa unajisifia, amezuia mabehewa 124 yasiingie nchini kwa sababu yaliyoingia ni dhaifu na inawezekana ni feki yako chini ya viwango. Halafu mnakaa hapa mnajisifia, ukiuliza Nundu ameona kura ya maoni anaweza asipite. Bunge lililopita alikuwa mkali, sasa nashangaa sekunde kadhaa jamaa kageuka, vipi? Kumbe kuna hatari ya kura ya maoni, inabidi unajipendekeze wakufikirie kwenye ufalme, kumbe umeshachelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya mambo tueleze kwa ukweli, tuache uwongo. Leo nchi hii wafanyabiashara wanaandamana, wafanyakazi wanaandamana, wakulima na wafugaji wanaandamana, wanauana. Leo kuna hatari ya mgawanyiko wa kidini baina ya Wakristo na Waislam, yote ni sababu yenu, hamjiulizi tatizo ni nini, mliaminiwa labda iwe kwa kuiba, iwe kwa ukweli, mkapata dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nyie mnapata dhamana, anasimama Mheshimiwa pale anasema eti sisi huku ndiyo tunafanya nchi isitawalike, sisi huku ndiyo tunafanya makusanyo ya mapato yasifanikiwe, lakini mnasahau kwamba juzi juzi tu hapa, kuna ushahidi wa dhahiri na

shahiri, kwamba bilioni zaidi ya 300 zimezolewa *BOT* pale, halafu juzi Ikulu inasafisha watu, hivi hizo ni akili ni matope? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu likija suala la kimaendeleo mnajisifia shule za Kata hivi shule za Kata mmejenga nyie au wananchi? Mnavyojisifia maabara hivi mmejenga nyie au wananchi? Jiulizeni hata mara moja, yale mahela mliyoiba juzi, hatuzungumzii ufisadi mwingine wa nyuma huko wa kutosha. Mngekuwa mnawekeza kwenye shughuli za wananchi, Tanzania leo ingefika wapi? Tuwe *serious* tuache unafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maafa, mafuriko Dar es Salaam; Mheshimiwa Waziri Mkuu lazima ukiri kwamba ofisi yako imeshindwa kusimamia suala la maafa, matatizo yaliyotokea Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2011, ikaundwa Tume chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ya kuangalia ni kwa namna gani tutazuia haya matatizo, 2015 hakuna hata moja lililotatulia. Yaani nyie kikubwa mnachoweza kukifanya atakwenda Mkuu wa Mkoa atauza sura, atakwenda Waziri Mkuu atauza sura, atakwenda Rais atauza sura, mkitoka hapo shughuli imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana hivyo hivyo na aibu, mradi wa viwanja 20,000 vya Wizara ya Ardhi, mradi huo ulitakiwa pamoja na mambo mengine uwe na miundombinu Mbweni kule, leo ni aibu Mbweni kumejaa maji, Serikali imewauzia wananchi viwanja kwa gharama kubwa, haijajenga miundombinu, mnakuja hapa mnajisifia, mnajisifia nini? Utasema maneno ya Wapinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI, chini ya akina Kigwangalla inasema Tawala za Mikoa zilipokea asilimia 18 tu ya mapato ya makusanyo ambayo Serikali ilitakiwa ipeleke kwenye maendeleo asilimia 18. Sasa kama hampelekei maendeleo kwa wananchi, mnajivunia hapa mmetekeleza, mmetekeleza nini! Halafu ni muhimu mjue, siyo kazi yetu sisi kuwasifia nyie kila siku kwa ajili ya kuwapa masifa hapa. Kila siku tunawapa vipaumbele mnaishia kuvi-*copy* na kuvi-*paste* mnashindwa kuvitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *agenda* ya Katiba Mpya haikuwa ya kwenu, tulisema nchi imeparaganyika tuanze na Katiba, mmepoka, mmefika katikati yamewashinda mmechemka. Mkajifanya mnadanganya wazee, sisi tuna akili, tukisema tunatoa pensheni kwa wazee, tunajua vyanzo ni vipi? Sasa nyie kazi yenu kukopi halafu maakili na maunjanja ya kutekeleza, hamna. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee, muda haupo upande wetu, unga mkono hoja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, naanza kwa kushukuru, kwa sababu msema ukweli mpenzi wa Mungu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sasa hivi nina miaka mitano humu ndani, tangu nipate Ubunge, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo makubwa sana. *(Makofi)*

Kwanza kabisa naanza kumshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake mahiri. Tumeona nchi nyingi sana zina matatizo, lakini Rais wetu ameweza kui-

maintain nchi yetu na sasa hivi tunaishi kwa amani, hakuna migogoro yoyote. Sasa wewe kama humshukuru hata Rais anayefanya kazi nzuri kama hii, sijui utashukuru Rais gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niishukuru tena Serikali, ninaposema Serikali Mawaziri, Mawaziri wamefanya kazi nzuri na ninaposema wamefanya kazi nzuri, naweza nika-*quote* wamefanya kazi nzuri kwenye Jimbo langu, kwa sababu nimechaguliwa na wananchi na kazi yangu ni kuunganisha kati ya Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri nimewafuata kwenye Jimbo langu, wamekuja Mawaziri 15 tangu nichaguliwe na siyo kwamba wamekuja kutembeatembea tu, wamekuja kufanya kazi. Kwa hiyo, niwaambie kitu kimoja, niliongea na Waziri wa Elimu, nilisema Jimbo kwangu kuna tatizo, masuala ya madarasa nikamwambia shule ya sekondari Itengule ina tatizo kubwa zinatakiwa bajeti ya milioni 200, alinipa milioni 200 na imefanya kazi kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia shule ya Malangali ile haijafanyiwa ukarabati, inabidi ziende milioni 53, Waziri alipeleka milioni 53 pale na ukarabati umefanyika. Nikamwambia Waziri wa Maji, kwenye Jimbo langu kila siku nalalamika maji hapa, nikasema kwenye Jimbo langu kuna tatizo la maji, nikamwona Waziri wa Maji, nimeuliza maswali karibu maswali matano, lakini ameyajibu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ninavyoongea, Kijiji cha Kilimazoo kule ameshaleta milioni 850 na mtandao wa maji tumeshamaliza tayari na juzi alikuja Naibu Waziri alikuja kufungua yale maji, amejenga matenki mengi sana. Kwenye Kijiji cha Maduma, nilimwambia kijiji kile hakina maji kuna matenki walijenga pale, ameleta milioni 75 na sasa hivi mradi karibu tunamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kijiji kingine cha Sasawala ambacho tulikuwa tunalalamika, hivi ninavyoongea Mkandarasi kesho kutwa anakwenda kusaini mkataba kule, ameshaleta milioni mia 200. Sasa unasema Serikali haifanyi kazi, haifanyi kazi wakati inafanya kazi? Labda hufanyi kazi wewe. Labda hufanyi kazi wewe! Wewe unalala, umekaa tu unasema Serikali haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea sasa hivi wananchi kwa kushirikiana na Serikali pamoja na sisi Wabunge, karibu asilimia 80 maabara zimekwisha. Sasa wale watoto wa sayansi bila maabara watasomaje, lazima wasome sayansi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge mwenyewe nilivyosimama hapa, nina Kata 15 nimechimba visima katika Kata 10, kama Mbunge nimechimba visima Kata 10, maana visima 19 virefu bila kutegemea Serikali nimechimba mimi Mbunge, ndiyo kazi hiyo inayotakiwa, mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, wewe umefanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea hivi sasa wafadhili wameniletea magari mawili kwa ajili ya *project* ya maji, mapya yako pale. Wafadhili hawawezi kukupa kitu kama wewe hufanyi kazi. Kila siku kulalamika tu, unalalamika nini, piga mzigo, piga mzigo, unalalamika kitu gani hapa. Tusidanganyane, nchi hii tukiwa tunashindana kwa longolongo hatuwezi kwenda mbele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ninyi Wapinzani mkitaka kuweza muanze kujenga barabara, mjenge hospitali, muandike kama chama mmefanya nini na siyo longolongo tu.

Tukishindana kwa vitendo, lazima tutashinda, lakini kwamba tunapiga longolongo, sijui maneno hayasaidii kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie kitu kimoja ambacho inabidi tuwe makini sana. Sasa hivi Wizara ya Nishati nawapongeza sana wamefanya kazi kubwa sana ya umeme vijijini. Hivi ninavyoongea kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini, nadhani kufikia mwakani vijiji vyote vitakuwa na umeme, kwa sababu nikiangalia Malangali ile, Mbaramaziwa mpaka Yowanze mpaka Nyigo nguzo tayari na nyaya wameanza kuweka. Hiyo ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine hata nyumba za bati hakuna, nimesema weka hata kwenye nyasi, wanaweka umeme. Sasa wewe unalalamika, unalalamika unatoka nchi gani? Unatoka Tanzania hii? Au mimi sijaona, kwa sababu kwenye Jimbo langu tunakwenda *speed* sana. *Serious*! Sasa hivi hata shule za sekondari hizi mnasema shule za kata, shule za kata kwenye Jimbo langu la Mufindi kule Shule ya Mgowole ni Shule ya Kata na imekuwa ya kwanza Kitaifa na sasa hivi tunaiita *Tanzania One* iko pale. Sasa mnasema siyo maendeleo, maendeleo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa hivi, barabara za lami zimepita kila mikoa, barabara za lami zinapitika. Sasa hivi Waziri wa Ujenzi alikuja kwangu alishaniahidi tayari na kwenye *program* alishaweka Barabara ya Nyororo mpaka Mgololo, Mafinga mpaka Mgololo amekubali anataka kuweka kiwango cha lami na alishapiga bajeti, inatakiwa bilioni 75, sasa afanyeje jamani! Maendeleo ya nchi hii hayaji kwa longolongo yanakuja kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Waziri Mkuu anazunguka nchi nzima anawaelimisha wananchi, sasa hiyo siyo kazi tena, mnataka afanyeje? Aje awafanyie nini sasa? Kutoa elimu kwa wananchi ni kazi kubwa sana, Waziri Mkuu kila siku tunamwona anazunguka Majimbo, kuna Waziri wa Chama cha Mapinduzi, namshukuru sana Mheshimiwa Kinana amezunguka Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, akizunguka siyo anazunguka anapiga blabla anafanya kazi, mimi kwangu kule ameshaleta mifuko 100 ya simenti, wa chama huyo, ameleta kule. Analeta sasa hivi mabati 400 kwenye Jimbo, hapigi longolongo anapiga mzigo. Sasa ninyi mnakwenda mnahutubia, mnapiga longolongo, hiyo longolongo wala haisaidii.

Nawaambia Chama cha Mapinduzi kitaendelea kushinda kila siku kwa sababu tunapiga kazi. Kwenye Jimbo langu kule kuna watu wengine hata Wapinzani wanakunywa maji niliyochimba mimi wala siyo Mfuko wa Jimbo. Wanakunywa maji, sisi tunachimba maji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa tungemuongezea dakika kidogo *eeh*! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mendrad endelea!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, acha tuseme ukweli, kuna watu wengine nawashangaa, wanapita vilabuni wanahonga pombe. Unahonga pombe maji nimechimba mimi, wanatumia maji yangu wanapikia pombe. Hayo siyo maendeleo kuhonga pombe, honga visima! Honga visima pale! Piga mzigo. Wengine wanasema Kigola anachimba visima, nachimba visima ili watu wanywe maji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea sasa hivi nimeshakarabati visima 48 bure, bila kuchangisha mwananchi, fanya kazi ndiyo sisi tutakuamini, lakini wewe unakuja hapa unapiga mdomo, sijui chama hakishindi, hakishindi! Hakishindi wakati tunapiga kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu mitaa yote tumeshachukua wala hakuna Chama cha Upinzani, unapinga kitu gani? Barabara kwenye Jimbo langu kuna barabara 12 zimeshatengenezwa tayari, barabara 12 sasa unataka upite wapi? Ipi Tanzania mnayozungumza ninyi, lakini Tanzania ninayoifahamu sasa hivi tunakimbia, ni mbio na kwenye kampeni watapita kwenye barabara tulizotengeneza sisi. Chama cha Mapinduzi kimetengeneza barabara, watapita pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine mimi Mbunge nimepeleka hela ya kwangu ya mshahara nimetengeneza barabara, tena mwende mkaulize pale, barabara ya Ibati ile nani katengeneza, nimetengeneza mimi. Sasa hivi nadaiwa hela nyingine inabidi nikamlipe Mkandarasi, nalipa mimi mwenyewe. Sasa watu wanalia lia unalia lia nini hapa? Sasa wewe unalia nini, lazima upige mzigo, watu wasituletee mambo mengine ya ajabu ajabu hapa. Kazi ni kitu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna mpango, Chama cha Mapinduzi kimeshatangaza kwamba, kwenye upande wa shule za sekondari watafuta ada. Mimi Mbunge nimeshaanza kulipia watoto, karibu watoto 250 tunalipia kule na tunaendelea na tunatafuta wafadhili walipie na Serikali ikifuta, inasema inaweka mpango itafuta, kila kitu kinakwenda kwa *program*. Huwezi ukaja tu hapa unasema hivi na wewe mwenyewe umelala, umefanya nini wananchi watakuuliza, hata Mungu anakuuliza, umefanya nini?

Wewe unakuja kuchonganisha hapa, hivi kilikwenda hivi kilikwenda, piga mzigo, piga mzigo, hii kazi piga mzigo. Kuna watu wanaanza kuwachonganisha vijana wamemaliza vyuo vikuu wanapita pale eti wanawachonganisha, wanawapa 200, 300 hazisaidii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mendrad!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tulitamani uendelee na kuendelea. Mendrad Kigola amenikumbusha katika Wilaya ambazo CCM ilichukua Vijiji vyote Kongwa mojawapo. Kwa hiyo, tarehe 25 Mwezi wa Kumi tafuteni hukohuko tu, lakini Kongwa hamna njia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Deo Songa!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie. Niwashukuru wananchi wa Njombe Kaskazini kwa kunipa ushirikiano kwa kazi mbalimbali ambazo nilikuwa nikishirikiana nao na Serikali juu ya kufanya shughuli za Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuzungumzia suala la umeme. Niombe sana Wizara hii ya Nishati na Madini namna ambavyo wananchi kule wanasubiri suala la umeme kutoka Makambako mpaka Songea kupitia Kata ya Ryamkena, Igongolo, Kichiwa na Ikuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuja Naibu Waziri alituahidi kwamba mwezi wa Saba mradi huu utaanza, Niombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba mradi huu wananchi wanautegemea kwa hamu kubwa sana, lakini niishukuru sana serikali kwa namna ambavyo

ilivyokuja kutuahidi kwamba Kijiji cha Mloa na Utengule na Namawande namna ambavyo watatupa umeme katika awamu hii ya mradi huu wa *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji. Niishukuru Serikali pia kwa namna ambavyo katika Jimbo langu baadhi ya maeneo wametupa fedha za mradi wa maji. Ombi langu kubwa niombe sana mradi ule mkubwa tunaosubiria hapa Mjini Makambako na Njombe Serikali iweze kututalia ili wananchi wasipate tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ni juu ya suala la wafanyabiashara. Suala hili niombe sana Serikali ilitatue ili wananchi hawa wafanye biashara, wako tayari kulipa kodi. Hivi sasa hawajalipa mihula miwili, muhula huu wa mwezi wa Tatu na mwezi unaokuja wa Sita. Niombe sana ile Kamati ambayo iliundwa na Waziri Mkuu iweze kulitatua mapema ili wafanyabiashara hawa waendelee kulipa kodi kama ambavyo walikuwa wamekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nizungumzie suala la wawekezaji. Najiuliza kila wakati hivi wawekezaji wa ndani hawatakiwi? Kwa mfano, ilipokuwa inauzwa Kilimanjaro alipotaka kuwekeza Reginald Mengi hakupata na bei ilikuwa ni ile ile akapata mwekezaji wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nizingumzie upande wa UDA mfano, huyu *Simon Group* ni mwekezaji wa ndani, lakini kila wakati amekuwa akipigwa vita utafikiri anatoka Burundi. Niombe sana wawekezaji wa ndani nao waheshimiwe kama ambavyo wawekezaji wa nje tunawakaribisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe hela ambazo zinakuwa tumezitenga kwenye bajeti zinazotakiwa kwenda kwenye Halmashauri kufanya kazi, niombe ziende kwa wakati ili kusudi miradi ile iliyopangwa iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sasa naomba niongelee suala la, watu wamekuwa wakizungumzia hapa kwamba Serikali hii ya CCM imechoka. Mimi niwaambie kitu kimoja, hivi anayekwenda kuungana na kuwa UKAWA nani amechoka? Nani amechoka? Si hawa! Kwa sababu, mfano hapa mimi hapa *Jah people* mtu anakuja anataka kupigana na mimi, halafu wanakusanyika watu sita wanaungana kupigana, si wameniogopa maana yake wamechoka hao. Wamechoka hawa na ndiyo maana wameungana UKAWA na hawataweza, hiyo UKAWA yao hiyo, hawana uwezo.

Serikali hii iko imara inafanya kazi kubwa, wao wakienda kwenye mikutano kazi yao ni kukinga bakuli. Sasa tutawapa Serikali hawa? Kukinga bakuli kuchangisha michango kwa wananchi, halafu wanasema maabara zimejengwa na wananchi, hamkuona kama Serikali imetia mkono pale, hamjaona? Serikali imetia mkono imeshirikiana na wananchi kujenga maabara. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa, leo nimekuja hapa nimeingia asubuhi saa tatu, nimetoka Makambako saa kumi na moja, nimekatisha hapa hii barabara. Zamani ingekuwa masaa kumi hapa, hamuoni hayo? Mnataka Serikali ifanye nini? Ninyi wenyewe hapa mnachangia, halafu mnakwenda mnasema Waziri tunaomba kwetu tuna tatizo la umeme. Sasa si ndiyo Serikali inafanya kazi? Mnataka nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa kweli Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imefanya kazi kubwa ambayo inatisha. Kama unasema imekopa sasa bilioni 30, si

ndiyo hizo zimefanya kazi, tatizo liko wapi, tatizo liko wapi? Serikali inafanya kazi kubwa sana na hamtapata ng'oo!

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Mendrad Kigola pale, wewe Mbunge mwenyewe fanya kazi, nenda kwenye Jimbo langu pale, najenga shule kutoka chini mpaka juu mwenyewe *Jah People*! Nashirikiana na wananchi, nenda pale sekondari, shule za msingi. Nenda pale sasa najenga Zahanati kumi nimeanzisha chini mwenyewe. Ninyi mnafanya nini? Mkija pale aah, sijui kimepita hapa, ng'oo, hakuna cha kunini hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, niombe sana barabara ya kutoka Lupembe kwenda Njombe kwa sababu ilishapangwa kwenye bajeti…

MBUNGE FULANI: Jenga mwenyewe.

MHE. DEO K. SANGA: Iingizwe kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu *TBC*. *TBC* ndiyo chombo tunachokitegemea sana kutoa habari kuhabarisha kwa wananchi, Wilaya ambazo sasa hivi wanapata habari ni Wilaya karibu 80 tu, niombe tutenge fedha ili ziweze kufanya kazi ya *TBC* kuhabarisha katika Wilaya zote 165.

MBUNGE FULANI: Jenga mwenyewe!

MHE. DEO J. SANGA: Nitajenga nina uwezo. Huyu ndiyo *Jah People* au unamsikia tu! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, unajua Serikali hii ya CCM wakati fulani hata hawa wasomi wa vyuo mbalimbali vikuu ikiwemo *Udom* tunatakiwa tumpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ubunifu wa kujenga *Udom,* lazima tumpongeze kwelikweli, hata ninyi mmesoma huko na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ni lazima Serikali hii tuipongeze kwa kazi nzuri ya CCM. CCM oyee! *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Oyee! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Huyo ndiyo *Jah People*. Nimemwona Machali kasimama sasa changia, changia moja kwa moja Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilufi!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwa ni pamoja na Wizara mbalimbali ambazo ziko chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kuwapa taarifa Waheshimiwa Wabunge wanaotokana na Chama cha Mapinduzi kwamba, ni utaratibu wa kawaida kwa Mbunge yoyote awe wa Upinzani au awe wa Chama cha Mapinduzi kwenda kum-*consult* Waziri yoyote kwamba eneo fulani kuna matatizo Fulani, kwa sababu ni Watanzania wanaolipa kodi na kodi zinakusanywa na Serikali hatukusanyi sisi Wabunge.

Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa Mzee wangu ambaye amemaliza kuchangia sasa hivi Mheshimiwa Deo Sanga *a.k.a Jah People,* siyo dhambi na siyo kosa kumwona Mbunge wa Upinzani akienda kum-*consult* Waziri yoyote, kwa jambo lolote, kwamba Serikali inatakiwa kutatua tatizo hilo, siyo dhambi, ni suala la utaratibu na ni kwa sababu kodi zinalipwa na watu wote, wawe ni wapinzani wawe siyo wapinzani wote tunalipa kodi. Kwa hiyo, wajibu wa Serikali ni kuhakikisha inapeleka maendeleo kwa wananchi kwa maeneo yote pasipokujali itikadi za vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuitake Serikali iache kupiga longolongo na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi waache kupiga longolongo wahakikishe mipango ya maendeleo hapa nchini inatekelezwa kama wananchi walivyotarajia na siyo kama CCM wanavyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kufanya *budget analysis* kuhusiana na Wizara ya TAMISEMI ni dhahiri utaona kwamba Hamlashauri zina-*starve*, ziko kwenye hali mbaya, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziko kwenye hali mbaya. Kama Serikali inaweza ikapeleka bajeti kwa nchi nzima *overall* ni asilimia ambayo haizidi 24 kwenye Halmashauri, hayo maendeleo ambayo tunayahitaji huko kwenye vijiji, kwenye kata tutayafikiaje? Kama siyo mchanga wa macho!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapowaambia wakati mwingine kwamba, Serikali ni kana kwamba imechoka, siyo kwamba tunawaonea. Katika asilimia 100 unapeleka asilimia 24 kwenda kui-commit kwenye maendeleo, hayo maendeleo tutayapata saa ngapi? Tutayapataje? Tuambieni kama katika asilimia 100 mmepeleka asilimia 24 hayo maji mnayotudanganya yatapatikanaje? Barabara zitajengwaje? Madarasa yatajengwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu asikilize ndiyo tunamwambia, waache kuwalaghai Watanzania, Watanzania wana-*starve* huko waliko hali ni mbaya, mnakuja kutupiga danadana mnadanganya watu mahali hapa. Hamumwogopi Mungu? Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Hawa Ghasia hamumwogopi Mungu? Mmekaa mpo mpo, hii mikono nafanya hivi ili msikie, maana yake mnaambiwa halafu mnajifanya hamsikii. Kusikia mnasikia, lakini ni wavivu wa kufanya maamuzi. Kaeni pembeni, kaeni pembeni, muone kama tutashindwa kufanya yale ambayo Watanzania wanahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanapata matatizo kwenye maeneo yao, angalia ni Serikali hii ambayo imetoa Waraka na kuzielekeza Halmashauri zitenge asilimia 10 kwa ajili ya vijana na wanawake. Hata hivyo, taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa iliyosomwa katika Bunge la Mwezi Machi na Aprili ilionekana zaidi ya bilioni 200 hazikuwa *committed* kwa ajili ya kuwasaidia wanawake na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya TAMISEMI na-*declare interest* kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI ambao tumechambua bajeti ya TAMISEMI hali ni mbaya. Sasa hivi hizo ajira ambazo Serikali imekuwa ikizungumza kwamba inakusudia kuzitoa kwa vijana na kuwawezesha vijana. Watawawezeshaje wakati wameshindwa kuzisimamia Halmashauri, wameshindwa kuziagiza Halmashauri zikatoa pesa kwa ajili ya maendeleo ya vijana, zikatoa fedha kwa ajili ya maendeleo ya wanawake, itawezekanaje kwa kuwa na watu ambao ni wajanja wajanja tu, sijui wameingiaje mahali hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wananchi msisubiri hadi pale ambapo pengine mtakuwa mmechoka sana, hawa jamaa wamechoka na hawana jipya lingine. Fanyeni maamuzi, itakapofika Oktoba 25, fanyeni maamuzi hawa hawana jipya. Vijana mnadanganywa kwamba mnawezeshwa, lakini hakuna chochote kwenye Halmashauri. Nenda

kwenye kona mbalimbali, ni Halmashauri gani iliyoweza kutekeleza kupeleka fedha za vijana na wanawake kwa asilimia mia moja. Hakuna ni sifuri. Mnakuja hapa hapa mnakuja kutupiga maneno maneno, mnataka tuwaambieje, maana yake tumewashauri sana, lakini hamwelewi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusiana na barabara, ni fedheha leo hii tunapozungumza, na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba unisikilize. Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo tunapozungumza, barabara, mawasiliano kati ya kutoka Kasulu kwenda Kigoma yamekatika kwa sababu hali ya barabara ni mbaya kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na hata fedha ambazo pengine mlitenga mwaka wa fedha 2014/2015, shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuanza kujenga barabara ile kwa kiwango cha lami, kazi zimelala, barabara ile hata kuweza kufanyiwa *periodic maintenance* hakuna.

Halafu mnategemea ikifika wakati wa kampeni, mje Kigoma muwaambie tunaomba kura, Kigoma tunasema CCM mnaelekea kabisa kupotea, tutawafuta mwaka huu, kwa sababu hamna jipya lingine, kama hamuamini, tarehe 25 Oktoba.

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakimrushia maneno mzungumzaji bila utaratibu)

MHE. MOSES J. MACHALI: Tunawaambia mnakusanya kodi, ninyi bezeni tu, ndiyo tunawaambia hivyo na wananchi hapa wanasikiliza, wanatuona kitu gani ambacho tunafanya. Tunataka kuona, hatuhitaji kuona ahadi ambazo ni hewa, hatuhitaji kuona ahadi ambazo hazitekelezeki, kodi mnakusanya, tuambieni mnapeleka wapi! Mnakula, jibu naambiwa huko, inawezekana kweli, ndiyo maana yametokea mambo ya *ESCROW,* watu wamepiga pale, halafu wanakuja, anajitokeza *Chief Secretary,* anakuja anasema hawa walionewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama walionewa, hawa watu wengine mnawapeleka Mahakamani kufanya nini. Kama walionewa, hao wengine ambao tunaona hawakusafishwa, hawakuwa *cleared*, mnakusudia kuwapeleka Mahakamani ili wakafanye nini, si mseme wote kwamba ile *deal* ilikuwa ni *clean deal.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika, Serikali hii ni Serikali ya kuwagandamiza wananchi na ndiyo maana mmekuwa mnatoa ahadi, Mheshimiwa Waziri Mkuu tumekueleza matatizo ya wakulima katika pori la Kagera Nkanda, lakini kwa miaka takribani minne ambayo nimekuwa Mbunge hapa, tumekueleza, alikuwepo *DC* mmoja *DC* wa ajabu ajabu, bwana Danny Makanga. Nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuweza kumpumzisha akakae pembeni kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmekuwa na viongozi wasiokuwa na huruma, wanakwenda kufyeka mazao ya watu kwenye pori la Kagera Nkanda, mmeshindwa kufikiria, mmeshindwa kuendana na Sheria ya Uhifadhi wa Misitu ya mwaka 2002, ambayo inatoa fursa ya kuweza kubadilisha matumizi ya ardhi na iweze kutumika kwa ajili ya shughuli nyingine ambazo zina maslahi mapana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ile, tumewashauri, hamsikii, tunawaambia kwamba wananchi wale zaidi ya miaka 40 wamekuwa wanalima kwenye eneo hilo, leo mnakuja kuwaambia kwamba kwa sababu eti walichagua Wapinzani hamwezi mkawaruhusu wakaendelea kulima huko. Hivi hii nchi mmeifanya kwamba, wakichagua CCM ndiyo kwamba mtawaruhusu, lakini naomba niwaambie wananchi wa Wilaya ya Kasulu, wananchi wa Mkoa wa Kigoma, wanazo akili zao timamu, wanajua pumba na mchele.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka Serikali hii itakapokuwa imeondoka madarakani. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kilufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Chambiri.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri nyingi ambazo amekuwa akizifanya pamoja na TAMISEMI kwa ujumla, viongozi wote, niwashukuru sana kwa ushirikiano ambao wamenipa kwa muda wote ambao nimekuwepo madarakani, tumeshirikiana kutatua kero nyingi ambazo nitazieleza baadaye. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ushirikiano aliouonesha kwa wananchi wa Mbarali na mimi pamoja na wananchi wa Mbarali tunawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa mliotupatia katika kuondoa kero mbalimbali ambazo zilikuwa zimejitokeza Wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sana kwa hatua ambayo tunakwenda nayo ya maendeleo kwa Taifa hili. Tumejitahidi angalau hata kusogeza kiasi pato la Mtanzania mmoja mmoja kutoka mwaka 2005, tulikuwa na wastani wa shilingi laki tatu na sitini na mia nane hamsini na tano, lakini kufikia mwaka 2014, tumesogea na kufika milioni moja laki saba na ishirini na tano, kiasi ambacho kimsingi bado sana, tunahitaji kuongeza bidii ya kuinua uchumi wa wananchi wetu ili kusudi waweze kuwa na pato la kutosha kuweza kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeweka utaratibu wa maendeleo wa miaka 15, ambao umegawanywa katika vipindi vya miaka mitano mitano. Nishukuru sana kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015, ambayo ni miaka mitano ya mwanzo, tumejitahidi kutekeleza miradi mbalimbali kulingana na uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, tutasema sana hapa ndani, tutapiga kelele sana, lakini kubwa kuliko yote ni kuhakikisha kwamba uchumi kupitia rasilimali zetu unaimarishwa kwa kusimamiwa vizuri na kuhakikisha kwamba rasilimali hizi hazichezewi na watu wachache, zinasimamiwa kikamilifu kuhakikisha kwamba pato la Taifa linapanda ili tuweze kutekeleza miradi ya wananchi ambayo mingi bado haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali na hususan Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kusimamia kuhakikisha kwamba umeme unasambaa vijijini. Nimweleze kwamba sasa tutahakikisha Wilaya ya Mbarali ambayo nimekuwa nikiipigia kelele siku nyingi kwamba hatuna umeme ni Kata nne tu katika Kata 20 zilikuwa zimepata umeme, lakini kwa sasa hivi nashukuru sana kwa kupitia mpango huu wa *REA* sasa karibu vijiji vingi vya Wilaya ya Mbarali vinawekewa umeme na nashukuru sana na naomba niseme Mkandarasi ambaye anaendelea na kazi kule Mbarali aongeze *speed* ili kusudi vijiji vingi viweze kupata huduma hii muhimu ya umeme ambayo ni sehemu ya maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme si starehe, umeme ni maendeleo, umeme ni ajira. Naamini, kama mpango huu utatekelezwa, ambao naamini utatekelezwa kulingana na mikakati ambayo imewekwa, ukifika vijiji vyote, naomba tu, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye alikuwa amefika kule kwangu kufanya uzinduzi, nimshukuru sana kwa kazi nzuri ambayo aliifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile, kwa vile tuko kwenye awamu ya kwanza, nimwombe Mkandarasi ambaye anaendelea na kazi kule Mbarali, kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yamepimwa, vijiji vyote vinapata umeme na hasa kuna maeneo yale ya Vijiji vya Uturo, Ukwavira, alikwenda akapima, lakini bado hajapeleka nguzo na nilikuwa nimemfuata, nikamsisitiza ahakikishe kwamba, vile vijiji vinapata umeme wamekuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Vijiji kama vya Ekanioga na Lugelele na vyenyewe na Kata ya Igava na Kata ya Mawindi, kuna baadhi ya maeneo bado wamenilalamikia kwamba amekwenda ameweka alama, lakini bado hajapeleka nguzo, niombe kupitia Bunge hili kwamba Mkandarasi aongeze *speed*, wananchi wana hamu na maendeleo, wana hamu na umeme kuhakikisha kwamba maeneo yote yanapata umeme ili ajira iongezeke kwa vijana, lakini vile vile waweze kufanya maendeleo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru sana Serikali, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini vile vile niishukuru sana Kamati ya Maliasili na Utalii pamoja na Mheshimiwa Waziri Nyalandu, kwa kazi nzuri ambayo amewasaidia wananchi wa Mbarali kuhakikisha kwamba eneo ambalo lilitaka kuchukuliwa na hifadhi kimakosa linarejeshwa kwa wananchi wa Mbarali. Naomba niwashukuru sana ndugu zangu kwa kuona umuhimu huo na kuwajali wale wana Mbarali, kwa kweli naomba niwashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichobaki kule kwa sasa ni kuona mpaka ule unawekwa, kwa sababu ilionekana kuna baadhi ya watendaji wasio waaminifu na wasio waadilifu, kwa makusudi kabisa wakijua ile hifadhi ni mpya, sisi ndiyo tumeridhia vijiji baadhi viingie kwenye hifadhi, lakini wakapindisha na kutuchukulia vijiji vingine 21 kinyume cha utaratibu, lakini pamoja na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kamati ya Maliasili na Utalii pamoja na Mheshimiwa Waziri, kuhakikisha kwamba eneo hilo linabaki na wananchi, lakini na wale waliofanya makosa hayo, siku nyingine ingefaa wawe wanachukuliwa hatua kwa sababu hawa ndiyo wanaochonganisha kati ya wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi kuna migogoro katika nchi hii ni kwa sababu ya watendaji wachache wasio waaminifu, wanafanya kinyume wanamega maeneo ya wananchi na hivyo kusababisha migogoro kati ya wananchi na Serikali na hiki ndicho kilichotokea Mbarali. Sisi wana Mbarali tunasema tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa haya yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ile *GN* ambayo waliipindisha, nina hakika kwa asilimia kubwa, Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi wa Mbarali na ameniahidi na mimi mwenyewe na Kamati kwamba atahakikisha wanashughulikia mipaka ile ikae vizuri na wanaweka ili kuondoa kero kati ya wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Serikali, nipongeze kwa kushiriana na wananchi wa Mbarali kwenye miradi mbalimbali ya kilimo. Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya pekee katika nchi hii zenye miradi mingi ya umwagiliaji na tunalisha eneo kubwa la Tanzania na hata nje ya nchi, mchele mzuri unaotoka Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa siyo mwingi wa fadhila kama sitatoa shukurani, miradi ile mingi bado inaendelea kuboreshwa na Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha miradi hiyo inaboreshwa. Vile vile kwa kuwa lile eneo ni muhimu sana kwa kilimo cha umwagiliaji, kuna miradi ambayo imekuwa iliendelezwa, hasa baada ya maombi ya wananchi kwa Serikali yao. Kwa mfano mradi wa Mwendamtitu unakwenda vizuri, bado tu

kukamilika. Tuombe Serikali iendelee kutoa fedha ili mradi ule ukamilike, vijana wengi wapate ajira kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kabisa niwaambie ndugu zangu, vijana wameitikia, wanalima kweli kweli. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iendelee kupeleka fedha mradi huu ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile uko mpango wa kujenga bwawa pale Madibira, mpango ule ukiboreka utakuwa ni sehemu ya mfano kwa kilimo cha kiangazi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika aongeze bidii ya kupeleka fedha na kusimamia kuhakikisha kwamba mpango huo wa Serikali unakamilika ili kusudi wananchi waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, pia tuna mpango wa kuondoa tatizo kati ya mwekezaji wa Kapunga na wananchi wa Chimala na maeneo yale ya Kapunga, kwamba, kuna *intake* ambayo tumeiomba Serikali iwasaidie wale wananchi kwa sababu yale maji sasa yanamilikiwa na mtu mmoja ili waweze kupata *intake* yao eneo la Mpungammoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Serikali imekubali kwamba itasaidia kujenga *intake* hiyo ili wananchi wale waweze kupata hiyo ajira muhimu ambayo itaajiri vijana wengi ambao wamekosa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, naomba niishukuru sana Serikali na hasa TAMISEMI kwa kushirikiana kuondoa kero za wakulima wa Mbarali ambao wamewawakilisha wakulima wengine wa nchi hii ambao walikuwa wanatozwa ushuru wa mazao wanapotoka mashambani, wamefanya kazi, lakini mtu mwingine anakuja bia kujali kwamba huko hakuna biashara inayofanyika, wakawa wanatozwa ushuru, lakini kupitia TAMISEMI, Mheshimiwa Mwanri, namkumbuka sana, Mheshimiwa Hawa Ghasia namkumbuka sana, walisimama imara na kutoa tamko la Serikali kwamba jambo hili haliwezekani. Anayelipa ushuru ni mfanyabiashara…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kilufi nakushukuru Modestus. Ahsante sana kwa mchango wako muda hauko upande wako.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Chambiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Bungala!

MHE. KISYERI W. CHAMBIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka hii mitano imefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema Serikali ni vigumu sana ukatembea barabarani ukakutana na mtu anaitwa Serikali, Serikali inawakilishwa na watu. Kwa hiyo, tunaposema kwamba Serikali imefanya kazi, tunawaangalia viongozi wetu wakuu, tunamwangalia Rais wetu na msaidizi wake mkuu ambaye ni Waziri Mkuu, wamefanya kazi kubwa sana kwa nchi hii na nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii miaka mitano, toka hii Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani, yamefanyika mambo ambayo ukikaa ukafikiria, labda utafikiri tu ni yale ambayo yalikuwa yanafanywa kwa kutamkwa na ile Taa ya Alibaba katika kitabu cha Alfu Lela

Ulela, huwezi kuamini kwamba yamefanywa na watu kwa muda unaostahili. Tumefanya kazi ambayo Wapinzani wanaona wivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kwanza na upungufu ambao haujatimizwa kwa ahadi katika Jimbo la Babati Mjini. Mwaka 2010 Rais katika kampeni zake aliahidi kilomita mbili za barabara ya lami, mpaka leo haijajengwa na fedha hatujapata.

La pili, katika vijiji kumi, maji, miradi imeanza, Kijiji cha Malangii na Nakwa, miradi iko asilimia 50 fedha haijapelekwa. Vijiji viwili, Kijiji cha Halaa na Haraa, bado kabisa kuanza mradi, fedha haijapelekwa, tunaomba hizi fedha zipelekwe. Nasikia mtu ananipongeza anasema hongera, hiyo ni sawa kabisa, sababu hakuna barabara ndefu ambayo haikosi kona.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii miaka mitano, ndani ya Jimbo letu la Babati, zimefanyika kazi kubwa sana ambazo hazijawahi kufanyika toka tupate uhuru. Tumeweza kutengeneza barabara kilomita 133.5, umeme unaenea katika kila sehemu kwenye Jimbo. Tumemaliza kujenga maabara zetu zote, ndani ya shule zetu za sekondari katika mji wetu wa Babati bila kuchangisha mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetengeneza zahanati katika vijiji vyetu karibu vyote na tumemaliza kujenga zahanati. Tumetoa mikopo ya asilimia tano kwa akinamama na vijana na naamini kwamba Halmashuri yetu ndiyo itakuwa pekee labda ndani ya nchi nzima kumaliza mia kwa mia katika miaka mitano, madai wanayodaiwa na vijana na akinamama ile asilimia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza ujenzi wa mji mpya, sababu wakati Babati inakuwa Makao Makuu ya Mji, tulianza kwenye kijiji na kijiji hakikupita zile taratibu za kukua na sababu hiyo tumepanga Mji mpya wa Babati, tumeshapima viwanja 12,700 na tumepanga mji wa kisasa kabisa, hii yote ni sababu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wapinzani wanajivunia sana Kanda ya Kaskazini na wakiiona Babati wanaimezea mate sana, wakiamini kwamba hiyo itakuja kuwa himaya yao, lakini hizo ni ndoto za mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchaguzi uliopita, walipojigamba kwamba wangeteka Kata zote za mjini, waliambulia kutopata Kata hata moja na CCM kushinda na ushindi wa asilimia 79. Tarehe 25 tunawangojea kwa hamu sana kusudi sasa ile misumari iliyobaki katika jeneza tuikamilishe, tuwazike ndani ya ardhi futi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza sana, hawa ndugu zetu, wanaongea sana, wana kelele nyingi sana, lakini kitu ninachogundua ni kwamba, wamezeeka kabla ya muda wao. Kuna ugonjwa, wale Madaktari wanaita *HGS*, unaitwa *Hughson Greenford Syndrome*. Mtoto anayezaliwa na ugonjwa huo akifika miaka mitano sita ameshazeeka kabisa analingana na mzee wa miaka 80, huu ndiyo ugonjwa walionao. *(Makofi)*

Wamezeeka kabla ya wakati wao. Sababu wamezeeka kabla ya wakati wao, tunaona dalili katika ugonjwa wao, maandamano, kelele nyingi. Wanachochea Watanzania bila hatia kufa, basi mniruhusu leo nitangaze kifo chao cha tarehe 25 Oktoba, kwamba, tunatangaza rasmi kwamba sasa CHADEMA na UKAWA rafiki zao tunawazika na hawataonekana tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kusisitiza kwa kumalizia kwamba ndani ya Mji wa Babati, tuna shamba ambalo linaitwa *Singu Estate,* hili shamba lilikuwa la kwetu, mali ya

wananchi, wakapewa watu wa *Breweries*. *Breweries* baadaye wakaliacha wakauzia mtu, ambapo ilikuwa haki yetu sisi wananchi wa Babati tupewe hilo shamba. Sasa ninachoomba Serikali ifanye taratibu za kufuta *lease* kabisa ya hilo shamba kwa sababu itatusaidia kupanga mji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chambiri. Mheshimiwa Bungara, atafuatiwa na Mhesimiwa Margareth Mkanga.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameipendelea Serikali ya CCM kuishi miaka 50 na mwaka huu nafikiri ndiyo utakuwa mwisho wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko Bungeni hapa kwa ajili ya kuwatetea wananchi. Kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali na kuishauri Serikali, lakini inaonesha ndani ya Bunge letu kuna Wabunge wanaitetea Serikali maana yake wanaibeba na kuna Wabunge wanatimiza wajibu wao kwa kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuoni ajabu watu wanaibeba Serikali ya CCM, hatuoni ajabu. Naamini Serikali ya CCM haijachoka, isipokuwa Serikali ya CCM inabebwa na sisi tunaowabeba, wananchi tumechoka. Kwa sababu Serikali ya CCM inabebwa, haiwezi kuchoka, isipokuwa wananchi wa Tanzania wanaoibeba Serikali hii zembe wamechoka, kwa hiyo Serikali haijachoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaiba hela, wanalindana, itachoka wapi. Watu wanataka maji hayapatikani, watachoka wapi; hawachoki kwa sababu wanalindwa. Isipokuwa Watanzania tumechoka kulibeba Serikali ambalo ni zembe. Chama lege lege huzaa Serikali lege lege. Kwa hiyo naweka wazi wenzangu, hii Serikali ya CCM haijachoka, Serikali inabebwa na wanaobebwa hawachoki. Sasa sisi wananchi tunaowabeba tumechoka.

(Hapa kuna Mheshimiwa alikuwa anamrushia maneno mzungumzaji bila utaratibu)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Uvumilie baba, ninyi si mmesema sana hapa, kwani si nafasi yangu hii!

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tanzania wa vijijini wamejengewa zahanati, dawa hawana; wamejengewa shule Walimu hawana. Halafu mnakuja hapa mnasifia barabara, barabara za kuja kwenu ninyi Dodoma, wakubwa ninyi, barabara mbovu. Nawaomba sana Serikali ya CCM, Watanzania wamechoka kukubebeni. Tarehe 25 mwezi wa Kumi Watanzania wamechoka, fungeni virago muondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, anakuja Mbunge hapa anajisifu, nimejenga hospitali halafu baadaye anaomba, we jenga tu basi, kazi yako si kujenga? Jenga barabara, jenga hospitali, jenga jenga jenga. Naomba sana, ninyi Wabunge wa CCM mnajiaga wenyewe, kasema Halima Mdee mnajitekenya wenyewe, mnacheka wenyewe. Na mimi nawaambia *wamandharaba nafsi laa yabuki*, anayejipiga mwenyewe halii tarehe 25 ndio mwisho wenu mwezi wa Kumi.

Hivyo mnawafanya Watanzania wajinga, hawaelewi, wanaelewa! Ninyi mnashiba, ninyi mna kila kitu, lakini Watanzania hali zao si nzuri. Nawaomba sana Wabunge wa CCM ukubalini ukweli na kama ukweli hamuukubali basi kwaherini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Selemani Bungara. Jimbo langu la Kilwa Kusini, kuna ahadi ya Mheshimiwa Kikwete, barabara ya Kwamkocho-Kivinje, kilometa nne na nusu, mpaka leo hakuna kitu. Inasemekana Mheshimiwa Kikwete mwezi wa Kumi pengine atakuwa anaondoka, namwomba tarehe saba mwezi wa saba mwaka huu sikukuu ya wakulima aje kufungua barabara ya Kwamkocho-Kivinje, aje kufungua, aje kufungua. *(Kicheko)*

Miaka mitano kaahidi kilometa nne inashindikana, namwomba tarehe saba mwezi wa Saba aje kufungua barabara hiyo. Mheshimiwa Maghembe maji mpaka sasa hivi Kilwa asilimia 47, tangu mwaka 2010 asilimia 47, mpaka leo asilimia 47. Naomba sana Mheshimiwa Maghembe mliahidi mtatoa milioni mia nane kwa ajili ya mradi, mtimize, mradi wa maji wa Mpala-Kivinje milioni mia nane senti tano hamjatoa. Katika bajeti hii upande wa maji vijijini mliahidi mtatoa Shilingi milioni mia nne na saba, mmetoa milioni mia mbili tu, bado miezi miwili na nusu sasa hivi.

(Hapa kuna Mheshimiwa alikuwa anamrushia maneno mzungumzaji bila utaratibu)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Daraja la Mkapa limekwisha, lakini naamini kabisa barabara ya kusini imekwisha baada ya kuingia mimi na Barwany. *(Kicheko)*

Eee, ndivyo hivyo baba, mlikuwa peke yenu CCM mlishindwa kujenga barabara, miaka hamsini hamkujenga, kuingia Barwany, kumbe wameelewaaa! Ndiyo mnamaliza sasa hivi, bila sisi msingemaliza ninyi. Ninyi sawa sawa na patasi bila kugongwa hamwendi. Patasi haifanyi kazi mpaka igongwe na CCM haifanyi kazi mpaka ipigwe. Hii patasi, patasi hata uionoe namna gani, lakini kama hukuigonga haifanyi kazi, ndiyo Serikali hii ya CCM hii. Haina maana yoyote.

(Hapa kuna Mheshimiwa alikuwa akimrushia maneno mzungumzaji bila utaratibu)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Wako, muda wangu mimi. Naomba sana Serikali ya CCM, mwaka 2015 Watanzania tumechoka na Serikali ya CCM lege lege.

(Hapa kuna Waheshimiwa walikuwa wakimrushia maneno mzungumzaji bila utaratibu)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Aah! Bwege si ndo nipo? Hamnitoe na hamna kunitoa mkimweka yeyote mimi hamnitoi na naendelea tu. Eeeee! Eeee! Mje wote Kilwa kufanya kampeni ng'o sitoki mimi, kwa sababu wananchi nimewafanyia yale wanayoyataka. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba sana Waziri wa Maji uje Kilwa, uje kuleta maji Kilwa Kivinje. Kama ukileta kosa, usilete kosa, *wamandharaba nafsi laa yabuki,* sisi hatuna wasiwasi. Ukinyoa kosa, ukisuka kosa. Miaka 50 Watanzania tumeichoka CCM, hatuitaki. Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Aaaa! Huyu ni Selemani Bungara, Mbunge wa Kilwa huko. Mheshimiwa Mama Mkanga, au Mama Mkanga ametoka kidogo, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati!

MHE. ABUU HAMOUD JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema, lakini vile vile kutuwezesha kuwepo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikupongeze wewe na kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni hii ya leo, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata tabu sana mwanzo hapa wakati ndugu zetu wanaongea, wanasema CCM haijafanya kitu. Nilikuwa napata shida, lakini nimesoma kitabu cha Waziri Mkuu, yako mambo yamefanyika. Kwa kipindi hiki cha miaka mitano leo hii ukiangalia kwanza Dar es Salaam, barabara ambazo zinajengwa na hasa mradi ule wa mabasi ya kwenda kasi, sasa nashangaa ndugu zangu hawayaoni haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye Kitabu cha Waziri Mkuu vile vile imeonesha uwanja wa ndege sasa hivi jinsi gani unavyokarabatiwa na unajengwa uwanja mwingine mpya. Vile vile kuna daraja la Kigamboni pale limeelezewa kwenye kitabu hiki cha Waziri Mkuu kazi ambazo zinafanyika, sasa haya yote hawayaoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiujumla tu kwenye kitabu hiki cha Waziri Mkuu na Mheshimiwa Chami jana alisema hapa, takriban barabara zimejengwa kilometa elfu tatu mia nane na kitu hizi. Sasa napata tabu wakisema kwamba CCM haijafanya kitu, sasa sijui kitu gani wanataka CCM ifanye. Hata hivyo, najua wanataka nini hawa, kwa sababu najua CCM imefanya mambo, sasa wanachotaka wao nakijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa hayo, kwenye Jimbo langu kuna mambo mengi yamefanyika, mengi sana tumefanya kwenye Jimbo letu. Kwanza kabisa ukiangalia katika mradi wa maji, kwanza kabisa Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya 2010/2015 kwenye Jimbo letu tumetekeleza kwa asilimia 95. Hata ushindi vile vile unafanana na utekelezaji wa Ilani. Katika ushindi tumeongeza kidogo tu, tumeshinda kwa asilimia 97. Tungetekeleza kwa asilimia 100 maana yake tungeshinda kwa asilimia 100, lakini kidogo tu, naamini tukimaliza maliza mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waarabu wana methali yao moja wanasema *walijununu fununu wal-haq-lifan, don't worry about me, aladh akhyana baada mamat mushur*. Tafsiri yake wanasema: "Kila mtu na akili yake, lakini vile vile kila mtu na wendawazimu wake, na kila mtu ana fani yake." Pia uwendawazimu haukai barabarani unakaa kichwani, ndiyo maana wakati mwingine unaweza kuamka asubuhi tu ukajikuta maneno yako si mazuri, uwendawazimu unataka kuanza. Sasa simalizii kwa sababu mmeshapiga makofi, mnaelewa nataka kusema nini.

WABUNGE FULANI: Aaaa!

MHE. ABUU HAMOUD JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo letu yako mambo tumeyatekeleza vizuri katika suala hili la mradi wa maji. Tuna mradi wa maji kutoka Chalinze unakwenda mpaka Lukenge kule takriban bilioni tatu, mradi mkubwa tu. Sasa watu wa Kibaha Vijijini ukiwaambia CCM haijafanya kitu, wanashangaa, kwa sababu kule toka dunia ianze hakukuwa na mradi wa maji, sasa hivi tuna mradi mkubwa tu wa maji kule. Mradi huu umetoka Magindu, Gwata, Gumba na Lukenge. Kazi imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuna mradi wa maji Mwanabwito, Kikongo, Lupunga, Soga, Kipangege, Boko Mnemela, Kisabi, Ruvu kwa Dossa, Vikuruti, Msongola. Huku kote toka dunia imeanza hakukuwa na maji, sasa hivi Serikali imelepeka maji, leo unatuambia hatujafanya kitu! CCM imefanya mambo makubwa sana, kazi yetu ndogo tu pale, fedha zipatikane kwa wakati tuweze kumalizia miradi yote kwisha na ikifika 2015 tunachukua tunaweka kama kawaida yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya umeme takriban vijiji 11 tumepata umeme. Kuna mradi wa Umeme unatoka Gwata, Gumba, Magindu, Ruvu Kitomondo, Makazi Mapya, Kikongo, Lupunga, Mpiji, Mwanabwito, Msufini, Vikuruti Miande na Kibwende. Miradi hii yote ya umeme tumepata kupitia Serikali ya CCM na kipindi hiki ambacho kimebaki. Kipindi kilichobaki kumalizia tu *REA* wapate pesa za kutosha ili tuweze kumalizia miradi ambayo imebaki baki. CCM imefanya mamb makubwa sana.

Ndugu zangu, yako mambo tu ya kuweza kufanya mambo vizuri zaidi tukafanikiwa tu, labda tuiombe sasa Serikali, kuna Kituo cha Afya pale Mlandizi, tumeomba muda mrefu sana na sasa tumeshakamilisha karibu vigezo vyote, tulitakiwa sasa Serikali itusaidie ipandishe hadhi ili tupate Hospitali ya Wilaya. Tukipata Hospitali ya Wilaya itapunguza kero kubwa ya *referral* ambapo watu wanatoka pale kwenda Tumbi. Kazi imefanyika, katika Halmashauri tunafanya kazi kubwa, kazi iliyobakia Serikali ipandishe kituo hiki ili kiweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa jana pia nilizungumza kwenye bajeti iliyopita, suala zima la barabara ya Makofia-Mlandizi-Mzenga. Tumeizungumza sana barabara hii kwa muda mrefu sana. Tunaiomba sasa Serikali iangalie jinsi gani ya kuweza kutusaidia katika barabara hii. Tukifanikiwa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami itapunguza kero kubwa kwa wananchi, lakini vile vile itakuza uchumi mkubwa kwa Wanakibaha Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake ya mwaka wa jana alizungumzia barabara ya Dar es Salaam ambayo inakwenda mpaka Mlandizi, itajengwa kwa barabara sita na ikitoka pale itajengwa kwa barabara nne mpaka Chalinze. Kwenye hotuba yake safari hii sijaiona, sasa baadaye akipata nafasi ya kuhitimisha pale basi atatujibu kuhusiana na barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilizungumzia sana suala la kile Kiwanda cha Nyama pale. Kiwanda kile kimechukua muda mrefu sana. Kiwanda kile kikijengwa kitapunguza kero kubwa ya ajira, itasaidia vile vile kukuza soko kubwa la wafugaji wetu pale, lakini itapunguza vile vile kama nilivyosema mwanzo suala zima la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la barabara ambayo tuliizungumzia ya kutoka Chalinze kwenda Magindu, Magindu - Lukenge, Lukenge - Bagamoyo Vijijini. Tumeizungumzia kwa kiwango kikubwa ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu barabara hii inaunganisha takriban Wilaya tatu ama Majimbo matatu. Jimbo la Chalinze, Kibaha Vijijini na Morogoro Vijijini. Barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumzia suala zima la Dar es Salaam. Dar es Salaam watu wote mashahidi na ukiangalia sisi Wabunge wote kwa asilimia kubwa tunaishi Dar es Salaam, kero ambayo imetokea juzi wote mashahidi tumeiona. Kazi yetu kubwa tu niishauri Serikali yangu iweze kujenga sasa barabara nyingi ipunguze kero ile. Kwa mfano pale Aga Khan ikijengwa barabara moja ile pembeni pembeni kwa baharini ile inaweza

kupunguza kero kubwa ya foleni hizi ambazo zinasababisha kero kubwa. Unaona sasa kengele ya pili hiyo eee?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Lissu!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Niwashukuru sana sana akinamama wote na wananchi wote ambao katika utekelezaji wa majukumu yangu wameweza kunisaidia sana na wamenipa ushirikiano mkubwa. Nimpongeze Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuweza kuliongoza Bunge letu hili. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote waliopo katika Wizara yake kwa kutuletea hii hotuba ambayo ni nzuri sana na imeleta ufafanuzi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba sisi Wabunge tunapopata nafasi ya kuchangia humu, hebu tuwatendee haki wananchi wetu tunaowawakilisha, tusije hapa kupiga vijembe. Najua muda wake bado, mwezi wa Kumi unakuja na Bunge likiisha tutaendelea kupiga hivi vijembe. Hivi unaposema kwamba Serikali ya CCM imechoka unamaanisha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye maandiko ya Biblia yanasema kwamba: "Toa kwanza boriti kwenye jicho lako ndipo utaona kibanzi kwenye jicho la mwenzako." *(Makofi)*

Hivi huu uchovu wanaouzungumzia hapa wameshauona kwenye Majimbo yao ya Upinzani? Mimi nakaa kwenye Jimbo la Upinzani, kuna mambo mengi na mabaya sana ambayo wananchi wanayalalamikia. Hivi wenyewe hawayaoni? Hawaoni kama wamechoka? Kuna Wabunge wengine wanajiita Mawaziri Vivuli, kazi kutwa kwenda kuwasumbua Mawaziri wenye dhamana, kwani hatujui?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mmoja leo amechangia, amemsema sana Waziri wa Maliasili, lakini amesahau kumsema Waziri Kivuli. Nakumbuka Mheshimiwa Zitto alisema sana kuhusu huyo Waziri Kivuli, matatizo yake hamuyaoni? Kwa nini mnazungumza tu kwamba Mawaziri wetu wamechoka, ninyi Mawaziri Vivuli hamjachoka? Mbona wananchi wanajua mnachokifanya? Hivi leo hii Mbunge mzima wa Upinzani anashindwa kusema mambo ambayo ameyawasilisha Bungeni mpaka aje Mheshimiwa Tundu Lissu amsemee? Hivi kweli hajachoka huyo?

MJUMBE FULANI: Kwenye Jimbo lake!

MHE. RITTA E. KABATI: Jamani kwenye Jimbo lako mpaka mtu akusemee? Hivi leo hii sisi tunapitisha bajeti hapa Bungeni, lakini wanakwenda kuwahamasisha wananchi, wanakwenda kuchoma barabara ambazo tumezitengea pesa, wanakwenda kuchoma magari ya Serikali ambayo tumeyapangia bajeti, je, huu ni uzalendo? Halafu leo hii mnawaambia wananchi kwamba eti watuhukumu, watuhuhukumu kwa kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaisahau siku ambayo wananchi walihamasishwa, vijana wetu wakaandamana barabarani, ilikuwa ni siku ya Jumapili, sitaisahau kwa sababu hata mimi niliumizwa na akinamama wengi waliumia, hatukufanya ibada kwa sababu ya vitu ambavyo si vya ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwatendee haki wananchi wetu tunaowaongoza, wametutuma Bungeni kuja kuwasilisha matatizo yao na kero zao ili zipatiwe ufumbuzi, wananchi hawajatutuma tuwaambie waandamane. Pia, sitasahau, nilikwenda hospitali nikawakuta vijana wamelazwa kwa ajili ya maandamano, lakini wamesusiwa hata hawaangaliwi. Nilikuta vijana wamewekwa ndani, wakubwa wenyewe wanajitoa, lakini watoto wetu ambao tumewazaa sisi akinamama tuna uchungu mkubwa….

MJUMBE FULANI: Pole!

MHE. RITTA E. KABATI: Watoto wameachwa wenyewe, mimi kama Mbunge nilikwenda kuwatoa na wengine nikawawekea dhamana. Jamani, tunakwenda wapi?

Mnakwenda kwenye vyuo mnawahamasisha vijana wetu, mbona vijana wenu hatuwaoni kushika na kutangulia na mabango? Hetu tuitendee haki bajeti hii na tuwatendee haki wananchi. Sasa hivi wananchi hawawezi kupotoshwa kwa maneno ya hapa Bungeni, wananchi wetu wataona kazi mnazozifanya kwenye Majimbo yenu, mbona mna Majimbo? *(Makofi)*

MJUMBE FULANI: Kabisa!

MHE. RITTA E. KABATI: Kwa nini msifanye kazi zionekane halafu mje kusema hapa? Hebu tuitendee haki bajeti ambayo imewasilishwa ili tunapomaliza tukumbukwe kwa hilo, tutakumbukwa kwa nini?

MBUNGE FULANI: Kwa matusi.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ambayo kwa kweli nisipoyasema na kuyatolea shukrani kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi nitakua sijajitendea haki na sijawatendea haki wananchi wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa uhaulishaji wa msitu wa Kiesakilolo, kwa kweli ule msitu nimeusema mno. Namshukuru sana Mama Ishengoma, wakati ule alikuwa Mkuu wetu wa Mkoa, tuliambatana mpaka Wizarani kwa Waziri ili kuhakikisha kwamba ule msitu unahaulishwa ili tuongeze kipato, ajira na uchumi kwa wananchi wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba siku zote nikileta *issues* za wananchi hapa, Mbunge mwenzangu ananikorogakoroga, lakini nasema hivi, wananchi wanaona, ifike sehemu sisi wote ni Wabunge hivyo unapokuwa Mbunge wa Viti Maalum ni Mbunge ambaye unatakiwa uwawakilishe wananchi. Wanawake tunaweza, wananchi tupeni dhamana, nchi hii bila wanawake haiwezi kufika popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa nchi hii sasa hivi ni mwanamke na wala siyo siri, zamani tulikuwa tunasema mpaka tuwezeshwe, lakini sasa hivi tuna Benki ya Wanawake ambayo imekuwa ikiwawezesha wanawake, ipeni ruzuku. Tunaomba zile 10% Mheshimiwa Waziri utuambie, Halmashauri ambazo hazitoi haziitakii mema Serikali yetu na tutakuwa bega

kwa bega. Tunakujua Mheshimiwa Waziri ni mwanamke mwenzetu, hivyo basi pambana ili wanawake na vijana wetu watendewe haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru TAMISEMI kwa Hospitali ya Wilaya, yalikuwa ni majengo ambayo hayafunguliwi siku zote. Nilileta swali na nikamwambia Mheshimiwa Mwanri na yeye ni msikivu kabisa, alikuja Iringa mara moja akafanya ukaguzi hospitali ikafunguliwa hapohapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, wakati huo alikuwa Waziri wa Afya, mara moja nilikwenda Wizarani, Hospitali ile ikasajiliwa na kupewa mgawo. Mwenyezi Mungu awabariki na wananchi wa Iringa hawaitasahau Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni gari la wagonjwa, suala hili nimelizungumza sana. Mheshimiwa Mwanri anakumbuka siku nilipoleta swali Mheshimiwa Msigwa akanipinga, siyo siri. Naomba gari la wagonjwa kwenye hospitali yetu ya Iringa kwa sababu vituo vyote vya afya hakuna magari, wanawake wanapata shida, vifo vya akinamama na watoto vinatokea ni kwa sababu pia hakuna magari. Wanachukuliwa kwenye bajaji na hata mikokoteni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna tatizo la gari ya wagonjwa katika Hospitali ya Misheni ya Tosamaganga. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Taifa wa UWT walikwenda kwenye ile hospitali ulipofanya ziara, lakini bado mpaka leo gari halijaletwa Tosamaganga na aliyekuwa Waziri Marehemu Mheshimiwa Mgimwa, Mwenyezi Mungu amweke mahali pema, alikuwa analishughulikia sana na wewe najua ulikwenda kumwambia Mwenyekiti wa UWT Taifa, lakini mpaka leo hii bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipouliza swali siku ile niliuliza kwa Mkoa mzima, Wilaya zote hazina magari, choka mbaya, hata Hospitali ya Mkoa nayo haina magari na yaliyopo yamechoka. Hili lilijithibitisha pia wakati walipopata ajali watu 50, walikufa, nampongeza Mkuu wa Mkoa wa sasa na Wakuu wa Wilaya, kwani walifanya kazi kubwa sana, maiti 50 siyo mchezo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwani muda umekwisha, ni kengele ya kwanza!

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Christina Lissu atafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mawazo yangu katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi wakati Mheshimiwa Mary Chatanda anachangia mjadala huu aliongelea habari za ufisadi katika Jimbo analoliita la Ikungi. Kwanza nimpe taarifa kwamba nchi hii haina Jimbo la Ikungi, ni ajabu kabisa kwa Mbunge wa CCM kutokuyajua maeneo ya utawala ya nchi hii kwani nchi hii haina Jimbo la Ikungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika maelezo yake Mheshimiwa Mary Chatanda alimhusisha Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki katika maelezo yake na kwa hiyo nikajua kwamba habari alizokuwa anazieleza ni habari za Jimbo la Singida Mashariki na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ambapo mimi ni Mbunge na ni mkazi wa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokujua maeneo kwanza ni shida, kwa watu wasioyafahamu maeneo halisi wanapelekwa kufanya kazi katika maeneo hayo, kwa hiyo, hatuna Jimbo la Ikungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe Mheshimiwa Mary Chatanda kwamba Jimbo la Singida Mashariki ambapo mimi mwenyewe ni mkazi na Mbunge wa Viti Maalum katika Wilaya ile, halina ufisadi katika Mfuko wa Jimbo, hakuna ufisadi katika Mfuko wa Jimbo. Habari hizi zilianza mara tu Jimbo hili lilipokwenda kwenye Upinzani, Madiwani wa CCM wakaanzisha suala la ufisadi. Kwanza nikupe taarifa…

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge alitakiwa atangaze maslahi kwamba, huyo Mbunge ambaye anaogopa kumtaja jina ni kaka yake Mheshimiwa Tundu Lissu.

Kwa hiyo, kwanza anatakiwa ku-*declare interest*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina umepewa taarifa.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake sina haja ya kuitaja kwa sababu wote mnajua kwamba mimi ni dada wa Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini hili nalizungumza kama Mbunge na kama mkazi wa Jimbo la Singida Mashariki. *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, habari hizi zilipoanzishwa na Madiwani wa CCM Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina, samahani kidogo, naona kuna Mheshimiwa Mbunge amesimama.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, utanilipia muda wangu.

NAIBU SPIKA: Ndiyo, Makatibu muutunze muda wa Christina.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, unaelewa kwamba katika utaratibu wetu humu ndani, unatakiwa ku-*declare interest* unapozungumza masuala ambayo ni *monetary value,* vitu ambavyo vina *monetary value* na siyo *relationship, you don't to declare interest in relationships, we all do it*. Mheshimiwa Hawa Ghasia hasomi kanuni, mpe kanuni asome.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wenje sawa, Mheshimiwa Christina!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wa CCM walipoanzisha sakasaka la Mfuko wa Jimbo la Singida Mashariki, kwanza nikwambie, kwa mara ya kwanza baada ya miaka 50 ya Uhuru ndiyo wananchi wa Singida Mashariki wamejua kwamba huwa kuna Mfuko wa Jimbo, miaka yote tulikuwa hatujui habari ya Mfuko wa Jimbo. Kwa mara ya kwanza wananchi wa Singida Mashariki ndiyo wamejua kwamba kuna Mfuko wa Jimbo.

TAARIFA

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Taarifa!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watulie.

Mheshimiwa Chatanda aliongea akamaliza.

TAARIFA

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa hizo taarifa Mkurugenzi alimtuma Mkaguzi wa Halmashauri alifanya ukaguzi ….

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mifuko ya Jimbo haikuwepo!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: …katika Mfuko ya Jimbo mara mbili, Mkurugenzi alimtuma Mkaguzi wa Halmashauri afanye ukaguzi wa Mfuko wa Jimbo mara mbili na kaguzi zilifanyika na matokeo yalionekana na hakuna ufisadi wowote, naomba niwape taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wana CCM hawajapokea vizuri kichapo cha wananchi wa Singida Mashariki mwezi wa Kumi mwaka jana wasubiri hitimisho mwezi wa Kumi. Wananchi wa Singida Mashariki wana imani isiyo na kipimo juu ya Mbunge wao, kwa hiyo, hizi propaganda hazitawabadilisha wananchi wa Singida Mashariki juu ya imani kubwa waliyonayo kwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chatanda angetusaidia kama angeiuliza Serikali yake ya CCM kwa nini hamjapeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani tunaona kwamba Serikali katika utekelezaji wa hotuba ya bajeti ya mwaka huu fedha zilizopelekwa mikoani, fedha za ndani ni 17% ya fedha za maendeleo ndiyo zimepelekwa mikoani. Hili ndiyo ambalo Wabunge wa CCM wanatakiwa waiulize Serikali yao, 17% ya fedha ndiyo zimekwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepeleka katika Halmashauri fedha za ndani 24% tu, halafu Serikali wanakuja wanalaumu eti ooh wafadhili sijui wasaidizi sijui wahisani hawajaleta fedha za maendeleo, je, hizi ambazo Serikali ilitakiwa itoe kwa fedha za ndani mbona ni kiwango cha 20% au chini ya 20%?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Serikali iliyochoka, kupeleka 17% mikoani, kupeleka 24% ya fedha za maendeleo katika Halmashauri mnatarajia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliyochoka kwa miaka mitano imeleta mradi wa vitambulisho vya Taifa. Katika kitabu cha Waziri Mkuu mwenyewe ukurasa wa 21 anaelezea mafanikio yaliyopatikana katika mradi wa vitambulisho vya Taifa. Wameweza kuandikisha vitambulisho kwa Mikoa mitano tu Tanzania Bara na ni wastani wa watu 5,000,000 tu kwa miaka mitano ndiyo wametoa vitambulisho. Kama siyo Serikali iliyochoka ni kitu gani? Miaka mitano watu 5,000,000 tu kwa mradi ambao ulikuwa wa kipaumbele kama huu wa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Waziri Mkuu anaeleza mafanikio yaliyotokana na mradi wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*. Bila aibu Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake anatuambia mafanikio yaliyopatikana katika elimu ni wastani wa 81%.

Mheshimiwa Naibu Spika, niambie kwa elimu ya nchi hii ni madarasa gani wamejenga? Madawati yako wapi? Vifaa vya kufundishia viko wapi? Walimu wenye uwezo wako wapi ili tufikie hiyo 81%? Serikali ilishusha viwango vya ufaulu ili ionekane watoto wamefaulu, lakini unaposema tumefanikiwa katika elimu kwa 81%, hivi ni mazingira gani katika elimu yaliyosababisha mafaniko hayo? Mbona sisi hatuyaoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Waziri Mkuu anaendelea kutuambia, mafanikio ya maji katika nchi hii mradi wa *BRN* ni 80%. Hivi nchi hii unapoongelea mafanikio ya maji kwa 80% haya maji yako wapi? Kwako Kongwa hapo hakuna maji, kwetu Singida hakuna maji, nchi hii haina maji…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Chatanda nilikuona umesimama, ilikuwa ni taarifa au ni nini ile?

WABUNGE FULANI: Aaaa!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, acha niendelee kuwakumbusha, ni hotuba ya Serikali yao…

NAIBU SPIKA: Pokea taarifa Mheshimiwa Christina.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, sijamaliza, kilimo…

NAIBU SPIKA: Pokea taarifa, halafu utamalizia dakika zako, nilimwona alikuwa amesimama.

Mheshimiwa Chatanda!

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kuona kwamba dada mtu amekazana kweli kweli kumtetea kaka yake. Alichotakiwa kufanya ni kumshauri na kumsisitiza kaka yake kwamba anatakiwa asipinge maendeleo katika Wilaya ya Ikungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo fedha za Mfuko wa Jimbo anatakiwa azipeleke kwa mujibu wa utaratibu unaotakiwa, hao waliokwenda kukagua ndiyo hao hao anaowatisha, halafu wanampa pesa anazipeleka mkononi badala ya kuzipeleka kwa mujibu wa taratibu ambapo zinatakiwa ziende kwenye *account* ya vikundi ambavyo vinapewa. Huo siyo ufisadi?

WABUNGE FULANI: Ufisadi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina, taarifa hiyo!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sielewi kama huyu ni Mbunge wa Tanga, Arusha au Singida, kwa hiyo hana kitu anachoniambia. *(Makofi)*

TAARIFA

MJUMBE FULANI: Taarifa!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu, anaelezea mafanikio katika kilimo, anasema kilimo kimefanikiwa kwa 77%, aibu! 77% ya mafanikio ya kilimo yako wapi? Yako wapi mashamba ya mfano? Yako wapi mashamba ya umwagiliaji? Zipo wapi pembejeo? Kwetu Singida tunalima alizeti, lakini sijaona mtaalam aliyeletwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi juu ya kilimo cha alizeti. Hii taarifa ni ya kwenye habari za maandiko lakini haitatufikishakwenye ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa suala la afya katika hotuba ya Waziri Mkuu, lakini cha ajabu, mimi najua *MSD* inakufa, lakini Waziri Mkuu hajatueleza mpaka sasa deni la *MSD* ili *MSD* iendelee kuisaidia nchi hii, wamelilipa kwa kiasi gani? Najua ni mabilioni ya pesa, *MSD* iko hoi taabani na itashindwa kuhudumia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la gesi asilia….
NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina kuna taarifa!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili Watanzania wasipotoshwe.

Mheshimiwa Mbunge ni vizuri angetembea katika ukweli, *MSD* ni chombo ambacho ni imara na ndiyo sababu nchi za *SADC* zimeichukua *MSD* ya Tanzania kuwa *Procurement Unit*, ingekuwa imefikia hali hiyo, *SADC* chombo kikubwa katika vyombo vya maeneo, nchi 17 tangu mwaka jana zimetembelea *MSD* kama chombo bora cha mfano, *MSD* sasa hivi wanapeleka dawa mpaka kwenye Zahanati na *MSD* sasa hivi tunashukuru imekuwa mfano bora, imejipanga vizuri kuboresha huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hiyo tunashukuru *Global Fund* pamoja na *Bellinda Milgates* wanafanya kazi nzuri ili kuiboresha na kuwa chombo cha mfano. Kwa hiyo, maneno hayo siyo ya kweli. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina malizia!

MHE. CHRISTINA M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa na wewe unaruhusu mtu anaeleza mambo ambayo hajibu mambo ambayo nilikuwa naeleza. Nimeuliza deni la *MSD* wamelipa shilingi ngapi mpaka sasa hivi? Kama Waziri haelewi mjadala ninaousema ndiyo hayo wanakwenda kutupotosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la gesi asilia. Tunajua kwamba, nchi yetu ina neema ya gesi. Sasa niishauri Serikali na nashauri kwa jicho la ukali kabisa na macho yangu ni makubwa Mwenyezi Mungu amenijalia, tunaitaka Serikali, mwaka huu tunajua tuliambiwa kwenye Kamati ya Bajeti, Serikali itaanza kupata mapato kutokana na gesi, sasa namwambia Waziri Mkuu, tunataka tuone kwenye Bajeti Kuu ya Serikali mapato ya gesi kuwe na *line item specific* kwa ajili ya mapato yatakayotoka kwenye gesi. Isije ikawa tena hadithi kwamba, kuna taasisi imeundwa itakayopokea fedha za gesi halafu ilete gawio la asilimia kadhaa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulipelekwa kutembelea nchi ambazo uchumi wake unategemea gesi; tumekwenda Norway, Sweden, Uholanzi na kadhalika. Nchi zile katika bajeti zao unaona kabisa *income* inayotokana na gesi inaoneshwa kwenye bajeti. Kwa hiyo, unaona kabisa mchango wa gesi na mafuta kwenye Bajeti Kuu ya Serikali, inaonekana na unaona inaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika sura ya bajeti ambayo Waziri wa Fedha aliileta safari hii Bungeni ambayo atakuja kuwasilisha hatujaona kipengele cha gesi kikijitegemea ili Watanzania waone shilingi ya kwanza inayohusiana na gesi itakapoingia kwenye Serikali inayohusiana na gesi tuiangalie. Mwaka unaofuata tuone inaongezeka ili baadaye tusije tukapigwa changa la macho kama ambavyo tumefanywa kwenye madini, tunaambiwa yanachangia lakini kwa kweli hatujui yanachangia wapi na kwa kiasi gani.

Kwa hiyo, niitahadharishe Serikali, wafanye kama nchi ambazo wameiga mfano na kule walikotupeleka kujifunza. Serikali zile zinazotegemea uchumi wa mafuta na gesi wanaonesha kabisa kwenye bajeti ile sehemu ya mapato ya Serikali yanayotokana na mafuta na gesi kwa mwaka huu ni kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sura ya bajeti yetu imekuja kama *business as usual* wakati tunaambiwa tujiandae kwa uchumi wa gesi. Pamoja na hilo sura ya bajeti inakuja na shilingi trilioni 22...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Christina, muda sasa umekwisha.
MHE. CHRISTINA M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anastazia Wambura!

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia, nadhani nitakuwa mchangiaji wa mwisho jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mchango mrefu kidogo lakini ni bora niache baadhi ya masuala, ili nichukue nafasi hii kumjibu Mheshimiwa Christina au kumpa taarifa kwa suala moja la maji. Naomba Mheshimiwa Mbunge afahamu tu kwamba, kuna tofauti katika utekelezaji au ukamilishaji wa miradi na upatikanaji wa maji. Alivyosema kwamba, ukamilishaji wa miradi ni asilimia 85 haikuwa na maana kwamba, ndiyo upatikanaji wa maji. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametwambia wazi kabisa kwamba, upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nitoe tu mfano kwa Mkoa wetu wa Mtwara. Nimekutana na Wataalam wa kila Halmashauri katika Mkoa wa Mtwara na wamenipa takwimu nzuri sana katika utekelezaji wa hii miradi ya maji. Kuna ambao wametekeleza kwa silimia 85 na wengine asilimia 75. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna mradi wa Chiwonga kule Newala, umetekelezwa kwa asilimia mia moja, lakini upatikanaji wa maji kwa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, ni asilimia 29 kule vijijini. Kwa hiyo, hiki ni kitu kimoja tofauti kabisa, utekelezaji wa miradi na upatikanaji wa maji ni tofauti. Katika mradi huu wa Chiwonga umetekelezwa kwa asilimia mia moja, lakini wananchi hawapati maji kutokana na Mkandarasi kutokabidhi mradi. Kwa hiyo, tunaweza tukasema upatikanaji wa maji yale ni sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwe tunatofautisha baadhi ya hizi takwimu, tusizichanganye na kuwapotosha wananchi. *(Makofi)*

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Pokea taarifa Mheshimiwa Anastazia. Haya Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Anastazia kwa kuchangia hotuba hii akiwa na *data* kamili. Naomba nimpe taarifa moja kwamba, kwa kuwa ameonesha kabisa kila anachochangia kina takwimu za kuonesha maendeleo ya utekelezaji wa Ilani, yaliyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na kwa kuwa kila Mbunge wa Chama cha Mapinduzi aliyesimama hapa ameonesha utekelezaji mkubwa sana wa Ilani katika Jimbo lake akiwa na *data* kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa wapo Wabunge wengine hasa wa Upinzani wanaposimama wanaonesha kwamba, Serikali haijafanya kazi, lakini bila kutoa data nzuri, je, Mheshimiwa Mbunge yuko tayari sasa kuwaambia Watanzania wawachague Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu wanasimamia vizuri utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anastazia Wambura, taarifa hiyo!

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kabisa kabisa. Nashukuru sana kwa taarifa hiyo na niko tayari kabisa kuwaambia wananchi wawachague Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Pia naweza nikatoa mfano mmoja kwamba, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri ambao wamesimamia Chama cha Mapinduzi, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, ambayo ni mpya imeanza mwaka 2008 na mwaka 2010 upatikanaji wa maji pale ulikuwa ni asilimia 26, lakini mwaka 2014 upatikanaji wa maji ni asilimia…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machali kuna nini tena?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa kuhusiana na suala la utaratibu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) na 64(1) (a) kwamba: "Mbunge anapokuwa Bungeni hatatoa taarifa ambazo hazina ukweli".

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeainisha mahali hapa kwamba, Serikali imekuwa inasuasua kwenye kupeleka fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na ndiyo maana ukipitia taarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imedhihirisha kabisa kwamba, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni asilimia 24 peke yake ya fedha za miradi ya maendeleo, kiasi kwamba miradi ya maji inasuasua vijijini na mijini. Miradi ya kilimo halikadhalika inasuasua, sasa unawachagua Wabunge wa CCM kwa sababu gani wakati Serikali imeshindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwa ni hilo tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anastazia endelea!

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei hiyo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ile ya Nanyumbu ilikuwa na upatikanaji wa maji kwa asilimia 26 mwaka 2010, lakini sasa hivi ni asilimia 47 na zaidi. Hizi zote pia ni jitihada za Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dunstan Mpaka ambaye yuko kule na Mwenyekiti wa Halmashauri ambao hadi sasa wamehamasisha wananchi kuchangia kwa kukatwa kwenye zao la korosho kiasi fulani cha fedha na wanachangia wamepata shilingi milioni 400 wameagiza mtambo wao wa maji wa kuchimba visima virefu na wameshauzindua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusiwapotoshe wananchi na wakati mwingine tuna tabia ya kuwakwamisha wasijitolee kuchangia maendeleo yao. Hili tatizo nimelikuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine kwa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, upatikanaji wa maji ni asilimia 29, lakini kuna tatizo, wafuasi wa Vyama Pinzani wanang'oa na kuharibu miundombinu. Hili ni tatizo kubwa sana na sababu ni kuifanya CCM ionekane imeshindwa. Hili ni la kweli na nimelipata katika vikao. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Uongo!

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba, kuna usemi unaosema; "Hujafa hujaumbika" na wenzetu wageni wanasema hivi; "*Everything is okay at the end, if it is not okay then it's not the end.*" Kwa hiyo, naomba pale mahali ambapo bado hatujamaliza, tuzingatie tu ushauri tunaopewa na Waheshimiwa Wabunge, fedha tunazopata kwa mfano kwenye miradi ya maji tupeleke kwa wakati na fedha za kutosha. Kwa mujibu wa Wataalam wanasema fedha zikipelekwa za kutosha tutafikia lengo la milenia la upatikanaji wa maji vijijini ambalo ni asilimia 74 au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hicho tu ndicho cha msingi, lakini kuanza kulaumiana hapa kwamba, hiki hakijatekelezeka, hiki nini na kutaka kuiwasha nchi moto ili kusudi tu tuimalize, mambo yatekelezeke wakati nchi yetu imeshaharibika haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji labda tu ni-*summarize* kwa kusema kwamba, Mkoa wa Mtwara upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 40 na hii ipo chini kabisa ya wastani wa Kitaifa ambao tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ninachokiomba ni kwamba, Serikali sasa iangalie pia yale maeneo ambayo ni ya lazima sana kupeleka fedha kwa sasa hivi, zile fedha ambazo zilikuwa zimetengwa mwaka jana zipelekwe ili kusudi na sisi tuweze kuvuka kile kiwango, tufikie angalau ule wastani wa Kitaifa. Hii ni kwa sababu

akinamama wanapata shida, kuna akinamama ambao wanaliwa na simba porini kwa ajili ya kufuata maji usiku. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali tulizingatie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli miradi mingi iko kwenye utekelezaji wa hali ya juu, kama nilivyosema asilimia 85 na 75 na mingine zaidi hata ya asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kuzungumzia suala la afya. Niipongeze sana Serikali kuhusu suala la afya kwa sababu imejitahidi sana kuongeza vituo vya afya na zahanati na hata kwa ujenzi wa baadhi ya hospitali. Kwa mfano; kuna Hospitali ya Rufaa sasa hivi inajengwa na Mheshimiwa Naibu Waziri alifika kule Mtwara kwa ajili ya kuangalia maendeleo yake. Hizi ni jitihada nzuri sana za Serikali yc Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jitihada hizi tunaziona, labda na mimi nigusie tu utekelezaji wa malengo ya milenia ya kupunguza vifo vya Wazazi. Katika Mkoa wa Mtwara tumejitahidi, hatutaki akinamama wafe lakini tukiangalia takwimu Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu wanaofariki na ukilinganisha na malengo ya milenia, utekelezaji wake Kitaifa mwaka 2012 tulikuwa ni wanawake 432 kati ya wazazi 100,000. Sasa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu ni vifo 79 ambayo ni maendeleo mazuri. Tunasikitika kuwapoteza hao waliopotea, lakini tunakwenda vizuri kwa sababu lengo la milenia tunatakiwa tusizidi akinamama 133.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ulichukuliwa naomba unifidie. Vile vile Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, kwa maana ya Mtwara Vijijini na wao wako vizuri, vifo vya akinamama ni 137 ambao ni *close* kabisa na lengo la milenia la 133. Manispaa vifo ni 239, Tandahimba ni 288, lakini kuna dosari katika Wilaya ya Masasi ambayo ni vifo 436, hii imezidi wastani wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zipo na mapendekezo na maombi ni mengi ili kusudi tuweze kuboresha hii hali. Nianzie na Wilaya ya Nanyumbu, wao wanaomba sana kile Kituo cha Afya cha Nanyumbu sasa kinastahili kabisa kuwa Hospitali ya Wilaya, wanaomba kipandishwe hadhi ili waweze kupata mgawo mzuri kwa ajili ya kununua dawa na kupunguza hizi rufaa ambazo wanawapa akinamama kwenda Masasi kule Mkomaindi. Inawezekana hii ndiyo sababu inayochangia vifo vingi katika Wilaya ya Masasi kwa sababu wanachelewa kufika kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kule Nanyumbu wanaomba Serikali itimizie ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Kituo cha Afya kule Mikangaula kwa sababu wao wameshatenga shilingi milioni 50 kwa kuanzia, kwa hiyo Serikali itekeleze hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, Mikindani, Hospitali ya Wilaya ambayo ni Likombe ilikuwa kituo cha afya, sasa hivi inapokea wagonjwa wengi na akinamama wengi, wodi ile ndogo, eneo ni dogo sana, mpaka Madaktari wanaandika dawa wakiwa nje. Wakati mwingine chumba kimoja kinatoa huduma hata nne. Kwa hiyo, hilo ni tatizo. Hili likiangaliwa na wananchi wakipewa fidia na hospitali ile ikipanuliwa tuna imani kabisa tutapunguza idadi ya vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna maombi kwamba vyumba vya kujifungulia virekebishwe, miundombinu iboreshwe ili kusudi akinababa nao waweze kuingia…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso nina dakika tatu tu zimebaki hapo.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Leo mchana wakati Mheshimiwa Chatanda anachangia alinitaja kwa jina na akajaribu kuelezea na naomba ninukuu *hansard* hapa anasema:

"Jana nimemsikiliza Cecilia, Mbunge wa Karatu anayetoka Halmashauri inayoongozwa na CHADEMA na akasema kuna ufisadi uliopindukia. Akasema Mwenyekiti wa Halmashauri amefanya ufisadi na yeye mwenyewe ni shahidi. Anaendelea kusema leo asubuhi nilimuuliza Cecilia hivi yule Mwenyekiti wa Halmashauri lile tatizo lake limeishia wapi la ufisadi alioufanya pale Halmashauri?

Anaendelea kusema: Sikiliza Dada Chatanda yule sijui kama atagombea, yale mambo aliyoyafanya kwenye ile Halmashauri hana nafasi ya kuweza kupita. Akaendela kusema Halmashauri ya Karatu anaijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme sijaongea na Mheshimiwa Chatanda zaidi ya kusalimiana pale getini wakati tunaingia kwenye ukaguzi na Mheshimiwa Makalla kama angekuwepo angekuwa shahidi kwa sababu tuliingia wote pale, tukasalimiana gari langu likasachiwa nikaondoka. Anasema nimezungumza naye leo asubuhi kitu ambacho ni uongo, lakini anasema Halmashauri ya Karatu kuna ufisadi na mimi ni shahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mimi ni Diwani katika Halmashauri ya Karatu, kwa hiyo ni sehemu ya Halmashauri ya Karatu. Hata hivyo, Mheshimiwa Chatanda wakati akiwa Katibu wa CCM, Mkoa wa Arusha aliwahi kufika na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda yuko pale ananisikia, walikuja Karatu na Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema Karatu ni miongoni mwa Halmashauri zilizofanya maendeleo kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuja Mheshimiwa Rais kufungua mradi wa maji, alikuwepo Mheshimiwa Majaliwa na Mheshimiwa Maghembe, Mheshimiwa Rais akasema Halmashauri zote zije kujifunza Karatu. Kwa hiyo, kusema kwamba leo kuna ufisadi Karatu na mimi ni shahidi anapotosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba, sijui Mwenyekiti wa Halmashauri hatagombea na nini. Hatujaongea haya na mimi si msemaji wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Karatu. Suala la kugombea ama kutogombea ni utashi wake. Mwenyekiti wetu wa Halmashauri ni kiongozi wa muda mrefu, ni kiongozi wa Halmashauri kwa miaka 10 na ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, anajua taratibu zote, mimi si msemaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kutoa hiyo taarifa ambayo amelipotosha hapa Bunge na kupotosha watu kwa ujumla. Ahsante.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Chatanda unaipokea taarifa hiyo kwa kifupi.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu ni kweli kabisa hata Naibu Waziri wa Kilimo alikwenda hivi karibuni na yeye anayezungumza sasa, alikuwepo huko wakati wananchi wa Karatu juu ya suala la ushirika pale Mwenyekiti yule amefanya ufisadi wa hali ya juu na huyu binti mimi na yeye tumeongea leo hapa. Sasa anajitetea kwa sababu nimesema siri aliyoniambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo ndiyo aliyoyazungumza.

(Hapa kulikuwa na minong'ono miongoni mwa Wabunge wakionekana kumpinga mzungumzaji)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba athibitishe anayoyasema. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano. Mkitazama muda wenu mtaona kwamba, haupo upande wetu. Kwa jinsi hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.58 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa Tarehe 15 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)